

CHUO KIKUU CHA KENYATTA
SHULE YA FANI NA SAYANSI ZA JAMII
IDARA YA KISWAHILI

ITIKADI KATIKA RIWAYA ZA SAID AHMED MOHAMED

NA
MURITHI JOSEPH JESSE

TASNIFU ILIYOWASILISHWA KATIKA IDARA YA KISWAHILI KWA
MADHUMUNI YA KUTOSHELEZA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMIFU
YA CHUO KIKUU CHA KENYATTA

JANUARY 2017

IKIRARI

Tasnifu hii ni kazi yangu asilia na haijapata kuwasilishwa kwa madhumuni ya shahada yoyote katika chuo kikuu kingine.

SAHIHI

TAREHE

MURITHI JOSEPH JESSE

NAMBARI C82/14056/2009 (MTAHINIWA)

WASIMAMIZI:

Tasnifu hii imetolewa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa Chuo Kikuu .

SAHIHI

TAREHE

PROF. GEOFFREY KITULA KING'EI

IDARA YA KISWAHILI

CHUO KIKUU CHA KENYATTA

SAHIHI

TAREHE

DKT. RICHARD MAKHANU WAFULA

IDARA YA KISWAHILI

CHUO KIKUU CHA KENYATTA

SHUKRANI

Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nguvu na hekima ya kuweza kuikamilisha kazi hii. Uwezo na rehema zake pekee ndizo zimenifaa katika utafiti huu hadi kufikia kikomo. Shukrani za kipekee ziwaandee wasimamizi wangu Prof. G. King’ei na Dkt. R. M. Wafula walioniongoza katika kuiandika kazi hii. Maarifa yao na misaada yao ya vitabu na makala mengine yalinifaa sana kuufanikisha utafiti huu. Aidha nawashukuru Dkt. Timothy Arege, Dkt. Evans Mbuthia, Prof. Mwenda Mbatiah, Prof. Rayya Timammy, Prof. Mwenda Mukuthuria, Dkt Joseph Gakuo na wahadhiri wote walionifaa na kunihimiza nilipokuwa nikifanya utafiti huu. Shukrani pia nazitoa kwa Bi. Rachel Maina kwa kuihariri kazi hii. Nawashukuru pia washirika wote wa familia yangu hasa bibi yangu mpendwa Mary Ng’endo aliyenifaa sana kwa kunihimiza na kuniombea safari ilipokuwa ngumu. Watoto wangu Ray na Prince nawashukuru kwa uvumilivu wao. Kwa wote nasema Mungu awabariki sana na awaongezee hekima na maarifa zaidi.

TABARUKU

Tasnifu hii naitabarukia bibi yangu mpendwa Mary Ng'endo na watoto wangu
niwapendao sana Ray na Prince.

IKISIRI

Utafiti huu unashughulikia itikadi katika riwaya za Said A. Mohamed ili kubainisha ikiwa itikadi zake zimekuwa zikibadilika katika zaidi ya miaka thelathini ya utunzi wake. Jambo hili ni muhimu katika fasihi kwani wahakiki wengi wanapozungumzia msimamo na mielekeo ya mwandishi kuhusu maisha na ulimwengu uliomzunguka, huchukulia kwamba msimamo huu ni mmoja na tengemano. Itikadi ndio huelekeza misimamo, mielekeo na imani ya mtunzi. Ni muhimu kuchunguza swala hili kwa kina ili kudhihirisha ikiwa itikadi hizi zinabadilika na kwa nini mtunzi S. A. Mohamed anabadilisha itikadi zake. Utafiti huu ulizingatia riwaya teule za S. A. Mohamed ambazo ziliteuliwa kimaksudi kuwakilisha vipindi tofauti katika utunzi wake. Riwaya hizo ni *Asali Chungu* (1978), *Kiza Katika Nuru* (1988), *Dunia Yao* (2006) na *Mhanga Nafsi Yangu* (2013). Tulichunguza itikadi zinazojitokeza katika kila riwaya kwa kuzingatia maudhui, dhamira, wahusika, mtindo na usemaji uliokuwa ukitawala katika kila kipindi ili kudhihirisha mtunzi anabadilisha itikadi yake kila baada ya kipindi ili kazi zake ziwe faafu kwa jamii lengwa. Nadharia ya udenguzi na ile ya kimaadili ndizo zilizotumika katika utafiti huu. Nadharia ya udenguzi ilitufaa kuangazia namna maana ya dhana ya itikadi inavyoahirishwa katika kila kipindi. Nadharia ya kimaadili ilitufaa kuangazia historia na muktadha wa kijamii ulioibusha kazi zilizotafitiwa. Mbinu za utafiti ambazo tulitumia ni maktabani na nyanjani. Maktabani, tulisoma riwaya teule na kudondoa maudhui, wahusika, mbinu za lugha na sanaa alizotumia mtunzi na kuonyesha itikadi zinazojitokeza katika kila riwaya. Vitabu vyote alivyoandika vilisomwa ili kutupa mwanga zaidi kuhusu maswala anayoshughulikia katika utunzi wake kwa jumla. Makala yaliyoandikwa na wasomi wengine kuhusu swala la itikadi pia yalisomwa na kunukuliwa ipasavyo. Nyanjani, tulimhoji mtunzi kwa njia ya moja kwa moja ili kutufafanulia zaidi kuhusu utunzi wake. Aidha, tuliwahoji wasomi wengine ambao wameshughulikia kazi zake ili kupata maoni yao kuhusu itikadi za mtunzi huyu na kuimarisha muktadha ulioibusha kazi zake. Kwa kuzingatia haya yote tuliweza kuonyesha kuwa itikadi katika riwaya za S.A Mohamed zinabadilika katika kila baada ya kipindi fulani cha utunzi. Mtafiti alipata kuwa itikadi tawala ilibadilika kutoka umwinyi, ubepari na utandawazi katika vipindi tofauti vya utunzi. Nayo itikadi ya mtunzi ilibadilika kutoka mapinduzi ya marekebisho, mapinduzi ya nguvu na mapinduzi ya nafsi. Mtafiti alidhihirisha kuwa itikadi ni dhana badilifu na nyumbufu na mtunzi hubadilisha itikadi yake ili kazi yake iwe faafu kwa jamii lengwa.

ABSTRACT

This research evaluated the use of ideology in S. A. Mohamed's novels to find out whether it impacts his works over a period of time. The study was informed by the fact that many critics tend to assume that the attitudes, thoughts and views of the writer are the same and stable all the time. Since at specific times, these attitudes, thoughts and views are informed by a certain ideology it was important to evaluate the ideologies of a writer for a longer period to see whether they remained the same or they changed after a certain period and if so why the changes happened. It was found out that the ideologies of the writer changed to fulfil the needs of the writer's audience, and reflect the changing aspects in society in relation to politics, economy, religion, traditions and general way of life. The researcher did this by analyzing ideologies in four novels written by S. A. Mohamed which were selected purposively to fulfil the needs of the research. These novels are *Asali Chungu* (1978), *Kiza katika Nuru* (1988), *Dunia Yao* (2006) and *Mhanga Nafsi Yangu* (2013). The researcher analysed the themes and characters in each novel and sought to analyse the changes reflected by the writer. Furthermore, the researcher investigated how the changes signalled the change of the writer's ideology after a certain period of time and then sought to establish why the change occurred. The theories that were used in this research were deconstruction theory which helped the researcher to demonstrate why ideology is not constant and the moral theory which guided the researcher to focus on the society and the audience that the writer aimed to reach in his works. The researcher used the library and field work method to conduct the research. In the library the main texts under analysis were read, the plots, themes, characters and style were analysed. Other texts written by the writer were read and they enriched our understanding of the issues under investigation. In addition, all texts related to the topic were read and they gave the researcher a thorough understanding of the research area. The researcher also went to the field and held discussions with the writer S. A. Mohamed and got his personal views on his works in general and specifically on the works under evaluation. A questionnaire was also used to ask the writer questions in relation to his work. The critics' views were included by the use of a questionnaire and discussions in order to get their insights into the works under investigation. It is our conviction that by doing all this, we were able to show that the ideologies of the writer kept changing after every period of time to the point of contradicting himself. This is in an effort to fulfill the needs of his society in general and his responsibility in particular. Thus the ideology of a writer keeps changing to reflect the changes in the society.

YALIYOMO

SHUKRANI	iii
TABARUKU.....	iv
IKISIRI.....	v
ABSTRACT.....	ii
UFAFANUZI WA DHANA MUHIMU	vii
SURA YA KWANZA	2
1.0 USULI WA UTAFITI.....	2
1.1 UTANGULIZI	2
1.2 SWALA LA UTAFITI	5
1.3 MASWALI YA UTAFITI.....	6
1.4 MALENGO YA UTAFITI.....	7
1.5 SABABU ZA KUCHAGUA MADA.....	7
1.6 UPEO NA MIPAKA	10
SURA YA PILI.....	13
2.0 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA.....	13
2.1.1 YALIYOANDIKWA KUHUSU ITIKADI KATIKA KAZI ZA S. A. MOHAMED.....	13
2.1.2 YALIYOANDIKWA KUHUSU ITIKADI KATIKA RIWAYA YA KISWAHILI	18
2.2 MISINGI YA NADHARIA	23
2.2.1 NADHARIA YA UDENGUZI	24
2.2.2 NADHARIA YA KIMAADILI.....	30
2.3 HITIMISHO.....	36
SURA YA TATU	38
3.0 MBINU ZA UTAFITI	38
3.1 UTANGULIZI	38
3.2 MUUNDO WA UTAFITI	38

3.3 ENEO LA UTAFIGI	39
3.4 SAMPULI LENGWA	40
3.4.1 MBINU ZA USAMPULISHAJI	40
3.5 UKUSANYAJI WA DATA	42
3.6 UCHANGANUZI WA DATA	43
3.7 VIFAA VYA UTAFIGI	44
3.8 UWASILISHAJI WA MATOKEO	44
3.9 HITIMISHO	45
SURA YA NNE	47
4.0 ITIKADI NA MTAZAMO WA MTUNZI	47
4.1 UTANGULIZI	47
4.2 HISTORIA YA MTUNZI S. A. MOHAMED	47
4.3 HISTORIA YA SIASA NA UCHUMI WA ZANZIBAR	53
4.3.1 KIPINDI KABLA YA UKOLONI	53
4.3.2 KIPINDI CHA UKOLONI WA WAARABU NA WAINGEREZA	54
4.3.4. KIPINDI CHA MUUNGANO 1964 NA KUENDELEA	58
4.4 MITAZAMO MBALIMBALI KUHUSU DHANA YA ITIKADI	60
4.5 UHUSIANO WA ITIKADI NA MTAZAMO WA MTUNZI	75
4.6 HITIMISHO	78
SURA YA TANO	81
5.0 ITIKADI KATIKA RIWAYA ZA ASALI CHUNGU NA KIZA KATIKA NURU	81
5.1 UTANGULIZI	81
5.2.0 MUHTASARI WA RIWAYA YA ASALI CHUNGU	82
5.2.1.0 ITIKADI YA WATAWALA	86
5.2.1.1 ITIKADI YA KIMWINYI	86
5.2.1.3 ELIMU	92

5.2.1.4 UTAMADUNI	93
5.2.1.5 MFUMO WA KUUMENI.....	94
5.2.1.6 NDOA NA FAMILIA	99
5.2.1.7 DINI	101
5.2.1.8 MAADILI	103
5.2.1.9 ASASI ZA UTAWALA.....	107
5.2.2.0 ITIKADI YA MWANDISHI	110
5.2.2.1 ITIKADI YA MAPINDUZI	110
5.3.0 ITIKADI KATIKA <i>KIZA KATIKA NURU</i>	120
5.3.1 MTIRIRIKO WA VITUSHI KATIKA <i>KIZA KATIKA NURU</i>	121
5.3.2.0 ITIKADI YA KIBEPARI	122
5. 3. 2. 1 MFUMO WA KIUCHUMI	123
5.3.2.3 ELIMU NA KAZI	130
5.3.2.3 NDOA NA FAMILIA	130
5.3.2.4 DINI	132
5.3.2.5 ASASI ZA UTAWALA.....	134
5.4.0 ITIKADI YA MWANDISHI	138
5.4.1 MAPINDUZI YA NGUVU.....	138
5.5 HITIMISHO.....	153
SURA YA SITA.....	157
6.0 ITIKADI KATIKA <i>DUNIA YAO NA MHANGA NAFSI YANGU</i>	157
6.1 UTANGULIZI	157
6.2 MUHTASARI WA RIWAYA YA <i>DUNIA YAO</i>	157
6.3 ITIKADI YA WATAWALA.....	162
6.3.1 ITIKADI YA UTANDAWAZI.....	162
6.3. 1.2 MFUMO WA KIUCHUMI.....	163
6.3.1.3 SAYANSI NA TEKNOLOJIA.....	164
6.3.1.4 ELIMU	166
6.3.1.5 UTAMADUNI	168

6.3.1.6 NDOA NA MAPENZI.....	169
6.3.1.9 ASASI ZA UTAWALA NA SIASA.....	176
6.3.1.10 MABADILIKO YA KIJAMII	177
6.5 MUHTASARI WA RIWAYA YA <i>MHANGA NAFSI YANGU</i>	185
6.6 ITIKADI KATIKA RIWAYA YA <i>MHANGA NAFSI YANGU</i>	186
6.6.1 ITIKADI YA UTANDAWAZI.....	186
6.6.3 ELIMU	190
6.6.4 UTAMADUNI	194
6.6.5 ASASI YA NDOA	195
6.6.7 DINI	205
6.6.8 MAADILI	207
6.6.9 ASASI ZA UTAWALA.....	209
6.6.10 MFUMO WA KUUMENI.....	210
6.6.10 UBAGUZI WA RANGI	214
6.6.11 HITIMISHO.....	217
SURA YA SABA	225
7.0 HITIMISHO NA MAPENDEKEZO.....	225
7.1 UTANGULIZI	225
7.2 MUHTASARI WA TASNIFU.....	225
7.4 CHANGAMOTO ZA UTAFITI	235
7.5 MAPENDEKEZO	235
MAREJELEO.....	238
KIAMBATISHO I.....	246
MASWALI KWA MTUNZI	246
KIAMBATISHO II	247

UFAFANUZI WA DHANA MUHIMU

Itikadi: Ni mawazo, imani, mielekeo, mafunzo na malengo ya mtunzi yanayojitokeza katika kutimiza majukumu ya kijamii, kidini, kitamaduni, kisiasa na kiuchumi na namna anavyoyawasilisha mawazo haya kwa jamii lengwa.

Maudhui: Jumla ya maswala au mambo yanayoshughulikiwa katika kazi ya fasihi. Maswala haya hutokana na jinsi mtunzi alivyoikuza mada ambayo ni msingi wa utuzi wake.

Usosholisti: Mtazamo unaotilia mkazo kuishi kidugu na kuthaminiana na kujiepusha na ukandamizaji, ubaguzi na kujilimbikizia mali.

Ukomunisti: Mfumo unaohusu ujenzi wa jamii yenye usawa wa binadamu wote katika uzalishaji, umiliki na ugawanaji wa mali, isiyo na matabaka na mapambano.

Ubepari: Mfumo wa kiuchumi unaohusu umiliki wa mali na nyenzo za uchumi kwa wachache na kuwanyanyasa walio wengi wanaobakia masikini.

Matabaka: Makundi yanayojitokeza kutokana na mfumo wa kiuchumi na siasa ambao kundi moja humiliki nyenzo za kiuchumi na mali inayozalishwa na jingine humiliki nguvu za kazi yake.

SURA YA KWANZA

1.0 USULI WA UTAFITI

1.1 UTANGULIZI

Mwandishi S. A. Mohamed ni mtunzi maarufu wa fasihi ya Kiswahili. Ameandika vitabu vingi vikiwemo riwaya, tamthilia, ushairi, hadithi fupi na vinginevyo. Katika uwanja wa riwaya, ameandika katika mawanda marefu ya wakati kwa zaidi ya miaka thelathini. Katika wakati huu wote, amekuwa akiusaili msimamo wake kila baada ya kipindi fulani. Hii inaonyesha kuna uwezekano mkubwa kwamba amekuwa akibadilisha itikadi zake za utunzi kila baada ya kipindi fulani. Watafiti wengi wa kazi za fasihi wameshughulikia maudhui na baadhi yao wameshughulikia swala la mtindo. Katika kazi zao, swala la itikadi za mtunzi linajitokeza pembezoni tu wala si kama swala nzito la kutafitiwa. Aidha, wachache waliojishughulisha na swala la itikadi kama Chuachua (2011), Swaleh, (2011) na wengineo hawajalishughulikia katika mpito wa wakati.

Marx na Engels (1977) wanasema kwamba, itikadi hujumuisha fikra zote na maoni ya wanadamu kuhusu wanayosema na wanayofikiria kuhusu siasa, sheria, maadili, dini na falsafa. Ni fikra zote ambazo hutokana na mtu kujidanganya na kutoweza kuona ukweli kikamilifu. Maoni haya hutokana na mfumo wa uchumi wa wakati maalum. Wanaeleza kwamba, itikadi ni fikra zote zinazotokana na hali ya uchumi na kwamba historia ya jamii zote ni historia ya mapambano ya kitabaka. Kwa maoni yao, jamii bila matabaka na utawala ndio yenye usawa na historia ya jamii yoyote husukumwa na nguvu za kiuchumi wa jamii na namna ya kujipatia riziki. Kadri mfumo wa uzalishaji mali unavyobadilika

ndivyo fasihi idhihirishavyo mabadiliko katika tanzu zote. Muundo mzima wa kijamii hubadilika kadri mfumo wa uzalishaji mali unavyobadilika. Mfumo huu na historia huelekeza hali zote za kijamii, kisiasa, kiuana na kadhalika.

Hegel (1977) anasema kwamba itikadi ni jumla ya fikra ambazo hujumuisha malengo, matarajio na matendo ya mtu. Ni mtazamo wa kiulimwengu wa mtu ambao humuongoza kutenda anayotenda. Fikra hizi kwa mujibu wa Hegel (1977) ni matokeo ya mabadiliko ya wakati na kubadilika kiroho hadi kufikia kiwango cha uhuru wa fikra. Kwa hivyo, kadri muda unavyosonga ndivyo mawazo na mitazamo ya mwanadamu hubadilika ili kuufikia au kuukaribia uungu au mawazo ya kupevuka kiroho na kupata uhuru wa fikra. Mwanadamu hupaswa kutumia mawazo au fikra zake kujaribu kuelewa jamii yake, utamaduni wake, sheria na maadili. Ni katika mapito ya wakati ndivyo imani zake na fikra zake hubadilika ili kuufikia uungu au ulimwengu wa kiroho.

Mhakiki wa Kifaransa, Althusser (1981) anaendeleza dhana ya itikadi na kusema kuwa ili kuendeleza itikadi ya utawala na udhibiti, vyombo viwili hutumiwa. Kuna vyombo ambavyo huendeleza utawala na udhibiti moja kwa moja kama vile serikali, utawala, jeshi, polisi, mahakama na magereza. Aidha, kuna vyombo ambavyo huendeleza itikadi za kiutawala na udhibiti kama vile vyombo vya habari, elimu, familia, kanisa, siasa na utamaduni. Vyombo hivi hufanya kazi kwa njia huru kiasi bila kuwa na lengo la moja kwa moja la kudhibiti na kutawala. Kwa hivyo mielekeo, mitazamo na fikra za watu huelekezwa na vyombo hivi ama kwa nguvu au kwa ukubalifu wao wenyewe hivyo ni

vigumu kwa watu wa kawaida kuendeleza itikadi yao wenyewe ya kuhusiana na hali zao na kuendeleza maslahi yao ya udhibiti na kudumisha hali ilivyo ya utawala. Kwa hivyo, kila mtu mwishowe huwa na itikadi ama za kutawala au kutawaliwa au kunyanyasa au kunyanyaswa ambazo huwezesha kutekeleza majukumu anayotekeleza katika jamii kwa wakati fulani.

Akifafanua dhana ya itikadi, mwanafalsafa wa Kiitaliano Gramsci (1985) anaeleza kuwa itikadi hupata nguvu kimsingi kutokana na kile anachokiita ukubalifu na ukawaida wala si matumizi ya nguvu. Ukawaida humaanisha kuwa watu huweza kupata fikra, mitazamo na mielekeo fulani kutokana na matendo na tabia waliozoea na kuzama akilini mwao. Kwa hivyo, wao huchukulia kwamba ni jambo la kawaida mambo kuwa namna yalivyo ilhali kiasilia, fikra, mitazamo na mielekeo hii ilitokana na tabaka tawala na huendeleza maslahi ya tabaka hilo tawala. Mitazamo hii hujitokeza kwa vigeu kama jinsia, rika, utamaduni, rangi na kadhalika ambapo watu huchukulia kwa mfano ni kawaida kwa jinsia ya kiume kuwa na mamlaka dhidi ya jinsia ya kike.

Kwa hivyo itikadi ni mikusanyiko ya imani, mielekeo, mitazamo na fikra zote ambazo humwongoza mwanadamu yeyote au kikundi cha watu kutenda au kutekeleza wanayofanya katika kipindi fulani cha wakati. Ni mawazo, mafunzo na malengo ya mtunzi yanayosawiri utekelezaji wa majukumu ya kidini, kisiasa, kiuchumi na kijamii kwa ujumla wake kwa mujibu wa Chuachua (2011: uk. 7). Ni jumla ya fikra, imani, mawazo na mielekeo inayomwelekeza msanii katika kuwasilisha ulimwengu wake kwa

jamii lengwa kupitia maudhui anayojadili, dhamira yake, wahusika aliochagua na namna anavyowasawiri na mtindo aliotumia.

Katika utafiti huu tulimwangazia S. A. Mohamed, mtunzi ambaye ameandika riwaya, tamthilia na ushairi kati ya makala mengine mengi. Tulizingatia riwaya alizoandika kwa kipindi cha muda wa zaidi ya miaka thelathini ili kubainisha itikadi zinazojitokeza katika vipindi tofauti. Itikadi hizi huenda zilichangiwa na mabadiliko ya mfumo wa uzalishaji mali kama Marx (1973) anavyodai ama fikra zake zinabadilika ili kuukaribia uroho kama Hegel (1977) anavyodai. Aidha, mtafiti alichunguza iwapo itikadi hizi zinabadilika kutokana na dhana ya ukubalifu na ukawaida kama Gramsci anavyodai au ni kutokana na vyombo vya utawala na udhibiti kama polisi na jeshi ama ni kuendelezwa na vyombo vya itikadi kama Althusser anavyosema. Ni katika mikabala hii ambayo utafiti huu ulilenga kutathmini itikadi katika riwaya teule za mtunzi S. A. Mohamed. Aidha, tuliangazia itikadi za mtunzi huyu kama zimebadilika kwa mapito ya wakati na kujidhihirisha vipi katika kazi zake za riwaya katika vipindi tofauti vya utunzi wake kwa upande wa maudhui na wahusika.

1.2 SWALA LA UTAFITI

Baadhi ya wahakiki wanapozungumzia mtazamo wa mwandishi kuhusu maisha na ulimwengu unaomzunguka hufikiria kwamba mtazamo huu ni tengemano, mmoja na haukumbwi na mitafaruku ya ndani kwa ndani. Ni kama mwandishi huongozwa na itikadi fulani kila mara. Itikadi huwa kama imani yake inayosawiri mtazamo wake

kuhusu maendeleo ya kijamii, kiuchumi na kiteknolojia. Utafiti huu uliainisha na kutathmini itikadi katika riwaya teule za S.A. Mohamed kwa vipindi tofauti kwa lengo la kubainisha kuwa kila baada ya kipindi fulani, mwandishi anabadilisha itikadi zake kwa kujihakiki mwenyewe ili kuhakikisha kwamba kazi zake zina ufaafu kwa jamii lengwa.

Kinyume na mtazamo wa Karl Max aliyesema kwamba itikadi ni ung'amuzi potoshi kila mara, itikadi ni dhana badilifu na nyumbufu kulingana na maendeleo ya jamii kiuchumi, kisiasa na kijamii. Jambo hili kadri tujuavyo halikuwa limefanyiwa utafiti katika riwaya za S.A. Mohamed. Katika uchanganuzi huu, mtafiti alitumia riwaya nne za S. A. Mohamed ambazo ni *Asali Chungu* (1978), *Kiza Katika Nuru* (1988), *Dunia Yao* (2006) na *Mhanga Nafsi Yangu* (2012). Mtafiti aliangazia maudhui na wahusika katika kila riwaya ili kubaini ikiwa itikadi zinazojitokeza zinabadilika katika mapito ya wakati kila baada ya kipindi fulani cha utunzi. Aidha, mtafiti alibaini ni kwa nini itikadi hizi zinabadilika katika nyakati tofauti na kuonyesha kuwa msimamo na mwelekeo wa mtunzi huyu si mmoja na tengemano. Jambo hili liliashiria kwamba dhima ya mtunzi ni changamano zaidi kuliko ilivyofikiriwa awali.

1.3 MASWALI YA UTAFITI

Utafiti huu ulilenga kuyajibu maswali yafuatayo:

- (a) Kuna uhusiano gani baina ya itikadi na mtazamo wa mwandishi kwa kurejelea riwaya za S. A. Mohamed?

- (b) Ni itikadi ipi inayojitokeza katika riwaya ya *Asali Chungu* na *Kiza Katika Nuru* kutokana na usawiri wa maudhui na wahusika.
- c) Itikadi inayojitokeza katika *Dunia Yao* na *Mhanga Nafsi Yangu* kwa mujibu wa maudhui na wahusika ni ipi na ama kuna mabadiliko yoyote?
- d) Mabadiliko yanayotokea yanadhihirisha vipi marekebisho na kujisahihisha katika mielekeo na mitazamo ya mtunzi na yanaashiria mabadiliko yepi kuhusu dhana ya itikadi?

1.4 MALENGO YA UTAFITI

Utafiti huu ulilenga malengo yafuatayo:

- (a) Kuonyesha uhusiano uliopo baina ya itikadi na mtazamo wa mwandishi S. A. Mohamed.
- (b) Kudhihirisha itikadi inayojitokeza katika riwaya ya *Asali Chungu* na *Kiza Katika Nuru* kutokana na usawiri wa maudhui na wahusika.
- (c) Kuchunguza itikadi inayojitokeza katika riwaya ya *Dunia Yao* na *Mhanga Nafsi Yangu* kwa mujibu wa maudhui, wahusika na mabadiliko yanayojitokeza.
- (d) Kuonyesha mabadiliko yanayojitokeza kwa upande wa usawiri wa maudhui na wahusika yanaakisi kujirekebisha na kujisahihisha na mtazamo kuhusu dhana ya itikadi.

1.5 SABABU ZA KUCHAGUA MADA

Katika utafiti huu, tuliteua riwaya nne za S. A. Mohamed ambazo ni *Asali Chungu* (1978), *Kiza Katika Nuru* (1988), *Dunia Yao* (2001) na *Mhanga Nafsi Yangu* (2012).

Kazi hizi ziliateuliwa kwa sababu mtunzi huyu ni maarufu katika uwanja wa fasihi ya Kiswahili na anaweza kuchukuliwa kama kielelezo cha waandishi waliokomaa katika lugha na fasihi ya Kiswahili (Mbatiah 1990:6). Aidha, ameandika vitabu vingi mno katika mawanda marefu kiwakati. Riwaya zake ziliateuliwa kwani ni katika utunzi wa riwaya ambapo S.A Mohamed amebobea sana kwa kutunga riwaya nyingi kwa kipindi kirefu zaidi na kujadili maswala mengi kwa kina zaidi (Mbatia 1996:13).

Riwaya nne tulizochagua ziliweza kutupa data ya kutosha ili kutosheleza mahitaji ya utafiti huu. Aidha, ni kazi ambazo zilitungwa katika vipindi tofauti vya utunzi wa mtunzi huyu na kwa vile tulitathmini itikadi katika vipindi hivyo tofauti, basi ni chaguo faafu kwa utafiti wetu. Nocera (2005) anasema kwamba riwaya ya S. A. Mohamed *Kiza Katika Nuru* (1988) imetafsiriwa katika lugha ya Kiitaliano na ni riwaya inayoonyesha mtunzi amepevuka kiutunzi. Kwa hivyo kazi zake zilifaa kuhakikiwa kwani zimepita mipaka ya kitaifa na kimataifa na zinashughulikia mawanda mapana sana.

Tulijikita katika riwaya za S. A. Mohamed kwani huyu ni mtunzi maarufu na kama Njogu (2001) anavyosema, kazi za S. A. Mohamed zinahitaji kusomwa na kuhakikiwa kwa undani zaidi ili kudhihirisha kama anabadilika kuanzia mwanzo wa utunzi wake hadi sasa. Aidha,riwaya ambazo tumeteua hazijahakikiwa sana katika tahakiki nyingi ambazo zimetolewa na kwa hivyo tutakuwa tumechangia sana uhakiki wa riwaya na fasihi ya Kiswahili kwa jumla.

Swala la itikadi ni muhimu kwani ndio huelekeza matendo na fikra zote za mwanadamu. Mofolou (1974) anasema kuwa itikadi ndio nguzo muhimu katika mabadiliko na mapinduzi yoyote katika jamii. Rossiland (1990) anasema kuwa itikadi ndio huwaongoza watu wote kuhusu siasa, dini, sheria na nyanja zote za maisha. Njogu (1997) anashadidia kauli hizi na kusesitiza kwamba itikadi ya mtunzi humuelekeza kuchagua yaliyo faafu kwa jamii yake ili ayaangazie katika kazi zake na kuepuka yale potovu. Kwa vile ambavyo itikadi ndio nguvu inayomsukuma mtunzi yeyote katika utunzi wake, ilikuwa ni muhimu sana kutathimini itikadi ya mtunzi maarufu kama S. A. Mohamed katika vipindi tofauti alivyoandika ili kuona ama itikadi yake inabadilika kadri ambavyo jamii inabadilika.

Mofolou (1974) anasema ya kwamba kila mapinduzi ambayo yamewahi kufanyika duniani kama vile Marekani, Urusi na Ufaransa yaliongozwa na itikadi fulani. Kwa hivyo itikadi ni muhimu kwa sababu ndio humuongoza mwanadamu kutenda matendo mazuri au mabaya. Ni nguvu ambayo husukuma vitendo na fikra zote katika jamii. Kwa hivyo ni dhana ya kimsingi ya kufanyiwa utafiti kwani ndio huelekeza jamii kutekeleza mabadiliko au kukaa na kusubiri majaliwa.

Ilikuwa dhahiri kwamba kadri tulivyofahamu hakukuwa na mhakiki yeyote wa fasihi ya Kiswahili ambaye alikuwa ameshughulikia swala la itikadi ya mtunzi Mohamed hasa katika mapito ya wakati na jinsi ambavyo itikadi hizo zimebadilika katika vipindi tofauti. Aidha, hakuna mhakiki wa fasihi ya Kiswahili ambaye alikuwa ameshughulikia dhana ya

itikadi kwa kuzingatia mikabala tofauti kama ya Antonio Gramsci na Louis Althusser. Ni imani yetu kuwa tulichangia katika uwanja wa uhakiki na uendelezaji wa fasihi ya Kiswahili kwa kuangazia mada hii muhimu na ya kimsingi katika maisha ya wanadamu na matendo yao katika jamii.

1.6 UPEO NA MIPAKA

Mtunzi S. A. Mohamed ameandika vitabu vingi vikiwemo rwaya, tamthilia, hadithi fupi na vinginevyo. Katika utafiti huu, tulijikita katika riwaya nne kati ya zile zilizoandikwa naye. Riwaya hizi zilitufaa na kutupa data ya kutosha kuangazia swala la itikadi katika kazi zake. Riwaya ambazo mtunzi huyu ameandika ni *Asali Chungu* (1978), *Utengano* (1980), *Dunia Mti Mkavu* (1980), *Kiza Katika Nuru* (1988), *Tata Za Asumini* (1990), *Babu Alipofufuka* (2001), *Dunia Yao* (2006), *Nyuso Za Mwanamke*, (2008), *Mhanga Nafsi Yangu* (2012), na *Mkamandume* (2013).

Riwaya ambazo tulichagua ziliwakilisha asilimia arobanne ya riwaya zake zote na kwa hivyo kilikuwa kiwakilishi mwafaka cha riwaya alizoandika kufikia sasa. Riwaya hizi nne ni *Asali Chungu* (1978), *Kiza Katika Nuru* (1988) *Dunia Yao* (2006) na *Mhanga Nafsi Yangu* (2012) ambazo ziliteuliwa kimaksudi ili kuwakilisha vipindi tofauti katika utunzi wa S. A. Mohamed. Mugenda na Mugenda (1999) wanasema kuwa uteuzi wa kimakusudi lazima uambatane na kategoria ambazo mtafiti atatumia katika uteuzi wake. Kategoria ambayo mtafiti alitumia ni ile ya vipindi tofauti vya utunzi wa S. A. Mohamed. Aidha, vipengele ambavyo mtafiti alizingatia katika kila riwaya ni maudhui na wahusika .

1.7 HITIMISHO

Katika sura hii mtafiti ameshughulikia usuli wa utafiti ambapo ameweka msingi wa utafiti huu kwa kueleza dhana ya itikadi na mikabala ya itikadi inayozingatiwa katika utafiti huu. Mikabala hiyo ni mkabala wa Karl Marx (1973) unaoelezea itikadi kama ung'amuzi potoshi, mkabala wa Louis Althusser (1981) unaoelezea itikadi huendelezwa na asasi za serikali kwa matumizi ya nguvu au vyombo vya kiitikadi na mkabala wa Antonio Gramsci (1985) unaoelezea itikadi kama dhana inayoletwa na ukubalifu na ukawaida. Swali la utafiti pia limeshughulikiwa katika sura hii. Swali hili ni kuchunguza itikadi zinazojitokeza katika riwaya za Mohamed S.A na kuona ikiwa zinabadilika katika kila katika kipindi tofauti cha kiutunzi kinyume na Karl Marx alivyosema kuwa itikadi ni ung'amuzi potoshi kila mara. Aidha, mtafiti ameonyesha maswali yanayoshughulikiwa katika utafiti huu ambayo ni uhusiano wa itikadi na mtazamo wa mwandishi na itikadi zinazojitokeza katika riwaya teule zilizoandikwa na Mohamed S.A ambazo ni *Asali Chungu*, *Kiza Katika Nuru*, *Dunia Yao* na *Mhanga Nafsi Yangu* na kuonyesha mabadiliko yanayotokea yanadhihirisha vipi marekebisha na kujisahihisha katika mielekeo na mitazamo ya mtunzi.

Malengo ya utafiti huu pia yameshughulikwa katika sura hii. Malengo haya ni kuonyesha uhusiano uliopo baina ya itikadi na mtazamo wa mwandishi na kudhihirisha itikadi zinazojitokeza katika riwaya teule za Mohamed S.A. Aidha, kuonyesha ama itikadi zinabadilika na ikiwa ni hivyo kudhihirisha kuwa Mohamed anajirekebisha na

kujisahihisha katika vipindi tofauti vya utunzi wake na hivyo itikadi ni dhana badilifu na nyumbufu. Hili lilimaanisha kuwa msimamo wa mtunzi si mmoja na tengemano kwani mtunzi huongozwa na itikadi fulani hivyo itikadi kama inabadilika basi pia msimamo wake unabadilika.

Sababu za kuchagua mada pia zimeshughulikiwa katika sura hii. Tumeeleza kuwa Mohamed ni mtunzi maarufu anayeweza kuchukuliwa kama kielelezo cha waandishi waliokomaa. Itikadi pia ni dhana muhimu ikichukuliwa kuwa matendo yote ya binadamu ulimwenguni huongozwa na itikadi fulani na kadri ya ufahamu wetu hakuna mhakiki ambaye amehakiki dhana ya itikadi katika kazi za fasihi hasa kwa kuzingatia mikabala mbalimbali na vipindi tofauti vya utunzi.

Mwisho mtafiti ameshughulikia upeo na mipaka ambapo mtafiti anashughulikia riwaya nne teule za S. A. Mohamed ambazo ni *Asali Chungu*, *Kiza Katika Nuru*, *Dunia Yao* na *Mhanga Nafsi Yangu*. Pia ameshughulikia itikadi zinazojitokeza kwa kuzingatia mikabala mitatu pekee; ule unaoendelezwa na Karl Marx kuhusu ung'amuzi potoshi, ule unaoendelezwa na Louis Althusser kuhusu itikadi na vyombo vya utawala na vya kiitikadi na mkabala wa Antonio Gramsci unaohusu ukubalifu na ukawaida.

SURA YA PILI

2.0 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA

2.1 UTANGULIZI

Katika sura iliyopita, mtafiti ameshughulikia usuli wa utafiti, maswali ya utafiti, malengo ya utafiti, swala la utafiti, sababu za kuchagua mada na upeo na mipaka. Katika sura hii mtafiti anashughulikia yaliyoandikwa kuhusu mada hii ili kupata mwanga zaidi kuhusu utafiti huu.

Kuna wahakiki wengi ambao wameshughulikia utanzu wa riwaya katika tahakiki zao. Kuna wale walioshughulikia itikadi katika kazi za S. A. Mohamed vile Kamunde (1983), Sirucha (1986), Njogu (1987), Mbatiah (1990), Muindi (1990), Osore (2008), Swaleh (2011) miongoni mwa wengine. Kuna walioshughulikia itikadi katika riwaya kwa ujumla wake kama Lugano (1989), Mbatiah (1999), Vonyoli (2004), Musembi (2008), ChuaChua (2011) na Sanja (2012).

2.1.1 YALIYOANDIKWA KUHUSU ITIKADI KATIKA KAZI ZA S. A.

MOHAMED

Kamunde (1983) amejadili namna wahusika walivyotumiwa kujenga maudhui ya kilio cha wanyonge. Ameonyesha namna ambavyo S. A. Mohamed ametumia wahusika wanyonge ambao wananyanyaswa kuendeleza maudhui ya kilio cha wanyonge. Amehakiki riwaya ya *Utengano* (1980), *Asali Chungu* (1978) na *Dunia Mti Mkavu* (1980). Amelenga kueleza wahusika mbalimbali wanavyodhihirisha unyonge wao. Anasema kwamba S. A. Mohamed ameeleza kwa uwazi kuhusu mifumo itumiwayo

kuwadhalilisha wanyonge ambayo ni siasa, uchumi na maswala ya jamii. Anaibua swala la itikadi ya kijamaa kwa ujumla tu, ambapo anasema wanyonge hudhalilishwa kwa sababu za kitabaka. Anaonyesha kuwa katika jamii iliyogawika kitabaka lazima iendelee kukumbwa na mitafaruku wanyonge wakitafuta haki. Utafiti huu ni tofauti na wetu kwani sisi tuliangazia itikadi ya mwandishi kwa undani kwa kutumia riwaya teule kuwakilisha vipindi tofauti maalum. Aidha, tuliangazia vipengele viwili yaani maudhui na wahusika na kubaini mabadiliko ya itikadi za mtunzi katika vipindi tofauti. Pale alipotumia mkabala mmoja wa itikadi, mtafiti alitumia mikabala tofauti ya itikadi katika utafiti huu.

Sirucha (1986) aliangazia hadhi na hali ya mwanamke katika riwaya za S. A. Mohamed; *Asali Chungu* (1978), *Utengano* (1980) na *Dunia Mti Mkavu* (1980). Anaonyesha kuwa itikadi za kijamii, kiuchumi na kisiasa zinatumiwa kumdunisha mwanamke. Anasema kwamba itikadi na utamaduni ni taasisi ambazo zinatumiwa kuwapumbaza wanawake ilhali itikadi ya kuumeni inamfanya mwanamume kuwa kitu cha thamani. Utafiti huu utatufaa kuelewa baadhi ya kazi za S. A. Mohamed. Hata hivyo Sirucha (1986) habainishi kinagaubaga ni itikadi zipi za kiuchumi na kijamii au utamaduni zinazomtatiza mwanamke na hashughulikii mabadiliko ya itikadi za mtunzi katika mapito ya wakati. Aidha, kazi alizoshughulikia ni za kipindi kimoja. Utafiti wetu ulijihusisha na kuangazia itikadi maalum za mtunzi kwa kipindi kirefu cha zaidi ya miaka thelathini na kuangazia namna zilivyobadilika katika mapito ya wakati.

Njogu (1987) ameshughulikia maudhui ya mapinduzi katika riwaya za visiwani Zanzibar. Anaonyesha vile maudhui haya yanavyojitokeza katika kazi za watunzi watatu; Mohamed S. Mohamed, S. A. Mohamed na Shafi A. Shafi kwa kuzingatia mtazamo wa ki-Marx. Tahakiki yake ilitufaa katika kuelewa baadhi ya mitazamo ya u-marx na kutoa mwanga kuhusu S. A. Mohamed na kazi zake za awali alizochunguza. Utafiti huu ni tofauti na wetu kwani pale ambapo ameangazia maudhui, sisi tuliangazia itikadi ya mtunzi katika kipindi kirefu cha wakati, zaidi ya miaka thelathini.

Mbatiah (1990) alishughulikia dhana ya kukua kwa mwandishi katika riwaya ya Kiswahili kwa ujumla wake. Aliangazia riwaya nne za S. A. Mohamed ambazo ni *Asali Chungu* (1977), *Utengano* (1980), *Dunia Mti Mkavu* (1980) na *Kiza Katika Nuru* (1988). Aliangazia pia riwaya za Shaaban Robert ambazo ni *Utubora Mkulima* (1967) na *Siku ya Watenzi Wote* (1968). Alilenga kubainisha na kujadili kwa ujumla vipengele vya ukuaji wa muundo, ploti na wahusika kama wameboresha kazi zao za baadaye. Aliona kwamba waandishi hawa wamepevuka na S. A. Mohamed amejirudia sana katika itikadi zake za kijamaa. Anadhihirisha kwamba Shaaban Robert alitatizwa sana katika ukuaji wake na itikadi zake za kidini na kuathiriwa sana na Uislamu katika mawazo yake. Naye S. A. Mohamed aliathiriwa sana na itikadi zake za kijamaa kwani amewachora wahusika wake kitabaka na wanaweza kuaminika. Utafiti huu ulitupa mwanga kuelewa mazingira ambamo S. A. Mohamed aliandikia baadhi ya kazi zake na kuelewa jinsi alivyopiga hatua katika utunzi wake. Aidha, utafiti huu ulitonyesha namna itikadi za mtunzi zinaweza kuathiri kazi zake na kuelekeza namna anavyosawiri wahusika wake, maudhui na mtindo

wake wa utunzi. Hata hivyo, utafiti huu ni tofauti kwa vile sisi tuliangazia itikadi za mtunzi ilhali huyu alizingatia fani zaidi. Aidha, pale ambapo anaangazia watunzi wawili kuona nani aliyepiga hatua zaidi ya mwingine sisi tulijikita katika kazi za S. A. Mohamed pekee na kuangazia riwaya nne za vipindi tofauti. Aidha, pale ambapo anatumia nadharia ya u-marx pekee, sisi tuliongozwa na nadharia changamano kwa kutumia misingi ya nadharia za udenguzi na kimaadili.

Usawiri wa wahusika makahaba katika riwaya nne za S. A. Mohamed umeangaziwa na Muindi (1990). Riwaya ambazo amechunguza ni *Asali Chungu* (1977), *Utengano* (1980), *Dunia Mti Mkavu* (1980) na *Kiza Katika Nuru* (1988). Ameonyesha jinsi ambavyo mwanamke amesawiriwa katika riwaya hizo. Utafiti huu ulitusaidia katika kuelewa baadhi ya kazi za S. A. Mohamed. Anaeleza kuwa itikadi za kuumeni zinamuinua mwanamume na kumdhalilisha mwanamke na huchangia pakubwa wanawake wengi kuingilia ukahaba. Jambo hili hutokana na hali duni ya kiuchumi na utamaduni ambapo mwanamke huitwa kahaba na mwanamme kuonekana kama hajafanya jambo lisilostahili. Lakini tofauti na utafiti wetu, yeye ameangazia kipengele cha wahusika wanawake, sisi tumeshughulikia vipengele vya maudhui na wahusika huku tukionyesha itikadi ya mtunzi katika kila kipindi na jinsi alivyobadilisha itikadi zake katika juhudi za kuifaa jamii yake katika mapito ya wakati kuanzia mwanzo wa utunzi wake hadi sasa.

Kwa kurejelea kazi za waandishi wawili, Osore (2008) amejadili matumizi ya mbinu za ostononiya ambayo huleta upya katika kazi ya kifasihi. Amechanganua kazi za S. A.

Mohamed ambazo ni *Utengano* (1980), *Dunia Mti Mkavu* (1980), *Asali Chungu* (1978), *Kiza Katika Nuru* (1988) na *Babu Alipofufuka* (2001). Vilevile ameangazia kazi za Euphrase Kezilahabi ambazo ni *Rosa Mistika* (1971), *Kichwa Maji* (1974) na *Gamba la Nyoka* (1978). Ameangazia mbinu kama usambamba, kejeli, tashbihi, taswira na nyinginezo na kuonyesha namna ambavyo watunzi hawa wamefaragua mbinu zao za utunzi ili kuzipa kazi zao ladha na upya ili ziendeleo kuwa faafu kwa jamii lengwa.

Anaonyesha kwamba watunzi hawa wamebadilisha mbinu zao za utunzi kuambatana na mabadiliko ya itikadi zao. Ikizingatiwa kwamba itikadi huathiri mawazo na namna mtunzi anavyoivasilisha kazi yake, ni muhimu kufanya uchunguzi wa kina kubaini itikadi maalum zinazopelekea S. A. Mohamed kubadilisha mbinu zake za utunzi na mtindo wa kazi zake katika mapito ya wakati. Osore ameongozwa na nadharia ya uchanganuzi wa matini katika utafiti wake. Utafiti wake huu umetufaa katika kuelewa mbinu ambazo mtunzi S. A. Mohamed ametumia katika riwaya zake. Hata hivyo, utafiti wake ni tofauti na wetu kwani pale ambapo yeye anazingatia mbinu za utunzi sisi tumezingatia itikadi za mtunzi na jinsi zinavyobadilika katika vipindi tofauti vya utunzi wake. Utafiti wetu umejikita katika vipengele tofauti kama vile maudhui na wahusika kinyume na utafiti wa Osore unaoangazia mbinu za utunzi. Pale ambapo utafiti huu unashughulikia watunzi wawili sisi tumeshughulikia mtunzi mmoja S. A. Mohamed. Aidha, kazi za S. A. Mohamed ambazo tumeshughulikia ni kuanzia mwanzo wa utunzi wake hadi sasa huku tukiangazia vipindi maalum vya utunzi wake. Licha ya hayo,

nadharia tulizotumia ni mbili, ile ya udenguzi na ya kimaadili ilhali katika utafiti wa Osore umetumia nadharia moja tu, ile ya uchanganuzi wa matini.

Yanayodhihirika ni kwamba hakuna mtafiti yeyote kadri ya ufahamu wetu ambaye alikuwa amefanya utafiti kuhusu itikadi katika riwaya za Said Ahmed Mohamed wala kushughulikia dhana ya itikadi katika mikabala tofauti katika mapito ya wakati jambo ambalo mtafiti alilishughulikia kwa kina.

2.1.2 YALIYOANDIKWA KUHUSU ITIKADI KATIKA RIWAYA YA KISWAHILI

Katika sehemu iliyotangulia, tumeangazia namna watafiti mbalimbali walivyoshughulikia itikadi katika kazi za S. A Mohamed. Baadhi yao wamelinganisha kazi za S. A. Mohamed na za waandishi wengine. Katika sehemu hii tumeeleza namna watafiti mbalimbali walivyoangazia itikadi katika riwaya ya Kiswahili kwa jumla.

Lugano (1989) amehakiki jinsi Kezilahabi anavyowasawiri wahusika wa kike kwa kutumia vigezo vya uchumi, jamii na siasa. Aliona kwamba mwanamke amechorwa kama kiumbe duni, kifaa tu cha kuuzima uchu wa mwanamme. Itikadi za kuumeni na utamaduni zinachangia zaidi hali hii na sharti zibadilishwe. Utafiti wake ulitufaa kuelewa itikadi kama vile inavyojitokeza katika kazi za watunzi wengine na jinsi inavyowaathiri wahusika katika kazi zao.

Mbatiah (1999) ameangazia riwaya tasnifu ya Kiswahili chanzo chake na maendeleo yake. Aliangazia watunzi Shaaban Robert, Euphrase Kezilahabi, Mohamed Suleiman Mohamed na Shafi Adam Shafi. Ameonyesha kwamba watunzi wa Tanzania bara kama Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi wameshughulikia maudhui ya utaifa, uhuru, mkataba wa Arusha na ujamaa. Nao watunzi wa Zanzibar kama Mohamed Suleiman Mohamed, Shafi Adam Shafi wameshughulikia maudhui ya umwinyi, ukoloni na ukombozi wa Zanzibar. Anasema kuwa watunzi wa Zanzibar wameathirika sana na historia yao hivi kwamba kazi zao zimeisawiri zaidi. Katika utafiti wake aliangazia kazi za S. A. Mohamed kwa kiwango kidogo hasa upande wa maudhui na uhusiano wake na hali halisi ya kijamii. Anaonyesha namna ambavyo itikadi ya kibepari na kiislamu zinatumika kuwakandamiza wanyonge. Hali hii husababisha wanyonge kukaidi na kutekeleza mapinduzi. Anamaliza kwa kutoa kauli kuwa riwaya ya Kiswahili imepiga hatua kubwa sana na kuwa katika kiwango kimoja na riwaya nyinginezo ulimwenguni.

Utafiti huu ulitufaa kuelewa historia ya riwaya tasnifu ya Kiswahili na hali ya kihistoria ya Tanzania bara na Zanzibar iliyokuza kazi hizi. Hata hivyo, utafiti wetu ulijikita zaidi katika itikadi za mtunzi S. A. Mohamed ambaye Mbatiah anampa nafasi ya pembezoni. Aidha, tuliangazia itikadi hizi na namna zilizvojitokeza katika kazi zake teule mpaka sasa, jambo ambalo Mbatiah (1999) hakulishughulikia.

Tafiti za Vonyoli (2004) na Musembi (2008) zimechunguza riwaya mbili za Katama Mkangi. Vonyoli amejadili riwaya za *Mafuta* (1984) na *Walenisi* (1995). Ameangalia

namna hadithi inavyotumiwa na waandishi kama chombo cha maudhui. Amechanganua maudhui yaliyomo kwenye hadithi hizo na kuonyesha namna hadithi za jadi zimetumiwa na Mkangi kutoa maudhui ya kisasa. Maudhui hayo yanachangiwa zaidi na itikadi za kisiasa, kiuchumi na kijamii. Anasema kuwa itikadi za kuumeni, kibepari na utamaduni ziliathiri zaidi maudhui katika kazi za kisasa. Utafiti huu unatufaa katika kuangazia itikadi za jadi ambazo huenda zimemwathiri S. A. Mohamed katika kazi zake. Utafiti wake ni tofauti na wetu kwani anajikita tu katika kipengele cha maudhui ilhali sisi tumeshughulikia vipengele vya maudhui na wahusika ili kuonyesha itikadi za mtunzi na mabadiliko yake. Aidha, tumetumia nadharia za udenguzi na kimaadili ilhali yeye alitumia nadharia ya uhalisia wa kijamaa.

Naye Musembi (keshatajwa) amezungumzia dhana ya taswira na ukinzano kama kichocheo cha zinduko katika riwaya zile zile alizochunguza Vonyoli ambazo ni *Mafuta* (1984) na *Walenisi* (1995). Kwa kutumia nadharia ya uyakini wa kijamaa na nadharia ya kimtindo amechanganua taswira za kuonekana na za hisi alizotumia Mkangi ili kubainisha maudhui ya kisiasa, kiuchumi na kijamii yaliyojikita katika taswira hizo. Utafiti huu ni tofauti na wetu kwani sisi tumeangazia vipengele mbalimbali kama vile maudhui, mtindo na wahusika katika kubainisha itikadi za mtunzi katika vipindi tofauti maalum ilhali yeye anashughulikia taswira pekee. Aidha, ameshughulikia riwaya za Katama Mkangi ilhali sisi tulishughulikia riwaya teule za S. A. Mohamed. Yeye anumia nadharia ya kimtindo huku sisi tukitumia nadharia za udenguzi na kimaadili.

Swaleh (2011) anashughulikia uhakiki wa jinsi ambavyo jinsia ya kike imesawiriwa na kuchorwa katika riwaya ya Kiswahili. Anarejelea riwaya nne: *Rosa Mistika* ya Kezilahabi (1971), *Mwisho wa Kosa* ya Burhani (1987), *Nguvu ya Sala* ya Wamitila (1999) na *Tumaini* iliyoandikwa na Momanyi (2006). Ameangazia namna muundo na mtindo huchangia kusawiri maudhui ya jinsia. Akapata kwamba jinsia ni swala la kijamii na husawiriwa tofauti kulingana na jamii lengwa ya kazi hizo. Katika utafiti wake, itikadi ya kuumeni inaonekana kutumika kumkandamiza mwanamke na kumwinua mwanamme. Ili kujikomboa jinsia ya kike lazima ibadilishe itikadi hii kwa kuupinga mfumo wa itikadi za kuumeni. Namna ambavyo jinsia itasawiriwa hutegemea zaidi mtunzi atakavyoipanga kazi yake, atakavyoiwasilisha kulingana na athari za utamaduni, siasa na kiuchumi.

Ameonyesha namna itikadi ya mtunzi humuongoza katika usawiri wake wa wahusika, muundo na mtindo wa kazi yake, maudhui yake na falsafa yake kwa jumla. Utafiti huu ulitufaa hasa kwa kutufafanulia umuhimu wa itikadi na athari zake kwa mtunzi wa jamii. Hata hivyo, hajaangazia itikadi na mikabala yake tofauti kama mada maalum na namna itikadi ya mtunzi hubadilika katika mapito ya wakati. Aidha, hajaonyesha uhusiano uliopo baina ya itikadi za mtunzi na kazi zake kwa kipindi kirefu, jambo ambalo lilifanywa kwa kina katika utafiti huu.

Chuachua (2011) ameshughulikia swala la itikadi katika riwaya za Shaaban Robert. Anaonyesha kuwa Shaaban Robert amezingatia itikadi ya ujamaa uliopea kupitia mambo kama umoja na ushirikiano, mapinduzi ya kilimo, mapinduzi ya kisoshalisti na mikinzano

ya kitabaka. Anasema kuwa Shaaban Robert aliathiriwa na uandishi wa wakati wa ukoloni, harakati za ukombozi, migogoro kati ya Ulaya Magharibi na Mashariki, dini ya kiislamu na uchumi wa Tanzania. Anaeleza kuhusu kiu ya ulimwengu, utetezi wa mwanamke, kuwapo kwa matabaka na njia ya maadili, swala la mapinduzi, ugumu wa kufanya mapinduzi, udhaifu wa wanadini, usafi wa roho na ulazima wa kutafuta ukweli.

Utafiti huu ni muhimu kwani umetupa mwanga kuhusu dhana ya itikadi na athari yake kwa mtunzi huyu. Hata hivyo Chuachua haonyeshi mabadiliko ya itikadi za Shaaban Robert katika mapito ya wakati. Kwake, itikadi ya ujamaa uliopea anayopendekeza Shaaban Robert ni moja na tengemano kuanzia mwanzo hadi mwisho wa utunzi wake. Utafiti wetu uliangazia S. A. Mohamed na namna itikadi yake inabadilika katika mapito ya wakati kwani itikadi ni dhana badilifu na nyumbufu si moja na tengemano yaani kadiri jamii inavyobadilika ndivyo itikadi za mtunzi hubadilika. Aidha, Shaaban Robert ni mtunzi wa zamani ilhali S. A. Mohamed alianza kutunga zamani na mpaka sasa kwa hivyo ilikuwa ni muhimu kuchunguza itikadi zake katika mapito ya wakati na katika mikabala tofauti.

Sanja (2012) ameshughulikia maudhui ya ndoa na dini katika riwaya za *Kala Tufaha* na *Paradiso*. Anaonyesha kuwa kuna itikadi ya kidini ya kusadiki na kuheshimu mamlaka kama yalivyo bila kujali matakwa ya Mola. Anasema dini haina uwezo wa kudunisha ndoa bali itikadi za kidini huzua udikteta na kuhalalisha ubaguzi wa kijinsia katika ndoa. Kazi yake ilitufaa katika kuangazia namna mtunzi S. A. Mohamed ameathiriwa na itikadi

ya dini hasa katika usawiri wake wa ndoa na jinsia katika kazi zake. Kazi yake ni tofauti na yetu kwani sisi tulishughulikia swala la itikadi na ubadilifu wake katika mapito ya wakati.

Tahakiki hizi zote zinashughulikia itikadi kama dhana ya pembezoni wala si mada kuu na pale ambapo ni mada haikuwa imeshughulikiwa katika mapito ya wakati wala kuonyesha itikadi katika mikabala tofauti. Aidha, tahakiki hizi zote kadri ya ufahamu wa mtafiti zilikuwa zimeshughulikia maudhui katika riwaya na maelezo ya itikadi katika nyanja ya dini na siasa na kwa mtazamo wa ki-Marx pekee; itikadi kama ung'amuzi potoshi kila mara. Tofauti na tafiti hizi, utafiti wetu uliangazia itikadi ya mtunzi na jinsi inavyobadilika katika mapito ya wakati ili aweze kutimiza malengo, matumaini na matamania ya jamii yake katika vipindi tofauti vya utunzi wake. Mtafiti pia aliangazia dhana ya itikadi inavyojitokeza katika mikabala tofauti hasa mikabala inayoendelezwa na Antonio Gramsci na Louis Althusser. Aidha, mtafiti aliangazia ikiwa katika kubadilisha itikadi yake, mtunzi S. A. Mohamed ameishia kupinga mtazamo wake wa awali na kwa hivyo kazi ya fasihi hujidengua yenyewe kwa mujibu wa mtazamo wa nadharia ya udenguzi.

2.2 MISINGI YA NADHARIA

Utafiti huu uliongozwa na nadharia mbili: ile ya udenguzi na ile ya kimaadili. Nadharia hizi zilitufaa kutekeleza malengo ya utafiti huu vyema. Malengo haya yalikuwa ni kuonyesha uhusiano uliopo baina ya itikadi na mtazamo wa mwandishi, kudhihirisha

itikadi inayojitokeza katika riwaya za *Asali Chungu* na *Kiza Katika Nuru* kutokana na usawiri wa maudhui na wahusika. Pia kuchunguza itikadi inayojitokeza katika riwaya za *Dunia Yao* na *Mhanga Nafsi Yangu* kwa mujibu wa maudhui na wahusika. Vilevile kuchunguza iwapo kazi hizi zinaakisi kujirekebisha na kujisahihisha katika mitazamo na mielekeo ya mtunzi na kwa nini. Nadharia ya kimaadili iliweza kufaa utafiti huu kwa kuangazia kwa nini mtunzi anabadilika na labda ni katika kujaribu kuifaa jamii yake ili kazi zake ziwe faafu kwa jamii katika vipindi tofauti.

2.2.1 NADHARIA YA UDENGUZI

Nadharia ya udenguzi iliasisiwa mnamo miaka ya 1960. Ni nadharia ya baada ya muundo, lengo likiwa kupinga mitazamo ya lugha iliyokuwepo katika karne ya ishirini katika nchi za Kimagharibi. Ilianza huko Ufaransa na Jaques Derrida na kuchangiwa na wengine kama Foucault, Roland Barthes, Jean Baudrillard, Paul de Man, J. Hillis Miller, Jacques Lacan na Barbara Johnston. Udenguzi huona maana za lugha kama zilizomo ndani ya lugha yenyewe wala si mfumo wa kufungamanisha maneno na ukweli. Kwa wanaudenguzi lugha ni msimbo ulio na maana zinazojipinga na kujibomoa na zile maana nje ya msimbo huo yaani ni msimbo unaojifafanua.

Derrida (1976) anasema kwamba udenguzi hujaribu kuchambua matini kwa kuingilia maana zake mbalimbali kwa lengo la kubainisha vile maana hizo zinajijengua kiwango cha kujipinga zenyewe. Kwa hivyo ikiwa maana hizi zinajijengua zenyewe na kufikia kiwango cha kujipinga basi kazi ya fasihi imejivunja yenyewe. Aidha, kila usomaji wa kazi ya sanaa ni toleo jipya la kazi hiyo kwani maana mpya hujitokeza ambayo huenda

ikapingana na ile ya awali. Kwa mujibu wa Derrida kila kielekezi huelekezwa na kingine na kuendelea kuelekezana bila kikomo. Hii inamaanisha kwamba hakuna vielekezi wala wala vielekezwa asilia katika matini kwani ni vielekezi vya vielekezwa, jambo ambalo linaleta dhana kuwa hakuna matini asilia wala ile ya mwisho. Aidha, Derrida anasema kuwa kila matini huwa na maana nyingi na usomaji wowote wa matini lazima uzingatie jambo hili.

Inavyobainika ni kwamba, kuna uwezekano wa maana nyingi kujitokeza katika matini moja na kwa hivyo maana ni telezi na kila usomaji huenda ukaibua maana tofauti hata ambazo zinapingana. Kwa ujumla wake Derrida anasema kuwa maneno na matini huwa na maana nyingi ambayo huenda tayari imejidengua pindi neno hilo linapotamkwa au kuandikwa. Pia, maana ya maneno ni telezi kwa sababu maana hizo huendelea kucheleweshwa, hakuna maana asilia ya neno ambayo inaweza kurejelewa na hakuna kitu asili na kizima hivyo hakuna matini asilia ambayo haina utata.

Mtaalam mwingine ambaye ametoa mitazamo yake kuhusu udenguzi ni Barthes (1977). Anasema kuwa mwandishi anapoandika kazi yake ya kifasihi jukumu lake huishia pale. Alipomaliza utunzi wake uhai wa kazi yake hujitenga na mtunzi. Tahakiki zote zinazofuata haziathiriki na mtunzi kwa vyovyote vile. Ni jukumu la mhakiki kusoma kazi hizo ili atoe fasili yake kwa kufuata mantiki na muktadha wa jamii yake na welewa wake. Ijapokuwa mtafiti anakubaliana na Barthes kwamba kazi ya fasihi ina maana nyingi, hakubaliani naye asilani kwamba mwandishi hufa mara tu anapokamilisha kutunga kazi

yake. Udenguzi unaweza kutokana na maneno na mazingira ya mwandishi. Inavyobainika ni kwamba kuna uwezekano wa fasili nyingi kutolewa kwa kazi moja hivi kwamba uhakiki wa kidenguzi wa kazi moja unaweza kuendelea kutoa fasiri tofauti za jambo moja baadhi yazo zinazopingana maadamu wana ushahidi wa kutosha (Wafula na Njogu, 2007)

Barthes (1977) anasema kwamba mwandishi na kazi yake hawana uhusiano na hivyo si muhimu kuuzingatia muktadha wake wa kihistoria, kijiografia, kijamii, kidini, kabila na kadhalika. Aidha maana za kazi hizo huwa katika maandishi ya kazi hiyo na kila matini huwa na maana nyingi. Msimamo wa mtafiti ni kuwa muktadha wa mtunzi ni muhimu zaidi katika uelewaji na ufasiri wa kazi hizo kwani mtunzi hawezi akajitenga na jamii anayoiandikia na akifanya hivyo kazi yake ya kisanaa itakuwa potovu.

Njogu na Chimerah (1999) wanasema udenguzi hushughulikia vile lugha na maana zinavyoingiliana na kufanya kazi pamoja na kwa hivyo ni juhudi za kufikia nguvu na uwezo wa matini kama chombo kilichojifafanua. Lugha kama ishara ina uwezo wa kujifafanua tunapoitazama kwa undani na kwa hivyo maandishi ni muhimu kuliko usemi. Maana za maneno katika fasihi huwa katika kiashiria na kiashiriwa na kila maana ya neno huelezwa kutumia neno lingine au maneno huwa na maana nyingi ambazo hufafanuliwa na maneno mengine ambayo yanapofafanuliwa huzua maana nyingine zaidi na zaidi. Ikiwa kiashiria kimoja kinaweza kuzua viashiria vingi hivyo huzua vingine vingi basi lugha ni kama mnyororo wa viashiria. Ni muhimu kuelewa kuwa Derrida

alikuwa mwanamuundo lakini baadaye aliupinga mtazamo wa kimuundo kwamba lugha ni mfumo na kama kioo cha ulimwengu kihalisia. Aliendelea kusema kwamba maana za maneno huendelea kucheleweshwa na ni vigumu kufikia maana mahususi ya neno kwani maana zake daima huhamishwa.

Kwa hivyo hamna maana asili ya neno ambalo tunaweza kurejelea kueleza maana fulani yaani maana ni kitu cha mpito, mara imo mara haimo. Kusoma matini ya kifasihi ni kutafuta maana isiyoshikika kwani ni telezi na ni kitu cha mpito. Hii inaibua uwezekano wa kuibua maana nyingi kwani hakuna neno la mwisho katika uwelewaji. Anafafanua kwamba kila sentensi huelekezwa na sentensi nyingine na kila matini huelekezwa na matini nyingine. Kwa hivyo maana ni tokeo la ishara kujipambanua na ishara nyingine. Kwa ujumla mihimili ya nadharia ya udenguzi inaweza kuelezwa ifuatavyo:

- (a) Maana za matini katika lugha ni nyingi kwa kufuata utaratibu wa umuundo wa kiashiria na kiashiriwa hivyo matini zozote huwa na uwezekano wa kuwa na maana nyingi.
- (b) Maana za matini huahirishwa na hivyo maneno na dhana hazina maana thabiti hivyo ni telezi.
- (c) Uainishaji wa dhana zote kiulimwengu kwa kuzingatia uwili, mke/mume, kizuri/kibaya, kilicho hai/kisicho hai kwa hivyo dhana zinazokinzana zinakaribiana kimaana.

- (d) Maana za lugha si thabiti, huelea juu ya maneno, maneno na matini hujenguana na kupingana zenyewe na hivyo matini huwa na mielekeo mingi ya maana hivyo kuibua fasili nyingi.
- (e) Maana haipatikani katika ishara moja pekee lakini huwa katika hali ya kuwepo na kutokuwepo, mara imo mara haimo.

Nadharia ya udenguzi ilifaa utafiti huu kwa kufuata mihimili ifuatayo. Mhimili unaosema kuwa kuna uwezekano kuwa na fasili mbalimbali ulitusaidia katika kufasiri dhana ya itikadi na kazi za fasihi kwa njia nyingi na kutoa maana tofauti kuliko ile iliyojulikana hapo awali. Mhimili huu ulitumiwa kuangazia fasili mbalimbali zinazowakilishwa na itikadi za S. A. Mohamed katika riwaya za *Asali Chungu* (1978), *Kiza Katika Nuru* (1988), *Dunia Yao* (2006) na *Mhanga Nafsi Yangu* (2012). Tuliweza kuibuka na fasili tofauti kabisa na zile zilizotolewa na wahakiki wengine hapo awali.

Mhimili wa pili unaosema kwamba maana za maneno huahirishwa ulifaa utafiti huu kwa kuonyesha namna ambavyo dhana ya itikadi inavyohamishwa. Katika vipindi tofauti vya utunzi, S. A. Mohamed anabadilisha itikadi zake au misimamo yake na hivyo maana ya neno si thabiti; ni telezi, mara imo mara haimo. Aidha, ilidhihirishwa kwamba itikadi ni dhana badilifu; hubadilika kulingana na hali ilivyo katika vipindi tofauti.

Mhimili ule unaoelezea kwamba baadhi za maana katika matini huweza kupingana ulitumika kuonyesha jinsi ambavyo itikadi na msimamo wa S. A. Mohamed umebadilika

katika vipindi tofauti vya utunzi wake. Vile anavyozidi kubadilika na kujirekebisha kimaudhui na kimtindo katika kazi zake ndivyo anavyojijengua na hivyo msimamo wake hauwezi kutengemaa. Hivi ni kusema kuwa misimamo yake kuhusu siasa, dini, mfumo wa uzalishaji mali, maswala ya kijinsia na mingineyo inabadilika kulingana na mabadiliko ya vigeu vingine.

Nadharia ya udenguzi ina upungufu wa kutilia mkazo zaidi matini na maneno na kutozingatia muktadha na historia ya mtunzi na jamii lengwa katika kazi za fasihi. Barthes (1977) anadai kwamba mtunzi anapoandika kazi yake, wajibu wake huishia pale na kwa hivyo si muhimu kuzingatia muktadha wake wa kihistoria, kidini, kikabila na kijamii kwa ujumla. Maandishi tu ndio muhimu na kama Njogu na Chimera (1999) wanavyosema udenguzi ni uhakiki unaojikita katika kuzingatia matini kama chombo kinachojitosheleza na kinachoweza kufichua maana bila kurejelea muktadha. Sifa kubwa ya udenguzi ni uzingatifu wa lugha na matini.

Ni imani ya mtafiti kuwa maana toshelevu ya matini haiwezi kuwepo bila kuzingatia muktadha wa mtunzi ama mazingira ambamo alitungia kwani binadamu ni zao la jamii na huathiriwa na mazingira na muktadha wake tangu utotoni kupitia elimu, vyombo vya habari, mifumo ya uzalishaji mali, dini na kadhalika. Kwa vile utafiti wetu unahusu tathmini ya itikadi ya mtunzi ambayo hujumuisha mkusanyiko wa imani ya kikundi cha watu, mtu binafsi au jamii nzima, ni muhimu kuzingatia mihimili ya nadharia ya kimaadili ili kufidia upungufu wa nadharia ya udenguzi.

2.2.2 NADHARIA YA KIMAADILI

Nadharia ya kimaadili imeendelezwa na wanafalsafa kama Plato, Aristotle, Socrates, Kanti, Sairini na wengineo. Nadharia hii inahusu maadili ya jamii kama uzuri, fadhili na wema. Watu wanapaswa kutekeleza wajibu wao kutegemea mahitaji ya jamii yao. Lengo kuu ni kuishi maisha yenye fadhila yanayowiana na viumbe wengine na kwa hivyo binadamu anafaa aishi kwa heshima na kutenda mema, ukarimu na kutoumiza wengine na kufanya maamuzi yanayofaa jamii yake. Nadharia hii ilifaa utafiti huu kwa kuangazia ni kwa nini mwandishi S. A. Mohamed anabadilisha itikadi zake na kujirekebisha kila baada ya kipindi. Labda ni kutokana na ile azma yake ya kuishi maisha na kuifaa jamii yake ili kazi zake ziwe faafu kwa jamii anamotungia katika vipindi tofauti vya utunzi wa kazi zake.

Nadharia hii ina mitazamo tofauti. Aristotle (1952) anasema kwamba mwanadamu ni kiumbe ambaye huishi na wanajamii wengine. Wao hutegemeana na kuathiriana wanapoishi pamoja. Ili mtu awe mwema lazima afanye mazoezi na atumie fikra zake mwenyewe kuendelea na kutenda matendo ya fadhila hadi afikie lengo la uzuri mkuu ambapo ataishi kwa utulivu, furaha na ustawi. Awe wa kutenda fadhila au wema kwa lengo lake mwenyewe, atende mema kwa ajili ya wema wenyewe. Maoni haya yalifaa utafiti huu kwa kuangazia ni vipi itikadi za Said Ahmed Mohamed zimeathiriwa na jamii yake na jinsi anavyojaribu kujisahihisha katika misimamo yake ili aweze kuishi vyema na wanajamii ambao kazi zake zinalenga.

Hough (1966) anasema kwamba fasihi hujumlisha tajriba yote ya mwanadamu maishani na ufaafu wake hupimwa kwa kiwango ambacho huchangia ukamilifu wa vitendo vya wanadamu. Hivyo ni kusema kuwa fasihi lazima ichangie kuboresha na kuendeleza maisha ya wanadamu katika jamii. Fasihi lazima iwakilishe mifano bora kwa jamii ambayo inaweza kuigwa na wanajamii na pia kutoa maonyo kwa wanajamii. Hii ina maana kuwa fasihi huwa kama kipimo bora cha yaliyo mema katika jamii kwa ujumla wake jambo ambalo hutegemea mtu binafsi na mazingira yake kiwakati, tabaka lake, utaifa wake na kadhalika. Kwa hivyo ni dhahiri kuwa maadili hutegemea nyakati tofauti na ikiwa kazi ya kifasihi ni kielelezo kikuu cha maadili ya jamii ambayo hutegemea mtunzi na mazingira yake, ni kweli kuwa mazingira haya yanapobadilika lazima kazi ya fasihi ibadilike ili kuendeleza maadili yanayofaa jamii kwa wakati maalumu na kusababisha mabadiliko ya itikadi zake.

Kwa mujibu wa Hough (1966) kila fasihi ni dhana ya kijamii. Uumbaji wa fasihi ni tendo la kijamii kwani huzungumzia watu au makundi ya watu. Fasihi lazima ijihusishe na maswala ya jamii kikamilifu. Mtunzi wa kazi ya fasihi huzingatia maswala ya kijamii na huathiriwa na mazingira na tabaka linalomzalisha. Matokeo ya kazi yake huenda yakawa tofauti na yale aliyodhamiria na yanaweza kupingana na mawazo yake mwenyewe.

Plato (1969) anasema kwamba maadili ni dhana ya Uungu yaani kuna ushawishi wa viulimwengu ambavyo viko katika hali ya kipepo. Maana ya maisha ni kufikia umbo la

juu la elimu analoita wazo la zuri, yote mema na ya haki yanayotoa umuhimu wa thamani. Kwa maoni yake, binadamu wamefungwa kuyatekeleza yale mazuri na hakuna yeyote anayeweza kufanikiwa bila fikra za kifalsafa. Maoni haya yaliufaa utafiti huu kuangazia mtunzi S. A. Mohamed anapobadilisha itikadi yake ya kimtindo hasa katika riwaya ya *Dunia Yao* anaelekezwa na mawazo haya ya Plato kuhusu dhana za kiroho za Uungu.

Hobbes (1970) na Rousseau (1973) wanaafikiana kwamba jamii ni umbo la mwanadamu. Dunia katika hali asilia ni tesi, maisha ni mafupi, ya upweke na yenye mateso. Mwanadamu huishi na wengine ndio afurahie maisha na kuepuka utesi wa dunia asilia. Kwa hivyo jamii huendelea ikibadilika ili kuifanya hali ya mwanadamu kuwa bora zaidi. Maoni haya yalifaa kubainisha ni vipi jamii ambamo S. A. Mohamed anamoandikia inavyobadilika na vile inavyomfanya mtunzi mwenyewe kubadilisha itikadi zake za utunzi ili kuafikiana na malengo na mitazamo ya wanajamii wake.

Kant (1968) anaendeleza dhana kuwa dini na maadili ni muhimu kwa maisha ya wanadamu. Anasisitiza dhana ya fikra katika kutenda wema yaani fikra ndizo hupaswa kutawala matendo ya wanadamu wala si dhana ya kidini. Anaendeleza dhana ya uwajibikaji yaani wajibu wa kimaadili, vitendo vyote vinafanywa kulingana na kanuni fulani zisizobainika wazi ili vitendo viwe vya kimaadili lazima viambatane na kanuni ya lazima bila kujalisha. Mwelekeo huu ulifaa utafiti huu kutubainishia mtunzi S. A.

Mohamed anavyobadilisha itikadi zake ili kuwiana na vitendo vyake, utunzi wake na kanuni za kimaadili ya jamii yake katika vipindi tofauti vya uandishi wake.

Ilivyobainika ni kwamba maadili ni mafundisho yanayotolewa katika nafasi mbalimbali katika malezi ili kuelekeza binadamu atende namna ambavyo inamjenga yeye na jamii nzima. Mazingira yanaweza kudai yatekelezwe kwa njia tofauti kulingana na dini, utamaduni, falsafa, kadhia na mali za jamii inayohusika.

Achebe (1975) anasema kuwa mwandishi ni mtu wa kawaida na wajibu wake ni kuitumikia jamii hata kama mawazo yake yanaweza kuhitilafiana na yale ya jamii yake. Anasema kuwa mtunzi anayejitenga na jamii anayoandikia anaweza kuandika kazi mbovu ama uhakiki mbaya. Kwa hivyo ni muhimu msanii yeyote kuzingatia jamii anayoandikia ili kazi yake iwe faafu na hivyo msanii hawezi kujitenga na jamii yake. Mawazo haya ya Achebe yanaoana na ya wa Thiong'o (1972) anayesema kuwa mwandishi wa kifaraka ana jukumu la kuelimisha waafrika kuhusu historia na hali yao ya sasa.

Mtafiti alinufaika na kauli hizi kwa kuzingatia ikiwa mtunzi S. A. Mohamed anabadilisha itikadi ili kuifaa jamii anayoiandikia na kutekeleza wajibu kwa jamii yake kama Achebe anavyosema. Achebe (1988) anasema kwamba fasihi hutuonyesha uhalisia, hutufunza maana ya matendo yetu na hutusaidia kudhibiti hali zetu za kila siku na kwa hivyo fasihi ni muhimu katika kuelewa maswala ya jamii na siasa. Hivyo ni kumaanisha

mtunzi hawezi akajitenga na jamii. Anasema kuwa mwandishi wa Kiafrika ana jukumu la kuelimisha Waafrika kuhusu historia yao na hali yao ya sasa. Akiendeleza dhana hii katika makala ya “The Novelist as a Teacher”, anasema mwandishi ni kama mwalimu wa jamii yake na ana wajibu wa kuizindua jamii yake ili ijiamini. Kwa hivyo ni dhahiri kwamba jamii humtegemea mwandishi kuwaelimisha na hivyo mtunzi ana wajibu kwa jamii anayoiandikia na hivyo hutekeleza wajibu muhimu na hujenga wahusika kutoka kwa jamii.

Ni kweli kwamba mielekeo ya Plato, Aristotle, Rousseau, Hobbes, Kant, Ngugi na Achebe kuhusu maadili yaliufaa utafiti huu. Kwa kuzingatia dhana ya Uungu ya Plato, matumizi ya fikra ya Aristotle, ubadilifu wa jamii ya Rousseau na Hobbes na muungano wa dini na maadili katika kuelezea dhana ya fikra ya Emmanuel Kant, tuliweza kubainisha S. A. Mohamed anavyobadilisha itikadi zake baada ya kipindi fulani ili kuafikiana na kuambatana na maadili ya jamii yake na pia kufikia ukuaji wa fikra zake kufikia dhana ya uungu au wema. Aidha, kauli za watunzi wa Kiafrika kama Ngugi na Achebe zilichangia katika kubaini labda mtunzi anabadilisha itikadi ili kazi zake ziwe faafu kwa jamii za Kiafrika ama ni katika juhudi za kuwaelimisha na kuwazindua.

Nadharia hii pia ilitufaa katika kuzingatia jamii na mazingira ambamo S. A. Mohamed alimoandikia katika vipindi tofauti vya utunzi ili kubaini mambo ambayo huenda yalimwathiri ili kuibadilisha misimamo yake. Aidha, mtafiti aliangalia na kuona kwamba anabadilika ili kuifunza jamii yake na kujitambulisha nayo kama Ngugi na Achebe

wanavyosema. Kadri jamii inavyobadilika kiuchumi, kiteknolojia na jinsi alivyohama yeye mwenyewe kutoka Tanzania kwenda Ujerumani na jinsi utunzi wake unavyoathirika anavyozidi kutangamana na jamii na mazingira tofauti katika vipindi tofauti katika utunzi wake. Kwa ujumla mihimili ya nadharia ya kimaadili iliyozingatiwa katika utafiti huu ni:

- (a) Fasihi ni zao la jamii.
- (b) Fasihi hutoa mifano ifaayo ya maadili kwa wakati maalum.
- (c) Mazingira ya mtunzi kijamii na kihistoria huathiri kazi yake.
- (d) Fasihi ni kielezo cha maadili ya jamii kwa wakati maaalum na mtunzi lazima azingatie maadili ya jamii yake kwa wakati wake ili kazi yake iwe faafu kwa jamii yake.

Kuna nadharia nyingine ambayo ingeweza kutumika katika utafiti huu. Nadharia hii ni nadharia ya ubadilikaji. Wamitila (2003) anasema kuwa nadharia hii inategemezwa kwenye mawazo ya Charles Darwin. Nadharia hii hudai kuwa sanaa ilizuka katika harakati za maingiliano ya binadamu na mazingira yake. Huchukulia kuwepo kwa usawa fulani katika maisha ya binadamu na hivyo kuna sifa fulani zinazopatikana katika hatua fulani za kila jamii. Sanaa hubadilika kutoka hatua ya chini hadi nyingine ya juu kadri wakati unavyobadilika. Nadharia hii hujikita zaidi kwenye maudhui na hivyo mtafiti hangeweza kuitumia kuangazia itikadi na namna zinavyobadilika katika mapito ya wakati kwani itikadi hujitokeza katika ujumla wa kazi inayosomwa. Aidha, nadharia hii haingeweza kuonyesha uhairishaji wa maana ya dhana ya itikadi katika kila kipindi cha

utunzi wa mwandishi S.A Mohamed jambo amabalo limeshughulikiwa vyema kwa kuzingatia nadharia ya udenguzi na kimaadili.

2.3 HITIMISHO

Katika sura hii, mtafiti ameshughulikia yaliyoandikwa kuhusu mada. Ameangalia vitabu na makala tofauti yanayoshughulikia itikadi katika riwaya za S. A. Mohamed na itikadi katika riwaya za Kiswahili kwa ujumla wake. Makala na vitabu hivi vimechangia sana utafiti huu hasa kwa kutoa mwanga kuhusu tahakiki tofauti zilizofanywa kuhusu riwaya na dhana ya itikadi. Lililodhihirika ni kwamba kuna wahakiki walioshughulikia dhana ya itikadi kwa pembezoni tu na kuitaja hapa na pale katika kazi zao bila kuishughulikia kikamilifu. Aidha, wahakiki kama Chuachua (2011) aliyeshughulikia dhana ya itikadi katika riwaya za Shaaban Robert walizingatia mkabala mmoja katika utafiti wao na pia hawakushughulikia itikadi ya mtunzi katika mpito wa wakati. Hivyo ikadhihirika kuwa kuna pengo lililohitaji kujazwa kwa kuangalia mabadiliko ya itikadi katika mapito ya wakati na kuangalia dhana hii katika mikabala tofauti ili kuonyesha kuwa itikadi ni dhana nyumbufu na badilifu. Tena ikiwa ni hivyo basi mtazamo na mielekeo ya mtunzi si mmoja na tengemano kama wahakiki wengi wanavyofikiria wanapohakiki kazi ya fasihi kuonyesha kuwa dhima ya mtunzi ni changamano zaidi.

Aidha, mtafiti ameshughulikia nadharia alizotumia katika utafiti huu ambazo ni nadharia ya udenguzi na nadharia ya kimaadili. Nadharia ya udenguzi inatumiwa

katika kutoa fasili mbalimbali ya dhana ya itikadi na kuonyesha kuwa ni telezi na changamano kuliko inavyofikiriwa na wahakiki wengi. Mihimili ya nadharia hii pia imetumiwa na mtafiti kutoa maana tofauti ya mambo yaliyowasilishwa kwenye matini zinazohakikiwa. Kwa upande mwingine nadharia ya kimaadili imejadiliwa katika sura hii. Nadharia hii imetumiwa katika kuangazia jamii ambayo mtunzi anayoandikia na kuonyesha kuwa mabadiliko yanayojitokeza katika kazi hizi ni katika juhudi za kufanya kazi zake kuwa faafu kwa jamii lengwa. Kama nadharia hii inavyosema, fasihi ni zao la jamii na kielelezo cha maadili ya jamii kwa kipindi maalum kumaanisha kipindi kikibadilika basi fasihi hubadilika na hivyo itikadi hubadilika pia na kuathiri mitazamo na mielekeo ya mtunzi. Hivyo nadharia ya udenguzi inatumika zaidi kuangazia matini zinazohakikiwa ilhali nadharia ya kimaadili imetumiwa kuangazia zaidi jamii lengwa na namna mtunzi anavyoathirika na kusababisha abadilishe itikadi.

SURA YA TATU

3.0 MBINU ZA UTAFITI

3.1 UTANGULIZI

Katika sura iliyotangulia mtafiti ameshughulikia yaliyoandikwa kuhusu mada na nadharia zinazotumika katika utafiti huu. Katika yaliyoandikwa imebainika kuwa kadri ya ufahamu wa mtafiti hakuna mhakiki aliyeshughulikia dhana ya itikadi katika mapito ya wakati na katika mikabala tofauti na hivyo kuzua haja ya kujaza pengo hili. Aidha, mtafiti amejadili nadharia anazotumia katika utafiti huu. Nadharia hizo ni nadharia ya udenguuzi inayomfaa katika kuangazia matini na kutoa fasili tofauti za matini na nadharia ya kimaadili inayoangazia zaidi jamii inayolengwa na mtunzi na namna inavyomwathiri na kumfanya abadilishe itikadi za kiutunzi kila baada ya kipindi fulani. Katika sura ifuatayo mtafiti anashughulikia mbinu anazotumia kufanikisha utafiti huu

3.2 MUUNDO WA UTAFITI

Utafiti huu unafuata muundo wa kimaelezo. Kulingana na Borg na Gall (1989), utafiti wa kimaelezo hulenga kujua 'kwa nini'. Utafiti wa kimaelezo ni utafiti ambao data hukusanywa bila kubadilisha mazingira kinyume na ilivyo katika utafiti wa kimajaribio. Utafiti wa kimaelezo unaweza kuwa wa kutagusana na watu au vitafitiwa katika kipindi kimoja au ukawa wa kuchunguza kwa kipindi kirefu. Utafiti huu unaangazia utunzi wa mwandishi S. A. Mohamed katika kipindi kirefu cha utunzi wake.

Uchunguzi wa kimaelezo waweza kuhusisha mahojiano ambayo yalishirikishwa katika utafiti huu. Ili kuchunguza iwapo itikadi za mtunzi zimebadilika katika mapito ya wakati,

maneno, sentensi na aya zinazoibua mitazamo yake katika vitabu teule vilichunguzwa. Data zilizopatikana kutokana na uchunguzi wa kazi zake pamoja na zilizotokana na kumhoji yeye na wahakiki wa kazi zake zilituwezesha kuibua itikadi zinazojitokeza katika utunzi wake na kuonyesha kuwa zimekuwa zikibadilika katika vipindi tofauti vya utunzi wake.

3.3 ENEO LA UTAFITI

Utafiti huu ulifanyiwa maktabani na nyanjani. Vitabu, majarida, tahakiki na makala yanayohusiana na mada ya utafiti yalisomwa ili kutupatia data ya kutosha. Makala katika mtandao na vitabu vilivyoteuliwa kwa minajili ya kufanikisha utafiti huu pia vilisomwa. Riwaya hizi teule ni *Asali Chungu* (1978), *Kiza katika Nuru* (1988), *Dunia Yao* (2006) na *Mhanga Nafsi Yangu* (2012) ambazo zilichanganuliwa kwa kina kwa kuzingatia maudhui, wahusika na mtindo ili kupata data ya utafiti. Tahakiki ambazo zimefanywa kuhusiana na mada hii zilisomwa ili kutoa mwanga zaidi wa mada ya utafiti. Vitabu na makala katika mtandao yanayoelezea nadharia ya udenguzi na ile ya kimaadili vilisomwa na kuhusishwa na utafiti ili kutoa mwanga zaidi kuhusiana na mihimili iliyoongoza utafiti huu.

Eneo jingine la utafiti huu ni nyanjani. Tulimhoji mwandishi kwa lengo la kubainisha ni mambo yepi ambayo yalipelekea yeye kubadilisha msimamo wake kila baada ya kipindi maalum. Mahojiano haya yalikuwa ana kwa ana na pia hojaji ilitumiwa ambayo tulimuomba mwandishi S. A. Mohamed atujazie. Aidha tulifanya mijadala na wahakiki sita katika Kaunti ya Nairobi hasa wale walioandika kuhusu kazi za mtunzi na wale

ambao wametangamana naye kwa karibu. Hili lilitokelezwa kwa matumizi ya mahojiano ya moja kwa moja na pia matumizi ya hojaji.

3. 4 SAMPULI LENGWA

Said Ahmed Mohamed ameandika vitabu vingi vikiwemo riwaya, tamthilia na ushairi. Kwa vile mada yetu inahusu itikadi katika riwaya alizoandika tumeteua riwaya nne kimaksudi kati ya alizoandika. Riwaya hizo ni *Asali Chungu* (1978), *Kiza Katika Nuru* (1988), *Dunia yao* (2006) na *Mhanga Nafsi Yangu* (2012). Riwaya hizi zimempa mtafiti data ya kutosha ya kuweza kushughulikia itikadi za S. A. Mohamed na kuonyesha kama zinabadilika katika kila kipindi cha utunzi wake. Wahakiki sita walioteuliwa kimaksudi walitoka katika Chuo Kikuu cha Kenyatta na kile cha Nairobi.

3.4.1 MBINU ZA USAMPULISHAJI

Uteuzi wa sampuli ya utafiti huu ulikuwa ule wa maksudi na pia utabakishaji. Riwaya nne ambazo zimeandikwa na S. A. Mohamed ziliteuliwa. Riwaya hizi *Asali chungu* (1978), *Kiza katika Nuru* (1988), *Dunia Yao* (2006), na *Mhanga Nafsi Yangu* (2012). Riwaya hizi zilitumika kama viwakilishi vya vipindi tofauti katika utunzi wa S. A. Mohamed ili kubainisha namna itikadi yake ya utunzi inavyobadilika katika mapito ya wakati. Uwasilishaji wa maudhui, wahusika na mtindo katika kila riwaya ulitumiwa kubainisha itikadi zinazojitokeza na kuona ikiwa zinabadilika kila baada ya kipindi. Mtafiti alidondoa sentensi, vishazi na sehemu maalum za riwaya ili kuonyesha jinsi zinavyoonyesha itikadi. Namna mtunzi alivyopanga vitushi vyake, maudhui anayojadili kama ukombozi, mapinduzi, maswala ya ndoa, ukoloni na ukoloni mamboleo, mifumo ya

kiuchumi na kadhalika yanaashiria mabadiliko ya itikadi yake. Aidha, namna anavyowateua wahusika wake kama Zuberi na Semeni katika *Asali Chungu*, Mvita na Juba katika *Kiza Katika Nuru* ni tofauti kwani Zuberi ni wa tabaka la juu, Semeni tabaka la chini. Juba na Mvita wote ni wa tabaka la juu lakini Mvita anapigania haki za wanyonge.

Kabla ya kuteua kazi hizi kimaksudi, mbinu ya utabakishaji ilitumiwa. Mtafiti alipanga kazi za S. A. Mohamed kutegemea vipindi mbalimbali vya utunzi wake. Kisha kazi zilizohakikiwa zikateuliwa kwa kuzingatia vipindi hivyo maalum vya utunzi ili kuonyesha itikadi zinazojitokeza katika vipindi tofauti. Kutoka kipindi cha miaka ya sabini mtafiti aliteua *Asali Chungu* na miaka ya themanini ikawakilishwa na *Kiza Katika Nuru*. Miaka ya elfu mbili kuendelea ikawakilishwa na *Dunia Yao* na *Mhanga Nafsi Yangu*. Uteuzi huu ulifaa utafiti huu katika kuangalia kama kuna mabadiliko ya kiitikadi katika vipindi tofauti vya utunzi wa riwaya hizi.

Vitabu vilivyoteuliwa vilitupatia data ya kutosha kufanikisha utafiti huu. Aidha, wahakiki sita ambao pia ni watunzi waliteuliwa kimaksudi ili kutupatia data iliyotusaidia kushadidia data kutoka kwa riwaya teule pamoja na data tuliropewa na mtunzi mwenyewe tulipomhoji. Ikizingatiwa kwamba tuliangazia vipengele vya maudhui na wahusika kwa utaratibu maalum na kushadidia matokeo hayo kutokana na data iliyotokana na mahojiano ya wahakiki wengine na mtunzi mwenyewe, tuliweza

kubainisha itikadi za mtunzi katika kila kipindi cha utunzi na kudhihirisha namna itikadi zake zinavyobadilika kila baada ya kupindi maalum.

Wahakiki waliohojiwa waliteuliwa kimaksudi kwani walitufaa kutupa data tuliohitaji. Tuliwateua kwa kuwa ni watunzi, wahakiki na wahadhiri wenye tajriba pana katika ufundishaji wa fasihi ya Kiswahili. Wote walioteuliwa wameandika makala kuhusu baadhi ya kazi za S.A Mohamed na wametangamana naye moja kwa moja katika vipindi tofauti.

3.5 UKUSANYAJI WA DATA

Data ilikusanywa katika maktaba ambapo riwaya teule zilisomwa. Maneno, sentensi na vifungu vinavyodhihirisha itikadi na mabadiliko yake zilinukuliwa na kuwekwa katika daftari mwafaka ili kurejelewa wakati wa uchanganuzi. Mambo yaliyowekwa katika daftari ni kama maudhui ya mtunzi katika vitabu vyote vinne, wahusika na sifa zao na mitindo ya utunzi wa kila riwaya. Mambo haya matatu yaliweza kudhihirisha itikadi ya mtunzi huyu imekuwa ikibadilika kila baada ya kipindi fulani. Maoni ya mtunzi kuhusu kazi hizi na itikadi zake na namna anavyobadilika yalinukuliwa na kuwekwa katika vifungu ili kubaini sababu zilizompelekea yeye kubadilisha itikadi zake. Aidha maoni ya wahakiki sita pia yalinukuliwa ili kubaini ikiwa ni kweli itikadi za S. A. Mohamed zimekuwa zikibadilika kila baada ya kipindi fulani.

3.6 UCHANGANUZI WA DATA

Data iliyopatikana ilichanganuliwa kwa kuzingatia malengo ya utafiti. Malengo haya ni kuonyesha uhusiano uliopo baina ya itikadi na mtazamo wa mwandishi, kudhihirisha itikadi inayojitokeza katika riwaya za *Asali Chungu* na *Kiza Katika Nuru* kutokana na usawiri wa wahusika na maudhui. Kadhalika, kuchunguza itikadi inayojitokeza katika riwaya za *Dunia Yao* na *Mhanga Nafsi Yangu* kwa mujibu wa maudhui, mtindo na wahusika na kuonyesha mabadiliko yanayojitokeza kwa upande wa usawiri wa maudhui na wahusika yanaakisi kujirekebisha na kujisahihisha katika mitazamo na mielekeo ya mtunzi na kwa nini. Ilikuwa katika kudhihirisha kwamba itikadi ni dhana badilifu na hubadilika ili kuifaa jamii au ili kazi ya mtunzi ziwe na ufaafu kwa jamii yake. Haya yameonyeshwa kupitia maudhui yanayoshughulikiwa katika vipindi tofauti na jinsi wahusika wamesawiriwa katika riwaya hizi na kudhihirisha kuwa mabadiliko ya vipengele hivi yanaonyesha mabadiliko ya itikadi na hivyo itikadi ni dhana inayobadilika. Aidha, nadharia ya udenguzi imetumiwa kudhihirisha kuwa kazi ya fasihi yaweza kuwa na fasili nyingi tofauti ambazo zinaweza kupingana, maana ni telezi na haiwezi kushikika. Dhana zinazokinzana zinakaribiana na maana haipatikani katika ishara moja pekee, huwa katika hali ya kuwepo na kutokuwepo.

Mihimili hii imeonyesha kuwa kadri S. A. Mohamed anavyozidi kubadilisha itikadi yake ndivyo ambavyo anajipinga mwenyewe na hivyo kuivunja kazi yake mwenyewe na ndivyo misimamo yake inavyobadilika kiasi cha kutoaminika. Mielekeo ya nadharia ya kimaadili ilifaa uchanganuzi wa data hasa kubainisha mambo yaliyopelekea S. A.

Mohamed kubadilika kila baada ya kipindi. Labda ni kwa lengo la kuhusisha na kuishi vyema na wanajamii wengine. kutaka kuwa mwema katika jamii anamoishi na ili kazi zake ziwe faafu kwa jamii anayoilenga ama kuielekaza na kuifunza jamii yake.

3.7 VIFAA VYA UTAFITI

Mtafiti alitumia vifaa kadhaa ili kuufanikisha utafiti huu. Kalamu na daftari zilitumiwa kunukuu maneno, sentensi, wahusika, maudhui na hoja nyinginezo zilizotumika katika utafiti huu. Pia mtafiti alitumia tepu rekoda kurekodi mahojiano na mwandishi na wahakiki wengine. Hojaji pia zilitumwa kwa mwandishi na watunzi wengine waliozijaza na kuzituma kwa mtafiti. Mtandao pia ulitumiwa pale ambapo mahojiano ya moja kwa moja hayakuwezekana.

3.8 UWASILISHAJI WA MATOKEO

Njia ya maelezo ndiyo iliyotumiwa kuwasilisha matokeo ya utafiti huu kwa sababu ni utafiti wa kifasihi unaojikita zaidi maktabani. Maelezo haya yalizingatia ufafanuzi wa maudhui na wahusika na kisha kuonyesha namna vipengele hivi vinavyodhihirisha itikadi mbalimbali za mtunzi na namna zinavyobadilika katika kila kipindi cha utunzi wake. Aidha, tulionyesha misukumo inayopelekea mtunzi kubadilisha itikadi au misimamo yake kama inavyojitokeza katika maudhui na wahusika katika kazi zake teule. Haya yote yalifanywa kwa kuzingatia malengo ya utafiti kwa misingi ya nadharia ya udenguzi na nadharia ya kimaadili.

3.9 HITIMISHO

Katika sura hii, mtafiti amejadili mbinu zilizotumiwa katika kuufanikisha utafiti huu. Ameeleza kuwa muundo wa utafiti huu ni wa kimaielezo ambapo maneno na sentensi zinatumika kuonyesha mtazamo wake na hivyo kuwezesha mtafiti kuibua itikadi zinazojitokeza kwenye kazi zinazohakikiwa. Mtafiti ameonyesha eneo la utafiti ni maktabani na nyanjani ambapo maktabani vitabu na tahakiki mbalimbali zilisomwa na nyanjani ambapo mtunzi na wahakiki sita walihojiwa, watatu kutoka Chuo Kikuu cha Nairobi, wawili kutoka Chuo Kikuu cha Kenyatta na mmoja kutoka kutoka Chuo Kikuu cha Mount Kenya. Mtafiti ameonyesha sampuli lengwa ni riwaya nne zilizoandikwa na S. A. Mohamed ambazo ni *Asali Chungu* (1978), *Kiza Katika Nuru* (1988), *Dunia Yao* (2006) na *Mhanga Nafsi Yangu* (2012). Aidha mtafiti ameeleza namna alivyotumia mbinu za usampulishaji za kimaksudi na utabakishaji kuteua sampuli ya utafiti wake.

Katika mbinu za ukusanyaji wa data, mtafiti ameonyesha kuwa ametumia mbinu ya maktabani na nyanjani ambapo alidondoa hoja maalum zinazohusiana na itikadi, wahusika, maudhui na mtindo. Nyanjani alizungumza na mwandishi na wahakiki sita waliompa data muhimu kuufanikisha utafiti huu. Kuhusu vifaa ameonyesha kuwa alitumia kalamu na daftari maalum kunukuu hoja na vifungu vinavyodhihirisha itikadi, hojaji katika kumhoji mwandishi na wahakiki wengine na mahojiano kwa kutumia mtandao na tarakilishi. Ili kuchanganua data ifaavyo, hoja, sentensi, wahusika na maudhui yalidondolewa na kuchanganuliwa kwa mujibu wa swala la utafiti, malengo ya

utafiti na nadharia ya udenguzi na ile ya kimaadili. Matokeo ya utafiti huu yanawasilishwa kwa njia ya maelezo kwa kuwa utafiti huu ni wa uhakiki.

SURA YA NNE

4.0 ITIKADI NA MTAZAMO WA MTUNZI

4.1 UTANGULIZI

Katika sura iliyopita, mtafiti amejadili mbinu alizotumia katika utafiti huu. Ameonyesha kuwa utafiti huu ulihusisha mbinu ya maktabani na nyanjani. Maktabani, vitabu vinavyohusiana na mada vilisomwa ili kutupa msingi wa kazi hii. Vitabu teule vilisomwa na maneno na sentensi kunakiliwa katika daftari maalumu. Data iliyopatikana ilichanganuliwa kwa mujibu wa nadharia ya udenguzi na kimaadili. Mahojiano yalifanywa na mtunzi na wahakiki sita kushadidia data iliyopatikana. Mwishowe imeonyeshwa kuwa matokeo yamewasilishwa kwa njia ya maelezo. Katika sura hii mtafiti amejadili mikabala mbalimbali ya dhana ya itikadi na historia yake, historia ya Zanzibar na mtunzi S. A. Mohamed kwa lengo la kuonyesha uhusiano uliopo baina ya itikadi na mtazamo wa mtunzi kwa kurejelea riwaya zake.

4.2 HISTORIA YA MTUNZI S. A. MOHAMED

Swala la historia ya mtunzi ni muhimu sana katika kujenga itikadi yake. Kutokana na dhana kwamba daima kuna ufungamano baina ya siasa, uchumi wa nchi na itikadi, ni dhahiri kwamba naye mtunzi huishi katika jamii na huiandikia jamii. Achebe (1975) anasema kwamba mtunzi ni sehemu ya jamii na hawezi kujitenga na jamii anayoiandikia. Aidha, Njogu (1997) anasema kuwa msanii lazima aielewe jamii yake na muundo wa jamii hiyo kwani wahusika hutokana na hali halisi za maisha. Mwandishi hawezi kujitenga na hali zinazoikumba jamii aizungumziayo kwa vile fasihi huathiriwa na

matukio ya kihistoria. Inavyodhihirika ni kuwa itikadi nayo hufungamana na matukio ya kihistoria yanayomwathiri mtunzi na hivyo kadri historia inavyobadilika katika vipindi tofauti, nayo itikadi ya mtunzi huzidi kubadilika ili kuifaa jamii yake na kazi yake iwe faafu kwa hadhira yake. Hivyo, mtunzi huathiriwa na hali za kiuchumi na kisiasa zinazoibua itikadi fulani katika vipindi maalumu.

Itikadi ya mtunzi ndiyo humuongoza kuhusu atakayozungumzia. Itikadi hiyo hutokana na mambo kama vile mwandishi alizaliwa wapi, lini, mazingira gani, kakulia vipi, alienda shule gani, amesoma vitabu gani, imani gani inayotawala katika mazingira yake na hali yake ya kiuchumi miongoni mwa mengine (Mohamed,1995:8). Kwa misingi hii, ni muhimu kuelewa historia ya mtunzi na muktadha wake wa kihistoria kwani daima historia yake hufungamana na itikadi atakayoaridhia kwa kipindi fulani ili kukidhi mahitaji ya jamii yake. Ikizingatiwa kuwa fasihi inahusu hali ya taathira hivi kwamba mwanasanaa huathiriwa na kuathiriana na maisha na kwamba mwanadamu ndiye muumbaji wa kazi ya fasihi, nayo matendo yote ya binadamu ulimwenguni huelekezwa na itikadi maalumu katika vipindi tofauti. Basi kuna ufungamano mkubwa baina ya historia ya mtunzi na itikadi itakayojitokeza katika kazi yake kupitia kwa maswala atakayojadili, mbinu atakazotumia na usawiri wake wa wahusikahivyo kuathiri kazi yake yote na mitazamo yake kuhusu maswala mbalimbali katika vipindi mbalimbali vya utunzi wake.

Said Ahmed Mohamed alizaliwa mnamo mwaka wa 1947 kisiwani Unguja. Alisomea shule ya msingi ya Darajani, Zanzibar mjini. Alijiunga na shule ya upili ya Gulioni ambayo kitambo ilijulikana kama King George VI. Baadaye alijiunga na Chuo cha Ualimu cha Nkrumah mjini Zanzibar mwaka wa 1966. Alifuzu na kuanza kufunza kama mwalimu wa shule ya msingi katika shule ya Kizimbani na baadaye akawa mwalimu wa shule ya sekondari ya Utaani mnamo miaka ya 1969-1974. Alifunza masomo ya Biolojia, Hesabu, Kemia na Kiswahili. Wakati huohuo alikuwa akiandika hadithi fupi katika vituo vya BBC na Deutsche Welle, mashirika ya Uingereza na Ujerumani mtawalia. Huu ndio wakati alipata wazo la kuandika riwaya ya *Asali Chungu*. Baadaye alijiunga na kidato cha 5 na alikuwa amepanga kufanya masomo ya sayansi lakini akakosa vifaa vya utekelezi na basi akaamua kusomea somo la sanaa.

Mohamed alijiunga na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambapo alihitimu shahada ya B.A katika isimu na fasihi katika mwaka wa 1976. Akarejea Zanzibar na akawa mwalimu mkuu wa shule za msingi na upili za Hamanani kwa miaka mitano. Mtunzi huyu alihitimu shahada ya uzamili katika Chuo Kikuu hicho hicho cha Dar es Salaam ambapo alisomea isimu tekelezi. Mohamed alifunza katika Idara ya Kiswahili mle Chuoni kwa muda mfupi na baadaye akajiunga na Chuo Kikuu cha Leipzig Ujerumani, ambapo alihitimu shahada ya uzamifu mwaka wa 1985. Alirudi kwao Zanzibar ambapo aliteuliwa na Rais wa Zanzibar kuwa Mkurugenzi wa pili katika Taasisi ya Kiswahili na lugha za Kigeni (TAKILUKI).

Mohamed alihama na kuja Kenya kufundisha Kiswahili katika kitivo cha Elimu cha Moi mnamo 1987 ambapo alikuwa mwenyekiti wa kwanza Idara ya Kiswahili. Mnamo mwaka wa 1990 alijiunga na Chuo Kikuu cha Nairobi, bewa la Kikuyu. Mwandishi huyu baadaye alienda Ujapani na kujiunga na Chuo Kikuu cha Masomo ya Kigeni kule Osaka ambapo alipata Uprofesa. Mnamo 1997 alijiunga na Chuo Kikuu cha Bayreuth Ujerumani hadi hivi karibuni ambapo alistaafu na kurudi kwao Zanzibar. Katika nyanja ya utunzi Mohamed alianza kutunga mashairi na hadithi fupi huku akiwa mwanafunzi wa shule ya msingi. Kwa mujibu wa King'ei (1997) Mohamed amewahi kufanikiwa katika utunzi wa tanzu tofauti kama ushairi, riwaya na tamthilia, jambo ambalo ni nadra sana kutokea katika taaluma ya fasihi kwa sababu wasanii wengi hufungika katika utanzu mmoja peke yake.

Baadhi ya kazi zake ni diwani za *Sikate Tamaa* (1980), *Kina Cha Maisha* (1984) na *Jicho la Ndani* (2002). Pia ameandika vitabu vya fasihi simulizi kama *Vito Vya Hekima*, *Simo*, *Milio na Tashbihi* (1974). Kazi zake za riwaya ni *Asali Chungu* (1977), *Utengano* (1980), *Dunia Mti Mkavu* (1980), *Kiza katika Nuru* (1988), *Tata za Asumini* (1990), *Babu Alipofufuka* (2001), *Dunia Yao* (2006), *Nyuso Za Mwanamke* (2010), *Mkamandume* (2012) na *Mhanga Nafsi Yangu* (2012). Isitoshe mwandishi S. A. Mohamed ametunga tamthilia kama vile *Pungwa* (1988), *Amezidi* (1995), *Kivuli Kinaishi* (1990), *Kitumbua Kimeingia Mchanga* (2000) na *Janga la Werevu* (2011). Pia ameshirikiana na Kitula King'ei kuandika tamthilia ya *Posa za Bikisiwa* (2008). Katika uwanja wa hadithi fupi, S. A. Mohamed ametoa mchango wake kwa mikusanyiko kama *Sadiki Ukipenda na Hadithi*

Nyingine (2002), *Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine* (2005) na akashirikiana na Ken Walibora kuhariri mkusanyiko wa *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine* (2007). Aidha kazi za Mohammed hazikukomea hapo kwani ameandika *Kunga Za Nathari ya Kiswahili: Riwaya, Tamthilia na Hadithi Fupi* (1995). Vile vile ametunga *Mbinu na Mazoezi ya Ushairi* (1990). Mnamo 1988 Mohamed alishinda tuzo ya mwandishi bora ambayo ni ya heshima kuu iliyotolewa na Chama Cha Waandishi cha Tanzania. Maswala muhimu ambayo yanazungumziwa katika kazi zake za kiubunifu ni matatizo yanayokumba bara la Afrika na chanzo cha matatizo hayo miongoni mwa maswala mengine.

Inavyojitokeza ni kuwa Mohamed ni mtunzi aliyetunga kazi za kifasihi kwa zaidi ya miongo mitatu na ameishi kwa muda mrefu katika vipindi tofauti vya historia ya jamii yake. Mabadiliko mengi ya kijamii, kiuchumi na kisiasa yametokea katika maisha yake. Katika vipindi vya mwanzo mwandishi aliathiriwa sana na itikadi za kijamaa (Mbatiah, 1990) na kuwasilisha kazi zake za awali kihalisia na kiyakinifu. Aidha, ikizingatiwa kwamba mwandishi ni mtu wa kawaida katika jamii yake anaonekana kuamini kuwa walioendeleza mapinduzi hawakuzingatia maslahi ya wanyonge na hivyo anaendeleza dhana ya mapinduzi si ya watu tu bali ya asasi za utawala na kujenga jamii yenye usawa.

Mohamed (1984) katika “Kupatana na Riwaya Zangu” anaafiki mabadiliko haya anaposema kuwa katika *Asali Chungu* na *Utengano* alifanya makosa ambayo ameyarekebisha katika riwaya za baadaye kama *Dunia Mti Mkavu* na *Kiza Katika Nuru* kutokana na ubinadamu na uanagenzi. Hii inaashiria mabadiliko kadri anavyokua ndivyo

anayopiga hatua kiutunzi jambo ambalo Mbatiah (1990) anakubaliana nalo na kusema kuwa S. A. Mohamed amepevuka sana katika matumizi ya nadharia ya Ki-Marx katika riwaya za baadaye kama *Kiza Katika Nuru* kuliko riwaya za awali kama *Asali Chungu*.

Msimamo wa mtafiti ni kuwa kadri S. A. Mohamed anapevuka kiusomi na kutembelea nchi tofauti ndivyo mawazo yake na itikadi zake zinaathirika kama vile matumizi ya mitindo ya uhalisia ajabu katika riwaya kama *Dunia Yao* (2006) na kuangazia maswala ya jamii pana kama teknolojia mpya kama matumizi ya tarakilishi na maswala mengine yanayoathiri dunia nzima kama inavyojitokeza katika *Mhanga Nafsi Yangu* (2012) ambapo kwa mfano baadhi ya wahusika kama Yakrobich ni Wajerumani.

Hii inaonyesha kuwa S. A. Mohamed ameathiriwa na kuiathiri jamii yake na hivyo itikadi yake haiwezi kuwa moja na tengamano katika vipindi tofauti vya utunzi wake. Hii ni kwa sababu itikadi ya mtunzi hubadilika ili kufungamana na mawazo yanayotawala katika kipindi fulani cha kihistoria katika jamii yake. Yafaa kazi zake ziwe faafu kwa jamii yake kwani yeye ni kama mwalimu anayeifunza jamii yake. Hivyo ni kusema kuwa historia ya mtunzi ikibadilika, kama inavyodhihirika katika maisha ya S. A. Mohamed, itikadi yake hubadilika na ikiwa itikadi ndio humuelekeza mtunzi kuchagua atakayowasilishia jamii na atakayoacha, ni dhahiri kwamba mitazamo yake kuhusu maswala mbalimbali hubadilika katika mapito ya wakati. Hivyo mtazamo wa mtunzi si mmoja na tengemano bali hubadilika kadri historia yake inavyobadilika.

4.3 HISTORIA YA SIASA NA UCHUMI WA ZANZIBAR

Swala la historia na siasa na uchumi ni muhimu kwani daima kuna ufungamano wa itikadi na hali halisi ya kisiasa na kiuchumi kwa kipindi fulani kwa sababu itikadi hufungamana na siasa na uchumi (Chuachua 2011:24). Hii ina maana kuwa, pindi mifumo ya kisiasa na kiuchumi inavyobadilika katika vipindi maalumu nayo itikadi hubadilika na hivyo kuathiri kwa kiwango kikubwa uandishi wa mtunzi. Ni katika muktadha huu ambapo tutajadili swala la historia na uchumi wa Zanzibar ambapo tunaamini swala la itikadi linaweza kujadiliwa vyema na kudhihirika kwa uwazi.

4.3.1 KIPINDI KABLA YA UKOLONI

Kwa mujibu wa Njogu (1997) katika *Uhakiki wa Riwaya za Visiwani* makaazi ya mwanzo visiwani yalitokana na uhamiaji wa makundi kutoka bara katika nyakati tofauti na yakawa na umoja wa kisiasa ambao ungeyafanya yaweze kukabiliana na taifa lolote la kigeni ambalo lingetishia kuvuruga umoja huo. Kufikia 500 kabla ya Kristo wageni wengi kama Waajemi na Waarabu walikuwa wakifanya biashara na mataifa ya Kiafrika yaliyokuwa yakiishi mwambao wa Afrika Mashariki. Kufikia karne ya kumi na moja, kundi la Waajemi lilikuja na utamaduni wao kukubaliwa na wenyeji wa Pemba na Unguja na hivyo walifungamana sana kiutamaduni na Waafrika. Jambo hili liliathiri utamaduni, lugha na siasa za visiwani.

Kiuchumi, miji ya visiwani ilikua na kuimarika sana kutokana na biashara kati ya wageni hawa na wenyeji wabantu waliokuwa wakizungumza lugha ya Kiswahili. Lugha hii iliimarika zaidi kutokana na maingiliano haya ambapo maneno ya lugha nyinginezo kama Kiarabu, Kihindi, Kiajemi kati ya nyinginezo yaliingizwa kweye lugha ya Kiswahili. Wageni hawa walichagua kulowela huko baada ya shughuli zao za kibiashara na hivyo kuifanya Zanzibar kuwa kitovu na kivutio kikubwa cha biashara na hivyo kwa sababu ya umaarufu huo mataifa ya Ulaya yalivutiwa sana na Wareno wakachukua hatamu za uongozi mnamo 1503 Baada ya Kristo na kutawaliwa na Kapteni Ruy Lourenco Ravasco Marques. Wareno walitawala kwa muda mrefu hadi miaka ya karne ya 1648 Baaada ya Kristo ambapo utawala wa Kisultan wa Oman ulikita mizizi na kuchukua hatamu za uongozi, visiwa hivi vikiwa vimeimarika kiuchumi, kitamaduni na hata wakiwa na lugha walioizungumza ya Kiswahili ilioenea sana kutokana na biashara na maingiliano na wageni hawa walioamua kulowela huko na kukufanya kwao kabisa.

4.3.2 KIPINDI CHA UKOLONI WA WAARABU NA WAINGEREZA

Ukoloni wa Kiarabu visiwani Zanzibar ulikuja pamoja na mfumko wa viwanda katika nchi za Ulaya. Malighafi nyingi zilihitaajika na watumwa walinunuliwa kutoka visiwani na kusafirishwa hadi Ulaya na Bara Hindi ili kufanya kazi viwandani. Zanzibar ni sehemu ya Mwambao wa Afrika Mashariki, ilikuwa na bandari nzuri na mikarafuu ilikua vyema jambo lililoifanya kituo kikubwa cha kibiashara na kivutio kwa wengi tena salama. Mnamo mwaka wa 1741 familia ya Mazrui ilifanya mkataba na utawala wa Oman. Mohammed Uthman Al-Mazrui alikataa kuukubali utawala wa Busaidi. Jambo

hili lilisababisha Busaidi kujiimarisha Zanzibar ili kuifanya kituo cha kibiashara na vilevile kituo cha kiutawala (Njogu 1997).

Mnamo 1804 Seyyid Said alichukua hatamu za uongozi baada ya kumuua binamu wa babake Bader Bin Seif. Ili kuimarisha utawala wake alifanya Zanzibar kuwa mji mkuu na akahamia huko pamoja na wafuasi wake mnamo mwaka wa 1832, hali iliyofanya Waomani wengi kuhamia Zanzibar. Chini ya utawala wa Seyyid Said, Zanzibar ilikua kwa haraka kama kituo cha kibiashara kati ya Waarabu na nchi za Marekani na Ulaya.

Aidha, alianzisha ukulima wa mikarafuu ambayo ilikuwa na soko katika nchi nyingi hivyo mashamba makubwa yalihatijika ili kuendeleza kilimo cha mikarafuu ambayo ilikuwa na faida kubwa. Tatizo ni kwamba mashamba makubwa yalipewa Waarabu waliopata wafanyakazi kwa nguvu kutoka visiwani na bara. Waafrika wenyeji wakanyimwa ardhi yenye rutuba na wakawa watwana na watumwa. Kwa upande wao, Waarabu waliendelea kujilimbikizia mali nyingi na kuwa matajiri wakubwa huku Waafrika wengi wakawa wakata na makabwela hohe hahe. Kutokana na haya, Wahindi wengi walihamia Zanzibar na kuanza kufanya biashara ya kusafirisha karafuu kutoka visiwani hadi Bara Hindi.

Mnamo mwaka wa 1884-1885, kongamano la Berlin liliandaliwa na kuigawa Afrika ili kuendeleza utawala wa kibepari. Waingereza walijikita visiwani ambapo mkataba ulifanywa mnamo Julai 1, 1890 na Zanzibar iliwekwa chini ya Himaya yao. Ukoloni

uliimarisha muundo wa kitabaka uliokuwepo na kuuendeleza hata zaidi. Sultan wa Zanzibar alitia saini mkataba Aprili 5, 1897 ambao uliwapa watumwa haki na uhuru wa kupeleka mahakamani maombi ya kupewa uhuru. Watumwa hawa walipewa visehemu vidogo vya shamba na iliwalazimu wakodishe na kufanya kazi kwa mamwinyi hao. Wale ambao hawakuweza jambo hili walibakia makabwela wa ulimwengu katika ardhi yao wenyewe.

Waingereza waliwapa Waarabu nafasi kubwa lakini pale biashara ya karafuu ilipoathiriwa Wahindi walianza kuchukua mashamba ya mamwinyi walioshindwa kulipa mikopo waliokuwa wamekopa. Hali hii ilisababisha kuibuka kwa makundi manne kutokana na mivutano na mikinzano hii. Makundi hayo yaliyoibuka ni ya Waingereza na Wahindi walioendesha viwanda na biashara, Waarabu waliomiliki mashamba, huku Waafrika wakiwa wafanyakazi.

Hii ilimaanisha kuwa rangi ya mtu ilimwelekeza katika tabaka fulani. Hivyo jamii ya visiwani ikawa ya miundo ya kitabaka hasa kutegemea rangi ya mtu. Nafasi za kiuchumi zikanasibishwa na sura ya kimaumbile. Nafasi za elimu na kazi za juu zilitolewa kwa Waarabu, Wahindi na Waingereza nao Waafrika walifanya kazi za sulubu. Akifafanua historia ya Zanzibar, Mukobwa (1985) anasema kuwa kufikia mwisho wa karne ya kumi na tisa Zanzibar ilikuwa imekaliwa na masetla wa Kiarabu ambao walimiliki uchumi na siasa za Zanzibar. Waafrika waliachwa wakiwa maskini kwani njia za kiuchumi

zilizimilikiwa na Waarabu na Wazungu. Wahindi walipokuja pia waliendelea kujiendeleza kiuchumi na waliajiriwa katika kazi nzuri na Waafrika walidharauliwa sana.

Mnamo 1890, serikali ya Uingereza iliweka mkataba na Sultan wa Zanzibar na kuifanya Zanzibar iwe chini ya himaya yake. Hata baada ya mkataba huu, Waarabu na Wahindi waliendelea kupewa kazi kubwa na vyeo, huku Waafrika wakibaguliwa. Mnamo miezi ya Januari (1961), Juni (1961) na Julai (1963) Chama Cha Afro-Shirazi Party (ASP) kilikuwa kikishinda uchaguzi wa kidemokrasia kwa sababu kilikuwa na Waafrika wengi na jambo hili lingemaanisha uwezo wa kiuchumi wa mabepari wa Uingereza na Kiarabu kupunguzwa.

Vyama ambavyo vilikubaliwa kuunda serikali ni Zanzibar na Pemba Peoples Party ambacho kilijiunga na Zanzibar National Party (ZNP) na kuunda muungano na kuwa na viti kumi na vinane dhidi ya Afro-Shirazi Party (ASP) ambacho kilikuwa na viti kumi na vitatu (Njogu 1997). Uhuru huu haukufurahiwa na Waafrika wengi ambapo Mohammed Shemte aliunda serikali. Nafasi za utawala na za kiuchumi zilitwaliwa na kupewa Waarabu ambao walikuwa waaminifu kwa Sultan.

Mapinduzi yakawa ni ya lazima ili Waafrika waweze kujikomboa na yalitokea mnamo Januari 12, 1964 kwa sababu Waafrika waliokuwa wengi walinyimwa nafasi ya kuendeleza mfumo wa kiuchumi ambao ungewafaa. Hussein Ebrahim katika utangulizi wa Tamthilia ya *Mashetani* (1971) anasema kuwa mapinduzi ya Zanzibar yalibadilisha

maisha ya watu binafsi na jamii za watu. Serikali ya Sultan wa Zanzibar ilipopinduliwa na Afro-Shirazi Party kuchukua mamlaka, mashamba makubwa yalitaifishwa na kufanywa mali ya umma. Watu wengi waliopoteza mali yao walitorokea miji ya pwani ya Afrika Mashariki kama Dar es Salaam na Mombasa. Kwa sababu wengi wao walikuwa na elimu walipewa vyeo katika serikali ya Tanganyika ambapo waliendeleza ukoloni baada ya kurithi vyeo na mienendo iliyoachwa na wakoloni. Kile kisichotarajiwa kilifanywa kuwa kaida na kaida zikasailiwa na kupinduliwa.

Waliokuwa matajiri baada ya mapinduzi walikuwa masikini na maskini wakaanza kupanda kiuchumi baada ya mapinduzi haya. Ni kama kuna kinyume mbele; mambo kubadilika walio juu wakawa wanaelekea chini na walio chini wakawa wanaelekea juu kiuchumi. Mapinduzi haya yaliongozwa na John Okelo (Lofchie, 1965) ambapo aliunda serikali iliyowapa mamlaka viongozi wa Chama Cha UMMA na wale wa ASP (Afro-Shirazi Party).

4.3.4. KIPINDI CHA MUUNGANO 1964 NA KUENDELEA

Baada ya muungano wa Zanzibar na Tanganyika mnamo mwezi wa April 1964 viongozi wenye siasa kali kama vile Okelo waliondolewa serikalini ili kuweza kurahisisha utawala. Kwa upande wa Tanganyika, serikali ya Nyerere ilikuwa ikifanya juhudi za kuvunja taasisi za kibepari kwa kupendekeza mfumo wa ujamaa. Majukumu ya kisiasa na kiuchumi yalitekelezwa na itikadi ya ujamaa na kujitegemea. Mfumo huu ulipata changamoto nyingi kama vile kutoungwa mkono na mataifa ya kimagharibi na kutoshirikishwa kwa wananchi ipasavyo. Aidha, badala ya mali kuwa ya umma, viongozi

walimiliki mali kwa manufaa yao na kuendelea kutumia vyeo vyao kwa kujitajirisha. Wale viongozi ambao walikuwa wakishikilia nyadhifa za uongozi hapo mwanzoni walitorokea nchi zingine au Tanzania bara. Wale ambao walipata vyeo hivi waliendelea kujilimbikizia mali. Kwa sababu hii kukatokea mivutano baina ya waliokuwa navyo na wasiokuwa navyo. Wale waliotoroka wakaendelea kuanguka kiuchumi na kuporomoka kimaisha.

Mapinduzi yaliyodhamiria kuleta usawa hayakufanikiwa jambo ambalo linajenga msingi wa wasanii wengi visiwani Zanzibar akiwemo S. A. Mohamed ambaye anajadili mivutano ya kiuchumi na kisiasa kihalisia na uhalisia wa kijamaa katika kazi zake za awali hasa *Asali Chungu*, *Dunia Mti Mkavu* na *Kiza Katika Nuru* kati ya nyinginezo. Ameonyesha vile uhuru ule Waafrika waliopata ni wa bendera tu huku wakiendelea kutawaliwa kisiasa na kiuchumi. Kwa ujumla ameonyesha kuwa ili kujikomboa ni muhimu kuchosha ubongo kwa kutafakari na kufikiri ili kuweza kupata uhuru wa kweli kama vile Mvita anavyofanya katika *Kiza Katika Nuru*. Wakoloni pamoja na mifumo yote ya kiukoloni (ya kisiasa au kiuchumi) lazima ing'olewe.

Hata hivyo katika kazi zake za awali *Asali Chungu* na *Utengano* hajaweza kukuza misingi na nadharia thabiti za kimapinduzi, jambo ambalo anaonekana kuliimarisha zaidi katika *Dunia Mti Mkavu* na *Kiza Katika Nuru* kuashiria mabadiliko ya itikadi zake za utunzi na hivyo mtazamo wake kubadilika na kuonekana kuupinga mtazamo wake wa awali kwamba mapinduzi yanaweza kutokea ghafla na si lazima yawe yamejengeka

katika msingi maalum na nadharia thabiti. Katika *Asali Chungu* kwa mfano hamna maandalizi yoyote ya mapinduzi wala ujenzi wa urazini kati ya wanamapinduzi ni kama ni jambo la sadfa tu au bahati na kama anavyokiri katika makala ya “Kupatana na Riwaya Zangu” Mohamed (1984) aliimarika zaidi katika *Dunia Mti Mkavu* na *Kiza Katika Nuru* ambapo mapinduzi yanaandaliwa vyema na urazini kujengwa vyema kati ya wanamapinduzi. Mambo haya yanajadiliwa kwa kina katika sura zinazofuata ambapo mtafiti anaangazia kila riwaya na itikadi zinazojitokeza kwa mujibu wa maudhui, mtindo na wahusika waliosawiriwa.

4.4 MITAZAMO MBALIMBALI KUHUSU DHANA YA ITIKADI

Miongoni mwa wasomi wa mwanzo kutumia dhana ya itikadi ni Cabanis Destute de Tracy, mwanafalsafa wa kifaransa katika mwaka wa 1796 kumaanisha mfumo wa fikra fulani (Wamitila, 2008:41). Dhana hii ni changamano na imeleta mijadala mingi kati ya wasomi tofauti. Ni dhana ambayo ni telezi kuelezea kwa sababu ya sifa yake ya kuweza kufasiriwa kwa njia mbalimbali kutegemea malengo na dhamira ya yule anayeitumia (Chuachua, 2011). Kwa ujumla itikadi ni mfumo wa mawazo fulani ambayo ni misingi ya nadharia za mfumo wa utawala kama vile itikadi ya kihalisia, itikadi ya kijamaa, itikadi ya kibepari, itikadi ya kidini, itikadi ya kuumeni na kadhalika (Msokile, 1992).

Kwa mujibu wa utafiti huu, mtafiti atatumia itikadi kwa kuzingatia mikabala mitatu. Mikabala itakayotumiwa itajumuisha ule wa Karl Marx (1973) ambao unachukulia itikadi kama ung’amuzi potoshi, mkabala wa Louis Althusser (1981) unaoichukulia itikadi kuwa

jumla ya dhana za kitamaduni ambazo hutawala watawaliwa kupitia vyombo vya serikali na vya kiitikadi na mkabala wa Antonio Gramsci (1985) unaelezea itikadi kuwa ni mfumo wa mawazo ya tabaka tawala ambayo huendelezwa kwa ukubalifu na ukawaida.

Kwa hivyo, itikadi ni jumla ya mfumo wa mawazo, fikra na imani, inayoongoza na kumwelekeza mtunzi katika kuwasilisha ulimwengu wake kwa maswala mbalimbali ya kisiasa, kiuchumi na kijamii. Ni imani inayojitokeza katika mfumo wa kisiasa, kijamii na kiuchumi (Wanyonyi, 2011). Itikadi ndio humuongoza mtunzi kuteua atatekeleza majukumu yake ya kisiasa, kiuchumi na kijamii kwa namna gani na ataacha mambo yapi na atazungumzia yapi. Mawazo haya yameshadidiwa na Chuachua (2011) asemaye kuwa itikadi ndiyo dira ituelekezayo kwenye sababu za mtunzi kupendekeza au kukemea jambo fulani. Aidha, itikadi ndio hutuonyesha namna mtunzi ametekeleza mafunzo yake, dhamira na falsafa yake na hivyo kuathiri kwa kiwango kikubwa uandishi wa mtunzi.

Hegel, 1977) anasema kwamba itikadi ni jumla ya maoni ya mtu kuhusu ulimwengu wake anaoishi. Mawazo haya huweza kubadilika vile muda unavyoendelea kupita na kufikia ulimwengu wa kiroho. Kwa hivyo itikadi huelekeza mtu kutenda anayotenda bila hata kujua ni kwa nini anavyotenda vile. Aidha, historia ndio humkuza binadamu na kumfanya atelekeze majukumu yake ulimwenguni. Fikra ambayo humuelekeza binadamu kwenye Mungu ndio muhimu na hubadilika kadiri historia inapoendelea. Jukumu la mwanadamu ni kujaribu kuelewa hali hizi ambazo huelezeka tu na wanafalsafa.

Anafafanua kwamba itikadi ni jumla ya fikra ambazo hujumuisha malengo, matarajio na matendo ya mtu. Ni mtazamo wa kiulimwengu wa mtu ambao humuongoza kutenda anayotenda. Fikra hizi kwa mujibu wa Hegel (1977) ni matokeo ya mabadiliko ya wakati na kubadilika kiroho hadi kufikia kiwango cha uhuru wa fikra. Kwa hivyo, muda unavyosonga ndivyo mawazo na mitazamo ya mwanadamu hubadilika ili kuufikia au kuukaribia uungu au mawazo ya kupevuka kiroho na kupata uhuru wa fikra. Mwanadamu hupaswa kutumia mawazo au fikra zake kujaribu kuelewa jamii yake, utamaduni wake, sheria na maadili.

Katika mapito ya wakati, imani zake na fikra zake hubadilika ili kuufikia uungu au ulimwengu wa kiroho. Maelezo haya kuhusu itikadi yanaonyesha kuwa ikiwa vile ambavyo muda unavyosonga ndivyo mawazo na mitazamo ya mwanadamu hubadilika basi itikadi nayo hubadilika na kwa hivyo mtazamo wa mtunzi hauna budi kubadilika. Hii ni kutokana na dhana kuwa itikadi ndiyo humuelekeza mtunzi hivyo kuuelekeza ule mtazamo wake na namna atakavyowasilisha ulimwengu wake kwa jamii lengwa, jambo ambalo linajitokeza katika riwaya za S. A. Mohamed.

Marx (1977) anasema kwamba, itikadi ni fikra zote ambazo msingi wake ni mfumo wa uzalishaji mali na teknolojia. Hujumuisha maoni ya binadamu kuhusu anayoyasema na anayoyafikiria kuhusu siasa, sheria, maadili, dini na falsafa. Mawazo hayo hugeuka pindi mfumo huu unavyobadilika hivyo itikadi na jamii huendelea kubadilika. Itikadi ndiyo ambayo hueleza na kuhalalisha mfumo wa siasa na kiuchumi wa jamii. Aliona itikadi

kama ung'amuzi potoshi, yaani imani ya uongo kwa kiasi fulani. Anafafanua itikadi ya kidini ambayo hutumiwa na mifumo ya kibepari na ukabaila kuwafanya watu waamini viongozi humwakilisha Mungu, kila kitu kimepangwa na Mungu na kila mtu ana nafasi ambayo Mungu amemratibia. Hivyo kuwa tajiri ni mpango wa Mungu na kuwa masikini ni mpango wa Mungu. Kwa hivyo, itikadi ni mawazo, mafunzo na malengo ya mtunzi yanayosawiri utekelezaji wa majukumu kiuchumi na kisiasa katika jamii husika. Dhana hii inajitokeza katika riwaya za S. A. Mohamed kama vile *Asali Chungu* na *Utengano*, ambapo wahusika kama vile Zuberi na Maksudi wanaona kuwa ni mpango wa Mungu wao kuwa matajiri na mabwanyenye nao kina Semeni, Dude, Sulubu na Kabi kuendelea kuwa masikini.

Marx (1979) anasema historia ya jamii zote ni mapambano ya matabaka mbalimbali. Anasema kuna uhusiano baina ya fasihi na uzalishaji mali kwa vile mapinduzi yanapofanyika na kufaulu mfumo wa uzalishaji mali hubadilika na taasisi zote za kitamaduni huchukua mkondo mwingine. Anasema kwamba wanadamu daima huwa katika harakati za kuifanya hali yao kuwa bora zaidi na ili mapinduzi yafanyike huwa na hatua tatu za kihistoria. Hatua hizi ni ishitiraki ambapo wanadamu waliishi kwa pamoja na kufaidi jamii. Hatua ya biashara ndogondogo iliyoendeleza na kukuza tabaka la wafanyakazi na baadaye mfumo wa kibwanyenye na kibeberu uliotokana na dhuluma za wafanyakazi kwa malengo ya mabepari wenyewe. Mfumo huu ukaleta makabiliano ya kitabaka hivyo kuleta mapinduzi na kuendeleza mfumo wa kijamaa unaoleta usawa wa binadamu wote. Kwake Marx, itikadi ambazo huangazia mambo ya kidini na kiroho ni za

kupumbaza na hali halisi ya kiuchumi ndio yapaswa kuelekeza imani na fikra zote za kijamii.

Mawazo ya Hegel (1977) na Marx (1973 na 1979) yana uhusiano katika kuonyesha kuwa daima jamii hubadilika na hivyo jamii ikibadilika fasihi yao hubadilika na misimamo yao kuhusu jamii hubadilika. Hata hivyo Hegel (1977) anaona kuwa mabadiliko haya hutokana na ukuaji wa kiakili na kiroho kwa mtu binafsi kihistoria . Kwa upande wa Marx mfumo wa kiuchumi ndio huwa msingi wa mabadiliko hayo wala si mtu binafsi ama akili. Kwa hivyo itikadi husukumwa zaidi na mabadiliko ya kiroho na kiakili kwa mujibu wa Hegel ilhali kwa mujibu wa Marx mfumo ya uzalishaji mali ndizo huendeleza itikadi. Tunapomwangazia mtunzi S. A. Mohamed, kazi zake nyingi kama Mbatia (1990) anavyosema zinasawiri mazingira halisi ya jamii yake na msimamo wake mkali wa kiitikadi umemfanya ajirudie sana katika itikadi zake za kijamaa. Maoni ya mtafiti ni kuwa mwandishi huiathiri jamii na fasihi kutokana na kule kukua kiakili na kiroho na pia huathiriwa na mazingira mfumo wa kiuchumi ukiwepo na hivyo kukubaliana na Mohamed (1995) kwamba mwanadamu anaishi maisha ya kuathiri na kuathiriwa na hivyo fasihi ni tokeo la taathira baina mwanadamu na mwanadamu mwenzake. Hivyo ni kusema kuwa itikadi ya mtunzi huathiriana na itikadi za jamii. Nazo itikadi za jamii huathiriana na za mtunzi kwani mtunzi ni sehemu ya jamii na maisha ya jamii humuathiri katika utunzi. Basi itikadi zinazojitokeza katika kazi zake ni matokeo ya taathira za jamii na yeye binafsi.

Stoika (1972) amejadili itikadi na majukumu yake katika ujenzi wa taifa hasa akiangazia Wilaya ya Shinyanga nchini Tanzania. Anasema kwamba itikadi mara nyingi hujitokeza wakati wa migongano ya kijamii au vita na huweza kubadilika na kufafanuliwa upya ili kuafikiana na malengo na matakwa ya wakati huo. Kwa mujibu wake mabadiliko ya itikadi za kisiasa na kiuchumi huenda yasilete mabadiliko ya kimsingi kule mashinani ili kubadilisha mielekeo na imani za watu katika juhudi za kuleta ujenzi wa taifa.

Maelezo haya yanaafikiana na mtazamo wa Karl Marx kwamba itikadi ni ung'amuzi potoshi. Hivi ni kusema kuwa licha ya tabaka tawala kudai kuwa hutawala kwa maslahi ya makabwela, huendeleza imani kwamba hali za makabwela zimesababishwa na Mungu na hivyo wao huendelea kuhifadhi nyadhifa zao za kiuchumi na kisiasa. Basi makabwela huendelea kuishi katika hali ya umasikini na hivyo hata ufafanuzi mpya ufanywe, lengo huwa si kubadilisha hali bali kuhifadhi nyadhifa zao na hali ilivyo na ndio mabadiliko ya kweli ni muhali kupatikana. Ni maoni ya mtafiti kuwa itikadi ni dhana badilifu; hali za kijamii zikibadilika nayo itikadi hubadilika ili kuwafaa watawala na jamii ya wakati huo. Hivyo mapinduzi hata yakifanyika kama S. A. Mohamed anavyoonyesha katika kazi zake, ni muhali hali ya makabwela kuwa bora kuliko ilivyokuwa. Kwa vile itikadi ndio hufumbata ule mtazamo wa mtunzi basi mtazamo na msimamo wake hubadilika ili kuafiki mabadiliko yaliyotokea. Kwa mfano, Tanganyika ilipoupata uhuru wake mnamo mwaka wa 1961, iliungana na Jamhuri ya Zanzibar na kuunda Tanzania ikiongozwa na Mwalimu Julius Nyerere. Ilianza kuubadilisha mfumo wa utawala kutoka mfumo wa ubepari uliokuwa ukiendelezwa na Waingereza na kutekeleza mfumo wa ujamaa.

Wasanii wengi akiwepo S. A. Mohamed wanaonyesha hali hizi katika kazi zao hasa kuonyesha namna viongozi hawa wa Kiafrika walivyoendelea kujilimbikizia mali kama akina Zuberi na Maksuudi na kuwadhulumu wananchi kama Zuberi anavyomfanyia Semeni katika *Asali Chungu* na Maksuudi anavyomnyang'anya Mwanasururu mali yake katika *Utengano* na hawachukuliwi hatua zozote. Mtazamo huu wa Marx unaungwa mkono na Lorraine (1979) kwamba itikadi ni imani ya uongo ambayo huendelezwa na tabaka tawala au la juu ili kuendelea kuhifadhi malengo na matamania yao ya kibinafsi. Kwa mujibu wake, itikadi za kidini na kibeberu hutumiwa kuendeleza malengo ya tabaka la juu ya kudumisha hali yao nzuri ya kimaisha.

Eagleton (1976) anasema kuwa itikadi ni fikra, amali na hisia ambazo mwanadamu hupitia katika jamii yake kwa kipindi maalum na huweza kupatikana tu kupitia fasihi. Kuelewa itikadi ni kuelewa historia ya yaliyopita na yale ya sasa kwa undani zaidi ambayo husababisha kuzinduka na kujikomboa. Kila kazi ya sanaa huchipuka kutokana na mtazamo maalum wa kiitikadi na jinsi mtunzi anavyouona ulimwengu.

Fasihi ni itikadi ambazo zimeelezwa kwa kutumia lugha na mbinu za sanaa wakati wa utunzi. Kwa sababu itikadi huwa na miundo na mipangilio maalum inaweza kuchanganuliwa kisayansi. Kazi za kisanaa zinapoendelea kimuundo ndivyo ambavyo kuna mabadiliko ya itikadi kuonyesha njia mpya za kuangalia uhalisia wa ulimwengu na kuuchanganua kati ya mtunzi na hadhira yake. Aidha, lugha na mbinu za kisanaa ambazo

mtunzi hutumia huwa zimejikita katika itikadi fulani za kijamii na katika ufasiri wake huweza kubadilika au kutobadilisha kutegemea historia ya wakati wake.

Kwa ujumla fasihi ni sanaa ambayo hujumlisha uhalisia wa yaliyokuwapo, yaliyopo na yaliyo na uwezekano wa kutokea. Hii inadhihirisha kuwa daima kuna ufungamano baina ya mtunzi na itikadi, ikizingatiwa kuwa mwanadamu mwenyewe ndiye muumba wa kazi ya fasihi (Mohamed, 1995), basi kazi za kisanaa kuendelea kimuundo ni zao la kubadilika kwa itikadi ya mtunzi. Kwa hivyo kadri itikadi zinavyobadilika na kwa sababu itikadi ndio huelekeza matendo yote ya binadamu ulimwenguni (Rossiland 1990) ndivyo mtazamo wa mtunzi kuhusu maswala ya kijamii utakavyobadilika kwa sababu mtazamo wa mtunzi huwa umefumbatwa katika ile itikadi yake inayojidhihirisha katika matendo yake. Jambo hili ni kweli kwani tunapochunguza kazi za S. A. Mohamed, kuna mabadiliko mengi kwa upande wa uwasilishaji wake kama vile katika *Asali Chungu* na *Kiza Katika Nuru* kuna hali za kiyakinifu zaidi kwa kuwasilisha wahusika kitabaka na wanaomkaribia binadamu wa kawaida kinyume na kazi kama vile *Dunia Yao* na *Babu Alipofufuka* zimejengeka katika misingi ya uhalisiaajabu na wahusika ni wa kifantasia.

Mhakiki Mwenda Mbatiah katika mahojiano katika Chuo Kikuu cha Nairobi tarehe 11/10/2015 anaafiki kuwa S. A. Mohamed amebadilisha mitindo yake ya kiutunzi kutoka mitindo ya kiyakinifu katika riwaya za awali hadi mitindo ya kinjozi katika riwaya za baadaye. Maoni haya ya Mbatiah yanaoana na ya wahakiki wengine tuliowahoji. Wahakiki hao ni Prof. Rayya Timammy na Dkt. Evans Mbuthia kutoka Chuo Kikuu cha

Nairobi, Prof. Mwenda Mukuthuria wa Chuo Kikuu cha Mount Kenya, Prof. Catherine Ndungo na Dkt. Timothy Arege wa Chuo Kikuu cha Kenyatta. Aidha, katika mahojiano na mtunzi S.A Mohamed anaafiki kuwa riwaya za *Dunia Yao na Mhanga Nafsi Yangu* zinajadili maswala ya utandawazi na wahusika wake ni wa kifantasia ilhali wahusika katika riwaya za *Asali Chungu* na *Kiza Katika Nuru* ni wa kihalisia na wamesawiriwa kitabaka. Ni kauli ya mtafiti kuwa itikadi ndio huelekeza matendo yote ya binadamu na hivyo maudhui ya utandawazi yanayojitokeza katika riwaya za baadaye za S. A. Mohamed na usawiri wa wahusika wa kifantasia ni ishara ya mabadiliko ya kiitikadi.

Mtazamo wa Shule ya Frankfurt kuhusu itikadi pia ni muhimu katika kazi hii. Waitifaki wakuu wa shule hii ni Theodor Adornno, Herbat Mercuse na Max Hokheimer. Shule hii ilianza huko Frankfurt mwaka wa 1923 na kuhamishwa hadi NewYork mnamo mwaka wa 1933. Waliendeleza nadharia ya uchanganuzi na kusema kuwa binadamu ni kiumbe aliye huru kifikra na ana utu na ubinadamu. Anaweza kuamua hatima yake na historia ya jamii yake. Kwa hivyo, jambo la muhimu ni kuchukua itikadi ya jamii na kuilinganisha na uhalisia unaodhihirika ili kujenga jamii yenye usawa. Itikadi kama vile uhuru wa mtu binafsi na soko huru inaweza kulinganishwa na uhalisia uliopo katika jamii hiyo kama vile unyanyasaji na ukosefu wa usawa wa binadamu na kutumia ule uwezo wa fikra huru na utu kujenga jamii yenye usawa. Mkabala huu kuhusu itikadi unaleta dhana kwamba itikadi hufungamana na jamii. Naye mtunzi huangalia itikadi iliyopo ama inayotawala katika jamii na akailinganisha na uhalisia kisha kusema yanayodhihirika kwa lengo la kujenga jamii yenye usawa.

Hivyo, itikadi huathiri ule mtazamo wa mwandishi kwani ndio dira inayomwongoza katika kuchagua maudhui atakayowasilisha, mbinu atakazotumia katika uwasilishaji wake, namna atakavyosawiri wahusika wake na malengo yake katika kazi yake yote hivyo huathiri uandishi wake wote. Tukiangazia mtunzi, S. A. Mohamed anachukua itikadi ya ujamaa iliyokuwa ikitawala katika vipindi vya mwanzo vya utunzi wake miaka ya sabini na themanini na kuilinganisha na uhalisia uliopo, kwamba licha ya itikadi ya ujamaa kupendekeza usawa na utaifishaji wa mali, viongozi waliendelea kujilimbikizia mali nao wananchi wengi wakabakia masikini. Ndiposa anamulika hali hii katika *Asali Chungu* na *Kiza Katika Nuru* na kupendekeza mapinduzi ili kuleta usawa wa kijamii. Hii inaonyesha kuwa itikadi inayotawala kwa kipindi fulani humwathiri mtunzi na mtazamo wake kuhusu jamii kwani yeye huwa ni sehemu ya jamii hiyo.

Althusser (1981) katika *Ideology and Ideological Apparatuses* anaendeleza dhana ya itikadi na kusema kuwa ili kuendeleza utawala na udhibiti, serikali au watawala hutumia vyombo viwili muhimu. Kuna vyombo ambavyo huendeleza utawala na udhibiti moja kwa moja kama vile wakuu wa serikali, jeshi, polisi, magereza na mahakama kati ya vinginevyo ambavyo huendeleza udhibiti moja kwa moja.

Vyombo hivi hutekeleza majukumu yao moja kwa moja hivi kwamba matakwa ya tabaka tawala hulindwa na kuhifadhiwa na kwa hivyo itikadi si ung'amuzi potoshi bali huendelezwa kwa matumizi ya nguvu. Anafafanua kwamba vyombo vya kiitikadi kama

kanisa, shule, vyombo vya habari, siasa, familia, sheria, vyama vya wafanyakazi na utamaduni pia hutumiwa kuendeleza itikadi ya tabaka tawala. Vyombo vya kiitikadi kama vile siasa hutumiwa kutawala. Kwa mfano utaifa, soko huria, ujamaa, demokrasia na kadhalika hutumiwa kuhifadhi hadhi ya tabaka tawala. Anasema kuwa dini ilitumika zaidi kabla ya mfumo wa kibepari kuendeleza itikadi na mawazo ya tabaka tawala.

Elimu ni chombo ambacho hutumiwa na mfumo wa kibepari ambapo kila mtu huwa na itikadi inayomuandaa kwa majukumu atakayotekeleza katika jamii yenye utabaka kama wanaonyanyaswa, mshirika wa unyanyasaji, mwendelezaji wa itikadi za tabaka tawala kitaaluma na kadhalika. Watawala huweza kudhibiti watawaliwa kwa nguvu au kwa ukubalifu wao na kwa hivyo itikadi huendelezwa ambapo kila mtu huwa ameandaliwa kwa wajibu wake katika jamii ya kitabaka hasa kupitia shule. Itikadi ambayo huendelezwa ni ya kuhifadhi hali kama ilivyo, yaani maslahi ya watawala huendelea kudumishwa kwa matumizi ya nguvu na mamlaka au kwa kutumia vyombo vya kuendeleza itikadi. Kwa ujumla wake Althusser anapinga mkabala wa Marx kwamba itikadi ni ung'amuzi potoshi kila mara na kuiendeleza dhana hii kwamba imani na mielekeo ya wanadamu yaweza kutokana na matumizi ya nguvu na udhibiti wa serikali na vyombo vya kiitikadi vinavyodhibitiwa na tabaka tawala ili kuhifadhi na kuendeleza maslahi yao.

Ni msimamo wa mtafiti kuwa katika kazi za S. A. Mohamed anazozitafiti, kuna dhana za ung'amuzi potoshi kama katika *Asali Chungu* ambapo wahusika kama Zuberi wanajificha

katika dini huku wakitenda maovu. Kisha katika *Kiza Katika Nuru* wahusika kama Bwan Juba wanafanya maovu na kujificha katika dini na kuendeleza maovu kiasi kwamba jamii zao zinachukua muda mrefu kuzinduka na kuelewa ukweli. Aidha, matumizi ya vyombo vya kiitikadi kama vile vyombo vya habari kutumiwa kueneza uongo katika *Kiza katika Nuru* na pia kuna matumizi ya nguvu kama mauaji ya Mvita aliyekuwa kiongozi wa ukombozi na kufungwa jela kwa Salma mchumba wake. Hili linadhihirisha kuwa mikabala ya Karl Marx na Althusser kuhusu itikadi inajitokeza katika riwaya za S. A. Mohamed na hivyo itikadi ni dhana changamano zaidi.

Gramsci (1985) anafafanua dhana ya itikadi kuendeleza dhana ya ukubalifu na ukawaida. Anasema itikadi hupata nguvu zake kutokana na dhana ya ukubalifu kinyume na matumizi ya nguvu. Jamii huendelea kuwa na umoja na udhibiti huendelezwa kwa nguvu na mamlaka kama vile polisi na jeshi au kwa vigeu vingine kama jinsia, rangi, kabila na utamaduni.

Hali hizi huchukuliwa kwamba ni za kawaida au za kimaumbile na kwa hivyo wanaonyanyaswa huenda hata wasijue wananyanyaswa. Jamii huendeleza itikadi hizi kwa mifumo ya kiutawala kama vile mfumo wa kuumeni, makabila tawala na tawaliwa. Itikadi ni mawazo au fikra za kiutawala ambazo huleta uhusiano na umoja wa jamii kimahusiano. Ukubalifu na ukawaida huleta udhibiti wa tabaka tawala dhidi ya watawaliwa na ni muhali kutupilia mbali nguvu zinazochangia ukubalifu na ukawaida katika jamii. Hili linaonyesha kuwa itikadi huendelezwa na ukubalifu na jukumu la

mtunzi na mhakiki ni kuhakiki nguvu hizi za udhibiti na njia ambazo nguvu za kisiasa zina mamlaka ya ukawaida na ukubalifu huu. Hufanya hivi kwa lengo la kutupilia mbali nguvu hizi, vikundi hivi, na mawazo haya ili kubadilisha ukubalifu na ukawaida uliopo.

Mambo yanayochukuliwa kama ya kawaida kwa jamii ni matokeo ya itikadi za tabaka tawala yaliyopenyezwa kwa vyombo vya itikadi zinazopendwa kama vile dini, shule, tamaduni na mashirika ya kijamii na kuendelezwa kwa mambo kama vile mifumo ya kuumeni, mahusiano ya kijinsia, makabila tawala na kadhalika na yanakubalika tu kama mambo ya kawaida yaani mambo yako hivyo kwani ndivyo yanavyopaswa kuwa. Maoni ya mtafiti ni kuwa Gramsci (1985) anaafikiana na Althusser kuwa itikadi hutokana na ukubalifu lakini kinyume na Althusser aliyesema kuwa itikadi huendelezwa kwa vyombo mbalimbali, yeye anasema itikadi hutokana na ukawaida na ukubalifu yaani watu huzoea hali fulani kuwa namna fulani na kuchukulia kuwa hali hiyo hupaswa kuwa hivyo. Pale ambapo Karl Marx anaona itikadi ni ung'amuzi potoshi Gramsci anaona ni ukawaida na ukubalifu.

Bennet na Royle (2011) wakimnukuu Paul De Mann wanasema kuwa itikadi ni mchanganyiko wa lugha na uhalisia asilia, kauli ambayo wanasema inaiweka fasihi na sanaa katikati ya siasa. Wanamtaja Althusser (1981) akisema itikadi ni ndoto isiyo na ukweli wowote inayowakilisha fikra za wanadamu na uhalisia wa maisha yao. Wanasema kwamba jukumu kuu la sanaa ni kutusaidia kuona kile ambacho inaturuhusu kuona na kile hutulazimisha kuona na ndipo itikadi hutokea. Kwa hivyo itikadi ndiyo huelekeza

imani na fikra zote za wanadamu na huwawezesha kujitambulisha na kujiona katika ulimwengu wao.

Wanawanukuu Balibar na Machrey (1981) ambao wanasema kuwa kazi za kifasihi huleta dhana ya umoja ambayo ni ya kiitikadi. Uhakiki hupaswa kuzingatia migogoro na mikinzano inayojitokeza katika matini kwani matini za kifasihi hutoa suluhisho la kiitikadi zinazopingana. Uhakiki unapozingatia migongano na mikinzano hii pana uwezekano mkubwa wa kuleta mabadiliko. Kwa hivyo mtunzi yeyote huhitajika kuzingatia mazingira yake ya kijamii, kitamaduni kiuchumi na kisiasa katika utunzi wake. Nayo kazi kuu ya mhakiki ni kuchanganua itikadi ambazo huwa zimefichika katika matini.

Chuachua (2011) anasema kuwa itikadi ni dhana changamano ambayo ni telezi kuelezea kwani huweza kufasiriwa kwa namna mbalimbali. Anafafanua itikadi kama mawazo ambayo ni msingi wa nadharia za mfumo wa kisiasa au kiuchumi. Anasema kuwa Shaaban Robert amezingatia itikadi ya ujamaa uliopea kupitia mambo kama umoja na ushirikiano, mapinduzi ya kilimo, mapinduzi ya kisoshalisti na mikinzano ya kitabaka.

Anasema kuwa Shaaban Robert aliathiriwa na uandishi wakati wa ukoloni, harakati za ukombozi, migogoro kati ya Ulaya magharibi na mashariki, dini ya kiislamu na uchumi wa Tanzania. Anaeleza kuhusu kiu ya ulimwengu, utetezi wa mwanamke, kuwapo kwa matabaka na njia ya maadili, swala la mapinduzi, ugumu wa kufanya mapinduzi, udhaifu

wa wanadini, usafi wa roho na ulazima wa kutafuta ukweli. Anaonyesha namna itikadi iliathiri mtazamo wa Shaaban Robert hivi kwamba kadri itikadi za utawala zilivyobadilika ndivyo utunzi wake uliathirika. Hii inaonyesha kuwa kuna ufungamano mkubwa baina ya itikadi na mtazamo wa mtunzi. Itikadi za kijamii zikibadilika basi itikadi za mtunzi pia huathirika kwa kiasi kikubwa kwani binadamu huishi maisha ya kuathiriana. Hivyo mtazamo wa mtunzi kuhusu maswala ya kijamii na kisiasa huathirika kiasi cha kubadilika na huenda akapinga mtazamo wake wa awali kuhusu maswala hayo hayo.

Kwa mujibu wa utafiti huu itikadi ilitumiwa kumaanisha mfumo wa mawazo, fikra na imani inayomwongoza na kumwelekeza mtunzi katika kuwasilisha maswala mbalimbali ya kisiasa, kiuchumi na kijamii. Mfumo huu wa fikra, imani na mawazo unaweza kutokana na ung'amuzi potoshi kama Karl Marx anavyosema, vyombo vya kiitikadi na vya udhibiti na ukubalifu kama Althusser anavyosema au kutokana na ukubalifu na ukawaida kama Gramsci alivyokiri. Chambilecho Mohamed (1995) itikadi ndiyo humwongoza mwandishi kutazama kila kipenu cha maisha na kukitolea hukumu katika ufanisi na upungufu wake. Itikadi ndiyo humuelekeza mtunzi katika kuwasilisha dhamira yake, maudhui yake, usawiri wake wa wahusika na kwa hivyo huathiri mielekeo na mitazamo yake kuhusu maswala mbalimbali anayowasilisha na namna atakayoyawasilisha hivyo kuathiri utunzi wa kazi yake yote.

Daima kuna ufungamano mkubwa baina ya mtazamo wa mtunzi na itikadi anayoiaridhia katika kazi yake. Kwa hivyo ni msimamo wa mtafiti kuwa kila mwandishi huathiriwa na itikadi fulani inayomwongoza katika kazi yake nzima. Itikadi hii inaweza kuwa inatokana na mabadiliko ya mtu binafsi, inaweza kutokana na mfumo wa kiuchumi na mazingira ya kijamii au ikatokana na vyombo vya kiitikadi au ukubalifu na ukawaida. Hii ni kwa sababu itikadi ni dhana changamano na telezi na hubadilika kadri historia na mazingira yanavyobadilika katika kiwango cha mtu binafsi kama S. A. Mohamed na katika kiwango cha jamii. Jambo hili tumelijadili katika sehemu inayofuata kwa kina kuonyesha namna mazingira ya kisiasa na kijamii yanahusiana na itikadi na mtazamo wa mtunzi.

4.5 UHUSIANO WA ITIKADI NA MTAZAMO WA MTUNZI

Mohamed (1995) anasema kuwa itikadi ni mawazo ya jumla yanayomwongoza mtunzi kutazama kila kipenu cha maisha na kutoa uamuzi kuhusu kufanikiwa au kutofanikiwa kwake. Ni kweli kuwa kila mtunzi huathiriwa na itikadi fulani inayokuwa kama dira ya kwake kupimia mwendo wa maisha na kujibu maswali ya jamii. Itikadi hiyo ya mtunzi hufungamana na itikadi za jamii yake kwani mwanasanaa huishi katika jamii maalum. Kuna itikadi za kijamii kama vile itikadi za kihalisi, itikadi za uhalisia wa kijamaa, itikadi za kibepari, itikadi za mifumo ya kuumeni na kadhalika ambayo ni mawazo ya kijumla yanayoiongoza jamii kuafikia malengo yake. Itikadi za jamii zinaweza kutumiwa kuwaunganisha watu wa mataifa au makabila mbalimbali, kuongoza sera za nchi na utekelezaji wa ujenzi wa taifa nzima. Mofolou (1974) anasema kuna aina nne za itikadi za kijamii ambazo ni zile za kudumisha hali kama ilivyo, itikadi za kimapinduzi, itikadi

za kiroho na itikadi za kiutopia. Itikadi ambayo jamii hufuata huelekeza imani zao, matendo yao, siasa zao ,sera zao, uchumi wao, na mawazo yao kuhusu ulimwengu na namna ya kukabiliana na changamoto zinazowakabili. Akifafanua dhana ya itikadi, Mohamed (1995) anasema kuwa itikadi ya mtunzi hutegemea mambo kama mtunzi alizaliwa wapi, alikulia katika mazingira ya aina gani, ana imani ipi ya kidini na nafasi ya kiuchumi kati ya mengineyo. Anasema kuwa mwanadamu ndiye anayeiumba na kuiwasilisha kazi ya fasihi na ndiye anayeathiri na kuathiriwa na maisha na hivyo kuathiriana na wenzake. Hii inaonyesha kuwa mtunzi kama sehemu ya jamii yake huathirika sana na itikadi ambazo jamii yake inazingatia katika utunzi wake na hana budi kuzingatia itikadi za jamii yake katika utunzi wake ili kazi zake ziwe faafu kwa jamii lengwa. Hata hivyo yeye kama mwalimu wa jamii yake, huwa na jukumu la kuielimisha na hata anaweza kwenda kinyume na itikadi za jamii kama vile itikadi za kudumisha hali ilivyo na akaendeleza itikadi za kimapinduzi kama njia ya kuifunza na kuielimisha jamii yake.

Hii ina maana kuwa, mazingira ya mwanadamu yanapobadilika basi, itikadi zake huathiriwa na huenda zikabadilika. Itikadi ndiyo inayotumiwa na mtunzi kupimia yale atakayowasilisha na namna atakavyoyawasilisha katika kazi yake ya fasihi, basi mtazamo wake lazima ubadilike na huenda hata akapinga mtazamo wake wa awali kuhusu maswala fulani na kuyatazama upya, kuyawasilisha upya na hata kuyahakiki upya. Ikiwa jambo hili litawezekana ni dhahiri basi kuwa mtazamo wa mtunzi hauwezi ukawa mmoja

na ulioshikamana kwani hufumbatwa katika itikadi zinazobadilika. Kwa hivyo kadri itikadi zinavyobadilika ndivyo msimamo na mtazamo wa mtunzi hubadilika.

Njogu (1997) anaunga kauli hii mkono na kusema kuwa mtunzi huchagua atakalowasilisha kwa jamii yake kufungamana na msingi wa itikadi yake. Hivyo ni kwamba itikadi ndio humpambanulia mema na mabaya, yale yanayoisaidia jamii na yale ambayo ni potovu. Inavyodhihirika ni kwamba itikadi ndio huufumbata ule mtazamo wa mtunzi kuhusu maswala ya jamii hasa yale anayotaka kuyawasilisha. Tukichukulia kwamba maana za maneno na dhana ni telezi (Derrida, 1976) itikadi ni dhana inayobadilika kila uchao, itakuwa ni dhahiri kwamba nao msimamo wa mtunzi kuhusu maswala mbalimbali ya kijamii hauna budi kubadilika kwani itikadi ndio huongoza mtazamo wa mtunzi. Rossiland (1990) anavyosema, itikadi huelekeza matendo ya wanadamu wote. Hivyo ni kusema kuwa hata utunzi wa mwandishi huelekezwa na itikadi na hauna budi kubadilika kufungamana na mabadiliko ya itikadi.

Itikadi nayo hutegemea mambo kama vile mtunzi kazaliwa na nani, kasomea wapi, imani yake ya dini na ngazi yake kiuchumi kati ya mengineo na kadri mambo haya yanavyobadilika ndivyo itikadi yake huathiriwa na kubadilika na mtazamo wake kuhusu maswala fulani ya kijamii kubadilika. Tukichukulia kwamba mwanadamu ndiye muumba wa kazi ya fasihi, na fasihi inahusu binadamu na mazingira yake (Njogu, 2001) basi mtunzi huyaathiri maisha na kuathiriwa nayo na pia kuathiriwa na wanadamu wenzake. Hivyo ni kusema kuwa, kadri maisha yanavyobadilika na kuathiri nyanja tofauti za

maisha kama vile siasa, dini, utamaduni, elimu, uchumi na kadhalika ambayo ni baadhi ya mambo muhimu yanayojenga itikadi ya mtunzi, ndivyo ambavyo itikadi ya mtunzi huathiriwa na kubadilika. Kwa sababu itikadi ndio ambayo huelekeza ule mtazamo wa mtunzi basi mtazamo wa mtunzi kuhusu mambo mbalimbali hauna budi kubadilika.

Kutokana na haya ni dhahiri kuwa daima kuna ufungamano baina ya itikadi ya mtunzi na msimamo wake kwani ndio huelekeza kazi yake yote ya kifasihi na namna atakavyoiwasilisha kwa jamii yake. Itikadi inapobadilika basi msimamo wa mtunzi unabadilika na hivyo yale atakayowasilisha na namna atakavyoyawasilisha yatabadilika ili kazi zake ziwe faafu kwa jamii lengwa na pia kutimiza majukumu yake kama mwalimu wa jamii yake na ulimwengu kwa jumla, Chambilecho Achebe (1975) kwamba mtunzi ni mtu wa kawaida na sharti aitumikie jamii yake bila kujitenga nayo. Jambo hili pia linaungwa mkono na Wa Thiong'o (1972) anayesema kuwa mtunzi wa Kiafrika ni kama mwalimu wa jamii, lazima awaelimishe kuhusu historia yao na hali yao ya sasa ili kuwazindua na kuwafahamisha hali zao halisi.

4.6 HITIMISHO

Katika sura hii, mtafiti alidhamiria kuonyesha uhusiano uliopo baina ya itikadi na msimamo wa mtunzi kwa kurejelea riwaya za S. A. Mohamed. Mtafiti ameeleza mikabala mbalimbali ya dhana ya itikadi ambapo alibaini mikabala mitatu muhimu kwa mujibu wa utafiti huu. Mikabala iliyojadiliwa ni ile ya Karl Marx iliyobaini kuwa itikadi ni ung'amuzi potoshi na kuungwa mkono na wahakiki wengi kama Njogu, Lorrain,

Rossiland na Stoika kati ya wengine. Mkabala mwingine uliojadiliwa ni ule wa Louis Althusser aliyesema kuwa itikadi ni dhana inayoweza kutokana na matumizi ya nguvu ya serikali, jeshi, magereza na vile vile vyombo vya kiitikadi kama kanisa, elimu, vyombo vya habari kati ya vinginevyo. Mkabala wa tatu uliojadiliwa ni mkabala ulioendelezwa na Antonio Gramsci anayesema kwamba itikadi ni dhana ambayo huendelezwa kwa ukubalifu na ukawaida. Kauli iliyojitokeza ni kwamba itikadi ni dhana telezi na changamano kuelezea kama wanaudenguzi wanavyosema kuwa maana ni telezi na haishikiki.

Aidha, mtafiti ameweka kazi za S. A. Mohamed katika muktadha wake wa kihistoria kuambatana na nadharia ya kimaadili kuwa fasihi ni zao la jamii na mtunzi hana budi kuwasilisha yaliyo faafu kwa jamii yake na kuyachuja yaliyo potovu. Amefanya haya kwa kuangazia historia ya Zanzibar na historia ya mtunzi ili kuona muktadha ulioibusha kazi zilizoandikwa na mtunzi huyu hasa kazi zinazochanganuliwa katika utafiti huu. Mtafiti ameweza kuonyesha kwamba, kutokana na utawala dhalimu ulioendelezwa na viongozi, kufuatia kukwama kwa njia nyinginezo zozote za kujikomboa, Waafrika waliachiwa njia ya mapinduzi pekee ili kujinasua katika utawala dhalimu. Mazingira haya ndiyo yaliyozua itikadi za kihalisia na uhalisia wa kijamaa zinazoonekana kujitokeza katika riwaya za awali za S. A. Mohamed na kupingwa katika riwaya za baadaye. Imebainika kuwa kadri historia ilivyobadilika ndivyo itikadi ilivyobadilika. Nao msimamo wa mtunzi ukazidi kubadilika kwani msimamo huelekezwa na itikadi. Kwa hivyo itikadi ina ufungamano mkubwa na msimamo wa mtunzi hivi kwamba ikibadilika

nao msimamo wake huathirika na kubadilika. Hii ina maana kuwa kazi yake ya fasihi pia hubadilika kwani ndiye anayeiumba na hivyo msimamo wa mtunzi hauwezi kuwa mmoja na tengemano kila wakati hubadilika kufungamana na mabadiliko ya itikadi.

Katika sura inayofuata, mtafiti ataangazia itikadi inayojitokeza katika riwaya ya *Asali Chungu* na *Kiza Katika Nuru* ili kuweza kuona namna historia, siasa na uchumi zilivyoibusha itikadi ambazo mtunzi anaaridhia katika riwaya hizi kwani kutokana na mjadala katika sura hii, itikadi katika riwaya hizi inaweza kufungamanishwa na miktadha mbalimbali ya kiwakati hasa tukizingatia miaka ambayo kazi hizi ziliandikwa.

SURA YA TANO

5.0 ITIKADI KATIKA RIWAYA ZA ASALI CHUNGU NA

KIZA KATIKA NURU

5.1 UTANGULIZI

Katika sura iliyopita mtafiti aliangazia uhusiano wa itikadi na mtazamo wa mtunzi. Ilibainika kuwa, kuna ufungamano mkubwa baina ya itikadi anayoaridhia mtunzi, na mtazamo wake kuhusu maswala mbalimbali anayozungumzia katika kazi yake. Hii ni kutokana na dhana kuwa itikadi ndiyo humuelekeza mtunzi katika kuchagua yale atakayowasilisha na namna atakavyoyawasilisha. Nayo itikadi hufungamana na muktadha wa kihistoria na kiuchumi kwani mtunzi ni mtu wa kawaida katika jamii yake na ni kama mwalimu wa jamii anayoiandikia hivyo hawezi kujitenga nayo.

Kwa hivyo, historia na siasa za jamii yake zinapobadilika, nayo itikadi ya mtunzi hubadilika na kwa sababu itikadi ndio huelekeza mtazamo wa mtunzi kuhusu atayozungumzia na atakayoacha ili kazi yake iwe faafu kwa jamii anayoiandikia, basi mtazamo wake hubadilika. Hivyo hauwezi ukawa mmoja na tengamano katika vipindi tofauti vya kihistoria, kisiasa na kiuchumi. Ni katika misingi hii ambapo katika sura hii, mtafiti anajadili itikadi ambazo S. A. Mohamed anaaridhia katika riwaya ya *Asali Chungu* (1978) na *Kiza Katika Nuru* (1988). Katika *Asali Chungu* mwandishi anawasilisha itikadi kuu ya kimwinyi kama itikadi ya watawala ambayo inajitokeza kwa matumizi ya asasi kama vile mfumo wa kiuchumi, matabaka na utabaka, dini, mfumo wa

kuumeni, asasi za utawala, maadili, ndoa na mapenzi, elimu na utamaduni. Vipengele hivi hutumiwa na watawala kuhalalisha mfumo huu wa uzalishaji mali wa umwinyi ili kuendelea kuhifadhi nyadhifa zao na hali zao za utawala. Mwandishi ana itikadi ya kimapinduzi kuwa kwa kurekebisha asasi za itikadi ya kimwinyi na kuzitumia kwa njia inayofaa, maisha ya wanyonge yatakuwa bora na hali zao zitaimarika.

5.2.0 MUHTASARI WA RIWAYA YA ASALI CHUNGU

Katika riwaya ya *Asali Chungu*, tunaonyeshwa wahusika mbalimbali ambao wameainishwa kitabaka. Wale wa tabaka la juu, wenye vyeo na mamlaka ni pamoja na Bwana Zuberi na Bi Amina. Kuna walalamikaji au walalahoi ambao ni wanyonge wanaonuka ufukara kama Dude, Baya, Shaaban Supu kati ya wengineo. Haya yanaonyesha kuwa jamii imegawanyika katika matabaka. Mtunzi anaonyesha uongozi mbaya kwa vile Bwana Zuberi anakosa kutekeleza majukumu yake ya kuwahudumia wananchi wanaoleta malalamishi kwake. Mzee Zuberi anaishi kwenye nyumba ya kifahari lakini kwa upande mwingine, tunaarifiwa jinsi mazingira ya wafanyakazi wake ni mabaya kwa mfano, vyumba vyao havina paa.

Pia, tunaelezwa jinsi maovu yanatekelezwa kama Zuberi kumnajisi Semeni. Binti Daudi na Zuberi wanapanga njama ya kumwendea Semeni kwa mganga ili akubali kushiriki mapenzi na Bwana Zuberi. Binti Daudi anatumiwa na Zuberi katika kuwakandamiza wafanyakazi kama vile kumtishia Mzee Omari amletee bintiye. Tunaona jinsi jamii imejaa unafiki vile tunaona jinsi wenye mali walivyo wakarimu katika mwezi wa kutoana

mashimoni ilhali mwandishi ametujulisha jinsi walivyo wakatili na wakandamizaji wa mafukara. Aidha, tunaweza kufahamu maisha ya mafukara na walalahoi kama vile Semeni, Pili, Baya, Dude na Shaabani Supu. Mwandishi ametumia mandhari, vyakula, mavazi, na tabia zao ili kutujulisha jinsi wanavyoishi:

Tunakula ugali na muhogo kibaba nusu viungo hivi hapa –
embe bichi, nyanya, mshumaa, tungule, papa mkavu, bizari na
.....(uk. 44).

Dondoo hili linadhihirisha namna ambavyo masikini hawa wanaishi katika hali ya unyonge hata kupata vyakula ni shida kubwa. Hii inachangia kuwafanya mafukara kama vile Dude na Bushiri kukosa matumaini maishani hivyo kuwa tayari kufanya lolote lile ili waweze kujikimu kimaisha.

Mtunzi anaendelea kutuonyesha jinsi maisha ya wanyonge yalivyo, hasa kama vile Dude anayezunguka mjini akitafuta kazi na vijana wengine. Pia, mwandishi anaonyesha jinsi matajiri wanaamini pesa na mali inaweza kununua chochote. Dhana hii ameonyesha kupitia kwa Amina ambaye anataka kuwa na uhusiano wa kimapenzi na Dude kwa kumlaghai kwa kutumia pesa na mali yake. Mwandishi anatarifu jinsi Mzee Zuberi ambaye alikuwa katili na mwenye vitendo vya unyama anajaribu kukimbilia kwa dini ya kiislamu pale anapougua maradhi ya moyo. Kwa mfano, anaonekana akisoma Kur’ani Tukufu na kila Ijumaa anawapa maskini sadaka angalau kujihami katika maovu yake kwa kutumia mali yake na kujikunjilia kwa dini naye mkewe anaendelea kufanya uasherati na mabarabaru kama vile Dude na kumlaghai mumewe kuwa Dude ni mfanyakazi.

Aidha, mwandishi anatarifu jinsi sherehe za kuaga mwaka zinavyoandaliwa pale mjini na matukio ambayo yanaambatana na sherehe hizo. Kwa mfano, kuna vyakula vingi, ulevi na ukosefu wa usalama. Pia unafiki wa Bi Amina unaonyeshwa pale anapomnyang'anya Dude ufunguo wa gari kwa sababu ya uamuzi wake wa kumsaidia Baya na kumpeleka hospitali licha ya amri yake kutofanya hivyo. Haya yanaonyesha jinsi Amina hakumpenda Dude kwa dhiti, haja yake ilikuwa ni kutimiza ashiki za kimwili tu. Ubinafsi na unafiki wa Amina unaonyeshwa kupitia majibu yake pale anapopokea habari ya kuwa Dude wanachumbiana na Binti yake aliyeitwa Shemsa. Hii ni kwa vile anakuwa na msimamo kuwa Dude hamuoi Shemsa kamwe. Alisema hivyo ili kuepuka aibu ya vitendo alivyotenda hapo awali ya uhusiano wa kimapenzi na Dude.

Mwishowe, Shemsa na Dude wanaoana na kuishi pamoja. Licha ya kuwa walipendana kwa dhiti, ndoa yao haikukosa dosari. Ilikuwa na panda shuka zake. Mfano, tunaona Dude kampachika mimba Latifa dadaye Shemsha alipoenda kukaa kwao ili kuwasaidia. Hapo awali alikuwa ameapa kuwa mwaminifu kwa mkewe na kutohusika katika uasherati kamwe.

Mwishoni mwa riwaya tunaona mapinduzi yakifanyika ghafla. Hii inatokana na ukandamizaji unaopelekea kuweko kwa mfumo wa kibwanyenye kutokana na mfumo wa umwinyi ulioenea katika jamii hii. Maskini wanadai haki yao na wanatekeleza maafa kama vile kuichoma nyumba ya Mzee Zuberi na Bi Amina. Hili linaashiria mwisho wa umwinyi na mwanzo wa jamii mpya au ujamaa yenye usawa na haki ya kila kiumbe.

Dude, Shemsha na kitoto chao pamoja na Latifa wanaokoka. Hawakuangamia ilhali Amina na Biti Daudi waliangamia. Naye Zuberi alikuwa ameaga dunia hapo awali kutokana na maradhi ya moyo.

Katika riwaya ya *Asali Chungu*, mwandishi anadhihirisha itikadi yake kuhusu mambo mbali mbali katika jamii yake. Kaida au imani yake kuhusu mambo ya jamii yake ameionyesha kupitia kwa wahusika aliowaumba katika riwaya yake, maudhui yanayojitokeza na lugha aliyoitumia. Haya yanadhihirisha itikadi yake kuhusu maswala mbalimbali katika jamii kwani itikadi ndio huongoza ule mtazamo wa mtunzi, mambo atakayowasilishia jamii anayoiandikia na namna atakavyowasilisha ulimwengu wake kwa jamii anayoiandikia. Mtunzi hufanya haya kwa ufundi ili kuhakikisha kuwa kazi zake ni pevu na zinasadifu jamii yake na zinakubalika na kuwakilisha ifaavyo maadili ya kijamii katika kipindi maalum.

5.2.1.0 ITIKADI YA WATAWALA

5.2.1.1 ITIKADI YA KIMWINYI

Katika riwaya hii, itikadi ya kimwinyi ndio inayodhihirika zaidi kama iliyotawala katika jamii hii. Mwandishi anaonyesha itikadi ya utawala wa kimwinyi ambao ni mfumo unaotambulika kwa vipengele mbalimbali ambavyo huhalalisha matendo ya tabaka tawala. Baadhi ya vipengele hivyo ni mfumo wa kiuchumi, matabaka, elimu, utamaduni, dini, uchawi, asasi za utawala na vinginevyo

5.2.1.2 MFUMO WA KIUCHUMI

Katika riwaya ya *Asali Chungu* mfumo wa kiuchumi unaojitokeza ni ule wa kimwinyi. Katika mfumo huu, watu wachache walimiliki nyenzo za uzalishaji mali huku wengi wakibakia masikini. Mfumo wa kimwinyi ni mfumo ambao wachache wana mali nyingi katika jamii ilhali wengine hawana chochote. Pia unaweza kuelezewa kama hali ya wachache kumiliki raslimali za nchi huku wengine wakibaki bila chochote. Njogu (1997) anasema kuwa mfumo wa kibwanyenye ulijitambulisha kwa ubadhirifu na ufujaji miongoni mwa tabaka tawala. Maisha ya tabaka hili huwa ni ya matumizi tu. Jambo hili husababisha kuibuka kwa tabaka la kimwinyi ambalo baadaye hufikia kilele chake katika uistiimari, jambo ambalo husababisha mikinzano mikali ya kitabaka.

Mfumo huu unajitokeza katika riwaya nyingi za visiwani kama *Nyota ya Rehema* na *Kiu* zilizoandikwa na Mohamed Suleiman Mohamed, *Kasri ya Mwinyi Fuad* na *Kuli* za Shafi

Adam Shafi kati ya nyinginezo. Katika riwaya hizi, waandishi wamesawiri wahusika wachache wanaomiliki mashamba makubwa na kuwaajiri wafanyakazi au kuwakodisha vikataa. Aidha, wafanyakazi wengi wapo viwandani na bandarini wakitafuta kazi za sulubu. Kwa mfano katika *Nyota ya Rehema* wakulima wanaoleta mazao kwa mwenye shamba wanatangaziwa wasichelewe kuleta kodi kwa Bwana Fuad ambaye ndiye mmiliki wa shamba. Katika *Kasri ya Mwinyi Fuad* Bwana Malik anamiliki shamba kubwa la fahari, lenye mikarafuu, matunda na mpunga. Ni katika mfumo huu wa umwinyi ambapo riwaya ya *Asali Chungu* ambayo pia ni mojawapo ya riwaya za visiwani inaonekana kujengeka.

Kwa mujibu wa Chuachua (2011:26) kipindi cha 1967-85 kinadhihirisha mfumo wa kijamaa. Anasema kuwa “hiki ni kipindi ambacho viongozi waliweza kumiliki mali na kuzilinda kutokana na nafasi walizonazo”. Mfumo huu ulikusudia kuwafanya wananchi kuweza kujitegemea. Ingawa haukuungwa mkono na mataifa ya kibepari viongozi walijitahidi sana kuafikia malengo yake. Mabadiliko makubwa ya kiuchumi yalitekelezwa kama vile utaifishaji wa mali ya umma na kuanzishwa kwa vijiji vya ujamaa. Wananchi wengi hawakuhusishwa katika mpango huu kwani majukumu mengi yalitekelezwa na chama. Hali ya uchumi ikawa mbaya na umasikini ukakumba nchi kwani viongozi wengi walitumia nafasi hii kujitajirisha na kutekeleza maovu mengine. Hali hii ilishuhudia ushindani wa viongozi katika kung’ang’ania mali na kuhodhi chochote walichopata na maadili ya viongozi yalionekana kutupiliwa mbali. Kilichothaminiwa na viongozi wengi ni mali na mali pekee ili kuendelea kuwa matajiri.

Wakanyakua mashamba makubwa na kuajiri wafanyakazi waliowalipa mshahara duni na unyanyasaji ukazidi. Huu ndio msingi wa kiuchumi ambao S. A. Mohamed anarejelea anaposema; “Hili shamba lote ni la Bwana Zuberi. Huku halina mwisho, na huku mpaka bondeni” (uk.92). Pia tunaarifiwa jinsi Zuberi anamiliki magari ya kifahari kama vile *vaaxhaul* (uk.95).

Kupitia kwa Zuberi na mkewe Amina mwandishi anatumia kuhusu mfumo huu. Yaani jinsi wanaishi katika jumba la fahari huku wanyonge wakiishi katika mazingira duni. Pia wafanyakazi wanavaa mavazi mabaya na kula vyakula vibaya. Mwandishi anasawiri wahusika mbalimbali ambao ni wala na walala hoi amewatumia kuonyesha jinsi uchumi wa jamii hii ulikuwa umezorota kutokana na tabia hii ya viongozi ya kuhodhi mali na kukaa starehe. Anaonyesha nyenzo za kiuchumi wa jamii yake na rasilimali nyingi katika jamii yake zimemilikwa na wachache kama vile Bwana Zuberi nao wale masikini hawana nafasi yoyote na inawabidi kufanya lolote ili waweze kujikimu. “Nikitoa mazao yangu yote niliyopanda matumbo manane nitayalisha nini” (uk.19).

Mwandishi anaonyesha jinsi uchumi ulikuwa umezorota kwa vile mapato ya kishamba cha Mzee Omari yanategemewa na familia nzima ambayo haina mapato mengine. Mzee Omari yu radhi kufanya lolote ili aweze kuikimu familia yake na kutimiza masharti ya Zuberi ambaye ndiye mkubwa na kiongozi. Mzee Zuberi bila aibu yoyote anamwambia Mzee Omari amletee bintiye afanye mapenzi naye chini ya majuma mawili la sivyo

ataumia kiuchumi. Mzee Omari anakataa mara ya kwanza lakini kutokana na ukosefu wa chakula inambidi afanye vile Zuberi alivyotaka. Maelezo haya yanadhihirisha namna mfumo wa kimwinyi ulivyojitambulisha kwa raha na starehe kwa mfano Zuberi aliishi katika anasa na mamlaka na kazi yake ni matumizi tu na ubadhirifu.

Kupitia mhusika Dude, mwandishi anaonyesha jinsi uchumi wa jamii yake ulivyokuwa mbaya kiasi ya kwamba wanajamii wanavaa nguo kuukuu zilizoraruka. Anamsawiri Dude katika hali ya kimasikini kabisa hivi kwamba hata kupata mavazi ni shida. Matatizo haya yote yanasababishwa na mfumo mbaya wa kiuchumi wa kimwinyi ulioendelezwa na mabwanyenye kama Zuberi. Bushiri kwa upande wake anaona ni afadhali kuwa jela ambapo anaweza kupata angalau chakula kuliko kuwa huru na afe jaa. Anasema;

Niliona bora utumwa wa kuwa mfungwa kuliko kuwa na uhuru katika ulimwengu ambao hauwezi hata kunipa chakula (uk.74).

Kupitia kwa mhusika Bushiri, mwandishi anaonyesha mfumo wa kiuchumi wa kimwinyi ulikuwa umezorotesha uchumi wa jamii kiasi ya kuwa wanaonelea kuwa jela ambapo watapata chakula ni bora kuliko kuwa huru bila chakula. Mohamed anaonyesha kuwa mfumo wa kiuchumi kwa hakika ndio msingi wa matatizo yote ya kijamii kwani wale matajiri kupindukia wanautumia vibaya kutekeleza maovu nao wale maskini kama Dude na Bushiri wako radhi kufanya lolote mradi wapate kipato. Anaonyesha kuwa mfumo wa kiuchumi wa kimwinyi ndio unaopelekea watu kuwa

radhi kufanya chochote hata kuwatoa mabinti zao kwa mabwanyenye ili wajinusuru kiuchumi.

5.2.1.2 MATABAKA

Matabaka hujitokeza ambapo kundi moja linamiliki nyenzo za uzalishaji mali huku jingine likimiliki nguvu zake tu. Tabaka la juu humiliki mfumo wa uzalishaji mali huku wafanyakazi wakimiliki nguvu na uwezo wa kufanya kazi. Jambo hili huzua matabaka ya juu na ya chini ambapo tabaka la juu linalojumuisha watawala huendelea kuwadhalilisha walio chini kitabaka na kiuchumi hasa kwa matumizi ya itikadi za kiutawala na wakati mwingine matumizi ya nguvu. Nguvu za kitabaka huwa na uzito zaidi ya vigeu vingine vya kijamii. Kwa mujibu wa Marx (1973) matabaka huwa katika hali ya mikinzano na kwa sababu jamii daima ziko katika harakati za kufanya maslahi yao bora, mikinzano hii huleta mapinduzi na uongozi kuchukuliwa na tabaka la wafanyakazi na mafalahi. Mivutano ya kijamii huchangia kuyaleta mabadiliko yanayohitajika katika jitihada za jamii za kilimwengu kuacha hali zao dhaifu, na kuukaribia utu kamili.

Mwandishi anaonyesha kuwa jamii yake imegawanyika katika matabaka mawili: matajiri na wenye vyeo, na maskini ambao ni wala na walala hoi. Anaonyesha walalamikaji ambao wanaonekana kutokuwa na chochote na baadaye katika sura ya pili, kupitia mandhari ya chumba cha mzee Zuberi ambaye anaonekana kuishi katika nyumba ya kifahari.

Njia nyingine inayoonyesha jamii hii imegawanyika katika matabaka mawili ni vile anavyoelezea aina ya vyakula vinavyoliwa na akina Pili na Semeni na kisha anaeleza vile kwa mzee Zuberi kuna vyakula vya kila aina. Mtunzi anaonyesha kuwa utabaka umekithiri kwani wale matajiri wa tabaka la juu wanapata kila kitu ambacho wanataka ilhali wale wa tabaka la chini wana matatizo chungu nzima. Anaonyesha utabaka huletwa na mfumo wa kiuchumi. Zuberi ana shamba kubwa ambalo linatoa mazao mengi na kwa hivyo kumuweka katika tabaka la juu pamoja na mkewe Amina. Nyumba yao ni kasri kubwa ambalo limejaa vitu vya thamani.

Kwa upande mwingine, kina Semeni, Dude, Bushiri na wengine wanaishi katika tabaka la chini. Hawa hawana vitu vya kimsingi kama chakula na elimu. Hali hii inasababisha wao kufanya lolote lile ili wayakidhi mahitaji yao. Dude anafanya mapenzi na Amina ili apate fedha za kujikimu, Bushiri anamletea Zuberi vidosho ili apewe hela za kujikimu, Semeni anashiriki ukahaba na ulevi kati ya maovu mengine. Hii inaonyesha kuwa jamii ikiwa na mfumo mbaya wa kiuchumi unaoleta utabaka mivutano hushuhudiwa baina ya matabaka haya na huona kila moja kuwa ni adui ya lingine. Hali hii husababisha uhasama, na mwishowe huleta mapinduzi kama ilivyofanyika katika *Asali Chungu* ambapo nyumba ya Zuberi inachomwa pamoja na Amina na Biti Daudi huku Dude, Shemsha na Latifa wakibakia hai.

5.2.1.3 ELIMU

Katika itikadi ya kimwinyi, elimu ni asasi inayotumiwa kuendeleza kizazi cha mabwenyenye. Mtunzi anaonyesha namna ambavyo elimu ni muhimu katika maisha kwani ilitumiwa kuwaweka watu katika matabaka mbalimbali. Mohamed anaeleza jinsi masomo ya Dude yanakatizwa akiwa darasa la sita kwa sababu ya ukosefu wa karo. Hili linaleta kuwemo kwa matabaka katika jamii kwa sababu ya ukosefu wa ajira unaotokana na elimu duni. Said Ahmed Mohamed anatueleza kuwa Dude alikuwa hodari shuleni lakini mahudhurio yake yalikuwa mabaya kwa sababu ya umasikini uliomkumba yeye na mamake Semeni.

Kwa upande mwingine watoto wa matajiri walipata elimu ya juu hata kuenda ng'ambo kusoma. Shemsha, mtoto wa Zuberi na Amina anasomea ng'ambo na kufaulu sana katika masomo yake. Haya yote mtunzi anaonyesha yanasababishwa na mfumo wa uzalishaji mali wa kimwinyi kwani waliopendelewa na mfumo huu ndio walioendelea na masomo yao. Mfumo wa aina hii huwafanya watu kuuza chochote walicho nacho ili waweze kujikimu mradi kuna mtu ambaye yuko tayari kukinunua. Kutokana na haya watu wengi walilazimika kufanya kazi za hadhi ya chini kama kuuza supu na wengi wao wakaingilia ukahaba.

Wahusika kama vile Dude anakubali kushiriki uasherati na Amina kutokana na uhitaji. Bushiri naye alitekeleza kazi ya kumletea Amina vijana kwa sababu ya umasikini. Semeni pia anashiriki ukahaba na ulevi baada ya kunajisiwa na Zuberi aliyekuwa

mwajiri wake ili angalau kujikimu kimaisha na kumlea Dude. Kwa hakika baada ya Semeneni kunajisiwa anaporomoka kabisa kuwa mlevi kupindukia na mwishowe kuaga dunia. Wasichana wengi na hata wavulana waliuza miili yao ili kujikimu. Ikizingatiwa kuwa vijana hawa wote hawakuwa na elimu, Mohamed anaonyesha elimu ni dira inayomuelekeza mja maishani na akiikosa basi ulimwengu wake utakuwa wa giza toloro.

5.2.1.4 UTAMADUNI

Neno utamaduni limefafanuliwa kwa namna nyingi. Katika anthropolojia ya Kimarekani neno hili lina maana ya namna mbalimbali ambazo watu wanaoishi katika sehemu mbalimbali ulimwenguni huanzisha na kuwasilisha tajriba zao za maisha na kutenda mambo kiubunifu. Huambatanishwa na mambo kama vile ushirikina na uchawi na imani za kimiujiza wakati mwingine hasa katika jamii za Kiafrika. Ushirikina nao hutumika kwa kutaja imani ambazo zina misingi ya kifikra tu bila misingi thabiti ya kisayansi. Uchawi ni nguvu za giza zinazotumiwa na jamii nyingi hasa za Kiafrika kwa ajili ya mtu kuumiza watu wengine kimazingira au kwa ajili ya kujifurahisha kwa kuwatesa watu wengine kwa kuwachukua au kwa kuwafanya waugue au wafe.

Hali hii inajitokeza pale ambapo Zuberi ameshindwa kumshawishi Semeneni afanye mapenzi naye kwa hivyo anamtuma Biti Daudi kwa mganga ili iwe rahisi Semeneni kukubali mpango wake. Biti Daudi anamwambia:

Umesahau? Si ulinituma nende kwa Shehe Kombo basi nimekwenda, naye kanipa maagizo. Anataka kucha saba za vidole vya miguu vya Semen, unywele wake, tambara la kanzu au kanga anayojitanda, yai fuza, marashi meupe, mbuzi mwekundu na kipande cha muwa mweusi. Pana dawa mbili zinazotakiwa- moja ya kupikwa apewe Semen anywe na ingine ifukiwe kizingitini. Siku ya pili Semen atakuwa chini ya miguu yako amini mambo ya ushirikina (uk. 24).

Kabla mpango huu kufaulu, Zuberi anatumia dawa na kumnajisi Semen. Hili linadhihirisha namna Mamwinyi walikuwa tayari kutenda lolote kutimiza ashiki zao za kimwili kwani walijihisi wenye mamlaka na mabosi.

5.2.1.5 MFUMO WA KUUMENI

Mfumo wa kuumeni ni mfumo wa kijamii ambao unaamini kuwa jinsia ya kiume ni yenye nguvu, mamlaka na yenye ufaafu zaidi kushinda jinsia ya kike katika vitengo mbalimbali kama vile siasa, uongozi na katika familia. Momanyi (1999) anasema kuwa katika mfumo wa kuumeni mwanamume husawiriwa akiwa mwenye nguvu na mamlaka. Husawiriwa akiwa mtawala, mwenye thamani ya juu, jasiri, mwenye maarifa hadi wakati mwingine hupewa mamlaka ya kiungu. Mwanamke naye husawiriwa kama mfuasi, mtegemezi, mpambaji wa mwanamume, mjinga na rahisi wa kudanganyika na kiumbe hatari kinachoweza kumuingiza mwanamume kwenye laana akakosa ukuruba wake na Mungu. Osore (2008) anasema kuwa mfumo huu hujengeka kwenye msingi kuwa jinsia ya kike ni tegemezi na hivyo bila jinsia ya kiume watu wote wa jinsia ya kike hawawezi kuishi .

Katika riwaya ya *Asali Chungu*, mfumo huu unajitokeza na kudhihirika zaidi kutokana na mfumo wa utawala wa kimwinyi uliodhihirisha ubosi na mamlaka. Jinsia ya kiume inatajwa kwa majina ya heshima na cheo kama vile, Bwana Mkubwa, Bwana DC (uk. I) lakini kwa upande mwingine, mwandishi amesawiri wahusika wa kike akitumia majina ya kuwadunisha na kuwadharau kama vile Bi. Kikongwe na janajike kuwarejelea wanawake (uk. 1).

Aidha, mwanamke anasawiriwa mwanamke kama mtu asiyekuwa na haki ya kumiliki chochote hali iliyodhihirika katika mfumo wa kimwinyi ambapo wanaume ndio walikuwa wanamiliki mashamba na mali hivi kwamba hata mwanamke alionekana kuwa ni sehemu ya mali yake. Hili linaonyesha kuwa kama mwanamke hana chochote basi ni kiumbe ovyo kinachohitaji kudharauliwa tu na hakistahili heshima zozote. Kazi yake ni kutulia, kunyamaza na kuwa mtegemezi wala si kutoa kauli zake ama kujitetea, kama tunavyomuona Bwana Zuberi akifyeka shamba la bibi mmoja na kuzichoma moto takataka kisha moto unaenea hadi unaangamiza mikarafuu yake na minazi.

Haya yote anayafanya bila idhini ya mwenye shamba. Yanaonyesha ukandamizaji na udhalimu wa Bwana Zuberi kwa wanawake unavyoendelezwa kutokana na mfumo wa kiuchumi wa kimwinyi unaomilikiwa na wanaume. Yanatilia nguvu mawazo ya Karl Marx (1973) kuwa mfumo wa kiuchumi huwa nguzo muhimu katika ukandamizaji wa jamii na huelekeza migogoro na matukio muhimu katika jamii. Jambo hili linaonyesha

kuwa mfumo wa kuumeni ni sehemu ya utawala kandamizi wa kimwinyi na unahitaji kuchunguzwa katika muktadha wa kiuchumi na utawala.

Aidha, mtunzi anaonyesha wanawake wanawakandamiza wanawake wenzao. Pale muda unapokwisha bila ya kuhudumiwa na Bwana DC, Kabore anasimama na kuwatangazia kwa dharau wanawake wanaokuwa bado wamekaa baoni, “Saa za ofisi zimekwisha. Itakuwa bora mkija kesho. Bwana DC atakuwepo kwa ajili yenu” (uk 18). Hili linadhihirisha kuwa baadhi ya wanawake wamekubali unyanyasaji kuwa jambo la kawaida na la ukubalifu kama Gramsci (1985) anavyosema kuwa watu wengine hunyanyaswa kutokana na itikadi yao kuwa hilo ni jambo la kawaida na mambo hupaswa kuwa hivyo yalivyo.

Mwandishi pia anadhihirisha mwelekeo wa Althusser (1981) kuhusu matumizi ya nguvu ili kuendeleza itikadi pale anaonyesha mwanamume kama mwenye haki ya kutenda lolote lile mradi atimize haja zake. Zuberi anatoka katika chumba chake cha kulala na kumwacha mkewe Bi. Amina, kisha anamwendea Semeni kwenye chumba alicholala na kummiminia Semeni dawa fulani kisha anamnajisi.

Momanyi (1999) anasema kuwa wanawake husawiriwa kama viumbe hatari wanaoweza kumuangamiza mwanamume na kumfanya apate laana mpaka akose ukuruba na Mungu wake na hivyo anafananishwa na ibilisi. Kwa mfano Mzee Shaabani anaeleza jinsi mwanamke alivyo mdanganyifu na asiyekuwa na mapenzi ya kweli. Yeye hukaa na

mwanamme mradi anafaidika kiuchumi kwani hawezi kuwa na mapenzi ya dhati. Mzee

Shaabani anaendelea kumweleza Dude tabia za Pili aliyempa talaka huku akisema:

Ingelikuwa wanawake hawatoki nje, ila kwa rai na hila, pia ingelikuwa haijambo lakini mtu kujiuza tena kwa mtu yeyote huo ni ushetani mkubwa...(uk. 34).

Mwandishi anaendelea kuonyesha matendo maovu ya mwanamke katika jamii yake kupitia kwa mhusika Dude kwani anamsawiri Baya akimfunza Dude mambo ya ngono. Mohamed anaonyesha namna mfumo wa kuumeni unamsawiri mwanamke akiwa kiumbe kiovu kinachofananishwa na shetani.

Wahusika wa kike pia wamesawiriwa kama walevi kupindukia na wenye kufanya tendo la ngono mahala popote na mwanamume yeyote. Mwandishi anaonyesha ulevi wa mwanamke katika jamii kupitia kwa wahusika kama vile Semeni, Pili na Baya na hakuna wahusika wa kiume walioshiriki nao vitendo hivyo wanaotajwa. Hii inaonyesha jinsi jamii inachukulia wanawake kuwa waovu zaidi huku ikipuuza uovu wa mwanamme kufungamana itikadi tawala ya kimwinyi iliyomtukuza mwanamme na kuchukulia kama mwenye mamlaka na ubosi.

Aidha, mwandishi ameangazia uhusiano kati ya Dude na Amina kwa mapana na marefu ili kuonyesha upotovu wa mwanamke katika jamii yake kajikosea heshima. Hii ni kwa sababu Amina ndiye anayemtafuta Dude na kumlazimisha kuwa mpenziye ilhali Dude hakutaka jambo lile ila kwa ile hali yake ya kutokuwa na mbele wala nyuma, maskini hohehahe (uk.91). Kupitia kwa mhusika Amina, mwandishi

anaendelea kuonyesha kuwa mwanamke anajidharau mwenyewe hivyo kujidunisha na kudhihirisha mkabala wa Gramsci (1981) kuhusu itikadi kuwa hutokana na ukubalifu na ukawaida. Wanawake katika *Asali Chungu* wanaona ni kawaida kunyanyaswa.

Mhusika aliyetumiwa na mwandishi sana katika kuendeleza uovu wa mwanamke na kudhihirisha mtazamo wa Gramsci kuhusu itikadi ni Biti Daudi. Tunaona jinsi anaongea na wafanyakazi wa Mzee Zuberi na Amina. Kinywa chake kimejaa matusi, dharau na dhihaka (uk14-15). Pia tabia zake za kumletea mzee Zuberi mabinti wafanye mapenzi naye (uk. 61). Kupitia kwa Biti Daudi tunaarifiwa kuhusu tabia zake za uasherati alipokuwa makamo. Yeye ashakubali kuwa maisha ya mwanamke ni ya kukandamizwa na kutokana na hali hii ya ukubalifu anawapeleka wasichana kwa Zuberi ili Zuberi afanye mapenzi nao (uk. 61).

Ni dhahiri kuwa mfumo wa kuumeni unatumiwa kumsawiri mwanamke kama kiumbe kiovu na kufananishwa na shetani mwenyewe. Licha ya kuwa vitendo vingi viovu anavyovifanya ni kwa ushirika na wanaume yeye anasawiriwa kuwa mkosa ambaye ndiye anayempotosha mwanamume kuambatana na itikadi tawala ya kimwinyi ambayo ilidhihirika kwa kuhodhi mamlaka na ubosi. Mfumo wa kuumeni ni mojawapo tu wa vigeu vya itikadi kuu ya kimwinyi ambapo mwanamke anasawiriwa kama kifaa tu cha kutimiza anasa na ubadhirifu wa mamwinyi.

5.2.1.6 NDOA NA FAMILIA

Ndoa ni muungano kati ya mwanamke na mwanamume kuishi pamoja kama mume na mke hadi kifo kiwatenganishe (TUKI, 2013). Katika ndoa, watu wawili wa jinsia tofauti hutakiwa kuungana na kupendana mpaka mwisho. Ndoa hufungamanishwa na tamaduni na imani mbalimbali za kidini hivi kwamba ni vigumu kutenganisha itikadi kuhusu ndoa bila kugusia maswala ya utamaduni na dini kwani maswala haya hufungamana. Katika dini ya Kiislamu, mwanamume huruhusiwa kuwaoa wanawake hadi wanne mradi ana uwezo wa kiuchumi wa kuwatimizia mahitaji yao kwa njia ya sawa bila kupendelea. Katika dini ya Kikristo, mwanamume hupaswa kumuoa mke mmoja pekee na kuishi naye hadi kifo na huwa hamna nafasi ya talaka. Hata hivyo, misimamo hii ya dini kuhusu ndoa mara nyingi hutegemea mkabala wa uelewaji wake wa dini anayoaridhia na namna ya uelewaji wake na imani yake.

Katika riwaya ya *Asali Chungu* ndoa inawakilishwa na wahusika mbali mbali ambao wanaishi pamoja kama mume na mke. Wahusika hawa ni kama, Zuberi na Amina, Shaabani Supu na Pili na Dude na Shemsa. Kupitia kwa wahusika hawa mwandishi anaonyesha namna ndoa haiheshimiwi na vile ndoa inadunishwa kutokana na athari za itikadi tawala ya kimwinyi. Mtunzi anawasilisha dhana kuwa msingi wa ndoa unapaswa kuwa mapenzi ya dhati jambo ambalo ni muhali kupatikana katika jamii inayotawaliwa na itikadi ya kimwinyi inayojidhihirisha kwa ubosi, starehe na mamlaka kwani mabwana wanahitaji kuhudumiwa na kustaladhi huku mabibi wakihitajika kuwahudumia.

Mtunzi anamsawiri Bwana Zuberi na Amina wakiwa katika ndoa ambayo imejaa uasherati na maovu mengine makuu. Kwa hakika, ndoa hii inanuka uozo kwa njia kubwa. Zuberi anamwacha mkewe kitandani na kwenda kwa Semen kisha anammiminia dawa ili aweze kufanya mapenzi naye kisha anarejea chumbani mwake aliyomo mkewe Amina. Naye Amina anafanya ngono na Dude huku akijifanya amemwajiri kazi ya kuwa dereva wake.

Mzee Shaabani anapoelezea kuhusu sifa za mke aliyewahi kuoa, anamuarifu Dude jinsi alimfumania Pili kinagaubaga akifanya mapenzi na wanaume tofauti na hivyo anaapa kutoa tena. Hili linaonyesha namna watu wachache wanaoshikilia uaminifu katika ndoa wanavyoweza kuvunjika moyo na kudhihirisha athari za mfumo wa kimwinyi ambapo wasio na mali hujikuta wakipoteza matumaini ya kuishi na kukata tamaa:

Kheri niishi hivi hivi nabanja nikitafuta, kuliko kutafuta mtu umlishe, umvishe, halafu ageuke kombe akupare rohoni?

Pia anaposema:

unitajiapo shamba au mwanamke, huona kama umenitajia mamangu (uk. 35).

Jambo jengine linaloonyesha itikadi ya mwandishi ya ndoa kutoheshimiwa ni kupitia kwa Dude na Latifa ambapo Dude anampachika mimba Latifa ambaye ni nduguye Shemsa. Latifa alikuwa ameenda kukaa kwao kuwasaidia na Dude anafanya mapenzi naye licha ya kuwa alikuwa ameapa katu hatahusika kamwe na uasherati. Mohamed anaonyesha ndoa ni kigeu cha kuendeleza itikadi ya kimwinyi anapoisawiri kuwa na raha na anasa. Zuberi ni mwenye raha anatafuta wasichana wachanga kwa usaidizi wa

Biti Daudi. Naye Amina mkewe anafanya mapenzi na Dude akijidai amemwajiri kuwa dereva wake. Kwa kusawiri ndoa kama mahali pa raha na anasa Mohamed anaonyesha itikadi ya kimwinyi namna inavyodhihirika katika ndoa na hivyo ni kigeu tu cha itikadi tawala.

5.2.1.7 DINI

Dini ni imani maalumu ya kumuamini na kumtii Mungu wa haki (TUKI, 2013). Dini ni asasi mojawapo ya kitawala ambayo huweza kutumiwa kuwapumbaza wanyonge wasione ukweli. Kwa mujibu wa Marx na Engels (1973) katika *On Literature and Art*, dini hutumiwa kueneza itikadi za uongo za tabaka tawala ili liendelee kudhibiti mamlaka ya utawala na nguvu za kiuchumi. Hufanya hivi kwa kueneza dhana ya majaaliwa kumaanisha kuwa Mungu ameratibu maisha ya wanadamu na yote wanayopitia ni mpango wa Mungu. Hili humaanisha kuwa kama wao ni maskini huona kuwa ni mapenzi ya Mungu wawe hivyo, kazi yao muhimu ni kutii na kumngojea Mungu tu. Hali hii hufanya wafikie kiwango cha ung'amuzi potoshi hivi kwamba hawatambui kuwa wananyanyaswa na kwa hivyo hawatetei hali yao kuwa bora kwani huamini ni majaaliwa au kudura ya Mungu.

Dini ni za aina mbali mbali kama zilivyo imani tofauti. Kwa mfano, kuna za Kikristo, Kiislamu, Kibudha, Kijing, Kimoon na nyinginezo. Dini inayosawiriwa na mwandishi katika riwaya ya *Asali Chungu* ni dini ya Kiislamu. Dini ya Kiislamu inaelezewa kwa mapana na marefu katika Kur'ani na inahusu kuwa na Imani kwa Allah ambaye ndiye muumba wa vyote. Mifano inayoonyesha kuwa jamii yake inafuata imani ya Kiislamu

ni mambo anayotutajia kama vile misikiti, Kur’ani tukufu, kusali na mafunzo ya Kiislamu.

Katika riwaya ya *Asali Chungu*, dini inatumiwa na wanajamii kama pahali pa kujificha na kujifanya kumkaribia Mungu ilhali wanatenda maovu yasiyohusishwa na dini au yasiyomfurahisha Mungu. Kwa mfano, mwandishi anaonyesha jinsi mzee Zuberi bado anajificha katika dini kwa kwenda sala ya alfajiri ilhali matendo yake ni maovu kupindukia. Kwa mfano, jinsi anamnajisi Semen huku akiwa amemuacha mkewe kitandani (uk14). Aidha, Biti Daudi, mwanamke aliyekuwa katili, mwenye dharau anajifanya kuwa na imani kwa Mungu anajifanya msalihina na kinyume chake ni kuwa yeye ni muovu na ndiye humpelekea Zuberi wasichana. Semen naye anasema kuwa anaogopa Mwenyezi Mungu na ndio hawezi kuyatenda maovu (uk 17) lakini baadaye tunamwona Semen akijitumbukiza kwenye anasa za dunia na kuyafanya yale aliyoyakataa.

Bw. Omari licha ya msimamo wake wa kidini inambidi ampelekee Zuberi msichana wake ili ajistareheshe naye baadaye asamehewe deni lake kwa Mzee Zuberi (uk. 20). Ingawa Bwana Omari alionekana kushikilia dini na imani kwa Mungu na kusema kuwa angalistahabu kufa kwa njaa kuliko kujivua nguo kwa kumpeleka bintiye kwa Zuberi, mwishowe anampelekea Zuberi bintiye baada ya majuma mawili. Hii inaonyesha kwamba dini inatumiwa kujificha.

Mtunzi pia anaeleza kuna mwezi wa kutoana mashimoni na ambao ukarimu siku hizo unakuwa mwingi. Mwandishi anaonyesha jinsi jamii wanajifanya kumkaribia Mungu hususan siku za sherehe za kidini ilhali wakati mwingine wanakuwa waovu, wachoyo na wenye kuwakandamiza maskini zaidi.

Dini inachukuliwa kimzaha na pia kama mahala pa kukimbilia au kujificha. Kwa mfano “sasa umeamua kusilimu” (uk 52). Dude anasema haya kuonyesha anachukulia dini kimzaha tu bila makini kutokana na kuathirika na maisha kwani wale aliotarajia wawe wafuasi wa dini kwa maneno na vitendo hawafanyi hivyo. Aidha Amina anasema “Mungu bariki nimeshajitayarisha”(uk 64) anapomaliza kujitayarisha ili akutane na Dude kwa nia ya kufanya uasherati kwa mara ya kwanza. Amina anapokuwa tayari kufanya uasherati anaomba baraka za Mungu na ni unafiki mkubwa. Haya yanadhihirisha dini ni kigeu cha itikdi tawala cha kuhimiza utiifu na unyenyekevu na kufanya watu waovu waonekane kuwa ni wema ili watawaliwa wasipiganie haki zao maana hawatambui wananyanyaswa na watu wanaojifanya wema na wenye huruma.

5.2.1.8 MAADILI

Maadili ni kanuni juu ya tofauti kati ya haki na uovu au wema na tabia mbaya (TUKI, 2013). Maadili ni dhana ambayo imezungumziwa na waandishi wengi wakiwemo Aristotle, Hough, Plato, Hobbes, Rousseau, Haris na Kant. Dhana ya kimsingi inayojitokeza ni kwamba maadili ni uamuzi wa kutenda wema au ubaya kutokana na dini,

imani fulani au akili ya mwanadamu kwa ujumla wake. Ni ule uamuzi wa kutenda anayofaa kuyatenda, kutekeleza yale anayopaswa kutekeleza, na kuyatekeleza namna yanavyopaswa kutekelezwa.

Fikra hizi na maamuzi haya humsaidia mwanadamu kuishi vyema na wanadamu wenzake na kutangamana nao vizuri katika jamii. Maadili huweza kuongozwa na sheria, miongozo, imani, dini, tamaduni na jamii kwa ujumla wake. Kila jamii huafiki maadili fulani na ni jukumu la mtunzi kuafikana na maadili haya, au kuyaelekeza kama Ngugi (1972) anavyosema kuwa mwandishi ni kama mwalimu katika jamii yake. Fasihi hupaswa kuwa kielelezo cha maadili ya jamii yake na hutoa mifano ifaayo ya maadili kwa wakati maalum, mtunzi hana budi kuelekeza jamii yake katika maadili ya jamii yake ili kazi zake iwe faafu kwa jamii anayoiandikia.

S. A. Mohamed anazungumzia namna maadili yanavyokiukwa katika kazi yake kupitia uasherati, ulevi, unafiki na kukashifu vitendo hivyo na kuonyesha kuwa anaamini katika jamii yenye maadili kama uaminifu, ukweli, haki na usawa kwa wanajamii wote. Akizungumzia uasherati ambacho ni kitendo cha kufanya ngono nje ya ndoa na uzinzi, mwandishi ameonyesha wahusika mbalimbali katika jamii yake wanajiingiza katika mambo ya uasherati na uzinzi hawafanikiwi katika maisha na wanakumbwa na changamoto nyingi. Wahusika hawa ni kama Mzee Zuberi, Pili, Semeni, Amina, Biti. Daudi, Dude, Latifa na wengine. Anaonyesha kuwa uzinzi na uasherati ni wa hali ya juu katika jamii anayoilenga katika utunzi wake (uk.25).

Amina, mke wa Zuberi ni mwasherati kwani anafanya mapenzi na Dude na kujifanya kuwa amemwajiri kazi na wengine wengi hata analetewa vijana barubaru na Bushiri naye anampa fedha. Dude naye ni mzinzi na mwasherati; anashiriki ngono kabla ya ndoa na hata baada ya ndoa yake na Shemsha. Hata baada ya kuapa kuwa hatashiriki uasherati tena, anafanya mapenzi na Latifa na kumpachika mimba ilhali ni dadake mkewe. Katika kilele cha kufichuliwa kwa maovu haya yote, mapinduzi ya ghafla yanatokea ambapo nyumba ya Zuberi inachomwa na Amina na Biti Daudi kuuawa japo Zuberi alikuwa ameaga dunia hapo awali.

Mtunzi anaonyesha kuwa licha ya jamii kujaa uozo huu wa hali ya juu, kuna matumaini ya kujenga jamii mpya inayozingatia maadili. Anafanya hivyo kwa kuionya jamii kuwa watendao matendo maovu watapata matokeo maovu kupitia kuporomoka na kuuawa kwa hivyo warekebishe maovu yao.

Aidha, mtunzi anazungumzia unafiki wa kiwango kikubwa. Unafiki ni kujifanya kuwa rafiki na hali ni adui; hali ya kutokuwa mkweli. Hutumika mara nyingi katika dini kumaanisha hali ya kujifanya msalihina ilhali wewe kwa kweli si mcha Mungu kwa nia ya kuonekana mwema mbele ya jamii. Wahusika kama vile Zuberi na Bi Amina wametumika kama kinywa cha mwandishi kuelezea unafiki ulioko katika jamii yake. Kwa mfano, tunaona jinsi anajifanya kuwapa masikini misaada ilhali tunajua kuwa yeye ni mkandamizaji. Pia kupitia kwa Bi Amina anajifanya kumpenda Dude lakini baadaye

anamnyang'anya ufunguo wa gari kwa sababu ya uamuzi alioufanya wa kumsaidia Baya wa kumpeleka hospitali licha ya amri ya Amina kutofanya hivyo na alikuwa bosi wake.

Kuhusu ulevi mtunzi anaonyesha kuwa unapotosha jamii na ndio sababu wahusika waovu amewasawiri kama walevi kupindukia. Ulevi ni hali ya kupotewa na fahamu kwa sababu ya kutumia pombe na madawa ya kulevya. Aidha ni hali ya kutumia vileo kama vile; pombe, chang'aa na madawa ya kulevya ambazo dalili zake ni unywaji wa pombe kupindukia. Anasawiri walevi kama vile. Pili, Baya, Semeni, Dude na Bushiri. Anaonyesha jinsi jamii yake inakumbwa na ulevi kiasi cha kudhoofisha afya ya wanajamii kama anavyotuarifu kuhusu afya ya Semeni na mwishowe Semeni anaaga dunia kwa sababu ya ulevi wake.

Kuhusu wizi mtunzi anaonyesha kwamba hutekelezwa na vijana waliokosa kazi na kwa hivyo ili kukidhi mahitaji yao wanatumia mabavu kuibia wenzao huku wakihatarisha maisha yao. Hawa wanaoiba wanaenda jela wakitoka huku hawaachi kuiba na kwa hivyo imani yake ni kuwa wanaiba kutokana na ukosefu wa mahitaji ya kimsingi. Anadhihirisha mtazamo wake kuwa mfumo wa kibwanyenye ukirekebishwa na hali ya kiuchumi kuwa bora basi wizi hautakuwepo.

Aidha, Mohamed anaonyesha imani yake kuwa kutokuwa na mapenzi ya kweli kupitia kwa Dude anapomuoa Shemsha na licha ya kuapa kuwa hatatoka nje ya ndoa kamwe anafanya mapenzi na Latifa dadake Shemsha na kumpachika mimba. Kwa upande

mwingine tunaona akituarifu kuwa mapenzi kati ya Dude na Shemsha yalikuwa ya kweli (uk.156). Hii inaonyesha hali ya itikadi tawala ya kimwinyi iliyotawaliwa na uongo, unafiki na uozo wa kila aina. Mtunzi anaaridhia kuwapo kwa mapenzi ya dhati, ambayo ingawa ni muhali kupatikana yanaweza kuwapo hasa anapoonyesha Shemsha akimpenda Dude pamoja na udhaifu wake wote na anahimiza marekebisho ya kitabia kwa upande wa wahusika kama Dude. Kwa wahusika kama Shemsha anaonyesha wamekubali hali kama ilivyo kufungamana na mawazo ya Antonio Gramsci (1985) ya ukubalifu na ukawaida.

5.2.1.9 ASASI ZA UTAWALA

Althusser (1981) anasema kuwa kuna asasi tofauti za utawala ambazo huendeleza itikadi za kitawala. Asasi hizo ni elimu, dini, mahakama, vyombo vya habari, vyama vya kisiasa na vyama vya wafanyakazi kati ya nyinginezo. Asasi hizi za utawala nahuhalalisha mifumo ya kitawala iliyopo ama kwa njia za ukubalifu au kwa matumizi ya nguvu kama vile jeshi na polisi. Asasi hizi za kitawala zinatumiwa kuzima juhudi za wanyonge wasitete haki na usawa. Nao utawala na asasi zake hujinasibisha na tabaka lenye nguvu za kiuchumi. Njogu (1997) anasema kuwa kule Zanzibar visiwani, utawala wa Kiingereza ulishirikiana moja kwa moja na Waarabu pamoja na mabepari wenye viwanda.

Sheria ni kanuni zinazotungwa na bunge la nchi fulani ili kusimamia taratibu za nchi hiyo na ambazo ni lazima zifuatwe na watu waliomo humo. Anayekwenda kinyume nazo, hupewa adhabu na mahakama ya sheria za nchi hiyo. Sheria katika jamii yake

inatumiwa kuwakandamiza wanyonge na kuwalinda mabwanyenye. Wahusika kadha wametumika kama kinywa cha mwandishi kuwasilisha haya. Kwa mfano, Mzee Zuberi kumnajisi Semeni (uk. 11) na hakuna sheria anachukuliwa na mahakama ama hata kufikishwa mahakamani. Isitoshe, Zuberi anamwagiza Mzee Omari amletee binti yake ili washiriki kitendo cha ngono. Ingawa hii inaonekana wazi kuwa ukiukaji wa haki za mtoto wa kike, Mzee Zuberi hayajali haya maana anajiona kuwa juu ya sheria. Kupitia kwa Zuberi, mwandishi anaonyesha tajiri kama mwenye haki ya kutenda lolote lile mradi atimize haja zake na sheria haizingatiwi.

Aidha, wale mahabusu walioko jela kwa matendo yao maovu kama vile wizi wanadhihirisha mtazamo wa mtunzi kuwa sheria ni ya wanyonge au maskini na walala hoi. Hii ni kutokana na sababu kuwa wote ni watu wa tabaka la chini ilhali wale wa tabaka la juu hawashikwi na kufunguliwa mashtaka. Licha ya hayo Bushiri ana uzoovu kujitia hatiani ili arudi jela anusurike. Anasema hivi, “Niliona bora utumwa wa kuwa mfungwa kuliko kuwa wa uhuru katika ulimwengu ambao hauwezi kunipa chakula” (uk. 3). Mwandishi kupitia kwa Bushiri anaonyesha jinsi haki za kimsingi za mnyonge zinakiukwa na kubaki kuwa ndoto. Hii inamaanisha kuwa sheria ni asasi tu ya kusaidia tabaka tawala kutawala wala si za kutekeleza haki. Hutumiwa kulinda maslahi ya mabwanyenye na kuhalalisha mifumo mibaya ya kiuchumi kwa kuhalalisha matajiri na nafasi zao za kiuchumi ili yeyote anayepigania haki zake anaonekana kuwa anakiuka sheria.

Kuhusu haki ambayo ni hali ya kuwa na usawa kwa kila binadamu mtunzi anaonyesha kuwa mnyonge anaonekana kunyimwa haki zake. Wahusika ambao ni walalamikaji ambao wamefika kwa madhumuni ya kuwasilisha malalamiko yao kwa Bwana DC hawahudumiwi na wanapuuzwa. Ni haki yao kuhudumiwa tena wamekuja hapo mara nyingi na kutembea kwa mwendo mrefu. Aidha Bwana DC anasawiriwa kama mwakilishi wa serikali dhalimu ya kimwinyi na hutumiwa kuendeleza itikadi ya watawala. Watu wakimuona tu wananyamaza na kunyenyekea ati ni utiifu lakini kwa hakika ni uendelezaji wa itikadi tawala ya kimwinyi.

Aidha tunaelezwa kuhusu mzee Shibu, mdai kodi ya viwanja vya Bwana Zuberi alivyopigania nchi katika vita vya pili vya dunia na aliporudi kwao hakutuzwa kwa vyovyote vile (uk:15). Hili linaonyesha jinsi wanyonge wanakandamizwa na kunyimwa haki zao katika jamii hii. Mtunzi pia ameonyesha kuwa wanyonge wenyewe wanakiuka sheria na kujihusisha na vitendo viovu. Kwa mfano Bushiri anaiba kwa kutumia mabavu na kufungwa jela mara kadhaa na kuhatarisha maisha yake. Aidha kina Dude, Baya, Pili na wengineo ni waasherati wakubwa. Wao wanakiuka haki za wanyonge kama wao na hivyo ukiukaji wa haki si tendo la matajiri tu bali la masikini pia.

5.2.2.0 ITIKADI YA MWANDISHI

5.2.2.1 ITIKADI YA MAPINDUZI

Mtunzi S. A. Mohamed anaongozwa na itikadi ya mapinduzi katika riwaya ya *Asali Chungu*. Anaonyesha kuwa kwa kurekebisha asasi za itikadi ya kimwinyi zenyewe kutafanya hali kuwa bora kwa watu wote. Itikadi hii inajitokeza kutokana na marekebisho anayoaridhia yafanywe katika asasi za kimwinyi kama mfumo wa kiuchumi, matabaka, elimu, utamaduni, dini, mfumo wa kuumeni, asasi za utawala, ndoa na mapenzi kati ya asasi nyinginezo. Itikadi anayoaridhia ni kuwa marekebisho ya asasi hizi yatabadilisha hali na hivyo haonekani kuamini katika mapinduzi ya nguvu bali mapinduzi ya marekebisho. Ndio sababu hata mapinduzi yanayotokea mwishoni mwa riwaya ni ya ghafla bila maandalizi yoyote wala mwongozo ufaao.

Njogu (1997) anasema kuwa mapinduzi huweza kutokea kama watawala hawazingatii hali mbalimbali za kijamii aidha kutokana na mapuuza au kutojali hali hizi. Mara nyingi watawala huwa wanafahamu udhaifu wa uongozi wao lakini hawarekebishi kwa sababu ya mivutano ya kisiasa, kiuchumi na kijamii ambayo huwa imeletwa na utawala huo. Dalili za udhaifu wa utawala hujitokeza katika mambo kama uvumi, malalamiko, maandamano, migomo na mwishowe huweza kulipuka na kuwa mapinduzi. Ni imani ya mtafiti kuwa mara nyingi utawala hushindwa kuchukua hatua madhubuti kwani huwa ni washirika wakubwa katika ukandamizaji. Wakati mwingine, kufaulu kwa mapinduzi katika nchi nyingine huenda kukachochea mapinduzi katika nchi nyinginezo kama

ilivyofanyika katika nchi za kiarabu kama Tunisia, Libya, Misri kati ya nyinginezo miaka 2010 na 2012 ambako mapinduzi ya kisiasa yalishuhudiwa pakubwa.

Itikadi hutekeleza nafasi kubwa katika mapinduzi ya aina yoyote kwa kumulika maovu ya tabaka tawala na kuwafanya wale wanaonyanyaswa wajihisi kitu kimoja na wawe na malengo na dhamira zinazowiana. Aidha, itikadi huwafanya wengi wao kujitolea mhangana na kuamini kuwa hata wao wenyewe wakifa, watakuwa wamechangia katika harakati za ukombozi na kuamini kuwa hali itakuwa bora zaidi mapinduzi yanapofanyika. Utabaka pia huchangia pakubwa katika kuleta mapinduzi kwani matabaka tofauti huzua mivutano inayoleta uhasama na chuki na uadui mkubwa kiasi kwamba wanaonyanyaswa huamua kulinda nguvu zao kwa kujihami kwa kila namna.

Nalo tabaka tawala hukazania kupinga na kudhibiti wafanyakazi na wale wanaonyanyaswa kwa njia zozote zile aidha kwa matumizi ya nguvu au vyombo vya kiitikadi kama Althusser (1981) asemavyo. Wakati mwingine hufaulu na kuleta dhana ya ukubalifu au ukawaida kama Gramsci (1985) asemavyo au kwa matumizi ya itikadi kama za kidini kama dhana za majaliwa ambazo hupumbaza watu wakashindwa kujipigania kama Marx (1973) asemavyo. Watawala wakishindwa hutumia polisi, mahakama na sheria kuhalalisha hali hizi lakini mapinduzi hutokea mwishowe kwani daima mnyonge hawezi kukandamizwa milele kama Kamunde (1983) anavyodhihirisha.

Kulingana na mwandishi, mfumo huu wa kiuchumi wa kibwanyenye na unyanyasaji ndio uliotawala katika *Asali Chungu*. Visa vingi katika riwaya hii vinaonyesha unyanyasaji kwa wanyonge, kama vile wafanyakazi, na pia wanajamii wengine. Kwa mfano Bi. Mkasi amesawiriwa akiwaza kuhusu jinsi kazi zimeongezeka katika nyumba na malipo yake halipwi na hata kama chama chao cha Waafrika kimo katika njama ya kuchukua mamlaka kwa nguvu hakuyashughulikia maneno hayo (uk175). Jambo hili linaonyesha jinsi mwandishi anaamini katika mapinduzi lakini yale ya kurekebisha mfumo wa kiuchumi ili uhuru na haki za mnyonge zipatikane katika jamii.

Baadaye ghasia hii ambayo inatokea mwisho wa riwaya (uk.386) inaonyesha itikadi ya mwandishi ya kuwa anaamini katika marekebisho ya asasi hii ya mfumo wa kiuchumi wala si kuubadilisha kabisa na ndio sababu mapinduzi haya yanachelewa na yanatokea ghafla bila maandalizi mwafaka. Aidha, wafanyakazi hawatetei wala kufahamu haki zao na hata kina Dude ambao hawakuuawa hawajapevuka kiasi cha kuongoza mapinduzi. Jambo hili linadhihirisha kuwa imani ya mtunzi kuhusu mapinduzi si imara na pevu; anaamini umuhimu wa marekebisho ya asasi wala si mapinduzi ya nguvu.

Kuhusu matabaka itikadi ya mtunzi ni kuwa jamii yenye usawa ni jamii ambayo haina utabaka. Anaona kuwa mfumo wa kiuchumi ukirekebishwa basi utabaka nao utaisha kwani huletwa na mfumo wa kiuchumi wa kibwenyenye. Mohamed anaonyesha kuwa mfumo wa kiuchumi uliokuwapo ulifuata itikadi tawala ya kimwinyi ambapo matajiri kama vile Zuberi wanamiliki mashamba makubwa na wanaishi katika jumba la kifahari

ilhali kina Semeni, Dude, Shaabani kati ya wengine wanaishi katika hali ya umasikini mkubwa. Itikadi ya mwandishi ni kuwa mfumo huu ufanyiwe marekebisho kwani masikini walihitajika kutoa jasho lao ili kufanya kazi mashambani mwa mamwinyi huku wakitozwa kodi. Mamwinyi nao waliwatumia manokoa waliojiona wamekaribiana na mamwinyi na kuwa hata wajeuri zaidi. Mohamed anaamini kuwa mfumo huu wa kiuchumi sharti urekebishwe ili ukandamizaji usiwepo. Hata hivyo kwa kukosa kuwaleta wafanyakazi pamoja na kuwapevusha kifikra viongozi waasi ambao wanaweza kufanikisha mapinduzi, ni msimamo wa mtafiti kuwa mwandishi katika kipindi hiki cha uandishi wake aliamini katika marekebisho ya mfumo wa kiuchumi na anaamini kuwa marekebisho haya yanaweza kufanywa na uchumi ukawa mzuri na hali ya maisha ya kina Dude, Bushiri na wengineo ikawa bora.

Mtunzi anaamini kuwa mfumo wa kiuchumi unaoleta utabaka unafaa kufanyiwa marekebisho ili kujenga jamii yenye usawa. Hii inajitokeza kutokana na kuwa Mohamed hasisitizi nafasi ya urazini wa kitabaka katika mapinduzi (Njogu, 1997). Mivutano na mikutano ya kisadfa ndio imepewa nafasi kubwa na hakuna makundi ya waasi wala jitihada za pamoja za kabadilisha mfumo huu. Ni msimamo wa mtafiti kuwa Mohamed anafanya hivyo kutokana na itikadi yake ya marekebisho hivi kwamba katika *Asali Chungu* anaamini kuwa utabaka unaweza kupunguzwa kama mfumo wa kiuchumi utarekebishwa ndio sababu hapendekezi mapinduzi moja kwa moja hata yanapotokea mwishoni mwa riwaya ni jambo la kisadfa tu, hamna maandalizi wala

waasi ambao wanaongoza wenzao kifikra waweze kuyafanikisha. Yamechopekwa ghafla.

Msimamo wa mtunzi kuhusu elimu ni wa kimapinduzi. Anaonyesha kuwa elimu ilitumiwa kuwachuja watu na kuwaweka katika matabaka fulani ili watekeleze majukumu ya kitawala na kufungamana na mawazo ya Althusser (1981) kuwa elimu ni kigeu kikubwa cha kuendeleza itikadi ya tabaka tawala. Wale walio katika matabaka ya juu waliendelea kupata elimu na kazi za hadhi nzuri kama watoto wa Zuberi, Shemsha na Latifa ilhali waliokosa elimu kama Dude, Semeni na Pili walilazimika kufanya kazi za kijungu-jiko zilizojaa hatari kama vile ukuli na uchukuzi. Mohamed anashikilia kuwa elimu ilikuwa na nafasi kubwa sana katika kuwaelekeza watu kwenye kazi za kitaalamu. Waafrika walipata elimu duni lakini Waarabu na Wahindi walipata elimu nzuri jambo lililowahakikishia kazi zenye hadhi ya juu, kama Zuberi ambaye ni mkuu wa Wilaya na Mukri ni Afisa wa Leba. Mtunzi anaonyesha kuwa ni muhali mfumo wa elimu ufanyiwe marekebisho kwani ndio ulichangia pakubwa kuleta utabaka na ulitumika katika itikadi tawala ya kimwinyi kuwabagua watu na kuwaweka katika matabaka tofauti na kuendeleza mfumo wa utawala wa kimwinyi. Anaamini kuwa mfumo huu ukirekebishwa basi watu kama vile Dude, Bushiri, Semeni kati ya wengineo wangepata kazi nzuri na hivyo hawangefanya maovu waliyoyafanya kutokana na matatizo ya kiuchumi.

Mtunzi anaamini kuwa uchawi na ushirikina ni mambo ambayo ni maovu na hutumiwa na watu waovu kufikia malengo yao. Anadhihirisha kuwa ni mambo yanayoaminiwa na watu wengi wakiwemo wa tabaka la juu mradi wapate kile wanachotafuta. Mohamed ana imani kuwa utamaduni wa aina hii unapaswa kurekebisha ili watu waweze kuwa na usawa. Anaona kwamba utamaduni hutumiwa na mfumo wa kimwinyi kuhalalisha vitendo vyao kama vile Zuberi kumnajisi Semeni kwa kuhisi kwamba lazima angeshiriki naye ngono kwani ni jambo la kawaida, yeye hajawahi kukataliwa na mwanamke. Mawazo haya yanafungamana na mkabala wa Gramsci (1981) kuhusu itikadi kuwa huweza kuendelezwa kwa utamaduni na kuleta hali ya ukawaida na ukubalifu. Watu hufikiria kuwa ni sawa kwa watu kutenda mambo fulani kwani ni utamaduni wao. Dhana hii ya utamaduni inaendelezwa zaidi katika mfumo wa kuumeni na dini tunaojadili katika sehemu ifuatayo.

Mohamed anadhihirisha namna mfumo wa kuumeni unaoshadidiwa na itikadi tawala ya kimwinyi inayompendelea mwanamume na kumfanya mwenye mamlaka na bosi. Basi mwanamke huonekana kama ndiye muovu zaidi na mkosa katika jamii. Hivyo imani ya mtafiti ni kuwa itikadi tawala ya kimwinyi ndiyo inayochangia zaidi kuuendeleza na kuudumisha mfumo wa kuumeni, kule kupenda kuhodhi mali na mamlaka. Hivyo mwanamke katika ndoa hupaswa kunyenyekea na kuchangia raha na starehe za mumewe kwani ni sehemu ya mali zake. Mohamed anaamini kuwa mfumo wa kuumeni huelekezwa na mifumo ya kiuchumi kufungamana na maelezo ya Karl Marx (1973),

matumizi ya nguvu na vyombo vya kiitikadi kama Louis Althusser (1981) na ukubalifu na ukawaida kama Antonio Gramsci (1985) anavyosema.

Hii ni kutokana na dhana kuwa kuna wahusika wa kike wanaonyanyaswa kwa misingi ya kiuchumi kama vile kufanya ngono ili wapewe fedha na vitu kama nyumba, kuna wale wanaonyanyaswa na mfumo huu kwa matumizi ya nguvu kama Semenini kunajisiwa na Zuberi na kuna wale wanaonyanyaswa kwa kukubali tu na kuona hiyo ni hali ya kawaida kama Kabore na Ruki kati ya wengineo. Hili linadhihirisha kwamba itikadi ya mfumo wa kuumeni haitokani na mfumo ya kiuchumi na ung'amuzi potoshi pekee kama Karl Marx alivyodai bali itikadi hii hutokana na mikabala tofauti. Katika *Asali Chungu* mfumo huu wa kuumeni ni kigeu mojawapo cha kuendeleza itikadi ya kimwinyi yaani utiifu kwa upande wa wanaonyanyaswa na ubadhirifu, raha na starehe kwa wenye mamlaka.

Itikadi ya mtunzi kuhusu maadili ya kijamii ni kwamba utovu wa maadili kama vile ulevi, wizi, uasherati na unafiki unatokana na mfumo mzima wa kimwinyi na hivyo asasi za mfumo huu zikifanyiwa marekebisho, maaadili yatatawala. Hili linadhihirika anapomsawiri Dede licha ya kuhusika katika maovu kama uasherati kuwa chanzo cha matumaini ya wanyonge kupitia mimba aliyompachika mke wake. Aidha, hakuuawa kina Amina wakiuawa wakati wa mapinduzi watenda maovu wengine wakiuawa.

Kuhusu unafiki anaonyesha kuwa wanafiki wataangamia lakini pia washirika wa unafiki kama Dude na Shemsha dadake Latifa ni wanafiki na hawaadhibiwi kwa hivyo wajirekebishe. Kuhusu wizi Mohamed anaaamini marekebisho ya mfumo wa kibwanyenye na kufanya uchumi kuwa bora, jambo litakalopunguza wizi na watu kama vile Bushiri kuweza kuwa na maadili. Anaonyesha kuwa fasihi ni kielelezo cha maadili ya jamii kwa wakati maalum na hivyo yeye kama mtunzi anaelezea maadili hayo kwa mapana na marefu ili kazi yake iwe faafu kwa jamii yake, kufungamana na nadharia ya kimaadili.

Itikadi ya mwandishi katika riwaya hii kuhusu dini ni kwamba inatumiwa kuwapumbaza wanyonge wasione hali halisi ya maisha yao na kufungamana na mawazo ya Marx (1973) kuwa dini huwa ni kigeu kikuu kinachotumiwa na watawala kuwakandamiza watu kwa kuwafanya wakubali dhana ya majaliwa yaani maisha yameratibiwa na Mungu. Aidha, Althusser (1981) anaonyesha dini kama asasi ya kitawala inayoleta utiifu na hivyo Gramsci (1985) kusema kuwa utiifu huu hujitokeza kama ukubalifu na ukawaida; kuamini kuwa hali ilivyo ndivyo inavyopaswa kuwa haiwezi kubadilishwa, jambo kuu ni kutii na kunyenyekea.

Mohamed anaona kuwa asasi hii inapaswa kurekebishwa yaani watu wazingatie yale wanayohubiri na maisha yatakuwa mema. Hili linaendelezwa kupitia kwa mhusika Dude anayesema kuwa kama Mungu yupo, kwa nini anawatukuza wengine na kuwaruhusu wengine wateseke. Ingawa ana uchungu na shaka kuhusu Mungu,

mwishowe anasema yeye tu ndiye mwenye uwezo ingawa anaona kwamba maisha yamejaa tofauti kwa sababu aliyeyaumba hakuziondoa.

Hili linadhihirisha kuwa mtunzi anaamini dini inahitaji marekebisho ili iwe suluhisho la kweli kwa mhusika kuchukua hatua madhubuti ili aweze kuboresha maisha yake. Kwake yeye ni kama dini inatumiwa kama kitulizo kutokana na kushindwa kutatua matatizo na kwa msimamo wa mtunzi kujificha katika dini na kungojea hali iwe bora hakusaidii chochote. Hali hii inaambatana na itikadi yake katika mapinduzi ya marekebisho ya asasi mbalimbali za mfumo wa kimwinyi kwani dini inatumiwa na mamwinyi kuhalalisha matendo yao na kuwafanya waonekane wema. Kwa mfano, Zuberi anakimbilia dini baada ya kutenda vitendo vya unyama lakini anapokaribia mauti anajaribu kujitakasa na kufanya hali yake ionekane kuwa bora. Aidha, Latifa aliteremka chini kwenda kuwapa sadaka masikini wa Mungu ilhali yeye anafanya mapenzi na Dude, mume wa dadake.

Kwa ujumla, mtunzi anaonyesha kuwa anaelekezwa na mawazo ya Marx (1973) na (1977) kuwa dini ni ung'amuzi potoshi. Dini huwadanganya watu tu ili waamini hali zao ni tofauti ili kukwepa matatizo yanayowakabili badala ya kukabiliana nayo hasa matatizo ya kiuchumi na hivyo kuamini hali inayowakumba ni majaliwa na hawawezi kuibadilisha. Kwa hivyo msimamo wake kuhusu dini ni kuwa ni mwongozo mwema maishani ambao humsaidia binadamu kujilinda kutokana na kutenda maovu kama Semen alivyofanya na hivyo asasi hii ikirekebishwa na kutumiwa vyema inaweza

kumwongoza binadamu na kuyafanya maisha yake kuwa bora. Maoni ya mtafiti ni kuwa Mohamed anafanya hivyo katika juhudi za kuifanya kazi yake kuwa faafu kwa jamii yake kuambatana na nadharia ya kimaadili kuwa fasihi ni zao la jamii ambapo dini ilitumiwa kama chombo cha kujificha na imani ya kidini ikatumiwa ili kudhibiti watawaliwa wasiuone ukweli kama Marx (1973) alivyosema na pia kama chombo cha utawala kama Althusser alivyosema (1981).

Mohamed anaamini kuwa asasi za kiutawala zinahitaji kufanyiwa marekebisho ili ziwafae wananchi badala ya mfumo wa utawala wa kimwinyi uliokuwapo. Anawasawiri watu wanapoenda kwa mkuu wa Wilaya Bw. Zuberi ambaye amesahau wajibu wake kwa wananchi na hatekelezi wajibu huo. Asasi hii inatumiwa na utawala wa kimwinyi kuwanyamazisha watu ambao wanabakia kulalamika kufungamana na Althusser (1981) anayeorodhesha watawala kama sehemu ya uendelezaji wa itikadi tawala. Watu wanapoambiwa waende nyumbani warudi kesho hawafanyi maandamano ama hata kuingia kwa nguvu ofisini isipokuwa Pili peke yake naye alikuja tu kuulizia kuhusu Semenji mtoto wake kuonyesha itikadi ya mtunzi kuwa watawala hutumiwa kuwanyamazisha watu waendeleo kuwa watiifu na wanyenyekevu. Asasi hii ya utawala ni mbaya lakini ikifanyiwa marekebisho itakuwa sawa.

Kuhusu mahakama na sheria ambayo Althusser (1981) anaorodhesha kama mojawapo ya vigeu vitumikavyo kuendeleza itikadi tawala, ni msimamo wa mtunzi kuwa

ifanyiwe marekebisho ili haki iweze kutekelezwa. Haiwasilishi kama asasi inayopaswa kuondolewa kabisa kimapinduzi kwani hatuoni maandamano yoyote au juhudi zozote za kuwaelimisha watu kuhusu haki zao na mifumo ya sheria, katiba, vyama vya kisiasa, na kadhalika. Ni imani ya mtafiti kuwa Mohamed anafanya haya kwa sababu ya imani yake katika marekebisho ya asasi za utawala wala si kung'oa na kupindua kwa nguvu kabisa mifumo ya utawala ya kimwinyi na vigeu vinavyosaidia kuendeleza itikadi tawala ya kimwinyi ili kazi yake iwe faafu kwa jamii yake na kujitambulisha nayo.

Aidha, kwa kudhihirisha mikabala mbalimbali kuhusu itikadi kama mkabala wa Marx (1973) ya ung'amuzi potoshi, mkabala wa Althusser (1981) kuhusu vyombo vinavyoendeleza itikadi, mkabala wa Gramsci (1985) kuhusu ukubalifu na ukawaida, ni dhahiri kwamba matini huwa na mielekeo mingi na inaweza kuwa na fasili nyingi kwani maana ni telezi kufungamana na nadharia ya udenguzi. Ni kama Derrida (1976:102) asemavyo kuwa “kila matini huwa na maana nyingi na usomaji wowote wa matini lazima uzingate jambo hili’.

5.3.0 ITIKADI KATIKA KIZA KATIKA NURU

Katika sehemu zilizotangulia katika sura hii mtafiti amejadili itikadi zinazojitokeza katika riwaya ya *Asali Chungu*. Imebainika kwamba, itikadi kuu inayotawala ni itikadi ya kimwinyi iliyojitambulisha kwa vipengele kama mfumo wa kichumi, utabaka, elimu, utamaduni, mfumo wa kuumeni, ndoa, dini, maadili na asasi za utawala.

Mohamed anaamini kuwa asasi zote zinazoendeleza itikadi tawala ya kimwinyi zifanyiwe marekebisho na hivyo kujitokeza kuwa anaaridhia itikadi ya kimapinduzi ya marekebisho. Aidha, mikabala mbalimbali kuhusu dhana ya itikadi imedhihirika katika *Asali Chungu* na kuibua uwezekano wa matini kuwa na fasili nyingi kwa mujibu wa nadharia ya udenguzi. Katika sehemu hii, mtafiti anajadili itikadi zinazojitokeza katika riwaya ya *Kiza Katika Nuru* ili kuweza kubaini ikiwa mtunzi anabadilisha itikadi hizi au la na ikiwa amefanya hivyo ni mambo yapi yanapelekea mabadiko haya.

5.3.1 MTIRIRIKO WA VITUSHI KATIKA KIZA KATIKA NURU.

Riwaya hii inaanza na ugomvi baina ya Bwan Juba na Mvita ambao ni mwana na babake ambaye pia ni bosi wake kazini. Hali hiyo inapelekea Mvita pamoja na Salma mchumbake kufutwa kazi. Juba pia anamfukuza Mbishi mwanawe wa pili nyumbani baada ya mabishano hasa alikuwa amemchora ukutani. Mkewe wa kwanza Kudura ametelekezwa kwani Bwan Juba anamshughulikia zaidi Bi Khalitty. Kudura analazimika kukopa ili angalau kumwandalia mumewe Juba chakula anapokuja kutembea. Mvita anapofutwa kazi anafanya kazi za viwango vya, chini jambo linalompa nafasi ya kutangamana na watu wa tabaka la chini na anaanza juhudi za kuwazindua. Anaenda kumtembelea mamake mara moja moja na kujaribu kumzindua aweze kutetea haki zake. Baadaye Kudura anazinduka hasa kutokana na kushuhudia Biti Japu akipigana na muuza nyama alipotaka kukataa kuwauzia nyama na kuwauzia watu mashuhuri akiwepo Shehe anayejitia hamnazo. Bwan Juba anapokuja kumtembelea, Kudura anamwandalia chakula lakini Juba anamtusi ndipo Kudura anaporudi jikoni na kurudi na pauro tayari

kukabiliana na huyu Juba mumewe ili autetee ubinadamu wake. Anazuiliwa na marafiki wa Bwan Juba, Mzee Hussein na Mzee Kidambwe.

Baadaye Bwan Juba anamfukuza nyumbani na anakwenda kuishi na watoto wake. Mvita anafanya juhudi kuwazindua wafanyakazi na wananchi na wanapofanikiwa, babake Juba anaogopa na kumuua kupitia kwa Shazia. Baadaye, Kudura na Mbishi wanamuua Juba kwa ushirikiano na Kitwana na Baker, lakini wanafikishwa mahakamani pamoja na Salma kwa mashtaka ya mauaji. Salma ameshitakiwa kwa mauaji ya Mvita naye Mbishi na Kudura wameshitakiwa kwa mauaji ya Bwan Juba. Kudura anajiua akiwa gerezani lakini kuna matumaini kwamba Salma ataachiliwa huru na kwa sababu ana mimba ya Mvita. Kuna matumaini kwamba kizazi kipya kitazaliwa kuendeleza harakati za kupigania haki na usawa hasa kupitia kwa barua anayopata akiwa gerezani kuwa watu wanamngojea aachiliwe ili waendeleze harakati za kutetea maslahi yao. Kwa ujumla ni kwamba kuna wahusika wa tabaka la juu kama Bwan Juba, Bw. Fadhili na Bw. Mtoro ambao wanafaidika na mambo kama yalivyo na hawataki mabadiliko ya mfumo wa utawala ulioachwa na wakoloni, yaani utabaka una nguvu hata kuliko familia.

5.3.2.0 ITIKADI YA KIBEPARI

Itikadi kuu inayojitokeza katika *Kiza Katika Nuru* ni itikadi ya kibepari. Itikadi hii inajidhihirisha kwa makali yake ya ukandamizaji kupitia vipengele kama vile mfumo wa kiuchumi, utabaka, elimu, utamaduni, mfumo wa kuumeni, ndoa na mapenzi, dini, maadili na asasi za utawala.

5. 3. 2. 1 MFUMO WA KIUCHUMI

Mfumo wa kiuchumi, ni mfumo wa mapato na matumizi ya watu katika nchi. Riwaya inapoanza tunapatana na Juba ambaye ana mali na cheo serikalini na kwa hivyo ni tajiri wa kutosha. Kadri ambavyo ni tajiri ndivyo anavyozidi kutaka zaidi na ndio sababu mojawapo kuu inayomfanya wapingane na Mvita mwanawe ambaye anaona kuwa babake anakosea kwa kuwanyanyasa raia na kujitajirisha yeye na aila yake. Bwan Juba haelewi vipi akamlea Mvita, na kumsomesha hadi Chuo Kikuu akitarajia kuwa yeye atakuwa mrithi wake anageuka na kuanza kumpinga. Mfumo wa kiuchumi unaoonekana kujitokeza ni ule wa kibwanyenye na kibeberu. Njogu (1997) anasema kuwa mfumo wa kibwanyenye ulijitambulisha kwa ubadhirifu na ufujaji miongoni mwa tabaka tawala. Maisha ya tabaka hili huwa ni ya matumizi tu. Jambo hili husababisha kuibuka kwa tabaka la kibepari na mfumo wa kiuchumi wa kibepari ukaibuka na kuzua tabaka la kibepari.

Ni katika mfumo huu wa ubepari ambapo riwaya ya *Kiza Katika Nuru* inaonekana kujengeka. Kwa mujibu wa ChuaChua (2011:28) kipindi cha 1986-92 kinadhihirisha mabadiliko kutoka kwa mfumo wa ujamaa hadi ubepari. Anasema kuwa “hiki ni kipindi ambacho viongozi waliweza kumiliki mali na kuzilinda kutokana na nafasi walizonazo” (uk.28). Jambo hili lilitokana na Azimio la Zanzibar ambalo lilionekana kutoa fursa ya kuongeza tofauti ya kipato kati ya aliye nacho na asiye nacho. Hali hii ilishuhudia ushindani wa viongozi katika kung’ang’ania mali na kuhodhi chochote watakachopata na

maadili ya viongozi yalionekana kutupiliwa mbali. Kilichothaminiwa ni mali na mali pekee ili kuendelea kuwa matajiri.

Katika muktadha huu, Juba anajaribu awezavyo kuhodhi mali kwa njia za magendo kwa kuwatumia vijana kama vile Baker ili aendeleo kujilimbikizia mali. Aidha, anamwambia Mvita kuwa:

Siye wewe niliyekutia chuoni kukujulisha Mungu wako?
Nikakupeleka skuli kukufungulia ulimwengu wako?
Halafu nikakupa uafisa wa maslahi ya nje ili upate kusafiri
sana, uchume, utukuke, ukue kiakili na uwe kama mimi
(uk:17).

Dondoo hili linaonyesha namna viongozi wa kibepari walivyokuwa kwamba baada ya kuhodhi mali kwa njia za magendo na wizi kama Bwan Juba iliwabidi watayarishe warithi wao ili kuendeleza tabaka tawala. Mvita hakubaliani na babaye, yeye anaona kuwa si vyema kuumiza watu walio wengi kwa maslahi ya kibinafsi. Wanapotofautiana na Bwan Juba anafutwa kazi kwa madai ya uchochezi pamoja na wafanyakazi wengine saba akiwemo Salma mpenzi wake. Aidha, anafukuzwa nyumbani na kuambiwa kuwa “Na kwangu pia usipite, usikutie mguu, nyumba uione paa....haya kwaheri mkorofi. Wewe na ulimwengu wako” (uk.25).

Jambo linalodhihirika ni kuwa, Bwana Juba yu radhi kupoteza mwanawe mradi ahifadhi mali yake na tabaka lake kifedha kudhihirisha makali ya mfumo wa kibepari. Kwa hakika, mwanzo anamtisha kuwa atamuua na mwishowe anamuua Mvita kupitia kwa

Shazia kuonyesha kuwa katika mfumo wa ubepari vigeu vingine havijalishi kama familia, dini au tamaduni. Kile muhimu ni mali na mali zaidi.

Aidha, Mohamed anatoa mawazo ya uyaakinifu wa kijamaa kuhusu uchumi. Katika mtazamo huu ambao ni wa Ki-Marx hali zozote katika jamii hutokana na mfumo wa kiuchumi na msanii huhitajika kuwasilisha hali halisi na mikinzano inavyojitokeza ili kuleta mapinduzi. Sanaa yaakinifu hutakiwa kumulika ukweli huo (Njogu 1997). Inavyodhihirika katika *Kiza Katika Nuru* ni kuwa mfumo wa kiuchumi ndio unaoonekana kusababisha mapinduzi yanayofanyika na kupelekea kuuawa kwa Bwan Juba. Walipobishana na Mvita na kumfukuza kazini, Mvita anaanza kufanya kazi bandarini kama kuli na kulima mihogo na kwa hivyo anapata nafasi ya kuwaelimisha na kuwaongoza wanajamii kwa kuwa sasa tabaka lake ni la chini na alikuwa amesoma, alielewa jamii yake. Mwishowe, Mvita anauawa kwa kile Juba anakiona kuwa kikwazo katika azma yake ya kuingia katika siasa ili aendelee kupata mali. Hata hivyo, mfumo wa kibepari unapozidi, watu huungana na kuubandua, jambo linalofanyika Juba anapouawa kwa ushirikiano wa Kudura na Mbishi kati ya wengineo. Hali hizi zote zinachangiwa na mfumo wa kiuchumi wa kibepari na makali yake ya ukandamizaji uliochukua nafasi ya umwinyi unaojitokeza zaidi katika *Asali chungu*.

5.3.2.2 MATABAKA

Matabaka ni sehemu ya mfumo wa uchumi na siasa yanayojitokeza ambapo kundi moja linamiliki nyenzo za uzalishaji mali huku jingine likimiliki nguvu zake tu. Tabaka la juu

humiliki mfumo wa uzalizi mali huku wafanyakazi wakiliki nguvu na uwezo wa kufanya kazi. Jambo hili huzua matabaka ya juu na ya chini ambapo tabaka la juu linalojumuisha watawala huendelea kuwadhalilisha walio chini kitabaka, kiuchumi hasa kwa matumizi ya itikadi za kiutawala na wakati mwingine matumizi ya nguvu. Nguvu za kitabaka huwa na uzito zaidi ya vigeu vingine vya kijamii. Kwa mujibu wa Marx (1973), matabaka huwa katika hali ya mikinzano na kwa sababu jamii daima ziko katika harakati za kufanya maslahi yao bora, mikinzano hii huleta mapinduzi na uongozi kuchukuliwa na tabaka la wafanyakazi kwa nguvu. Mivutano ya kijamii huchangia kuyaleta mabadiliko yanayohitajika katika jitihada za jamii za kilimwengu kuacha hali zao dhaifu, na kuukaribia utu kamili.

S. A. Mohamed anasawiri utabaka katika *Kiza Katika Nuru*. Mwanzoni mwa riwaya, tunakumbana na Juba ambaye anamiliki mali na ndiye mwajiri wa akina Mvita na Salma kati ya wengine. Tunaambiwa kuwa mali hii nyingi ilikuwa imepatikana kwa njia ya milungula, magendo na kuchukua pesa za kigeni na kuziweka nje (uk24). Licha ya kuwa Mvita ni mwanawe Juba, haafikiani na mawazo yake ya kuuendeleza utabaka. Yeye anaona kuwa ni muhimu kuwatendea watu wote haki. Anasema:

Hebu jitazame wewe babaangu unavyoishi, halafu mkadirie
mtu wa kawaida, kisha ujiulize uhalali wa mapato yako,
hakimu angetaka ushahidi gani?(uk. 24).

Linalodhihirika ni kuwa, Juba aliishi kwa utajiri mkubwa, na raha za kila aina jambo ambalo hujidhihirisha katika mfumo wa kibepari. Alikuwa anamiliki, kampuni na mali nyinginezo hasa nyumba yake kubwa aliyomjengea mke wake wa pili Bi Khaltiyy na

alitawaliwa na pupa ya kupata nyingine zaidi ndipo anashangaa Mvita anapoanza kupingana naye. Mohamed anaonyesha kuwa, utabaka ni adui mkubwa hasa katika mfumo wa kiuchumi wa kibepari ambapo utu na ubinadamu hauzingatiwi. Mvita anapofutwa kazi anabakia katika tabaka la chini kwa kulazimika kwenda kufanya kazi kama kuli na kulima mihogo hali inayomfanya aweze kupata nafasi ya kutangamana na mafalahi wengine wa ulimwengu.

Mohamed anaonyesha namna ambavyo tabaka la juu hutumia hila kama vile dini kuendelea kuficha ule uyanyasaji wao. Juba anajifanya Shehe wa msikiti wa Maweni na kuhubiri juu ya mapenzi na hata Mvita anapojaribu kuuliza maswali anakabiliwa na umma kuonyesha vile watu wa tabaka tawala huwa na mbinu za kiitikadi za kuhifadhi nafasi zao kama vile dini na mamlaka ya kiungu kama vile Marx (1973) anauita ung'amuzi potoshi na Althusser (1981) anaiita chombo cha itikadi. Watu wengi hawatambui kuwa Juba ni adui yao wala si Shehe ama kiongozi msalihina na mpenda Mungu anavyojifanya.

Aidha, kutokana na hali hii ya kitabaka, Juba anamfukuza Kudura baada ya kumtelekeza na kudai yeye ni mchafu, hajui kupika, anaishi mtaa duni, nyumba yake ni mbaya na chakula anachopika ni kibaya. Kudura ni kiwakilishi cha wanawake waliofanywa watumwa na mfumo wa kuumeni uliotumiwa kuendeleza itikadi tawala ya kibepari. Kudura anaonyesha namna mwanamke anadhalilishwa na mfumo huu hasa anapoamini kuwa hali yake hawezi akaibadilisha. Amemwachia maisha yake yote Mungu tu

ayaelekeze, kudhihirisha ung'amuzi potoshi kama Marx alivyosema. Kwa sababu ya kudhalilishwa wanawake walibakia katika tabaka la chini na hivyo Mohamed anaamini jinsia ya kike lazima ijasue kiuchumi na kisaikolojia kwa kupigania nafasi yao katika jamii.

Kwa kuwa wanajamii huwa katika harakati za kufanya hali zao kuwa bora zaidi, haina budi basi kuwa matabaka yanayowasilishwa na Mohamed yako katika hali ya mapambano na mivutano. Tabaka la juu liko katika mapambano ya kuhifadhi hali yao kwa kutumia njia zozote zile kama vile Mvita kuuawa na babake mzazi ili kuuhifadhi utabaka nao kina Mbishi na Kudura wanamuua Juba ambaye ni mwanawe na mumewe mtawalia. Hali hii inaonyesha namna itikadi ya mtunzi kuhusu utabaka ina mashiko kwamba kwake yeye nguvu za kitabaka na mivutano iliyomo inakiuka uhusiano mwingine wowote hata kama ni wa kifamilia.

S. A. Mohamed anaonyesha kuwa mivutano ya kitabaka pia huweza kupatikana katika tabaka moja kutokana na mashindano kati ya watu wa kundi hilo. Tabaka la chini huvutana hasa kutokana na kutoelewa adui halisi ndiye nani ambaye anasababisha udhaifu wao; aidha kutokana na ung'amuzi potoshi, vyombo vya kiitikadi au ukubalifu na ukawaida. Huvutana wao kwa wao na kuhisi kwamba wamemshinda adui hasa kama wamekosa mahitaji yao ya kimsingi. Mivutano hii inajitokeza hasa pale ambapo wanakijiji cha Maweni wanamfukuza Mvita anapotaka kuuliza swali msikitini (uk185).

Jambo hili linaonyesha namna hawa watu wa Maweni hawaelewi kuwa adui wao ni Bwan Juba na Mvita ndiye mtetezi wao na kudhihirisha ung'amuzi potoshi.

Kule kazini kwa akina Mvita ni wafanyakazi wachache waliofutwa kazi kwa kushirikiana na Mvita kutetea haki zao kuonyesha mivutano baina yao. Aidha, wale wazee waliomshika Kudura asimpige Bwan Juba ni wa tabaka linalokandamizwa kama Kudura lakini badala ya wamuunge mkono wanamshika na kumzuilia kumpiga Bwan Juba anayepata ujasiri na kumfukuza katika nyumba yake na kuenda kuishi na watoto wake Mvita na Mbishi. Wahusika kama Shazia pia ni wa tabaka la chini na ndio wanatumika kumuua Mvita kiongozi wa mapinduzi ya kitabaka ili wapate kipato kidogo. Mohamed anaonyesha kuwa si lazima wapiganiaji usawa wawe wanatoka katika familia masikini bali fikra za utu na ubinadamu zilizopevuka ndizo ambazo humsaidia kutetea watu. Pia, si lazima yawe yale mazingira alimokulia kinyume na anavyoonyesha katika *Asali Chungu*.

Mtazamo unaoafikiana na mawazo haya ni wa shule ya Frankfurt wa nadharia changanuzi unaoendelezwa na Theodor Adornal, Herbat Mercusen na Max Horkheimer. Walisema kuwa binadamu ni kiumbe aliye huru kifikra, anaweza kufikiria na kuamua hatima ya historia yake na kwa hivyo ana utu wake mwenyewe na anaweza kuibadilisha hali hiyo. Kwa hivyo, Mvita ingawa alikulia katika familia ya kitajiri, amepolekwa Chuo Kikuu na kupewa wadhifa mkubwa kazini na babake yu radhi kuacha, kuishi na tabaka la

chini kuwazindua na kuwaunganisha huku akijenga urazini kati yao ili waweze kubadilisha hali yao iwe bora si kudumu ikiwa dhaifu.

5.3.2.3 ELIMU NA KAZI

Mara nyingi mifumo ya kiuchumi hufungamana na elimu na kazi. Watu ambao hawana elimu hulazimika kufanya kazi za hadhi ya chini za kutumika na kuhudumia watu kama watumwa wao kwa kutii na kufuata lolote waambiwalu. Kinyume na hili ni kwamba watoto wa matajiri na mabepari walipata elimu nzuri kama vile Mvita, jambo lililomfanya kupata kazi nzuri. Hata hivyo anatofautiana na babake na kufutwa kazi hiyo, hali inayomfanya kutafuta kazi ambazo zilikuwa maarufu kule mijini za ukuli na uchukuzi (Njogu, 1997). Kwa sababu wafanyakazi wengi walikuwa hapa, ilikuwa rahisi kwake kutangamana nao na kuendeleza harakati za ukombozi. Elimu ndio inamsaidia Mvita kuendeleza harakati hizi. Ni kweli kuwa katika hali kama hii, wale watoto matajiri wanapata elimu nzuri na kazi nzuri. Wale wengi ambao hawakupata elimu hufanywa kuuza walicho nacho ili waweze kujikimu. Wanafanya kazi kama ya kuuza supu, maandazi, uji na kadhalika. Wengi wao huuza hata miili yao ili waweze kujikimu..

5.3.2.3 NDOA NA FAMILIA

Mtunzi anaonyesha ndoa kama kiungo muhimu cha jamii kinachofungamanishwa na utamaduni kama asasi ya kuendeleza itikadi tawala ya kibepari. Katika riwaya hii familia ya Bwan Juba imekumbwa na mikinzano mikubwa kiasi cha kuishia kwa tanzia ya

msururu wa mauaji jambo linalodhihirisha makali na ukatili wa ubepari. Kwanza Bwan Juba anamfukuza Mvita kazini kwani walitofautiana kiitikadi kuhusu namna ya kuendesha shughuli zao. Kwa maoni ya Bwan Juba kilichokuwa muhimu ni kuzoa mali na kuendelea kuhifadhi tabaka lao la kibepari ambapo aliona kuwa Mvita mwanaye alipaswa kufuata nyayo zake ili waendeleo kutajirika na kuhifadhi ubwana. Bwana Juba anashangaa kwani alikuwa amempeleka Mvita shuleni, akamfunza dini, alimpa uafisa wa maslahi ya nje katika kampuni yake, ili apate kusafiri sana, kutukuka, kukua kiakili, na kuwa kama yeye (uk. 17). Naye Mvita anaona kuwa ingawa ni kweli babake alimfanyia hayo yote si vyema kuendelea kuwanyanyasa watu wengine kwa sababu ya kujitajirisha yeye mwenyewe na aila yake tu. Anaona kuwa si vyema babake kuendelea na kula milungura, kufanya biashara za magendo na kuendelea kujilimbikizia mali ilhali raia wengine wanaishi kama makabwela. Wanapobishana, Bwan Juba anamfuta kazi na kudai kuwa anawachochea watu afisini na kumfukuza nyumbani (uk:25) na hata kumuua baadaye anapomuona kama kizingiti cha kumzuia kuwa mbunge.

Mbishi anafukuzwa nyumbani pia kwa kuzozana na babake kutokana na picha aliyoichora ukutani mwa nyumba kumdhihaki Bwan Juba na vitendo vyake vya magendo na wizi. Aliyebaki sasa alikuwa Kudura mkewe ambaye alikuwa akitaabika kila siku kwani alikuwa na watoto wadogo ambao baba yao hakuwajali wala kuwashughulikia kwani alikuwa ameo mke mwingine Bi Khaltiyyy ambaye alikuwa amemjengea jumba kubwa mjini.

Kudura mkewe Bwan Juba alimtii mumewe zaidi lakini alizinduliwa na Biti Japu walipokuwa wakinunua nyama na kuona namna alivyokuwa karibu kumchanja muuza nyama kwa shoka kwa kuwapuuza na kutaka kuuzia matajiri nyama. Bwan Juba anapofika nyumbani, anapewa chakula ambacho kwa hakika Kudura alikuwa amekopa huku akidharauliwa na wakopeshaji wake. Juba anamtusi na kumdharau. Kudura anaamua kupigana na Juba kwa kutumia pauro lakini mwishowe anafukuzwa nyumbani na kuenda kuishi na watoto wake. Familia nzima ya Bwan Juba imesambaratika na Juba baadaye anamuua Mvita, naye anauawa na Kudura na Mbishi na mwishowe Kudura anajiua. S. A. Mohamed anadhihirisha kuwa mbele ya uwezo wa kiuchumi na utabaka, familia ni asasi ambayo haina mashiko.

5.3.2.4 DINI

Dini ni imani kuhusu Mungu au miungu ambayo huchukuliwa kuwa ni ukweli na wanaoamini dini hiyo. Imani hii huonyesha kuwa kila kitu kimeamuliwa na Mungu na kazi ya binadamu ni kufuata tu amri itokayo kwa Mungu au miungu hiyo. Dini imetumiwa kuhalalisha ubwana na utwana, mbali na kuainisha majukumu ya mwanamume na mwanamke (Momanyi 1999). Aidha, Osore (2008) anasema kuwa dhana ya majaaliwa ni mojawapo ya falsafa ya majaaliwa ambayo imeendelea kutumiwa sana katika jamii nyingi za kiislamu. Dhana hii husema kuwa maisha humu duniani yashaandaliwa na Mungu na hivyo yeyote ambaye anaamini dini hii atakabiliana nayo na majaaliwa yao. Kwa hivyo, dhana hii hufasiriwa visivyo na kuelezwa kuwa kutokana na dini, mwanamke alipaswa kuvumilia mateso na madhila yanayompata kutoka kwa

mumewe kwani ni kudura yake. Aidha, dini huweza kutumiwa kuyaficha maovu ya watu wengi wakaonekana wema kutokana na unafiki wao na hali zao za nje. Inaweza kutumiwa kuwapumbaza watu wasiuone ukweli wa mambo yanayowaathiri huku wakiamini matatizo na madhila wanayopitia ni majaaliwa ya Mungu. Mungu mwenyewe atawapigania kwani kazi yao ni kutii amri za tawala zilizopo bila kudadisi kwani Mungu yupo na ni mjua yote na ameratibu kila kitu kitendeke kwa wakati wake.

Mhusika wake mkuu Bwan Juba, kando na kuwa tajiri mtajika, ni kiongozi wa serikali na bado ni shehe katika msikiti ulioko kijiji cha Maweni. Ingawa anashiriki magendo, wizi na udhalimu dhidi ya raia anajifanya msalihina na kuwa shehe jambo linaloonyesha unafiki mkubwa wa kidini. Siku moja akitoa hotuba katika msikiti wa Maweni, Mvita alipotaka kuuliza maswali inambidi atolewe nje; nusura auliwe na waumini ambao walikuwa wametekwa na hotuba ya shehe Juba.

Licha ya hayo, mtunzi anamwasilisha mhusika Kudura, ambaye anateseka sana katika ndoa yao na Bwan Juba lakini kwa sababu za kidini, yeye anavumilia mengi mpaka anapozinduka na kupigania haki zake ndipo alipofukuzwa. Kudura anaungama kimoyomoyo kuwa Mungu ni mkubwa, Mungu anajua yote (uk.75). Kupitia kwa Kudura, mtunzi anaonyesha namna dini inavyoweza kumpumbaza mtu asiuone ukweli kuhusu maisha yake kufungamana na mawazo ya Marx (1973). Kudura anaamini anayopitia ni mambo yaliyopangwa na Mungu kwani ndiye hujua yote hata Mvita anapojaribu kumzindua kwa kumwambia kuwa:

Ningetamani Mungu atuone....aone wanyonge.....mtesi hatesi
daima akifululiza.....lakini nisichokiamini mama ni
kusubiri, kusubiri nyuma ya pazia la Mungu yuko (uk. 77).

Kudura haonekani kuzinduka mpaka pale wanapopatana na Biti Japu na kuzinduka. Hii inaweza kuwa inasababishwa na ung'amuzi potoshi unaozungumziwa na Marx na Engels (1973). Wahusika wasalihina aliowachora S. A. Mohamed hasa mashehe kama vile Shehe Omari, Shehe Juba babake Mvita ni watu wabaya, wanaongoza magendo na udhalimu wa kila aina huku wakijifanya wasalihina wanaonyesha namna dini inaweza kuwa potovu na anaonekana kukubaliana na Marx (1973) anayesema kuwa dini ni itikadi ya jamii ya uongo inayotumiwa na tabaka tawala ili wanaonyanyaswa wasione ukweli wa hali zao na kwa hivyo kuzidi kuwa watiifu na wanyenyekevu hali inayoendeleza ubepari na mifumo mingine ya udhalimu.

5.3.2.5 ASASI ZA UTAWALA

Althusser (1981) anasema kuwa, kuna asasi tofauti za utawala ambazo huendeleza itikadi tawala. Asasi hizo ni dini, mahakama, vyombo vya habari, vyama vya kisiasa na kadhalika. Asasi hizi za utawala huhalalisha mifumo ya kiutawala iliyopo ama kwa njia za ukubalifu au kwa matumizi ya nguvu kama vile jeshi na polisi. Asasi hizi za kiutawala zinatumiwa kuzima juhudi za wanyonge wasitete haki na usawa. Nao utawala na asasi zake hujinasibisha na tabaka lenye nguvu za kiuchumi. Njogu (1997) anasema kuwa kule Zanzibar visiواني, utawala wa Kiingereza ulishirikiana moja kwa moja na Waarabu pamoja na mabepari wenye viwanda.

Katika *Kiza Katika Nuru*, askari wanatumiwa kuwashika Kudura, Mbishi na Salma na kuwashitaki kwa mauaji ya Bwan Juba na Mvita mtawalia. Askari ndio wanalinda gereza ambapo Kudura alijiua. Asasi ya utawala ya askari inatumiwa na utawala kuwakamata na kueneza hofu miongoni mwa raia ndio sababu kina Mvita wanafanya siasa kichinichini. Walikuwa wanajificha misituni na kula viapo huko wanapoendeleza juhudi za mapambano na Mvita anapouawa na Bwan Juba kupitia kwa Shazia, askari ndio wanaoenda kumshika Salma na kumshtaki.

Baadaye Salma alijikuta anainuliwa na askari wawili kwa nguvu na kutiwa ndani ya gari la polisi na maiti ikatiwa ndani ya gari la hospitali (uk. 247).

Hili linaonyesha matumizi ya nguvu na polisi kwani kazi yao ni kulinda maslahi ya mabepari kama kina Bwan Juba kwani Salma anashitakiwa mara moja na kuwekwa rumande bila hata uchunguzi wowote kufanywa kufungamana na mkabala wa Althusser kuhusu itikadi kuwa vyombo vya nguvu kama askari na jeshi huweza kutumiwa kuwanyamazisha watu wanaopinga itikadi tawala. Licha ya hayo, Bwan Juba haulizwi swala lolote na wauaji wenyewe kina Shazia wako tu wanafurahia na kupokea mali kwa kutekeleza kazi hiyo ya mauaji. Aidha, askari wanawashika Kudura na Mbishi na kuwashtaki, na mwishowe Kudura anajiua akiwa mikononi mwa askari akiwa amewekwa rumande chumba chenye upweke ambapo anajiua usiku wa manane na hakuna uchunguzi unaofanywa kuhusu kifo chake.

Mahakama nayo inatumiwa pia kama asasi ya kuendeleza utawala. Katika *Kiza Katika Nuru* mahakama inatumiwa kwa manufaa ya wale wanaomiliki nyenzo za uzalishaji mali. Watetezi wa haki za wanyonge wanashitakiwa kwa kuzingatia sheria zilizotungwa ili kuuhalalisha na kuuhifadhi mfumo wa kibepari. Kwanza, Mohamed anachora taswira ya jengo la mahakama kwa kulifananisha na uso wa kizee uliochukiwa na umri mrefu kwa mapuuza (uk 256). Hili linaonyesha kuwa mahakamani si pahali pa kupata haki kwani ilikuwa imepuuzwa na kwa hivyo, haikuchukuliwa kwa uzito na watu binafsi kama kina Juba. Mahakamani, Mbishi na Kudura walikuwa wote wamekiri kumuua Bwan Juba kwa tuhuma kuwa yeye ndiye aliyemuua Mvita na kwa hivyo walilipiza kisasi kwa kumuua.

Jambo hili linaonekana kuchangiwa na watu kutokuwa na imani ya mfumo wa mahakama na sheria ambao wanaona ni heri kuchukua sheria mikononi mwao na kudhihirisha namna mahakama ilikuwa imewachosha na hawakuwa wanatarajia haki. Wanakiri makosa hayo ya mauaji mbele ya hakimumu moja kwa moja kuonyesha uasi wa wazi dhidi ya makali ya itikadi ya kibepari. Kwa hakika Kudura anajiua hata kabla ya uamuzi kufanywa labda kutokana na dhana kuwa hakuna haki ingetendeka bado angehukumiwa kifo. Salma naye anajitetea mahakamani na hata kuwashinda mawakili waliosomea kutoa kauli na kusema kuwa Bwan Juba ndiye aliyemuua Mvita na ni mtetezi wa nguvu na mwenye tamaa (uk. 260). Mwishowe kuna matumaini kwamba huenda akaachiliwa huru kutokana na shinikizo la watu pale anapoletewa kijibaru na maneno haya yakiwemo:

“Mkweo Bi Kudura naye amekwenda. lakini wewe utatoka.....tuko pamoja nawe....nduguzo wa mjini na shamba (uk. 262).

Hili linadhihirisha kuwa mahakama inatumiwa kulinda masilahi ya mabepari na kuonekana kudhulumu wale wanyonge kwa kutowalinda kutokana na udhalimu na watu hawana imani na asasi hii. Hii ndio sababu wanyonge ndio wanaoshikwa na kushtakiwa kama vile Mbishi, Kudura na Salma ilhali wale wenye nguvu na mamlaka kama Bwan Juba wanaachiliwa huru licha ya kufanya maovu kama vile ufisadi, magendo, mauaji na wazi na kufungamana na mkabala wa Althusser kuwa mahakama na sheria ni asasi zitumiwazo na watawala kuendeleza itikadi ya kitawala.

5.3.2.6 VYOMBO VYA HABARI

Kuhusu vyombo vya habari, Mohamed kwenye *Kiza Katika Nuru* anaonekana kuvipa uwezo wa kupitisha ujumbe. Bwan Juba anapoelekea kumuona mkewe Kudura ana gazeti garini ambalo limeandikwa “the Truth” analitumia kujipepea. Hapo ndipo anaitumbulia macho katuni iliyokuwa na picha ya chatu kubwa, kinywa wazi ambalo limeandikwa “THE HAVE”, ikifukuza kipanya kidogo kilichoandikwa “THE HAVE NOT” na kuna chatu kubwa zaidi ambalo linangojea kuwameza wote wawili limeandikwa “THE POWER”. Inavyodhihirika ni kwamba Mohamed anaonyesha namna vyombo vya habari hutumika kama asasi ya utawala kuambatana na mkabala wa Althusser kuhusu itikadi na ndio sababu anacheka kwa kudharau ujumbe ulio pale kwani ujumbe unaojitokeza unawabeza wenye mali na wasi na mali na kuonyesha kwamba hawaelekei popote kwani wote wanatafuta mamlaka na ukubwa tu ndio sababu watamezwa na lile chatu lililoandikwa “THE POWER” (uk. 112).

5.4.0 ITIKADI YA MWANDISHI

5.4.1 MAPINDUZI YA NGUVU

Itikadi ambayo Mohamed anaaridhia katika *Kiza Katika Nuru* ni ya kimapinduzi ya nguvu. Mapinduzi ya aina hii huweza kutokea kama watawala hawazingatii hali mbalimbali za kijamii au kutokana na mapuuza au kutojali hali hizi. Mara nyingi watawala huwa wanafahamu udhaifu wa uongozi wao kwa sababu ya mivutano ya kisiasa, kiuchumi na kijamii ambayo huwa imeletwa na utawala huo. Dalili za udhaifu wa utawala hujitokeza katika mambo kama uvumi, malalamiko, maandamano, migomo na mwishowe huweza kulipuka na kuwa mapinduzi. Ni imani ya mtafiti kuwa mara nyingi utawala hushindwa kuchukua hatua madhubuti kwani huwa ni washirika wakubwa katika ukandamizaji. Wakati mwingine, kufaulu kwa mapinduzi katika nchi nyinginezo huenda kukachochea mapinduzi katika nchi nyinginezo kama ilivyofanyika katika nchi za Kiarabu kama Tunisia, Libya, Misri na nchi nyinginezo miaka ya 2010 na 2012 ambako mapinduzi ya kisiasa yameshuhudiwa pakubwa.

Itikadi hutekeleza nafasi kubwa katika mapinduzi ya aina yoyote kwa kumulika maovu ya tabaka tawala na kuwafanya wale wanaonyanyaswa wajihisi kitu kimoja na wawe na malengo na dhamira zinazowiana. Aidha, itikadi huwafanya wengi wao kujitolea mhanga na kuamini kuwa hata wao wenyewe wakifa, watakuwa wamechangia katika harakati za ukombozi na kuamini pia kuwa hali itakuwa bora zaidi mapinduzi yanapofanyika.

Utabaka pia huchangia pakubwa katika kuleta mapinduzi kwani matabaka tofauti huzua mivutano inayoleta uhasama, chuki na uadui mkubwa kiasi kwamba wanaonyanyaswa huamua kulinda nguvu zao kwa kujihami kwa kila namna. Nalo tabaka tawala hukazania kupinga na kudhibiti wafanyakazi na wale wanaonyanyaswa kwa njia zozote zile ama kwa matumizi ya nguvu au vyombo vya kiitikadi ambapo wakati mwingine hufaulu na kuleta dhana ya ukubalifu au ukawaida. Itikadi kama za kidini na utamaduni hupumbaza watu wakashindwa kujipigania. Wakishindwa kuwapumbaza hutumia polisi, mahakama na sheria kuhalalisha hali hizi lakini mapinduzi hutokea mwishowe kwani mnyonge hawezi kukandamizwa milele (Kamunde 1983).

Katika riwaya ya *Kiza Katika Nuru*, mtunzi anaonyesha kuwa mapinduzi yanayotokea yalikuwa jambo la lazima kwani utawala unaowakilishwa na Bwan Juba ulishindwa kujirekebisha licha ya kufahamu udhaifu wao, kutokana na mapuuza kwani utawala wenyewe uliunga mkono ukandamizaji na kuwa mapinduzi ya nguvu yalikuwa ndio njia ya pekee ya kujikomboa na kujinasua kutokana na makali ya utawala wa kibepari yaliyokithiri. Mohamed anaonyesha namna ambavyo Mvita anamfahamisha Bwan Juba maovu yake, naye Bwan Juba badala ya kuyarekebisha anamfuta Mvita kazi, kumfukuza nyumbani hata na wafanyakazi walioonekana kumuunga mkono kama Salma. Bwan Juba anamwambia Salma; “Chukua maneno haya - barua tunamwandikia mkombozi wetu Mvita”(uk 25).

Mtunzi anasema kuwa hili neno “mkombozi” alilitamka kwa bezo na dharau kuonyesha namna viongozi walipuzilia mbali hali duni ya walionyanyaswa na kuona kwamba hata waliojitolea kuwatetea kwamba hawawezi kufaulisha mapinduzi. Mohamed katika *Kiza Katika Nuru* ana itikadi kuwa shughuli ya mapinduzi ni hatari inayohitaji makini na uangalifu mkubwa na maandalizi ya muda mrefu. Mhusika mkuu Mvita anayemsawiri kama kiongozi wa mapinduzi amesawiriwa kama kwanza mtu aliyesoma hadi Chuo Kikuu kwa hivyo anaelewa maswala ya jamii yake vyema. Mvita anashiriki katika kuwazindua watu kwa muda mrefu hata mamake. Anafanya viapo vya usiku misituni wakiwa na Kudura mamake, anaenda mpaka misikitini hata kule Maweni babake anapohubiri kuzindua watu. Wakati huu wote anashirikiana na watu wa tabaka la chini kwa kuwa alipofutwa kazi alienda kufanya kazi ya kuli na kulima mihogo iliyompa nafasi ya kutangamana na watu wa kawaida na kuwa mmoja wao na kiongozi wao.

Baadaye, Bwan Juba anapotaka kupigania kiti cha ubunge anamuona Mvita kama kikwazo kikubwa na kuamua kumuua jambo analolifanikisha kwa kumtumia Shazia anayejifanya rafiki wa Mvita na Salma. Mtunzi anaonyesha kuwa, juhudi za mapinduzi hukumbwa na usaliti mkubwa hasa pale Mvita anapouawa. Hata hivyo, mtunzi anaamini kuwa kuwaua viongozi hakuwezi kudidimiza mapinduzi. Kwa hakika huchochea hali hii yaani kadri tabaka tawala huzidisha mapambano dhidi ya ukombozi, ndivyo nguvu za wakombozi huimarika. Anaonyesha haya kwani baada ya mauaji ya Mvita, Kudura, Mbishi na kwa ushirikiano wa Kitwana, Baker na wengineo wanamuua Juba nyumbani kwake na wanaingia humo kwa ustadi mkubwa na ujasiri; hata Kudura

na Mbishi wanapofikishwa mahakamani kwa kushtakiwa kwa mauaji ya Bwan Juba, wanakubali mara moja kudhihirisha itikadi ya mtunzi katika mapinduzi ya nguvu.

Mohamed katika *Kiza Katika Nuru* kwa hivyo anaamini, mapinduzi ni jambo gumu, huhitaji maandalizi na urazini wa kitabaka, huchukua muda mrefu, ni hatari na kuna vikwazo vingi kwa hivyo kuhitaji ushirikiano wa wake kwa waume waliojitolea mhangana nafsi zao na ujasiri mkubwa. Imani hii kuhusu mapinduzi ya nguvu ni kinyume na msimamo wake katika *Asali Chungu* ambapo ingawa mapinduzi yanafanyika na kushabihiana na mauaji ya akina Amina, Biti Daudi na nyumba ya Zuberi kuchomwa, huku akina Dude, Shemsha, mtoto na Latifa wakiachwa, haonyeshi maandalizi yoyote yanatokea kisdafa tu kama bahati nasibu. Hatuonyeshi hata wahusika wakuu kama Dude wakipevuka na kuielewa jamii yao kiasi cha kuweza kuongoza mapinduzi; kwa hakika ni wahusika waovu hata wakipewa mamlaka watatatiza jamii zaidi kudhihirisha itikadi yake ya mapinduzi ya marekebisho wala si mapinduzi ya nguvu.

Kwa hivyo, mtunzi hapa amebadilisha itikadi yake kuhusu mapinduzi kabisa. Awali katika *Asali Chungu* anaonyesha mapinduzi kama jambo rahisi ambalo hata msingi wake ni kunajisiwa kwa Semen; hakuna urazini wa kitabaka uliojengwa vyema, utekelezaji wa mapinduzi ni wa ghafla na kisdafa na kujitokeza kuwa na itikadi ya mapinduzi ya marekebisho. Lakini katika *Kiza Katika Nuru* itikadi anayoaridhia ni ya mapinduzi ya nguvu kwa kuonyesha makabiliano ya kifamilia, kidini, kisiasa, na kiutawala katika juhudi za kujikomboa kutokana na ukandamizaji uliokithiri mipaka ya

kibepari. Kauli ya mtafiti ni kuwa kama nadharia ya kimaadili inavyosema kuwa fasihi ni zao la jamii, kwa sababu miaka ya themanini ilikuwa ni miaka ya ujamaa kuelekea ubepari (Chuachua, 2011), mtunzi anabadilisha itikadi yake ili kuangazia yaliyokuwa yakitendeka katika jamii yake kwa wakati huo. Yaani ujamaa uliochanganyika na ubepari, mali kuzalishwa na watu wengi kwa pamoja lakini kumilikiwa na wachache, jambo ambalo huhitaji mapinduzi ya nguvu. Hii ni kinyume na ilivyo katika *Asali Chungu* miaka ya kipindi cha ujamaa (Chuachua, 2011) ambapo anaona marekebisho ya asasi zinazoendeleza itikadi tawala ya kimwinyi yanatosha huku ikizingatiwa kwamba mfumo wa kimwinyi haudhihirishi makali zaidi kama ulivyo mfumo wa kibepari. Anafanya haya ili kazi yake iwe faafu kwa jamii yake na katika kufanya hivyo, anaupinga msimamo wake wa awali kuhusu mapinduzi na kwa hivyo msimamo wake kuhusu mapinduzi si mmoja na tengemano.

Mtunzi S. A. Mohamed anaonekana kubadilisha itikadi yake ya awali ya kuhusu mfumo wa kiuchumi. Katika *Asali Chungu*, mtunzi anaamini kuwa mfumo wa kiuchumi ukifanyiwa marekebisho utakuwa sawa na hali ya kiuchumi itaimarika. Katika *Kiza Katika Nuru* dhana kuu inayoleta mapinduzi ni uchumi kwa hivyo mfumo wa kiuchumi na uchumi kwa jumla unapewa nafasi kuu katika kuelezea hali zote za kijamii. Hivyo, kwa maoni ya mtafiti, mwandishi anabadilisha itikadi yake kuhusu mfumo wa kiuchumi na kuuona kama msingi mkuu wa matukio yote katika jamii na lazima ubadilishwe na kung'olewa kabisa kwa matumizi ya nguvu ili mfumo mwingine uwepo. Haya yafungamana na mawazo ya Marx (1973) kwamba ili mabadiliko ya kweli kupatikana

mapinduzi ya nguvu kwa kutumia migomo na makabiliano huwa jambo la lazima. Hii ni kinyume na mtazamo wa awali ambapo anapendekeza marekebisho ya mfumo wa kiuchumi na hivyo ni dhahiri kuwa itikadi yake imebadilika kama mtunzi.

Aidha, ni kauli ya mtafiti kuwa, hali zinazowakumba wahasika wengine kama vile Kudura, Mbishi, Salma zinatokana na hali zao za kiuchumi. Kudura alikuwa mke wa nyumbani, ambaye hakuwa na kipato chake na alimtegemea Bwan Juba kwa kila kitu. Bwan Juba anapoanza kukataa kuwajibika, inambidi akope, ataabike na aishi katika mazingira duni. Mumewe anapokuja kutembea analalamika kuwa Kudura ni mchafu, nyumba ni chafu, chakula ni kibaya na mambo haya yanaleta mabishano hivi kwamba Kudura anafukuzwa. Ni msimamo wa mtafiti kuwa kama Kudura angekuwa na mali Bwan Juba hangemtesa sana kwani angejikwamua mapema, si kujidunisha na kumuona kama Mungu wa pili. Hata hivyo Kudura anajikwamua kwa matumizi ya nguvu na kupigana na Bwan Juba hadharani. Anapofukuzwa anaungana na Mvita kuongoza mapinduzi yanayofanikiwa wanapomuua Juba na hata anapopelekwa mahakamani anakiri mara moja kudhihirisha itikadi ya mtunzi ya mapinduzi ya matumizi nguvu.

Kwa ujumla, mfumo wa kiuchumi ndio unapeleka matukio yote ya riwaya mbele na kama tulivyosema hapo awali ni ishara tosha kuwa mwandishi amebadilika kwa kuweka mfumo wa uchumi wa kibepari na mali kama uti wa mgongo wa kazi yake. Anapendekeza mfumo huu ung'olewe kwa njia ya mapinduzi ya nguvu yaliyopangwa na kufanikishwa vyema si tu kufanyiwa marekebisho pamoja na asasi nyinginezo

zinazosaidia kuendeleza itikadi tawala ya kibepari. Hivyo, matukio yote katika riwaya yanaonyesha kuwa itikadi ya kibepari ndiyo iliyotawala, naye mwandishi anaelekezwa na itikadi ya mapinduzi ya nguvu, kinyume na ilivyo katika *Asali Chungu* ambapo itikadi yake ni ya kimapinduzi ya asasi za mfumo wa kimwinyi.

Maoni yetu ni kwamba, fikra za mtunzi kuhusu mfumo wa kiuchumi ni kuwa, watu wanapotatizwa na kutengwa na kuwa masikini, huenda wakajiingiza katika anasa na raha na katika harakati hizo wakafahamiana, wakahimizana na wakaendeleza ukombozi wao. Kwa ujumla mfumo wa uzalishaji mali na uchumi, zimepewa nafasi kuu katika *Kiza Katika Nuru*, jambo linaloambatana na itikadi Mohamed anayoaridhia ya Uyakinfu wa kijamaa kwa kuongozwa na Mkabala wa Ki-Marx. Mkabala huu unasema kuwa hali zozote katika jamii hutokana na mfumo wa kiuchumi na daima ziko katika kuathiriana na kujiendeleza.

S. A. Mohamed kupitia kwa Juba, Mvita na wahusika wengine anaamini kuwa jamii yenye usawa wa kitabaka ndio bora lakini lazima watu wa tabaka la chini waungane na wamfahamu adui yao ni nani ili waweze kufanya mapinduzi ya nguvu na kujenga jamii yenye usawa wa kitabaka. Anaonyesha kuwa ili kutetea hali za kijamii, si lazima mtu akulie katika tabaka hilo bali anaweza kujitolea mhanga kama Mvita kwa kutumia uhuru wa fikra. Anaonekana kubadilika pale ambapo anaonyesha watu kama Mvita wakiwa msitari wa mbele katika kutetea watu wa tabaka la chini ilhali katika *Asali Chungu* kina Zuberi na Amina wa tabaka la juu wanabakia vile vile.

Aidha, anaonyesha kuwa utabaka si lazima ufungamane na uzalishaji mali pekee; si lazima uwe wa familia ya kitajiri ndio uwe wa tabaka la juu au chini. Utabaka kwa mujibu wake unaweza kusababishwa na uhuru wa fikra ambapo mhusika kama Mvita anafutwa kazi na kuungana na watu wa tabaka la chini ili kutetea haki na usawa. Kwa hivyo, utabaka kila mara si lazima ufungamane na uchumi kinyume na ilivyo katika *Asali Chungu* na hivyo msimamo wake kuhusu matabaka na visababishi vyake umebadilika na kuupinga ule wa awali.

Kuhusu urazini wa kitabaka, Lukacs (1971) anasema kuwa ni hisia au uelewaji wa dhima ya historia katika tabaka au ule uwezo wa tabaka moja kuweza kushirikiana ili waweze kupigana na tabaka lenye nguvu na mamlaka. Ili urazini ufaulu, lazima waelewe mahitaji ya tabaka hilo na wayachukulie kuwa si halali, wafahamu mantiki ya tabaka lao na wajinasibishe na matakwa ya tabaka hilo, na wawe tayari kuchukua hatua kwa ushirikiano wa kisiasa ili kufanikiwa katika malengo yao ya kujiimarisha na kujihifadhi dhidi ya tabaka wanalopingana nalo. Kabla ya kupata urazini wao wenyewe hupingana na kuchukiana. Jambo hili huchukua muda mrefu ili watu wa tabaka la chini kuzinduliwa na kuelewa hali yao.

Haya anaonyesha kupitia Mvita na harakati zake za kuwafahamisha watu haki zao kuanzia alipokuwa ameajiriwa kazi na Bwan Juba hadi anapouawa zaidi ya miaka saba baadaye. Mohamed anaonyesha mabadiliko kwani katika *Asali Chungu*, watu wa tabaka

la chini wanaungana mara moja bila kufunzwa na kuamua kuleta mapinduzi. Tabaka hili la chini halielimishwi wala kufahamishwa na yeyote kuhusu hali zao na hata viongozi wao hawafunzwi wala kuonyeshwa wakiwa na fikra pevu wala masomo yanayowasaidia wale wa tabaka hilo kuzinduka. Aidha, urazini wa kitabaka katika *Asali Chungu* na mikinzano ya tabaka lao ni ya juu mno kiasi cha kutoaminika kwamba wanaweza kuibadilisha hali yao kwani hata hawamfahamu adui yao ni nani.

Katika *Kiza Katika Nuru* mtunzi anaonyesha kwamba lazima tabaka la chini liwe na urazini wa kitabaka, ambao huchukua muda mrefu na wakati mwingi kuwa na changamoto na hatari nyingi ili mwishowe mapinduzi na kung'olewa kwa tabaka la juu yawezekane. Yaani utabaka ni jambo gumu kuvunja na huhitaji matayarisho kabambe ya muda mrefu, makini na upevu wa fikra. Si jambo la sadfa na kubahatisha au la kighafla tu na hivyo dhihirisho kuwa mtazamo wake kuhusu utabaka umebadilika na anaaridhia itikadi ya mapinduzi ya nguvu ili kubadilisha hali ya utabaka. Basi msimamo wake si mmoja na tengemano yaani mapinduzi ya nguvu lazima yatokee ili utabaka ung'olewe wala si marekebisho ya mifumo ya kiutawala. Hili limedhihirisha mabadiliko ya kiitikadi kwa mujibu wa kipindi tofauti cha utunzi wake, hivyo msimamo wake si mmoja na tengemano.

Msimamo wa Mohamed kuhusu ndoa na familia ni tofauti na vile ambavyo umewasilishwa katika *Asali Chungu* kwani ingawa katika *Asali Chungu* Zuberi anafanana na Bwan Juba wa *Kiza Katika Nuru*, yeye hamfukuzi Amina na wanaishi naye

nyumba moja kuonyesha ile itikadi yake ya mapinduzi ya kurekebisha lakini katika *Kiza Katika Nuru* Bwan Juba anamfukuza mkewe Kudura baada ya kupigana naye hadharani na wanawe Mvita na Mbishi. Familia yake inasambaratika, kuzidi kudhihirisha itikadi yake ya matumizi ya nguvu na makabiliano ya moja kwa moja kubadilisha mambo.

Aidha, mwandishi anaonyesha ndoa kama asasi yenye utesi na ambayo inakabiliwa na hatari ya kusambaratika. Ndoa ya kwanza ya Bwan Jabu na Bi Kudura inakumbwa na matatizo chungu nzima. Bi Kudura alimsujudu bwanake kama mungu wake wa pili: “Badala ya kufikiri, yake na Mungu wake, anafikiri yake na binadamu mwenzake au mungu wake wa pili” (uk 76). Hili inaonyesha namna mwanamke alivyochukuliwa katika ndoa katika mfumo wa kibepari. Yeye ni mojawapo ya mali za bwanake na kwa hivyo ni jukumu lake kumhudumia na kumstarehesha mumewe. Kudura anamuheshimu na kusujudu bwanake kama Mungu wake. Anazunguka kwa mashogake akikopa ili ampikie mumewe, mtu aliye na cheo kikubwa serikalini na tajiri mkubwa. Huyu mume wake Juba hawajibiki, hatekelezi majukumu yake kwa mke na familia yake kinyume na dini ya kiislamu anayoiamini na kuihubiri. Katika dini hii, mwanamke hapaswi kutekeleza majukumu ya kiuchumi ya kifamilia bali majukumu haya ni ya mwanamume na wanawake wapaswa kuwategemea waume zao kwa mambo haya kabisa. Jambo hili linaweza kumfanya mwanamke awekwe katika hadhi ya chini kwani hana uwezo wa kiuchumi na kulinganishwa hadhi sawa na mwanamume katika jamii (Osore, 2008). Licha ya kuyapuuza majukumu yake, Bwan Juba anatarajia heshima na kulishwa.

Baadaye Kudura anapozinduka, anatetea utu wake, anafukuzwa na ndoa yao kusambaratika.

Kupitia kwa ndoa ya Kudura na Bwan Juba mwandishi anaonyesha ndoa na familia kama mojawapo ya asasi za itikadi ya kibepari na kufungamana na mkabala wa Althusser (1981) kuhusu familia na ndoa kuwa ni kigeu kimojawapo cha kiitikadi kinachotumiwa kuhalalisha udhalimu. Ni kupitia kwa ndoa ambapo Juba anaona ana haki ya kumtesa mkewe Kudura, naye Kudura katika hali ya kutaka kuidumisha ndoa yake anateseka kwa muda mrefu mpaka pale alipozinduliwa na Biti Japu. Kupitia kwa familia Bwan Juba anahalalisha vitendo vyake vya magendo na udhalimu kwa kumkumbusha Mvita kwamba yeye ni mwanaye na hana budi kumtii, na hawezi akampinga na anapompinga anamfukuza nyumbani na hata kumuua. Baadaye naye pia anauawa na Mbishi mwanaye wa pili na mkewe wa kwanza Kudura.

Hili linadhihirisha namna familia huwa na nguvu katika kuendeleza itikadi hasa kule kutii na kudhibiti mawazo na fikra za watu na maoni yao kuhusu ulimwengu. Kwa hivyo ingawa Marx (1973) anadai kwamba itikadi hutokana na ung'amuzi potoshi unaotokana na imani potovu ya kidini kila mara, ni msimamo wa mtafiti kwamba itikadi huweza kutokana na kuendelezwa na vigeu vingine kama familia na ndoa. Hivyo Mohamed anashikilia kuwa ndoa kama hizi zitupiliwe mbali kuambatana na itikadi yake ya kimapinduzi ya nguvu na kwa matumizi ya vita namna Kudura anavyofanya ili mwanamke aweze kujinasua na kujikomboa.

Msimamo huu ni kinyume na ule unaodhihirika katika *Asali Chungu* ambapo anaonyesha ingawa ndoa ya Zuberi na Amina imekumbwa na uasherati usio na kipimo lakini inaendelea; ndoa ya Dude na Shemsha pia imejaa usherati na hawatalikiani. Hivyo kuonyesha kuwa anaaridhia itikadi ya mapinduzi lakini ya marekebisho katika asasi ya ndoa na familia kwa wanaohusika wala si mapinduzi ya nguvu na makabiliano kamili ya asasi hii na wanaohusika kama mojawapo ya kigeu cha kuendeleza itikadi tawala ya kimwinyi katika *Asali Chungu* na ya kibepari katika *Kiza Katika Nuru* .

Kuhusu dini, Mohamed anaashiria mabadiliko katika itikadi yake ya dini hasa anapoonyesha kuwa dini haisaidii kitu (uk:183). Watu wanasali lakini hali yao ni ile ile ya kimasikini siku zote. Mtunzi anaonyesha kuwa mafunzo ya dini huwapumbaza wanajamii na hivyo kudhihirisha kuwa msimamo wake kuhusu dini ni mojawapo ya itikadi za utawala zinazotumiwa kuwapumbaza watu katika mifumo dhalimu kama ya kibepari na hivyo lazima ibadilishwe kwa njia ya kimapinduzi ya nguvu na ndio Mvita anaenda msikitini kukabiliana na Shehe moja kwa moja kwa kutaka kuuliza maswali na hata Biti Japu kutaka kupiga Shehe kwa shoka kuonyesha itikadi ya mtunzi ya mapinduzi ya nguvu ili kuibadilisha hali hii ya udanganyifu wa kidini.

Kwa ujumla, S. A. Mohamed kupitia kwa visa alivyosimulia, namna anavyowachora wahuika wake wakisaili maswala ya dini ya kiislamu na maswala aliyojadili; anatoa msimamo wake kuwa dini ifanyiwe mapinduzi' ing'olewe kabisa kwani hutumiwa

kuhalalisha maovu, viongozi na watu waovu, mifumo mibaya ya utawala, udhalimu na unyanyasaji zaidi, ya kupotosha watu ili wasipiganie haki zao huku wakiona hali yao iko hivyo kwani Mungu amepanga hivyo.

Kinyume na ilivyo katika *Asali Chungu*, mtunzi anaonyesha kubadilisha msimamo wake kuhusu dini. Kwanza, anaonyesha dini kama dhana ambayo inahitaji muumini kujisaili na kujiuliza maswali mwenyewe kama inaafiki mahitaji ya jamii ama hapana. Tunamuona mhusika mkuu Mvita katika uk. 183 akijiuliza maswali mengi na kuona dini kama imejawa na unafiki tu. Anaonyesha dini kama asasi hatari yaani badala ya kumletea mwanadamu wokovu na amani inamletea madhara kwa kumpumbaza asiune ukweli unaomzunguka ili ajikomboe. Aidha, kwa kumsawiri Mvita msikitini na kufanya mazingira ya msikiti kuwa uwanja wa makabiliano mtunzi anaafiki kwamba dini si takatifu tena, mahala patakatifu hakuna tena, dini haiheshimiwi tena pahala pa kuabudu hapaheshimiwi tena. Inavyoelekea ni kwamba, itikadi yake kuhusu dini na pahali patakatifu yaonekana kubadilika hasa ikizingatiwa kuwa ingawa katika *Asali Chungu*, anaonyesha unafiki hajaonyesha misikiti au pahala pa kuabudu pakiwa pahali penye fujo na makabiliano wala dini ikiwapumbaza wahusika kiasi cha kutoona ukweli wa mambo. Jambo ambalo linatokana na kubadilisha itikadi yake ya kimapinduzi katika *Asali Chungu* ni mapinduzi ya kurekebisha na katika *Kiza Katika Nuru* itikadi anayoaridhia ni ya mapinduzi ya makabiliano ya moja kwa moja.

S. A. Mohamed anaamini kuwa asasi za utawala zimepewa nafasi kubwa kuendeleza na kudumisha itikadi ya kibepari iliyotawala kwa kipindi hiki alichandika riwaya ya *Kiza Katika Nuru*. Asasi hizi zinatumiwa kueneza imani za tabaka dogo linalotawala na kuwafanya wanaonyanyaswa kutokuwa na matumaini ya kubadilisha hali zao kuwa bora. Hili ni kufungamana na mkabala wa Althusser (1981) kwamba itikadi huweza kuelekezwa kwa nguvu kama vile kutumia jeshi, polisi, mahakama na asasi nyinginezo za utawala au kwa kutumia vyombo vya kiitikadi kama dini, elimu, utamaduni na vinginevyo. Hata hivyo, mwandishi licha ya kuisawiri hali hii, msimamo wake umebadilika kuhusu asasi hizi kwani anaonyesha kuwa zinahitaji kufanyiwa mapinduzi na kung'olewa kabisa si kurekebisha tu kama ilivyo katika *Asali Chungu*. Kwa mfano Kudura anazinduka na kupigana na Bwan Juba hadharani, Mvita anakabiliana na babake msikitini moja kwa moja, Salma anajitetea sana mahakamani na kuna ishara kuwa ataachiliwa na mwishowe Bwan Juba anauawa na mapinduzi kufanyika. Kwa hivyo, mwandishi anaonekana kubadilisha itikadi yake ya hapo awali kuwa asasi hizi zirekebishwe ili zisitumike tu kuyalinda maslahi ya mabepari bali zifanyiwe mapinduzi ya nguvu na ziondolewe kabisa.

Mtunzi kupitia kwa gazeti anaonyesha namna Bwan Juba anavyolitumia kujipepea, anaonyesha kuamini kuwa jukumu la vyombo vya habari si kueneza ukweli bali itikadi za tabaka tawala. Kwa hivyo anakubaliana na Althusser (1981) anayesema kuwa vyombo vya habari ni mojawapo wa vifaa vinavyotumiwa na tabaka tawala kueneza uongo na itikadi zilizopo za kitawala ili waendeleo kudumisha hali kama ilivyo na kwa hivyo

kudumisha utabaka wa walionavyo na wasionavyo. Aidha, katika shughuli za kuendeleza mapinduzi Maharamu aliyekuwa mhariri wa gazeti lililokuwa limechapisha habari hizi hapo awali hapatikani na kila wakati Salma anasema kuwa wakipanga miadi huwa hatimizi. Jambo hili linaonyesha namna vyombo vya habari na wanahabari hutumiwa na tabaka tawala kutosema ukweli na kueneza propaganda za kiutawala ili kuficha maovu wanayotenda na kwa hivyo ni washirika wa ukandamizaji wa tabaka tawala.

S. A. Mohamed katika *Kiza Katika Nuru* anaonyesha namna asasi za utawala kama vile polisi na mahakama zinatumiwa kudhibiti hali na kuhifadhi maslahi na matakwa ya tabaka tawala kuambatana na mkabala wa Althusser kuhusu itikadi. Anaamini kuwa asasi hizi zinatumiwa kama vyombo vya ukandamizaji kwani polisi wanatumiwa kumshika Salma na kumshitaki mara moja, Kudura anashikwa pia na kufunguliwa mashtaka na anajiua akiwa rumande ilhali Juba hakushikwa kwa kushiriki mauaji ya Mvita kati ya maovu mengine. Mohamed anaamini kuwa mapinduzi ya nguvu yaliyopangwa vyema ndio hufanikisha juhudi za ukombozi kwani kama Althusser anavyosema vyombo vya kiitikadi vya serikali ni vingi mno. Kuna vile hutumia nguvu kama jeshi, polisi na mahakama na vile hutumia itikadi kuwafanya watu wanyamaze na wasitete hali zao duni na kuendeleza itikadi tawala.

Aidha, asasi za ndoa, familia na dini zimeonyeshwa kama asasi za kuendeleza itikadi za tawala ya kibepari kwa wakati huu, hivi kwamba Juba anataka Mvita aendeleze utabaka ingawa anakataa na kufukuzwa na mwishowe kuuawa. Naye Kudura ananyanyaswa

katika misingi ya ndoa na kisingizio cha dini kwa muda mrefu kabla ya kujitokeza na kutetea utu na ubinadamu wake na mwishowe kumuua Bwan Juba. Mtunzi anadhihirisha mabadiliko ya kiitikadi kwani katika *Asali Chungu* Zuberi na Amina wote ni wanafiki na hamna anayedanganyika na dini. Dude, Baya na wahusika wengine wa tabaka la chini hawatetei hali zao. Kwa hakika, wanashiriki kuwakandamiza zaidi kama Biti Daudi, Bushiri na wengineo hawazinduki kwani hali yao ni ile ile hata mapinduzi yanapofanywa wanaepuka kibahati kwani hawajaonyeshwa wakishiriki katika juhudi zozote za ukombozi au kubadilisha maisha yao kuwa bora hata kidogo na hivyo itikadi ya mtunzi imebadilika kabisa. Katika *Asali Chungu* itikadi anayoaridhia ni ya mapinduzi ya marekebisho ya asasi za mfumo mzima wa umwinyi ilhali katika *Kiza Katika Nuru* itikadi anayoaridhia ni ya kimapinduzi ya nguvu. Asasi zote zinazoendeleza itikadi tawala ya kibepari zing'olewe kabisa wala si kufanyiwa marekebisho.

5.5 HITIMISHO

Katika sura hii, mtafiti ameshughulikia itikadi katika riwaya ya *Asali Chungu* na *Kiza Katika Nuru*. Katika *Asali Chungu* ameonyesha kuwa Said Ahmed Mohamed anawasilisha itikadi tawala ya kimwinyi iliyojitambulisha kwa vigeu kama vile mfumo wa kiuchumi, matabaka, elimu, utamaduni, mfumo wa kuumeni, dini, ndoa, asasi za utawala na maadili. Aidha, mtafiti ameonyesha kuwa Mohamed anaaridhia itikadi ya kimapinduzi ya marekebisho katika riwaya ya *Asali Chungu*. Anaunga mkono mapinduzi ya marekebisho ya asasi zote zinazoendeleza itikadi tawala ya kimwinyi na

kuamini kuwa asasi hizi zikifanyiwa marekebisho basi jamii itabadilika na maisha yatakuwa bora.

Mikabala mitatu kuhusu itikadi pia imejitokeza katika mjadala wetu na kuweza kuibua fasili tofauti kuhusu dhana ya itikadi. Mkabala wa Marx (1973) unaoonyesha itikadi kama ung'amuzi potoshi umejitokeza pale wanyonge wanaamini hali yao ni majaliwa, maisha yao yameratibiwa na Mungu na hivyo hawawezi kufanya lolote kujikwamua kama Mkasi katika mawazo yake. Mkabala wa Althusser (1981) kuhusu itikadi na vyombo vinavyotumiwa kuuendeleza umejitokeza katika asasi za kitawala kama Bwana DC na sheria pamoja na dini, utamaduni, ndoa na familia na elimu. Nao mkabala wa Gramsci (1985) kuhusu itikadi wa ukubalifu na ukawaida umejitokeza pale wanyonge wananyanyaswa na wananyamaza, wanatii kwa unyenyekevu na kuona kuwa hali yao ilivyo ndivyo mambo yanavyopaswa kuwa. Mtafiti ameonyesha kuwa matini huwa na mikabala au mielekeo mingi ya maana na hivyo kuibua fasili na maana nyingi na hivyo kuthibitisha kuwa itikadi ni dhana badilifu na si ung'amuzi potoshi pekee kama Marx alivyodai na hivyo msimamo wa mtunzi si mmoja na tengemano kila mara bali ni changamano.

Katika sehemu ya pili ya sura hii, mtafiti alidhamiria kuonyesha itikadi ambazo mtunzi S. A. Mohamed anaaridhia katika riwaya ya *Kiza Katika Nuru* na kuona kama kuna dalili zozote za mabadiliko. Imedhihirika kuwa itikadi ambayo inajitokeza ni itikadi tawala ya kibepari ambayo inajidhihirisha kwa vipengele kama za mfumo wa kiuchumi, utabaka,

ndoa, familia, dini, elimu na asasi za kiutawala. Naye Mohamed anaaridhia itikadi ya mapinduzi ya matumizi ya nguvu dhidi ya itikadi tawala ya kibepari na vipengele vyake vyote vinavyoahalalisha ubepari.

Kwa ujumla wake, S. A. Mohamed amedhihirisha mabadiliko mbalimbali kuhusu itikadi yake. Ukiangalia itikadi zinazojitokeza katika *Asali Chungu* itikadi kuu ya watawala ni umwinyi na ile ya mtunzi ni mapinduzi ya marekebisho. Ukilinganisha na itikadi zinazojitokeza katika *Kiza Katika Nuru* ambapo itikadi kuu ya watawala ni ubepari na itikadi ya mtunzi ni mapinduzi ya matumizi ya nguvu. Kwa hivyo mtunzi anadhihirisha mabadiliko ya kiitikadi ambayo yanaathiri mielekeo na mitazamo yake katika kazi zake. Aidha imedhihirika kuwa itikadi imejitokeza kwa mikabala tofauti kama ung'amuzi potoshi ulioendelezwa na Karl Marx, vyombo vya kiitikadi kama Althusser Louis anavyopendekeza na ukawaida na ukubalifu unaoendelezwa na Antonio Gramsci. Kwa hivyo Mohamed anadhihirisha mabadiliko ya itikadi kwa kuaridhia itikadi ya mapinduzi yanayotokana na marekebisho katika *Asali Chungu* na baadaye katika *Kiza Katika Nuru* kuonyesha itikadi ya mapinduzi ya nguvu na makabiliano ili kuibadilisha kabisa itikadi ya watawala ya kibepari na kung'oa asasi zake zote. Jambo hili linadhihirisha kuwa msimamo wake si mmoja na tengemano na matini ya kifasihi inaweza kufasiliwa kwa namna mbalimbali kwa mujibu wa nadharia ya udenguzi.

Katika sura inayofuata mtafiti ataangazia itikadi zinazojitokeza katika riwaya za *Dunia Yao* na *Mhanga Nafsi Yangu* ili kudhihirisha zaidi kuwa katika kila kipindi cha utunzi S. A. Mohamed anabadilisha itikadi anazowasilisha katika kazi zake.

SURA YA SITA

6.0 ITIKADI KATIKA *DUNIA YAO* NA *MHANGA NAFSI*

YANGU

6.1 UTANGULIZI

Katika sura iliyopita, tulijadili itikadi zinazojitokeza katika riwaya ya *Asali Chungu* na *Kiza Katika Nuru*. Imedhihirika kuwa Mohamed amesawiri itikadi kuu iliyotawala ya kibepari kupitia kwa kuwasawiri wahusika wake kitabaka, mfumo wa kiuchumi, matabaka, utamaduni, ndoa, dini, mfumo wa kuumeni, asasi za utawala, mapinduzi kati ya maswala mengineo aliojadili. Ilibainika kuwa itikadi yake kama mwandishi ni ya kimapinduzi ya matumizi ya nguvu ili asasi zote zinazotumiwa na ubepari zing'olewe kabisa na kujenga jamii mpya. Imedhihirika kuwa Mohamed anaonyesha mabadiliko kuambatana na juhudi za kufanya kazi yake iwe faafu kwa jamii anayoilenga na katika kufanya hivyo ameupinga matazamo wake wa awali katika riwaya ya *Asali Chungu*. Katika sura hii tunajadili itikadi zinazojitokeza katika riwaya ya *Dunia Yao* na *Mhanga Nafsi Yangu* kuona ikiwa itikadi za Mohamed zinazojitokeza zinazidi kubadilika na hivyo kuipinga mitazamo yake ya awali hivyo kudhihirisha kuwa mtazamo wa mtunzi si mmoja na tengemano na hivyo dhana ya itikadi ni badilifu.

6.2 MUHTASARI WA RIWAYA YA *DUNIA YAO*

Mwanzoni mwa riwaya tunakutana na mhusika Ndi ambaye anaonekana kuzama njozini. Anajiumbia wahusika ambao si halisi. Kama vile Shaib au kwa jina lingine Ye

kumaanisha nafsi yake. Ndi yuko katika hali ya upweke ambao unapunguka wakati wanawasiliana na Mtima bintiye aliyoko Uingereza kupitia kwa barua pepe akitumia kompyuta aliyonunuliwa na Mtima pale Uingereza.

Tunaona tawasifu ya Ndi inayotuarifu kuhusu malezi yake, masomo hadi alipohitimu kwenda chuoni na akapata shahada. Kisha anatarifu kuwa kazi alizowahi kufanya kwenye nyadhifa mbali mbali serikalini. Pia tunaona kuseoneka kwake kulikoanza pale alipoporomoka baada ya kupoteza kazi yake. Anatarifu juu ya wahusika wengine wanaokumbwa na janga lili hili la maporomoko. Kwa mfano, Sakarati, Sadala, Mzee Hamudani, Silima na Siwa. Hali zao wote zinaonyesha yanayopitiwa na wengi katika jamii. Hii ni baada ya jaribio lake la kufanya mapinduzi. Hapo ndipo anapelekwa rumande na kisha anafungwa jela. Ndi anaendelea kutuarifu jinsi hali yake inakuwa mbaya kiasi cha kukosa hata senti. Ingawa njaa inamkumba anaonekana kususia chakula cha nyumba yake kwa vile anakiona kama chakula cha ukahaba. Hatimaye, anaamua kukila hasa pale anapoisoma barua ya Bintiye, Kilua.

Kisha, tunakutana na Bi Mize au ukipenda Bi.Sanaa anayemzuru Ndi na kuzua mjadala mpevu wa swala zima la sanaa na hulka yake. Anapendekeza kutokwama katika sanaa ya uhalisia. Bi. Mize anampeleka Ndi kwenye bustani na kumpa mawaidha kuhusu maisha. Ndi anaipokea barua pepe kutoka kwa Mtima inaomjulisha jinsi safari yake ya kwenda Uingereza ilivyokuwa na maisha yalivyo huko Uingereza .

Ndi anaendelea kusimulia jinsi familia yake ilivyotengana na jinsi watoto wake wote wamekumbwa na masaibu mengi na mivutano ya aina nyingi. Anapokea barua pepe nyingine kutoka kwa Mtima anayotumia kuelezea masaibu yanayomkumba Uingereza na anaonekana kuchanganyikiwa, abaki Uingereza au arudi nyumbani. Haya yanamsukuma mpaka anapata kiherehere. Jamaa mmoja alipomtembelea anagundua yu taabani na kumpeleka hospitalini. Ndi anashikwa na hofu kubwa kutokana na habari za Mtima.

Mtunzi anatuelezea kuhusu Dubwa anayeleta swala la falsafa ya dini kuhusu wafuasi wa dini kupururuka kutoka kwa dini moja hadi nyingine ili kunufaika kifedha na kutosheleza ubinafsi wao. Dubwa, kifunguamimba ambaye ameishi muda mrefu bila kukanyaga nyumbani anamjia Ndi katika ndoto, jambo ambalo linamshangaza. Akilini mwa Dubwa anawaza kuwa babake analaumu kwa kukawia kwake bila kufika nyumbani ingawa babake haoni makosa yake. Dubwa anaonekana kutokuwa na msimamo wa dini. Mara Muislamu, mara Mkristo, mara mfuasi wa madhehebu ya kuhubiri maangamizo na kuabudu giza kaburini.

Ndi anamwandikia Mtima barua pepe ambayo anaangazia jinsi uongozi umefika kuanzia enzi za Mwingereza kumkalia Sultani. Ndi anaendelea kusema kuwa licha ya Waafrika kunyakua uongozi mambo ni yale yale ya kikoloni kwa sababu imekaliwa na utandawazi, watawala wa dunia walioko nje kabisa. Jibu la Mtima ni kuwa ujumbe wa babake umemfungua macho kwa upande mmoja na kuwa upande mwingine unamzidishia

wasiwasi mazungumzo ya Mtima na babake yanamfanya awaze kurudi nyumbani lakini ghafla anabadili wazo lake anapokumbuka jinsi nyumbani kulivyo.

Uledi anampeleka Ndi kwenye kibanda na kumwamrisha atoe viatu kisha abishe hodi huku akisema “naomba nirudi kwetu.” Punde wanawake wawili wanatokea na kumwingiza ndani. Ndani kuna wanawake watatu Bi. M, Bi Mize na Binti Jabu. Nyuma yao mwanamke kijana zaidi, Yungi binti yake. Bi. M anaamrisha Ndi avuliwe nguo za kiume na avalishwe za kike. Juhudi za hawa wanawake zilikuwa ni kubadilisha roho na fikra za Ndi hasa katika ulingo wa sanaa. Wanamwosha kidonda kifuani ambacho alipata kwa kuogelea kwenye mchanga.

Bi. Mize anamwambia Ndi kuwa ni muhimu alidhibiti tukio hilo kichwani mwake ikiwa anataka kudumu kuwa mwandishi. Alibwie hadi atakapoketi mbele ya kompyuta aandike juu ya kuoshwa na kutakaswa kisanaa na wanawake. Wanataka awatetee na awasemee katika sanaa na mwishowe anaungama kuwa atatekeleza hayo. Kisha Bi. M anamwambia kuwa kwa lolote atakalotaka kufanya akumbuke nguvu maalum za wanawake kwa faida ya watu wa nchi hii wake kwa waume! Bi. M anaamrisha mumewe avalishwe nguo. Anatoka nje na kumpata Uledi karibu na mlango. Ndera anampeleka Ndi kwenye uwanja wa kago la wahenga. Lina watu wengi na wachache anawafahamu. Ni watu ambao wamewahi kuwa watumishi wa serikali. Kisha wanaona joshi ambalo linageuka kuwa joshi jitu. Joshi lile linaonekana likiwapa vileo vya aina fulani na kuwakatakaza.

Mwishowe linaanza kuwapeperusha na kuwaonyesha kule wamepotoka kwa kujaribu kuiga mambo ya kigeni na kuwapuuza wahenga.

Shaib, mhusika ambaye ni kivuli cha nafsi ya Ndi anasimulia kisa cha Ndi kwa Bi M na Yungi lakini hawamsikizi. Kusudi la simulizi lake ni kuwashawishi kuwa Ndi si mwendazimu kama ilivyosemekana. Badaye tunaona kitoto cha Bi. M na Ndi kwa jina Bisudi ambacho si cha kawaida kutokana na mambo kinayoyatenda. Tunaarifiwa kuwa Bi M alijifungua kitoto hiki siku ile ile maafa yalitokea chumbani mwao. Wakati Yungi alimfumania Jitu akimnajisi dadake Kilua. Papo hapo Yungi alichukua kisu tayari kumshambulia Jitu nacho. Ghafla babake akaja kumnyang'anya. Kwa bahati mbaya wakamwangukia Jitu na kile kisu kikamdunga. Yungi alimpeleka Kilua hospitalini ambaye aliaga dunia njiani kwa kuvunja damu sana. Baadaye polisi wakaja na kumkamata Ndi. Tunaona masimulizi ya Bi M kwa Ndi kuhusu kitoto chao. Ingawa masimulizi yenyewe ni ya ajabu sana hayaonekani kuibua hisia zozote kwa Ndi.

Mtima anamwandikia babake barua pepe nyingine inayomjulisha jinsi alivyoshikwa na kufungwa jela. Wakati huu anatumia kompyuta ya ofisi aliyokuwa akifagia kama mfungwa. Tunaona kuwa Ndi anaathiriwa na jambo hili pakubwa. Ndi anaanza kuzungumza na Ye, nafsi yake. Anaonekana mara kukata tamaa, mara anajipa moyo. Kisha katika mazungumzo yake na nafsi yake anaonekana kushikilia msimamo wake wa kukiamsha kizazi kipya.

Mwishoni mwa riwaya, Ndi anarejelea katika uhalisia. Tunamuona Bi.M akimwachia Bisudi ili amwangelie. Wanaonekana kuwa na uhusiano mwema. Pia tunaona Ndi akitaka kujua waliko watoto wake; Kilua, Jitu na Mtima. Kisha anahisi kuwa wote wamezaliwa upya ila jitu ambaye mimba yake haijitungwa. Kilua katika umbo la Bisudi, Bori katika umbo lake Ndi. Na jitu atakapozaliwa atazaliwa kijana wa kizazi kipya kinachojali nafsi ya kila mtu kama Bisudi. Tunamuona Ndi akimsimulia Bisudi hadithi yake, kisha anaruka juu katika maono na kushuhudia jinsi dunia yao ilivyo na machafuko. Kisha anajiua na anapofika akhera anawapata binti zake watatu Bisudi, Mtima na Yungi wakifanya maandamano kupigania heshima za Waafrika. Ndi anaonekana kuwa na imani nao. Maisha ya Ndi yanabadilika na kurudi katika hali ya uhalisia wa maisha. Kisha tunamuona Ndi na Bisudi wakizungumzia kuhusu sherehe itakayofanyika keshoye. Ndi anasema kuwa itakuwa sherehe ya kila mtu. Hili inaonyesha mwisho wa ubinafsi katika dunia yao na kuwepo kwa umoja.

6.3 ITIKADI YA WATAWALA

6.3.1 ITIKADI YA UTANDAWAZI

Kimsingi, utandawazi ni mchakato wa kuunganisha uchumi, siasa, jamii, uhusiano wa tamaduni na kadhalika baina ya nchi. Utandawazi unaifanya dunia kuwa kijiji kimoja kisicho kuwa na mpaka. Utandawazi unasisitiza uondoaji wa vikwazo vya kibiashara na kuifanya dunia kuwa soko moja, unahimiza soko huria, demokrasia, utawala bora usawa wa kijinsia na haki za binadamu.

Kwa mujibu wa Friedman (2005) Utandawazi ni neno lililoanza kutumika miaka ya 1990, likimaanisha kukifanya kitu kuwa katika kiwango cha kimataifa na kukihamisha nje ya mipaka na kukifanya kuwa cha wazi na kikafanywa na watu wa aina yote duniani. Utandawazi ni njia ambayo wenyeji au taifa hufanya mambo kuwa ya kimataifa, kufanya mambo pamoja duniani. Inajitokeza kwa vigeu kama mifumo ya kiuchumi na biashara, teknolojia, siasa, utamaduni na asasi za utawala.

6.3. 1.2 MFUMO WA KIUCHUMI

Uchumi ni jumla ya shughuli zote za binadamu zinazolenga kutosheleza mahitaji ya watu. Ni shughuli za uzalishaji, usambazaji na utumiaji wa bidhaa pamoja na kutolewa kwa huduma kwa njia mbalimbali Mtunzi anazungumzia mfumo wa ubepari ambao ni mfumo wa kiuchumi wenye matabaka mawili makuu; tabaka la matajiri na maskini. Kuna ulimbikizaji na uwekezaji wa mali ambao hutokana na ziada kuendeleza uzazi wa mfumo wenyewe.

Mwandishi kupitia kwa Bi. Mize, anaonyesha kuwa dunia anayoizungumzia inazingatia mfumo wa ubepari unaoleta matabaka katika jamii (uk. 51). Mfumo wa ubepari katika nchi ya mwandishi unaleta kuwemo kwa matabaka mawili katika jamii. Anaonyesha kuwepo kwa matabaka ambapo elimu ilitumiwa kuwabagua na kuwatayarisha katika jukumu tofauti. Anasema ilimbidi ashindane na watoto wa kitajiri ambao walitiliwa walimu wa faragha na udurusu wa vitabu vya ziada katika maktaba zao ili wafaulu

mtihani yao vizuri. Hii ndiyo sababu watoto wengi wa kimaskini hawakuweza kupanda ngazi ya elimu iliyowekwa wakati ule (uk.15).

Anasema kuwa baada ya mageuzi, kazi za ngazi za juu zilitengwa kwa wastahiki fulani na wala hazikutegemea kuwa na elimu, akili au busara, muhimu zaidi wewe ulikuwa nani, mtoto au mjukuu wa bwana gani kuonyesha kuweko kwa wenye majina makubwa na cheo na wengine wasiokuwa na chochote. Watu walipewa kazi kwa mujibu wa kujuana na mapendeleo na hivyo mfumo huu wa kiuchumi ni mbaya kwani unazidi kuibua utabaka ulimwenguni kote na hivyo dunia nzima imegawika kwenye matabaka mawili: lile la mabepari wa kilimwengu na la mafalahi wasio na chochote (uk 65) kutokana na ule unyakuzi wa mali ya umma na wachache katika dunia nzima.

6.3.1.3 SAYANSI NA TEKNOLOJIA

Riwaya ya *Dunia Yao* ambayo ni ya karne ya 21 iliandikwa kama utandawazi umeimarika kimataifa. Hii ni kutokana na teknolojia mpya kama vile kompyuta, kampuni za mtandao, barua pepe na vyombo vya habari kama vile televisheni. Mohamed anamsawiri Ndi, mhusika mkuu na msimulizi wa riwaya kuonyesha dhana ya utandawazi kwa njia kuu. Kwa mfano, Ndi anasema:

Kitu cha kwanza nilichokiona mezani ni kompyuta yangu. Zawadi alioniletea Mtima, Binti yangu... kainunua kuukuu mno, lakini kwangu ni mpya (uk.6).

Kifungu hiki kinaonyesha furaha aliyonayo kutokana na zawadi ya kompyuta ambayo inachangia sana utandawazi. Pia maneno ya Mtima kwenye barua aliyomtumia babake akimwambia kuwa atakapokwisha kujifunza kuitumia watakuwa karibu sana kuzungumza kupitia barua pepe bila shaka yanaonyesha utandawazi kwa vile licha ya Mtima kuwa mbali na babake kimaeneo au kijiografia wanaweza kuwa karibu sana kuzungumza.

Itikadi ya utandawazi inazidi kujitokeza pale ambapo Ndi anasimulia jinsi alijifunza kompyuta kwa bidii kwani alijua ni mwokozi wake katika maisha ya upweke na unyamavu kiasi cha kuihuisha (uk.11). Aidha, mwandishi anasimulia kuhusu kampuni ya mtandao ambayo inawezesha mazungumzo kupitia barua pepe ambayo Ndi anafurahia sana ili wazungumze na Bintiye Mtima ambapo kuna uhuru wenye hatari kutokana na usasa na mabadiliko ya haraka. Hivyo Ndi anakerwa na Bintiye Yungi aliyemkashifu na kumkemea hadharani jambo ambalo analihusisha na usasa na utandawazi.

Mwandishi anasema kuwa, ubinafsi katika karne hii umeimarishwa na sayansi na teknolojia na dunia imekuwa moja vibaya mno kwa sababu ya usahili wa uwazi wake na wepesi wa mawasiliano. Anasema maafa yakitokea pahala pamoja huenea duniani kote kwa sababu ya teknolojia (uk.48-49). Mwandishi anaonyesha kuwa teknolojia inachangia kuenea kwa maafa kwa kasi mno ulimwenguni, kutohifadhiwa kwa utamaduni na maadili mabaya katika jamii. Kwa mfano, kuwepo kwa ngono, ulevi, uchi, matusi, kelele na mavazi mabaya, madawa ya kulevya pamoja na kudhoofika kwa afya. Anatarifu kuhusu

CD ya “I need to know” ya Marc Anthony na chombo cha kuendesha CD alichokinunua zamani katika safari alizopata kwenda London kikazi alipokuwa mkuu wa idara ya matumizi (uk.56).

Mtima anawasiliana na babake kupitia kwa barua pepe kuonyesha umuhimu wa teknolojia katika kuwaunganisha watu licha ya kuwa mbali kijiografia na kijamii. Anasimulia jinsi safari yake kwenda Uingereza ilikuwa mpaka pale anapowasili na barua pepe inasaidia sana kuwaleta watu walio mbali kimaeneo pamoja na hii ndiyo dhana ya utandawazi inayojidhihirisha kwa maendeleo ya kiteknolojia ya haraka na kusababisha watu kuwa kama kitu kimoja (uk 95-96).

Mwandishi anatumia joshijitu ili kuonyesha hatari na maafa ya utandawazi katika jamii yake. Anaonyesha itikadi yake kuwa utandawazi uko kila pahali bila idhini na hiari ya wanajamii (uk.205-206).

6.3.1.4 ELIMU

Elimu ni tendo au uzoefu wenye athari ya kujenga akili, tabia ama uwezo wa kimaumbile wa mtu binafsi. Katika dhana ya kiufundi, elimu ni njia ambayo hutumiwa kimakusudi na jamii kupitisha maarifa, ujuzi na maadili kutoka kwa kizazi kimoja hadi kingine. Itikadi ya mwandishi kuhusu elimu na usomi ni kuwa inatafakari uchungu ulioko katika jamii. Wale ambao hupata elimu ya juu bali wamekosa ajira (uk.16). Mwandishi anaisawiri elimu kama ambayo haithaminiwi sana siku hizi na vile inavyopuuzwa hata waalimu

wake wamepungukiwa na maarifa, watoto wanafeli na mitihani inauzwa (uk. 42). Jambo hili linaonyesha kuwa elimu katika enzi ya utandawazi si tiketi ya kupata kazi nzuri kama ilivyo katika kazi zake za awali kama *Asali Chungu* na *Kiza Katika Nuru* bali ni asasi tu ya kuuendeleza ubepari wa kilimwengu na anadhihirisha uchungu alionao kutokana na watu kuwaajiri watu kwa kuzingatia udugu.

Kupitia kwa mhusika Bori mwandishi anaonyesha kuwa elimu ilionekana ya thamana hapo mbeleni kama akiwahimiza watoto wake wasome na hata kuwasimamia lakini sasa tunaona akikata kuhusu elimu kama anavyosema:

“Nadhani nilimwambia kwa sauti kali kama ya kukemea (lakini sina hakika) kwamba hapa tulipo, kusoma na kutosoma 8ni sawa. Elimu haimhakikishii mtu chochote mizani za kupimia mambo akilini mwake.....wale waliosoma walisoma kwa bidii wakidhani utakuja wakati elimu itawafaa. Haijafika wakati huo Bori. Haitafika enzi ya elimu kuwa na manufaa- si wakati wangu wala wenu (uk. 114-115).

Kifungu hiki kinaonyesha kuwa licha ya wengi kuwa na elimu ya juu wamekuwa na mtazamo mbaya juu ya elimu kutokana na hali ya ukosefu wa ajira kwa sababu ya mapendeleo ya kifamilia na ufisadi na hivyo maana ya elimu haionekani katika jamii ya kilimwengu. Mwandishi anaonekana kuamini elimu ni kipengele mojawapo cha utawala ambapo walio na elimu ya juu hawafaidiki sana huku wanaomiliki mifumo ya kiuchumi na biashara wakiendelea kutajirika na kujilimbikizia mali kufungamana na mkabala wa Althusser (1981) kuhusu itikadi kuwa elimu ni asasi mojawapo inayotumiwa na watawala kuendeleza itikadi ya kitawala ili kuhifadhi utabaka wao.

6.3.1.5 UTAMADUNI

Katika riwaya ya *Dunia Yao* mtunzi anaona kuwa utandawazi umekwisha ondoa mipaka na kuufanya ulimwengu jiji moja na kuathiri utamaduni kabisa. Kupitia kwa msimulizi mwandishi anaonyesha imani yake kuwa mavazi na mienendo ya Yungi imechangiwa pakubwa na utandawazi anaposema:

Hii ni fensi mpya, Carnival ya globalization, na kwa hivyo kila mtu alivaa kivyake, alijifanya kinyago kivyake... Hakuna adabu heshima au kujuliana. Hakuna ubaba au ubinti (uk. 128).

Dondoo hili linaonyesha imani ya mwandishi kuhusu athari za utandawazi kuwa utamaduni umeathirika sana, kupitia kwa mavazi ya Yungi, kule kujibizana na babake kunaonyesha imani ya mtunzi ya kuwa utandawazi umeleta ubinafsi kiasi ya kuwa hakuna anayemjali mwingine tena. Mtunzi anaonyesha kuwa mabadiliko ya kitamaduni yamesababishwa na utandawazi na kufanya watu kuujali ubinafsi wao pekee.

Anaonyesha jinsi wananchi wa kawaida wanaingia katika sherehe kuonyesha namna utandawazi umeathiri utamaduni wa dunia nzima na kuwa ni itikadi tu ya watawala wa nchi matajiri kuendeleza njama zao za kuendelea kutawala uchumi wa ulimwengu.

Wengine wamevaa kama Mao, Lenin na wengine kama Gandhi. Kuna pia waliovaa ki-churchill au kirais wa US, wengine ki-cowboy au ki-Western (uk. 175).

Mwandishi anaamini kuwa utandawazi umeenea na umeathiri mavazi ya jamii yake wameacha utamaduni wao na kuukumbatia wa kigeni. Na kama tunavyoona majina yaliyomo kwenye dondoo ni ya viongozi au waliowahi kuwa viongozi katika nchi za

ng'ambo wala si za kiafrika. Hii inaonyesha namna utandawazi ni dhana ambayo imeathiri dunia nzima hasa Afrika lakini mataifa ya kimasikini kama ya Afrika yanafuata mkondo tu huku mataifa yaliyoendelea kama Marekani yakitawala ulimwengu hivyo utandawazi ni kigeu tu cha kuendeleza utawala wa kibepari na kutawala nchi zinazoendelea.

Mohamed anaonyesha msimamo wake kuwa kuna hatari zinazotokana na mambo ya kiteknolojia na utandawazi ambazo wengi wanayakimbilia. Ogun mhusika ambaye ana sifa za kiungu anaendelea kueleza wenyeji kuhusu athari za utandawazi huku akionyesha jinsi manufaa yake ni kwa nchi zenye mizizi ya utandawazi. (uk. 192). Anaonyesha msimamo au imani kuwa utandawazi ni jambo la hatari na lenye athari mbaya kwa wenyeji kutegemea tu ubunifu wa nchi za kigeni hasa zile nchi zilizoendelea kwa sababu mwishowe manufaa huwa ni kwao pekee (uk. 193).

6.3.1.6 NDOA NA MAPENZI

Ndoa ni muungano kati ya mume na mke hadi kifo kitakapowatenganisha (TUKI, 2013). Kwa hivyo, tunastahili kuona watu waliooana kuishi pamoja bila kutengana. Lakini tunaona utengano kati ya mume na mke mara kwa mara katika *Dunia Yao*. Pia wengine wanaenda nje ya ndoa kama vile mke wa Sakarati. Kutokana na maelezo ya Sakarati, tunaona imani ya mwandishi ni kuwa, ndoa haiheshimiwi katika jamii kwa vile inaonekana kuwa Sakarati alielewa vyema mienendo ya mkewe na hakujali mpaka anapoanza majuto wakati walipatwa na ugonjwa wa ukimwi. Hii inaonyesha itikadi ya

kuwa ndoa zinakabiliwa na talaka, kutengana na pia kunyimana haki za “kufanya mapenzi”. Kwa jumla pia tunaona sehemu kubwa ya riwaya inaonyesha mume anakimbia majukumu yake katika ndoa. Mhusika ambaye amewakilisha swala hili ni Ndi ambaye anayakimbia majukumu yake. Hamjali mkewe Bi. M wala kumpa haki zake.

Niliwahi kuona kipindi kimoja cha TV, simulizi za kweli za msichana wa miaka ishirini na tatu wa Ki-Belgiji anayeishi Uingereza ...ameshakwenda na wanaume elfu mbili... ingawa ana mume wake na mume anajua na kuitambua kazi hiyo ya mkewe. Hii ndiyo dunia yao (uk. 90).

Kifungu hiki kinaonyesha kuwa ndoa haiheshimiwi kote ulimwenguni bali ni kipengele tu cha kuendeleza itikadi tawala ya utandawazi. Anadhihirisha kuwa changamoto katika ndoa ni swala linaloathiri dunia nzima kudhihirisha kuwa mawazo yake yamepevuka na kuangazia maswala yanayoathiri dunia nzima na kuonyesha kuwa familia na ndoa ni kipengele kimojawapo tu cha kuendeleza itikadi tawala ya kitandawazi.

6.3.1.7 DINI

Dini ni imani maalum ya kuamini na kumtii mungu wa haki. Dini zilizotajwa katika riwaya ni ya Kiislamu, Kikristo na Ki-Budha. Dini ya Kiislamu ndiyo inaonekana kuhusishwa sana na jamii ya mwandishi. Tukiangazia jamii ya mwandishi tunaona ya kwamba ingawa mambo ya dini yanajitokeza kila mahali, wengi hawayatili maanani. Kuna maadili mabaya na pia imani ya wanajamii inaonekana kuyumbayumba. “Mungu amemdondoshea kila mja tone dogo la sifa zake...” (uk.8). Kupitia kwa mhusika Ndi, mwandishi anaonyesha kuwa jamii yake ina imani kwamba Mungu ana sifa kuu ambazo anaweza kumrithisha binadamu. Msimulizi anaelezea kuwa dini ya Kiislamu ilitiliwa

maanani alipokuwa mchanga lakini siku hizi inatumiwa kuwadanganya watu na kuafikiana na mawazo ya Marx kuwa dini ni ung'amuzi potoshi inayotumiwa na watawala kuendeleza itikadi tawala ya kitandawazi na kuuendeleza ubepari. Anasema:

Dini zote kubwa na ndogo karne kwa karne zimekuwa zikipigana na ki-jiungu hiki lakini siku hizi dini zote kubwa zimekuwa zinatumiwa kukirutubisha kijiungu hicho (uk.48).

Kulingana na mwandishi, dini katika jamii yake imekwisha poteza maana yake halisi, yaani imepotoka. Anaonyesha unafiki wa imani na dini baada ya kusimulia mhusika Sadala kusimulia kisa cha mzungu mmoja aliyekuja kumchukua binti ya jirani mbele ya wazee wake na Shehe aliyekamatwa akiiba boflo dukani. Kupitia kwa hadithi ya Mwadi, mwandishi anaonyesha kuwa maadili ya dini ya Kiislamu yamepotoka na kupoteza maana (uk. 52) na kuwa pesa ndizo zinazojalisha kufungamana na itikadi ya kitandawazi. Bi Mize anasema kuwa dini imeasi mienendo ya kweli na kufuata pesa ambazo zinaleta chuki.

Dubwa anasawiriwa akitoka imani moja hadi nyingine, mara mwislamu mara mkristo na mara mfuasi wa madhehebu ya kuhubiri maangamizi na kuabudu giza makaburini. Mara anaokoka mara anarudia uislamu uliomzaa. Hili linaonyesha ule ulaghai wake wa mambo ya dini ili kujinufaisha wenyewe kiriziki na kifedha. Hii ndio maana wengi wanahama kutoka kwa dini moja hadi nyingine, jambo linalohusishwa na itikadi tawala ya kitandawazi. Ni dhana ya Althusser kuwa dini ni kipengele kimoja cha kuendeleza itikadi tawala. Hivi ni kusema kuwa ili kuendelea kudhibiti mataifa machanga na kimasikini,

dini zinatumiwa kuwafanya watu wa nchi hizo kuendelea kuziamini huku mataifa ya Ulaya yakizidi kupiga hatua kimaendeleo kama inavyodhihirika katika dondoo hili:

Hapa petu pana nafasi kubwa sana ya dini. Huko Amerika, Ulaya na Asia dini imeshakimbia ndio maana wanakimbilia kwetu kuja kueneza dini. Hapa petu bado dini inahitajika (uk. 141).

Hii inaonyesha namna dini inatumiwa kama kipengele cha utawala wa kilimwengu wa kitandawazi ili mataifa matajiri yaendeleo kuhifadhi na kuendeleza utajiri, biashara na mifumo ya kiuchumi na utawala huku mataifa yanayoendelea na ya kimaskini yakizidi kupotelea kwa dini mbalimbali kwani hawana suluhisho.

6.3.1.8 MAADILI

Maadili ni kanuni juu ya tofauti kati ya haki na uovu au wema na ubaya. Mwandishi amezungumza juu ya maswala ya maadili katika jamii yake na kimataifa. Lengo lake ni kuonyesha jinsi itikadi ya utandawazi imeathiri maadili kwa kuendeleza maadili potovu kama ubinafsi, ulevi, ukahaba, wivu, ubakaji, wizi, utengano, ulaghai, ukatili, unafiki na mengineyo.

Mtunzi anaonyesha ubinafsi ni hali ya kutojali wengine. Jamii ya mwandishi inaonekana kuwa na ubinafsi mwingi sana ambao unaonekana kupitia kwa wahusika mbalimbali. Kwa mfano, Ndi mhusika mkuu anaonekana kuwa na ubinafsi wa hali ya juu. Hili linamfanya ajitenge na familia yake na pia kutoroka majukumu yake kama mume na baba ya watoto wake. Tunaona namna anavyojifungia njozini na kuzungumza na nafsi yake

wakati mwingi badala ya kuzungumza na wahusika halisi. Muda wote anaonekana kutojali kinachoendelea katika familia yake. Hivyo familia yake inakuwa na utangano.

Wengine wote watoto wangu wapo hapahapa, lakini nimewapoteza. au, bora wamenipoteza au tumepoteana... wapo lakini hawapo mbele ya macho yangu na mimi mbele ya yao (uk. 6).

Mwandishi kupitia kwa Ndi na familia yake anaonyesha ubinafsi katika jamii yake kiasi cha kutojali wengine hasa watu wa familia.

Nimo tu mpaka nagaragara kwa wenzangu ambao kwa muda mfupi wameshanichoka. Sina budi lakini kung'ang'ana. Ndiyo maisha ya huku yalivyo. Kila mtu hubeba mzigo wake. Kila mtu hujitaka mwenyewe. Hamtaki mwingine (uk. 7).

Kupitia kwa maneno ya Mtima mwandishi anaonyesha jinsi hali ya ubinafsi imeenea hata katika nchi za kigeni kama Mtima anavyomwarifu babake hali ilivyo Uingereza. Aidha kupitia kwa maneno ya Ndi, mwandishi anaonyesha jinsi wazazi wanaepuka majukumu ya kuwaelekeza watoto wao kwa njia zinazofaa. Kwa upande mwingine tunaona kuwa hata watoto wenyewe hawako tayari kuyasikiza mawaidha ya wakubwa wao.

Na kwa hivyo mimi nina haki gani kumwamulia na kumwambia Yungi kwamba usoni kwake kuna hatari? Na Yungi kwa upande wake ana haki gani kuukaripia ung'ang'aniaji wangu? Anajuaje wakati pia umefika kwa baba wanaoweza kutia mimba na kuwakimbia watoto wa ajabu umefika? Na pengine mimi ni mmoja wa mababa hao! Aaa, labda sisi tunakitikia kijiungu kidogo kilichoketi ndani mwetu, kinachendesha ubinafsi wetu (uk. 27).

Maneno haya yanaonyesha kuwa ubinafsi umekita mizizi katika jamii ya mwandishi na hauonekani kama jambo la kushangaza. Ndi anakuta wasichana wawili wakipigana hadharani na hakuna mtu yeyote anayeingilia kukemea au kuamua. Anasema kwamba mbali na kuwa aliichukia picha hiyo alijifunza kuepuka mambo ya watu baada ya

kukumbwa na balaa mara nyingi alipojifanya mwamuzi (uk. 33). Kupitia kwa maelezo ya Ndi mwandishi, anaonyesha jinsi hali ya ubinafsi ilivyo katika jamii na hakuna anayemjali mwingine ikilinganishwa na hapo awali.

Mwandishi anaamini kuwa ubinafsi ulioko katika jamii ya kilimwengu umeletwa na sayansi na teknolojia ambazo ni nguzo kuu za utandawazi maana umeenea kote duniani hata huko London, Uingereza. Tunaona imani ya mwandishi kuhusu ubinafsi ni kuwa unaweza kumalizwa na kuibuke jamii yenye umoja na yenye kujaliana.

Aidha mtunzi anazungumzia ulevi ambao ni hali ya kutumia vileo kama vile pombe na madawa ya kulevya. Mwandishi kupitia kwa Uledi na mkewe waanaonyesha ulevi katika jamii za kilimwengu (uk. 39). Ndi anasimulia kisa cha bintiye Yungi, vile alivyoingia nyumbani na uchangamfu na kicheko cha kilevi. Kupitia kwa maelezo haya mwandishi anaonyesha kuwa mtoto wa kike ameingia katika mambo ya ulevi “... Na pombe imehanikiza uchachu. Inapikwa ovyo na kunywea kwenye jahara ya watu ovyo” (uk. 32).

Mwandishi anamtumia Uledi kuonyesha swala zima la ulevi katika jamii yake. Kwenye mazungumzo kati ya Ndi na Uledi, Uledi anasema, “Watakufa wote lakini mimi niko pale pale na ulevi wangu...” (uk. 38). Hili pia linaonyesha ulevi wa jamii. Ndi anaelezea kuwa anasikia Uledi alianza ulevi tokea utotoni (uk. 39). Kwa hivyo anaendelea kumtumia Uledi ili kuonyesha ulevi wa jamii. “...na ule moshi wa sigareti aliyokuwa akivuta...”(uk. 103). Mwandishi anaonyesha kuwa mbali na ulevi wa pombe mtoto wa

kike pia anashiriki kwenye ulevi wa sigara. “... vijana wake wawili wameshaingia katika jela ya wendazimu kwa unga” (uk. 129). Kauli hii imetumiwa na mwandishi kuonyesha kuwa vijana katika jamii ya kilimwengu wanatumia madawa ya kulevya na anaamini kuwa hii inatokana na athari ya utandawazi hasa Adala anapokamatwa alipokuwa akipitisha madawa ya kulevya kwenye uwanja wa ndege (uk. 157).

Mtunzi pia anazungumzia uasherati na ukahaba ambapo uasherati ni kufanya kitendo cha ngono nje ya ndoa ilhali ukahaba ni kufanya ngono ukitarajia malipo. Anaonyesha kuwa jinsia ya kike inajikimu kupitia kwa ukahaba kama kwa mfano anatarifu kuwa Yungi alikuwa kahaba na alivaa mavazi ya “mtindo wa FUNDI –kasahau-mshono” (uk.104).

Aidha, Sakarati anamwambia Ndi kuwa mkewe alikuwa akilala nje ya ndoa ili kuisawazisha dunia ya wao wawili na watoto wao (uk. 156). Mwandishi anaonyesha imani kuwa mwanamke anatoka nje ya ndoa ili kuchumia familia yake. Mambo haya yanatukumbusha jinsi Ndi aliishi kushuku kuwa mkewe Bi M alitafuta riziki ya familia yake kupitia kwa ukahaba. Kuna kisa cha msichana wa miaka ishirini na mitatu kuwa alikuwa amelala na wanaume elfu mbili licha ya kuwa ameolewa huku ubakaji ukiwa umekithiri (uk. 90). Utu umekosekana ndio maana watoto wachanga wanabakwa katika jamii za kilimwengu, ishara kuwa kuwa maadili yamezorota sana duniani kote kwa sababu ya sayansi na teknolojia zinazoletwa na utandawazi.

6.3.1.9 ASASI ZA UTAWALA NA SIASA

Siasa ni njia ya kufanya maamuzi katika taifa, mji au hata dunia nzima (siasa za kimataifa). Sehemu muhimu ya siasa ni majadiliano kati ya watu mbalimbali wenye nguvu au mamlaka. Katika demokrasia, kila mtu ana kiasi fulani cha nguvu. Kwa hivyo, siasa ya demokrasia ina maana ya watu wote kuchangia maamuzi. Wakati mwingi haya hayawezekani kutokana na mambo kama vile utawala mbaya wa ukoloni mambo leo ambao unaleta jaribio la mapinduzi na maandamano ili kuzipigania haki. Mtunzi anazungumzia sheria ambazo ni kanuni zinazoongoza nchi au jamii anatumulisha kuwa hazizingatii haki nchini. Na hata wanapojua hakuna anayeshughulika kuona haki inatendeka na hivyo sheria ni asasi tu mojawapo ya kuendeleza itikadi ya watawala kufungamana na mawazo ya Althusser (1981) kuwa sheria hutumiwa kuendeleza itikadi ya kitawala wala si kulinda haki. Aidha, mifumo ya kitawala kama demokrasia ni asasi mojawapo ya kunyamazisha watu wala si kwa maslahi yao.

Kuhusu utawala ambayo ni shughuli nzima ya uongozi inayojumuisha mchakato wa kutoa uamuzi, kupitia kwa vikundi kama vile vyama vya kisiasa, mtunzi anasema ya kwamba utawala ni jambo la kimsingi ambalo linapaswa kuzingatiwa kwa makini katika dunia nzima la sivyo dunia nzima inaweza kuangamia kutokana na utawala mbaya na wenye ukorofi na matumizi ya kimabavu. Kauli “polisi gani hao siku hizi wanajishughulisha na matatizo ya akina sisi.” (uk. 21) inaonyesha utawala mbaya, ambapo polisi wanaowakilisha serikali ya nchi wanatumiwa kuwanyamazisha watu na

kudhihirisha zaidi mkabala wa Louis Althusser kuhusu itikadi ambapo tabaka tawala huweza kutumia nguvu kama za polisi kuendeleza itikadi yao hata huko Ulaya.

Kuhusu mapinduzi ambayo ni kuangushwa kwa nguvu ya serikali au utaratibu wa kijamii kwa mfumo mpya, mtunzi anasema ya kwamba mapinduzi haya yanasababishwa na uongozi mbaya. Kutokana na utawala mbaya wajamii wanajaribu kufanya mapinduzi. Jaribio hili linapelekea Ndi na wahusika wengine waliokuwa na nyadhifa serikalini kupoteza kazi zao na kuishi katika upweke. Punde si punde polisi wanamjia kumkamata na kumpeleka jela. Mwandishi kupitia kwa Ndi anaonyesha utawala mbaya na kunyimwa haki ya kueleza kwa wanajamii, itikadi yake ni kuwa utawala ulioko unahitaji kubadilishwa ili ujamaa ulishe kila mtu” (uk. 84). Juhudi za mapinduzi huendelezwa kupitia kwa maandamano ambayo ni mkutano wa hadhira au harakati za kupinga dhidi ya kitu au kutoa maoni juu ya swala la siasa (uk. 210).

Maneno haya ya Bi.M kwenye sura ya mwisho yanaonyesha itikadi ya mwandishi ya kuwa, ili uhuru na haki itendeke katika jamii lazima wanajamii watumie nguvu. Hii ndiyo maana kunakuwa na maandamano ya ghafla mwishoni mwa riwaya.

6.3.1.10 MABADILIKO YA KIJAMII

Kulingana na mwandishi, jamii yake imo katika kasi ya mabadiliko ya kiuchumi, kijamii na kisiasa. Mabadiliko haya yanatokana na utandawazi ambao umepata kasi kubwa ya

kuwekeza kiuchumi na kitamaduni. Mabadiliko haya kwa sehemu kubwa, yanatokana na upeo wa matatizo ya kiuchumi yaliyosababishwa na maslahi ya kibiashara na utashi wa mataifa makubwa yanayolenga kila siku kupata faida kubwa kupita kiasi kutokana na dhamira ya utandawazi kutawala katika binadamu. Mabadiliko mengi yanatokea, kwa mfano lugha, uchumi, mavazi, maadili, mila, utamaduni, dini, muziki na chakula. Kwa mfano, Ndi ni mhusika aliyewahi kuwa na wadhifa wa juu serikalini na ambaye aliwahi kupigania haki za nchi yake. Hali yake mpya inatokana na kuporomoka kwake kihali na kiuchumi. Mwandishi amemtumia Ndi, mhusika mkuu kama chombo au mwakilishi wa maporomoko ya wengi katika jamii kihali na mali.

Ndi anasema:

Mengi niyaandikayo humu yalikuweco wakati ule na bado yapo sasa. Ila sasa yamevimba, yamefura, yanasonga ndani ya nyoyo zetu kama matapishi ya nyongo chungu yanayotapia kutoka kinywani” (uk. 5).

Kupitia kwa dondoo hii mwandishi anaonyesha jinsi machafuko katika nchi yanazidi kuwa mabaya kila kuchao. Anaonyesha namna dunia imeharibika na kuwa na maadili mabaya si ile aliyoiua mbeleni. Anasema ,“Vijana wakali siku hizi bana” (uk. 32) kuonyesha imani yake kuwa vijana katika jamii yake wamebadili lugha, miondoko na hata mavazi.(uk. 41). Mwandishi anaonyesha jinsi jamii imeaathirika na kubadilika. Mwandishi anaamini kwamba mabadiliko katika jamii yake ni jambo la lazima.

Mwandishi anaamini kuwa dini zimebadilika zikilinganishwa na dini zilizokuwepo kabla ya karne ya dunia yao. Mabadiliko hayo yanafanya dini kutopigana na kiji-ungu

(utandawazi) ambacho imekuwa ikipigana nacho awali ndiposa akasema, “Na naona kuwepo kwa dini mpya ambayo imeundwa na viji-ungu kama vile sayansi, teknolojia na utashi wa pesa” (uk.135). Jambo hili analisawiri vyema anapohadithia kuhusu shehe na imamu wa msikiti wao aliyekamatwa akiiba boflo dukani. Mwandishi anaonyesha jinsi dini imebadilika na kuwa pahali pa kujificha na kuafikiana na mawazo ya Karl Marx kuwa itikadi ni ung’amuzi potoshi na pia mkabala wa Louis Althusser kuwa dini ni asasi mojawapo ya kueneza itikadi za kitawala na kuwafanya watu watii na wakubali hali zao zilivyo.

Mohamed katika riwaya ya *Dunia Yao* anasawiri mabadiliko ikilinganishwa na riwaya alizoandika hapo awali kama vile *Asali Chungu* na *Kiza Katika Nuru* kati ya nyinginezo. Mabadiliko yake makubwa ni matumizi ya lugha ya kigeni ama ukipenda kuchanganya ndimi. Mara kwa mara panatokea kuchanganya ndimi katika muundo na mtiririko wa riwaya. Jambo hili anaonekana kulifanya tu kimakusudi. Hili inaonyesha kuwa amekumbatia mabadiliko kupitia kwa uvunjaji wake wa kanuni za lugha. Vile vile tunaona utohozi wa hali ya juu hata kwa maneno yenye maana halisia kwa lugha ya Kiswahili. Haya yote yanatokana na athari za utandawazi na kuonyesha kuwa anakubaliana na itikadi hii ya utandawazi.

Kule kuporomoka kwa Ndi ambako kunamfanya ajifungie njozini ili kukimbia ukweli na kubadilisha uhusiano wake na familia yake ni hali ya mabadiliko. Mwandishi anaonyesha itikadi ya mabadiliko ya dini kupitia kwa Bi Mize (Bi Muse) ambaye ni mhusika

anayemjia Ndi ndotoni. Kauli hii inaonyesha mwandishi ana imani kuwa dini ya Kikristo na Kiislamu imekwisha badilika na kuathiriwa na mambo ya kigeni. ”. (uk. 71).

Mwandishi anatumia mhusika Bi Mize (Bi Sanaa) ili kuonyesha umuhimu na haja ya mabadiliko ya kisanii. Kwa hivyo, ana mtazamo kuwa sanaa inapaswa kubadilika kiwakati na kwamba haifai kukwama kwenye uhalisia mtupu “Mtu anaweza kuzaliwa upya?...enh, Ndiyo! Inawezekana?” (uk. 73). Kupitia kwa mhusika Bi Mize mwandishi anaonyesha kuwa mabadiliko yanawezekana. Anadhihirisha uwezekano wa mabadiliko ya kiitikadi kuwa mwanzoni katika riwaya za awali alizungumzia hali halisi zilizoikumba jamii yake kikweli lakini sasa amebadilika na kutumia mitindo mipya ya kinjozi kuwasilisha maswala yanayoathiri dunia nzima.

Mwandishi kupitia kwa Ndi anaonyesha jinsi jamii yake imepoteza hisia na jinsi mabadiliko yamesababisha maadili mabaya. Hii ni kwa sababu tunaona kutoathirika kwa Ndi na habari anazozipokea kutoka kwa Kilua kuwa Yungi anaugua ukimwi kuonyesha mwandishi anaamini kuwa usasa umewafanya watu wa jamii yake kupuuza nguvu za kiasili kwa vile wamebadilika kimawazo. Tunamuona Ndi akielezea mavazi ya bintiye Yungi. Vazi la aibu mbele ya babake huku akivuta sigara linaonyesha mmomonyoko wa,utamaduni wa kiafrika. Hivyo mwandishi anaonyesha kuwa tabia na utamaduni wa vijana wa kiafrika umeathiriwa na utandawazi (uk. 104). Mazungumzo kati ya Yungi na Ndi, babake yanaonyesha mabadiliko ya mila na desturi za kifikira. Kwanza, tunamuona Yungi akimkabili babake hadharani huku akijaribu kumkosoa pale alipojaribu kufanya

mapinduzi. Kwa upande mwingine Ndi, babake anampa uhuru wa kuendelea kufanya atakavyo na mwili wake. Ajabu sana. Haya yanaonyesha mabadiliko makubwa ya tabia na desturi za kiafrika. (uk. 112).

Mohamed anaamini kuwa dunia iko katika harakati za mabadiliko katika kila nyanja. Lakini mabadiliko haya hayafai nchi changa kwani utandawazi ni itikadi inayoendelezwa na mataifa yaliyoendelea ili yaendeleo kuhifadhi nguvu zao za kiuchumi, biashara, utawala na teknolojia huku mataifa maskini na machanga yakizidi kutumbukia kwenye lindi la umaskini na uongozi mbaya kwani asasi za utandawazi haziafikiani na malengo yao ya kitaifa na mazingira yao halisi yaani anaupinga utandawazi kabisa kuwa haufai kwa mataifa changa unaleta madhara makubwa.

Kupitia kwa mhusika Ndi; msimulizi wa riwaya, mwandishi anakubaliana na uondoaji wa itikadi za kuumeni katika jamii yake na kuwajumlisha wanawake kwenye shughuli za maendeleo ya jamii. Anaona ni vyema wachangie bila kuachwa nyuma jinsi walivyokuwa wameachwa kwa karne nyingi. Hili linaonyesha imani ya mwandishi ni kuwa wanawake wamepata usemi katika jamii yake na pia wanasikizwa (uk. 185).

Nasema na wewe muumba! Wewe Ndiye uliyetandika ardhi hii, ikalala juu yake amani na utulivu. Kiasi kwamba hakukuwa na matata yoyote. Watu hawakuzozana wala kugombana au kupigana wakati ule... kwani sasa watu husema kwa vinywa vingi kwa sauti mbali mbali?" vijiji vinakimbiana na miji kutengana..."(Uk. 189-190).

Kifungu hiki kinaonyesha imani ya kuwa ardhi imebadilika si ile ya kale tena, machafuko yamo ardhini. Upeo wa mabadiliko katika dunia yao ni ambapo Ndi mhusika mkuu anarejea katika hali ya uhalisia wa maisha. Na kuanzia hapo anaanza kuwa na uhusiano wa karibu na jamii yake pasipo kuyakimbia majukumu yake. Tunaona akiachiwa Bisudi, kitoto chao. Pia anaonekana akisaidia kazi za nyumba bila ya kulalamika. Haya yanaonyesha itikadi ya mwandishi kuwa mabadiliko ni sehemu ya maisha katika jamii yake lakini yeye anayapinga (uk. 210).

Yungi amekwenda mkutanoni... si unajua kwamba wanataka kuvunja nyumba za eneo letu hili lote kwa kujenga hoteli ya Wataliana? Tumeshaunda umoja wa kupinga na kukataa. Yungi amechaguliwa kuwa kiongozi na kwa hivyo yumo mbioni, kukutana na wakaazi. Siku hizi kazi zinamtafuta kugombania haki kunamngoja (Uk. 210).

Kifungu hiki kinaonyesha itikadi ya mabadiliko ya aina nyingi katika jamii. Kwanza ni kule kubadilika kwake Yungi; kaacha tabia ya ukahaba na kuwa mwanaharakati wa kupigania haki. Itikadi ya mwandishi ni kuwa jamii yake inaweza kubadilika kimaadili na kuwa nzuri. Pili ni mabadiliko ya itikadi ya kuumeni. Mwanamke ameanza kupata nafasi ya kuunda chama cha kupinga na kukataa kinyume na hapo awali. Vilevile kule kupigania haki kwa Yungi kunaonyesha mabadiliko ya itikadi ya kuumeni katika jamii ambayo huchukulia kuwa mwanamke hana usemi katika jamii. Mwandishi anaonyesha kuwa ingawa jamii yake imekuwemo katika hali ya dhiki na uchungu kuna matumaini ya raha na tabasamu.

Ati kesho imeandaliwa sherehe yangu. Sherehe ya kuwepo sherehe ya msimamo wangu mpya, sherehe ya sanaa yangu! Mimi nikamjibu kuwa kesho itakuwa sherehe ya kila mtu anayeipenda nchi hii na anayeipenda Dunia Yetu (uk. 213).

Kwenye mtiririko na muundo wa riwaya hii tumeshuhudia ubinafsi wa hali ya juu p hakuna anayemjali mwenzake. Maoni ya mwisho hapo juu yanaonyesha mabadiliko ya jamii ya mwandishi kutoka hali ya ubinafsi na kuwa jamii yenye umoja na ushirikiano na ambayo inaweza kushiriki pamoja kwenye sherehe na hivyo kuonyesha kuwa msimamo wake kuhusu mabadiliko si mmoja na tengemano. Aidha, anaonyesha kuwa mabadiliko hutokana na maamuzi ya mtu binafsi wala si matumizi ya nguvu kama katika riwaya za awali na hivyo itikadi yake kuhusu mabadiliko ya kijamii imebadilika.

Kwenye maelezo haya, mwandishi amemtumia Ndi mhusika mkuu kama chombo cha kuwasilisha hisia zake kuhusu utandawazi. Ni dhahiri kuwa mwandishi ana uchungu kutokana na maafa na athari za utandawazi katika jamii yake. Kwa hivyo, itikadi yake ni kuwa utandawazi umekuja kumomonyoa kila kitu katika jamii yake kama vile utamaduni, shule, vyuo, desturi, mila, heshima, mustakabali wa watu na baya zaidi roho zao.

Anaonyesha utandawazi ulivyoathiri nchi za magharibi za kaskazini. Anapoangalia kusini na mashariki anawaona watu duni ambao wanapigana wenyewe kwa wenyewe. Hili linaonyesha itikadi ya mwandishi kwa nchi zenye mizizi ya utandawazi zinazipiganisha nchi duni kupitia kwa teknolojia na utandawazi. Wakati huohuo nchi hizi zinaendelea kuimarika huku nchi za kusini na mashariki zikididimia na matokeo yake ni mwanya mkubwa sana. Itikadi ya mwandishi kuhusu utandawazi ni kuwa maafa yake ni mengi sana yakilinganishwa na faida au ufaafu wake na hivyo msimamo wake kuhusu

utandawazi ni kuwa haufai kwa mataifa machanga bali ni itikadi inayoendelezwa na mataifa yaliyoendelea ili kujinufaisha na kuendeleza dhuluma na tawala zao za mifumo ya kiuchumi na biashara, teknolojia, asasi za utawala, nia ikiwa kuendelea kuhifadhi ubepari na ukoloni wao kwa mataifa machanga hasa ya Kiafrika.

Maswala haya ya utandawazi hayajitokezi katika riwaya tulizojadili yaani *Asali Chungu* na *Kiza Katika Nuru* jambo linalodhihirisha kauli yetu kuwa Mohamed anabadilisha itikadi zake katika vipindi tofauti vya utunzi wake. Aidha, misimamo yake katika maswala anayojadili si moja na tengemano, ni kama anakumbwa na mitafaruku ya ndani kwa ndani na hivyo kutia nguvu kauli yetu kuwa msimamo wa mtunzi huwa si mmoja na tengemano kama ilivyofikiriwa hapo awali na wahakiki wengi wa kazi ya fasihi. Kwa sababu itikadi ndio huelekeza misimamo hii basi ni dhana badilifu na telezi kufungamana na kauli ya nadharia ya udenguzi kuwa maana ni telezi na haishikiki.

6.4.0 ITIKADI KATIKA MHANGA NAFSI YANGU

Katika sehemu iliyotangulia, tulijadili itikadi ambazo zinajitokeza katika riwaya ya *Dunia Yao* na kuona kuwa itikadi tawala inayojitokeza ni ya kitandawazi ambapo vigeu vyake vikuu ni uchumi na biashara, teknolojia, utamaduni, dini, asasi za utawala na elimu. Nayo itikadi ya mtunzi ni ya mabadiliko ambapo tuliona kuwa anaamini kuwa utandawazi ingawa una manufaa yake unapaswa kurekebisha kwani ulivyo sasa unanufaisha tu mataifa tajiri ya Ulaya. Mataifa machanga hasa ya Kiafrika yanazidi kutumbukia katika lindi la umaskini kwa uigaji wa mitindo ya kitawala, kiuchumi na

kitamaduni ya kigeni. Katika sehemu hii, mtafiti anazingatia itikadi zinazojitokeza katika riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu* kwa mujibu wa maudhui na wahusika. Aidha, mtafiti ataonyesha mabadiliko yoyote yanayojitokeza kwa upande wa itikadi na msimamo wa mtunzi na kujadili ni kwa nini mabadiliko haya yanajitokeza.

6.5 MUHTASARI WA RIWAYA YA MHANGA NAFSI YANGU

Riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu* inatusimulia maisha ya mhusika mkuu Afida ambaye ana tamaa ya maisha ya ng'ambo au "Peponi". Tangu jadi yeye husawiri maisha ya Peponi kama yaliyojaa furaha, utajiri, shibe na afya kinyume na maisha ya "motoni" alikoishi yeye ambako kulijaa dhiki, njaa, umaskini na magonjwa. Hivyo basi anapopata mwaliko toka kwa shangaziye Bi. Marneti kwenda kuishi naye ng'ambo "Peponi", Afida anakusanya na kufunga virago vyake kwa haraka tayari kuondoka bila kuchelewa.

Anapofika kule "Peponi" mambo yanamwendea kinyume na alivyotarajia kwani anakumbwa na masaibu mengi. Mateso, chuki, ukatili na ubaguzi wa rangi yanamwandama, shangaziye akiwa katika mstari wa mbele kumkandamiza na kumchukia kwa sababu aliona mumewe Bw. Bawa anavutiwa na Afida aliyekuwa wa umri mdogo. Shangaziye anamshauri aolewe na "jibaba lizee" Bwana Neshboch ndiposa apate uraia kamili wa Peponi. Afida anatekeleza haya akidhani huu ndio ufunguo wa maisha yake kunyooka lakini wapi, inakuwa hasa ndipo ametia kidonda chake kwenye kaa la moto kwani Neshboch alimtungua mimba hivyo kufanya akatize masomo yake na kumuoa. Ndoa yao ilijaa vituko na sarakasi, akamuingiza kwenye ulevi wa pombe mwishowe anaachana naye.

Afida anashindwa kuendesha maisha yake na kuishia kuwa kahaba, mlevi sugu asiye na mbele wala nyuma. Anatungwa mimba nyingine na Sapataro ambaye hataki kukiona kitoto hicho hivyo basi kuishia Afida kukilea peke yake akitegemea msaada alopewa na serikali na vibarua alivyokuwa akifanya vya kuongeza pato. Lakini anaishia kukumbwa na ugonjwa wa saratani. Hata baada ya kufanyiwa oparesheni Afida anahisi kuwa maisha yamemlema na hivyo basi kuishia kujitoa nafsi yeye mwenyewe.

Mohamed alitaka kuangazia masaibu ambayo Waafrika wanakumbana nayo wanapoenda nchi za uzunguni/ng'ambo au "Peponi" kwa shughuli mbalimbali ikiwemo kutafuta riziki kuonyesha kuwa matatizo yanayokabili bara la Afrika yako kote ulimwengunilinaloashiria mtazamo wake wa mambo kuwa ni wa kimataifa. Katika *Mhanga Nafsi yangu*, Mohamed ameonyesha kuwa dunia nzima inakumbwa na matatizo tofauti, na pia kuna maendeleo kwa upande wa teknolojia. Mawazo na mitazamo yake inaonekana kulenga ulimwengu mzima kupitia maswala anayojadili, namna alivyosawiri wahusika wake na mtindo wa kazi yake kwa ujumla anaonekana kuaridhia itikadi ya utandawazi.

6.6 ITIKADI KATIKA RIWAYA YA MHANGA NAFSI YANGU

6.6.1 ITIKADI YA UTANDAWAZI

Utandawazi ni mtazamo ambao huangalia dunia kama moja na tengemano. Mtunzi anayeamini katika utandawazi huzungumzia mambo yanayoathiri dunia nzima. Huchora

wahusika wanaoweza kukubalika na dunia nzima au ulimwengu na mandhari ya kazi yake hujumuisha dunia yote. Mtindo wa kazi yake huonekana kukubalika kimataifa. Mohamed amejadili maswala mbalimbali ambayo ameyaonyesha kiulimwengu. Maswala hayo ni kama vile ndoa, mapenzi, magonjwa, elimu, uchumi, sheria, siasa, uongozi, dini na mengine yanayoonyesha kuwa ana mtazamo wa kitandawazi. Aidha, amewasawiri wahusika na kuwapa sifa za kimataifa na mawazo yaliyopevuka. Amesawiri mandhari ya dunia nzima kwa majina ya Peponi na motoni. Mtindo aliotumia wa kinjozi umemwezesha kusafirisha wahusika wake dunia yote kadri apendavyo. Haya yote yanadhihirisha kuwa mwandishi anaongozwa na itikadi ya urari mataifa ya kutazama mambo kiulimwengu mzima.

Kwa mujibu wa Friedman (2005), utandawazi au urari mataifa kwa Kiingereza ni neno lililoanza kutumika miaka ya 1990, likimaanisha kukifanya kitu kuwa katika kiwango cha kimataifa na kukihamisha nje ya mipaka, kukifanya kuwa cha wazi na kikafanywa na watu wa aina yote duniani. Utandawazi huhusishwa na vipengele kama mfumo wa kiuchumi na biashara, teknolojia, elimu, siasa, dini, ndoa, asasi za utawala na mifumo ya kidemokrasia, na utamaduni vilevile.

6.6.2 MFUMO WA KIUCHUMI

Uchumi ni mfumo wa mapato na matumizi ya watu katika nchi. Katika riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu*, watu wengi wanajihusisha na mambo kadha ili kujikimu kimaisha. Mfumo wa kibepari unajitokeza katika riwaya hii. Mfumo huu unadhihirisha kuwa watu wachache wanajilimbikizia mali yote na kuwaacha maelfu na mamia ya watu wakiwa

hawana chochote. Mfumo wa kibepari ni mfumo wenye matabaka mawili, tabaka la chini la watu wanaoishi kwa kufanya kazi, na tabaka la juu la watu wanaoishi kwa kufanyiwa kazi. Wanaoishi kwa kufanya kazi ndio wavujajasho na kwa maana hii, msingi mkuu wa mfumo wa kibepari ni unyonyaji wa tabaka. Unyonyaji hautokani na nia mbaya ya mtu binafsi bali ni msingi wa mfumo wenyewe bila kujali nia au dhamira za watu waliomo katika mfumo huo. Mfumo huu wa kibepari pia huwa na sifa ya ulimbikizaji na uwekezaji wa mtaji ambao hutokana na ziada ili kuendeleza uzazi wa mfumo wenyewe.

Ni bayana kuwa Neshboch na Bw. Bawa wanaendeleza mfumo huu wa kipebari pale tunapoona kuwa wao wamejilimbikizia mali nyingi pasipo kuwajali wengine.

Neshboch aliniomba tukale chakula nje peke yetu, nami nikakubali. Kwanza alianza kunitembeza kwenye utajiri wake uliokuwa utajiri wa majumba makubwa. Alinizungusha kwa gari lake la mercedes benz na kunionyesha yote aliyotaka kunionyesha usiku huo. Alinikaguza majumba yaliyokuwa kumi na tatu...(uk. 140)

Hii inaonyesha kuwa mfumo uliozingatiwa huko Peponi ni mfumo wa kibepari yaani kujilimbikizia mali kadri unavyoweza. Aidha, mali ilithaminiwa sana katika mfumo huu kiasi cha kuwa mali ndio huamua tabaka lako na maisha utakayoishi. Neshboch anaionea mali yake fahari kuu na ndio anumia kumshawishi Afida akubali mapenzi yake. Naye Afida kwa sababu ni zao la mfumo huu, basi anaamini kuwa akiolewa na tajiri ile mali pia ni yake na hivyo tabaka lake litabadilika vilevile. Hili linadhihirisha namna mfumo wa ubepari huathiri watu kiasi cha kuuasi utu wao na kukubali kufanya lolote mradi wapate mali. Afida anaasi dini yake ya Kiislamu, anasahau watu wao kule motoni, anamtupa mpenzi wake Shaaban na mwishowe hata masomo anaacha anapopachikwa

mimba na Neshboch kwa sababu ya mali. Aidha, Afida anasema kuwa kwa shangaziye Bi Marneti kumejaa vitu vya thamani na vya kisasa (uk. 26). Hili linadhihirisha kuwa mali ilichukuliwa kwa fahari kubwa kiasi cha kutaja vitu vyote vya nyumba vya shangazi yake jambo lilaloonyesha kuwa alitamani sana hata yeye kumiliki mali kama hii au hata zaidi. Hii ni kwa mujibu wa mfumo wa ubepari kwamba kadri unapopata mali ndivyo mabepari hutaka kuhodhi mali zaidi kwa njia halali au isiyo halali. Dhana hii inampelekea mhusika Afida kufanya lolote hata kufanya mapenzi nje ya ndoa na kuolewa na Neshboch mradi apate mali na uraia wa Peponi.

Mohamed anaonyesha kuwa mfumo huu wa ubepari umesambaa kote ulimwenguni na kusababisha umasikini mkubwa kwani kadri matajiri wanavyoendelea kuhodhi mali ndivyo masikini wanavyoongezeka. Umaskini ni hali ya kukosa mali au mambo muhimu kama chakula, nguo na pahali pa kulalia na hivyo ni hali ya ufukara. Hali hii kama mtunzi anavyoonyesha husababishwa na mifumo ya kiuchumi ya kilimwengu hasa umwinyi na ubepari ambapo wale matajiri humiliki nyenzo za uzalishaji mali na masikini hubakia hohehahe. Hali hizi huendelea kudumishwa kwa matumizi ya itikadi potovu ambazo huendelezwa na dini, utamaduni, asasi za serikali kama sheria, polisi, mahakama au ukubalifu na ukawaida tu.

Mtunzi anadhihirisha kuwa hali hizi zinakuwa katika mataifa yote na hili linafanya mtafiti kudhihirisha kuwa itikadi inayojitokeza ni ya utandawazi kutokana na vile

anavyowasilisha mfumo wa kiuchumi katika *Mhanga Nafsi Yangu* kwani mataifa yote yanaonekana kukumbwa na watu wachache matajiri na wengi masikini. Anasema hivi:

Maskini wa chini sana motoni, husimamisha vimeza na vigari
vyao vibovu kandokando mwa barabara kuuza mananasi,
machungwa na matunda mengine huku wakikusanya faida
chache ya kulisha koo zao kubwa....”(uk. 66).

Mtunzi anaonyesha namna pesa zinachukuliwa kuwa ndizo kila kitu huko Peponi, kuonyesha namna mfumo wa kiuchumi umeathiri mataifa yote ulimwenguni. Anasema haya kuhusiana na pesa kuwa kila kitu ni pesa na maisha yao yote hutegemea pesa jambo ambalo ni kweli kimataifa. Hivyo ni kuonyesha kuwa mfumo wa kiuchumi uliopo ni wa kibepari unaopendelea mataifa ya Ulaya huku mataifa machanga ya kiafrika yakizidi kuwa masikini. Nao Waafrika wanaokimbia makwao kama Afida wakidhania maisha yatakuwa bora wanazidi kuumia kwani mifumo ya kiuchumi, kiutawala, kibiashara na asasi zote zinazounga mkono itikadi ya utandawazi huzingatia maslahi ya waliozianzisha nao ni watu wa mataifa ya Kimagharibi.

6.6.3 ELIMU

Elimu ni mfumo wa mafunzo yanayopatikana shuleni, vyuoni na maishani. Kuna elimu ya aina tatu; ya dunia, ya kiakademia na ya kidini. Elimu ya dunia ni elimu ambayo mtu huipata kupitia maisha ya kila siku na huwa haihitajiki kwenda shuleni kuipokea. Kadri mtu anavyoishi ndivyo anavyojionea mengi na kutambua mambo mengi na hivyo basi kuongeza maarifa yake. Katika riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu*, Bw. Darwesh anaendeleza swala hili kwani tunafahamishwa kuwa ijapokuwa hakuenda shuleni kusoma

aliyafahamu mambo mengi ya dunia na kudhihirisha imani ya mtunzi kuwa licha kuwa na elimu ya kiakademia elimu kuhusu dunia ni muhimu zaidi.

Alikuwa akiniambia mara nyingi kwamba elimu haimo katika vitabu tu wala haimo katika vitabu vya kizungu tu bali ndani ya dunia hai tunamoishi na kupambana na matokeo yake...
(uk. 101)

Elimu ya kikademia ni ile aina ya elimu ambapo mkufunzi huenda shule ili kupata mafunzo kutoka kwa mwalimu au mhadhiri aliyehitimu. Elimu hii ya kiakademia huweza kupimwa kwa shahada au stashahada ambazo utaibuka nazo pindi kipindi chako cha masomo kitakapokamilika. Pindi unapopata elimu ya kiakademia jamii nzima hukutazamia upate ajira ili uyaboreshe maisha yako. Afida aliweza kupata elimu ya kiakademia toka akiwa kwao “Motoni” hadi “Peponi”. Haya yanadhihirisha umuhimu wa elimu ya akademika katika ulimwengu wa sasa. Elimu hii ni muhimu kwani hupanua ubongo wa anayeipokea na kumfanya awe na akili iliyojevuka. Mwalimu wa kina Afida alikuwa amejevuka kiakili na ndio sababu aliwaonya dhidi ya utashi wa vitu.

Mtunzi anaendeleza dhana hii ya elimu ya akademika kwa kuonyesha umuhimu wa fasihi kwani Afida anakumbuka mwalimu wao wa fasihi kule Motoni kuonyesha mafunzo ya mwalimu wake yaliyomwathiri sana hata akiwa Motoni. Afida anasoma Peponi na kuweza kuhitimu na kutuzwa zawadi kwa kuwa mwanafunzi wa kwanza wa Motoni kufaulu vizuri na kupewa fursa ya kutoa hotuba ya shukrani. Hili linaonyesha kuwa licha ya kuwa Mwafrika anafaulu sana masomoni na kuwapiku walio na asili ya Ulaya. Hali hii inaonyesha kuwa S.A. Mohamed anaamini katika fikra za utandawazi kuwa rangi ya

mtu haijalishi bali uwezo wake wa kiakili ndio humwezesha kufasiri dhana za kiakademia (uk. 96).

Aidha, Profesa Marjan alikuwa amesoma hadi akafuzu kuwa profesa na kupata kazi ya kusomesha Chuo Kikuu cha Peponi:

Profesa Marjan ni profesa wa mwanzo kutoka Motoni kuja kusomesha katika chuo kikuu cha Peponi. Somo lake kubwa ni falsafa kwa jumla na falsafa ya Motoni kwa undani zaidi...” (uk. 157).

Mohamed pia anazungumzia dhana ya ugonjwa hasa unaoathiri dunia nzima. Ugonjwa ni hali ya mtu kutojihisi vyema. Kuna ugonjwa ambao hupona na mwingine usipone. Sada dadake Afida twaarifiwa kuwa aliaga kutokana na ugonjwa usiopona wa ukimwi hivyo basi kukiacha nyuma kitoto kichanga (Kisura) ambacho Afida aliamua kukichukua na kukitunza kama chake. Mwandishi anasema “baada ya mamake mzazi kufa kwa janga la ugonjwa huu wa siku hizi usiopona, Afida amekitunza na kukidumisha kwa mambo yote.....” (uk. 11). Afida aliwahi kuugua homa ya malaria kama anavyoeleza mwandishi, “aliwahi kushikwa na homa ya malaria iliyomwingia kichwani nusura imtie wazimu au bora tuseme nusra impotezee maisha kabisa ...” (uk. 17). Afida alipofika Peponi hangeweza kustahimili baridi ya huko hivyo basi aliishia kuwa mgonjwa. “Asubuhi aliamka na kitetemeshi cha mwili na mafua makali ilibidi kupelekwa hospitalini. Shangazi yake Bi Marneti ndiye alimchukua kwa gari...” (uk. 31).

Shabani mchumba wake Afida pia aliweza kuugua ugonjwa wa moyo na mwishowe kuaga dunia: “Shabani mbona hivyo? Nilianza kuhaha, nime...lazwa... hospi... tali tokea juzi...nimepata maradhi ya moyo...” (uk. 86).

Bi Sinangoa alikuwa na ugonjwa wa kuvimba tumbo na madaktari walikuwa wameshindwa na kumtibu hivyo basi kuishia kwenda kwa waganga ambao pia hao walishindwa kumtibu: “limewesha waganga tumbo hili. Limebwia gunia zima la miti shamba...na madaktari wake wazitowazito....” (uk. 9). Shuhuda rafikiye Afida alishikwa na ugonjwa usiokuwa na tiba na hatimaye anaaga dunia: “unajua kwamba Shuhuda kalazwa hospitalini?...ninavyosikia kakumbwa na huu ugonjwa wa kisasa usiopona....” (uk. 161).

Mtunzi S. A. Mohamed kwa kuzungumzia ugonjwa wa ukimwi ambao unaathiri dunia nzima anaonyesha kuwa itikadi inayomwongoza katika utunzi wa riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu* ni ya utandawazi. Anaonyesha namna ugonjwa huu umesambaa kote duniani Afrika na Ulaya. Anaonyesha namna watu wanaoishi maisha ovyo kama kina Shuhuda hasa ya ukahaba wako katika hatari ya kuangamia kutokana na ukimwi. Katika hali hiyo anazungumzia aina za ugonjwa kama vile saratani na ugonjwa wa moyo ambayo yameenea sana kote ulimwenguni kwa sasa. Kwa kuzungumzia magonjwa haya mtunzi anajitokeza kuwa itikadi inayomwongoza ni ya utandawazi ndio sababu anazungumzia magonjwa yanayoathiri watu wote ulimwenguni kwa sasa.

6.6.4 UTAMADUNI

Utamaduni ni mtindo wa maisha unaotambulisha kundi fulani la watu kwa lugha yao, tabia zao, mila zao na mfumo mzima wa maisha ya jamii hiyo. Utamaduni unahusisha tabia, lugha ya mwili, mahusiano na salamu. Ni namna watu wanavyokula, wanavyovaa, wanavyoongea na hata wanavyofanya biashara. Katika riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu*, S. A. Mohamed anaonyesha namna utamaduni wa jamii ya Motoni na Peponi ulivyokuwa. Kule Motoni, Shabani haruhusiwi kumkumbatia Afida mbele ya wazee au jamaa zake licha ya kuwa mpenzi wa pekee wa Afida anayejulikana na jamaa yake Afida: “Shabani alimsogelea Afida, alitamani kumvamia na kumkumbatia lakini madhehebu ya utamaduni hayakumruhusu....” (uk. 14). Jamii ya kina Afida na jumuiya yao iliruhusu wasichana kuvaa buibui ambao halionyeshi mkatiko wa mwili na kuwahimiza kufunga kanga tokea kichwani hadi miguuni na kujifunika mtandio:

Kila mara baba alinionya kujifunika mtandio au kufunga kanga kila wakati na kuvaa buibui isionyesha mkatiko wa mwili...baada ya kubaleghe niligundua kwamba kila msichana kama mimi alivaa kama walivyovaa wenzake. Wote kusema kweli, walitakiwa kuvaa hivyo na jamii yao.....(uk. 74).

Afida mwanzoni aliathiriwa na utamaduni na hili linamsaidia sana kutofanya mambo kinyume na anavyohitajika na jamii yake Motoni hata alipoenda Peponi. Utamaduni unamsaidia sana kutoingia katika mtego wa Yakrobich ambaye alitaka kufanya mapenzi na yeye bila kujali wala kubali (uk. 123).

Licha ya hayo, mtunzi anaonyesha kuwa misingi ya kitamaduni imesambaratika. Afida baada ya kukaa Peponi kwa muda alisahau ahadi zake kwa jamaa zake, akasahau

uchumba wake kwa Shabani, akaanza kunywa vileo, akaolewa na Nesboch, akapata mtoto nje ya ndoa, anaolewa na baadaye anatalikiwa, anapata mtoto mwingine na hata mahari hayalipwi na arusi inahudhuriwa na watu wachache tu wa kifamilia. Mambo haya yanadhihirisha kwamba aliasi utamaduni wa Kiafrika (Motoni) na kufurahia maisha ya Ulaya. Mtunzi anaonyesha kuwa utamaduni hauna mashiko tena, watu hutenda vile wanavyotaka mradi malengo yao ya kibinafsi yanatimizwa ambayo ni mawazo ya kiulimwengu wakati huu. Utamaduni hauzingatiwi, haujalishi bali kufanikiwa katika kile unachofanya ili kutimiza malengo unayoaridhia kutimiza.

6.6.5 ASASI YA NDOA

Ndoa ni makubaliano baina ya mwanamke na mwanamme kufunga pingu za maisha. Kwanza, muungano huo lazima uwe wa hiari; wahusika hao wawe wa jinsia mbili tofauti yaani mwanamume na mwanamke. Biblia Takatifu inasema kuwa ndoa ni muungano usiovunjika mpaka kufa kati ya mwanamume mmoja na mwanamke mmoja waliobatizwa. Muungano huo unafanyika kwa makubaliano yao ya hiari ambayo yanathibitishwa na Mungu anayewapa neema zinazohitajika waweze kuyatimiza malengo ya ndoa. Mtazamo wa dini ya Kiislamu ni kuwa ndoa ni muungano wa mwanamume na mwanamke lakini mwanamume anaruhusiwa kuwaoa wanawake hadi wanne ikiwa ana uwezo wa kuwatunza na lazima awpende kwa usawa.

Ndoa ni taasisi muhimu sana katika jamii. Sheria, imani za kidini na hata mila na desturi nyingi duniani huthamini sana taasisi hii na kuilinda kwa gharama yoyote. Hata hivyo

polepole tunashuhudia taasisi hii kama zilivyo taasisi zingine, ikikumbwa na misukosuko ya kila aina. Maendeleo na uhuru vinapoongezeka, ndivyo taasisi hii inavyozidi kutishiwa kuendelea kuwepo. Jamii zote zinakabiliwa na kuongezeka kwa talaka baina ya wanandoa. Katika utamaduni wa Kiswahili, mara nyingi ndoa na talaka zilishikamana na imani ya dini na kwa wale wenye kuishika dini ya Kiislam, talaka ni kitu kinachoruhusiwa. Wanawake wengi walisubiri kupewa talaka na kuendelea na maisha yao ambapo kuolewa tena ilikuwa ni uwezekano. Wenye kufuata imani ya kikristo ile inayosema ndoa ni pingu za maisha, basi ilikuwa vigumu sana kutaka ama kupewa talaka. Pia mwanamke aliyeachwa huweza kujikuta haolewi tena kwa vile kikanisa ndoa ya mwanzo bado inatambuliwa na inamzuia mtu kufunga ndoa nyingine.

Said A. Mohamed anaongozwa na itikadi ya utandawazi kusawiri dhana ya ndoa. Anatuonyesha kuwa ndoa yaweza kuwa baina ya wazungu na waafrika pia. Anaongozwa na itikadi ya utandawazi kutuelezea dhana hii kwani anatuonyesha kuwa Mwafrika yoyote anaweza kuolewa na mzungu kwani siku hizi dunia imekuwa kama kijiji ambapo watu wanaweza kukutana kwa urahisi kwa sababu ya teknolojia, ndege zipo za kusafirisha watu, simu na kompyuta. Bi Marneti ambaye ni mwafrika ameolewa na Bw. Bawa ambaye ni Mwingereza. Afida ambaye ni mwafrika ameolewa na Neshboch ambaye ni Mjerumani. Si lazima mwafrika amuo mwafrika ndio maana Said A. Mohamed alituangazia kuhusu Shaban mwenye asili ya kiafrika akikataliwa na Afida (mwafrika mwenzake) na badala yake anaolewa na mzungu Neshboch.

Said A. Mohamed vilevile kwa kuzingatia dhana ya utandawazi alituangazia jinsi ndoa zote zinafanana iwe ndoa katika nchi za Afrika au ya nchi za ng'ambo. Misukosuko ya ndoa iko sawia haijalishi mahala mulipo. Ndoa za kiafrika hukumbwa na matata kama vita, ugomvi, fitina na talaka. Vilevile, ndoa za nchi za ng'ambo hukumbwa na yayo hayo ndiposa Said Mohamed alitumia wahusika katika ndoa kuangazia haya. Mfano, ndoa ya Afida na Neshboch inaishia katika talaka. Ndoa hii pia inakumbwa na fitina kutoka kwa Bi. Marneti na Bi. She-iza. Vita vimo hapa pia Neshboch anapompiga Afida nusura kumtoa uhai. Ni kitoto chao Dinda kilichomuokoa Afida.

Said A. Mohamed kwa upande mwingine alitaka kutuonyesha jinsi kizazi kipya cha siku hizi kisivyo thamini kanuni za ndoa kwani ndoa yapaswa kulindwa kwavyovyote vile na bibi anapaswa kupata mtoto ndani ya ndoa si nje ya ndoa kama alivyofanya Afida na Neshboch.

Mtunzi S. A. Mohamed ameonyesha ndoa mbalimbali katika riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu*. Kwanza, kuna ndoa baina ya Bi Mwamuda na Bw. Darwesh. Ndoa hii ilikuwa ya utulivu hawakuwa na msukosuko wowote ijapokuwa walikuwa maskini lakini waliweza kubarikiwa na watoto katika ndoa yao akiwemo Afida. Walitenganishwa na kifo wakati Bw. Darwesh alipoaga dunia na kumwacha bi Mwamuda. Pili, kuna ndoa baina ya Bi Marneti na Bw. Bawa. Bi Marneti baada ya kuolewa na mzungu alijulikana kwa jina la 'Bi. Bawa'.

Bi. Marneti naye siku hizi, kama Bi. Mwamuda alivvoelezwa na Afida bintiye kwamba baada ya kuolewa na mzungu, kabadilisha jina anajiita Bi. Bawa..... (uk. 13).

Hili linaashiria kuwa, kulingana na sheria za ndoa, unapoolewa mke anapaswa kulichukuwa jina la mume wake kuonyesha ndoa na familia ulimwenguni kote ni asasi ya kiitikadi ya kumnyamazisha mwanamke na kumfanya mnyenyekevu kuambatana na itikadi tawala kama Althusser (1981) alivyosema.

Uaminifu katika ndoa ni jambo moja la muhimu sana kwani huwa kama nguzo ya ndoa kokote kule ulimwenguni. Bila uaminifu katika ndoa basi huenda ndoa hiyo isiweze kukaa au kustahimili misukosuko ya kila siku na hii huweza hata kuishia kwa kuachana, au kupewa talaka. Ndoa hii yao pia ilikuwa haiishi ugomvi. Chanzo cha ugomvi waliokuwa nao mara kwa mara ilikuwa Afida. Tangu tu alipowasili Afida Peponi, kuishi na Shangaziye basi ndivyo ugomvi ulivyozuka kila siku baina ya Bi. Marneti na Bw. Bawa mumewe Marneti. Hili linaonyesha vile ambavyo ndoa inaweza kutatizwa na watu wengine wa familia wanapokuja kuishi nao.

Mtunzi anaonyesha kuwa ndoa ya Bi. Marnet na Bw. Bawa ilikumbwa na matatizo pindi Afida alipofika pale. Ni kweli kusema kuwa ndoa nyingi ulimwenguni huingiliwa na watu wa familia na kusambaratika au kukosa raha. Wakati mwingine hawa wageni wa kifamilia huwa hawana kosa lolote bali mvurugano huzuka kati ya wanandoa wenyewe kutokana na kutoaminiana au kuwa na matatizo ya ndani kwa ndani ambayo huchipuka kama mvutano kumhusu mgeni.

Inavyodhihirika ni kuwa, mtunzi S. A. Mohamed anaamini katika mawazo ya kiulimwengu kuhusu ndoa kuwa ni baina ya watu wawili na yule wa tatu anapojitokeza basi matatizo mengi huzuka. Ikichukuliwa kuwa katika ndoa nyingi kwenye nchi za ulaya, watu hukaa wawili bila maingilio ya kifamilia na huku Afrika mara nyingi watu wa familia hukaa pamoja. Mtunzi anaonekana kuamini katika ndoa ambayo watu hawakai pamoja na jamaa zao katika ndoa na kama ni msaada wanaweza kupewa wakiwa mahali walipo. Haya ni mawazo ya kiutandawazi au kiulimwengu ambapo watu wengi duniani wanaamini kuwa ili ndoa idumu kabisa, wawili walioana wapaswa kuishi hivyo yaani familia ya baba, mama na watoto kama wapo.

Mtunzi pia anaonyesha ndoa kati ya Afida na Nesboch. Afida alishawishiwa kukubali kuolewa na mzee Neshboch licha ya kumzidi zaidi kiumri. Alikuwa kama rika ya babake mzazi Afida, miaka sitini na miwili (uk. 138). Afida alikuwa na mpenzi mwingine Yakrobich ambaye walikuwa wa rika moja lakini kutokana na ushawishi wa Bi Marnet anakubali kuolewa na Nesboch. Ndoa hii kwa Afida ilikuwa iwe kama kivukio cha kupata uraia wa kuishi Peponi kuonyesha kuwa ndoa ni kigezo kikuu cha kiitikadi cha kuuendeleza mfumo unaotawala.

Hii inaonyesha namna ambavyo mali na utajiri huweza kumwathiri mtu yeyote katika maamuzi yake. Kwa sababu ya tamaa ya mali na uraia, msimamo wa Afida unayumbayumba kwa vile anaamua mambo kwa mujibu wa mali na utajiri. Hali hii

inawakilisha imani ya mtunzi kuwa, wasichana wengi wa kilimwengu siku hizi wana tamaa ya mali na utajiri na kwa hivyo ndoa zenye msingi imara wa mapenzi na ukweli ni muhali kupatikana hasa barani Afrika ambapo wasichana wengi wanapapia ndoa baina yao na wazungu ili kujinusu na matatizo ya kiuchumi. Hili linadhihirishwa kwa hakika na S. A. Mohamed anayeamini katika maswala yanayoathiri dunia nzima kama anavyojadili kuhusu ndoa na mapenzi.

Hapo ghafla, mwanga uliingia na kumeta kichwani mwangu. Polepole giza likaanza kupotea, kweli hatimaye ningehitaji mtu kama Neshboch kunidhamini nikianza kuomba uraia wa Peponi. Ndoa ingekuwa chelelezo muhimu cha kunipeleka kwenye uraia wa Peponi..... (uk. 144). Maadamu nimeolewa na Neshboch uraia wa Peponi sasa ulikuwa mikononi mwangu... (uk. 146).

Maelezo haya yanadhihirisha kuwa nia ya Afida kuolewa na Bw.Nesboch haikuwa kwa sababu ya mapenzi bali ilikuwa kujinufaisha yeye mwenyewe kwa kupata kibali cha kuwa raia wa Peponi. Ndoa ya Afida na Neshboch mwanzoni ilikuwa imejaa furaha na mapenzi tele. Anasema, “Kwa muda mrefu kiasi maisha ya ndoa ya mimi na Neshboch yalikuwa murwa kabisa.....” (uk. 162). Katika ndoa hii, walibarikiwa kupata kitoto kimoja kwa jina Dinda ijapokuwa kilizaliwa nje ya ndoa,“matokeo ni kwamba tulipata mtoto wetu nje ya ndoa...” (uk. 146). Ni bayana kuwa Afida alipata mimba/ujauzito ili autumie kama mtego wa kumnasa Neshboch akubali kumuuoia yeye Afida maadamu alikuwa na mimba yake. Hivyo basi, Neshboch alipochelea kumuoa licha ya yeye kupata ujauzito Afida alianza kuwa na shaka kuwa huenda mambo yasiende kama jinsi alivyokuwa anataka. Haya ni mawazo ya kiulimwengu kwani ni kweli kuwa wasichana wengi hutaka kupata mimba na matajiri halafu waweze kuwashawishi kuwa waoane.

Aidha, mtoto anayezaliwa anakubalika na jamii kwani hatuoni mahali popote akiitwa mwanaharamu wala Nesboch na Afida wakishutumiwa kuwa wametenda kitendo haramu ilhali uzinzi umefanyika. Hili linadhihirisha imani ya mtunzi ya mawazo ya kilimwengu kuwa mtoto akishazaliwa swali si alizaliwa katika ndoa au la, swala ni uwajibikaji wa wazazi wote wawili kumlea mtoto huyo. Tatizo ni kwamba, mara nyingi mtoto anapozaliwa ile azma kuu ya kufunga ndoa hupunguka hasa kwa jinsia ya kiume na huhitaji mwanamke mwerevu kuwa mvumilivu kama Afida alivyofanya na mwishowe kufanyiwa arusi na Nesboch.

Hata hivyo, suala la kufunga ndoa alilipiga chenga, nilipopita huku, yeye alipita kule, matokeo yakawa hapana lililofanyika. Neshboch hakatai wala hakukubali kunioa. Mno ni kutoa ahadi tu, leo kesho na kesho huku manyenje yanakuwa. Ingawa nililingiwa na wasiwasi na kero, nilivumilia kamwe sikukata tamaa (uk147).

Ndoa hii ya Afida na Neshboch pia ilikuwa na changamoto nyingi kwa kuwa msingi wake haukuwa mapenzi ya dhati bali maslahi ya kibinafsi na tamaa. Bi Marneti, Bw. Bawa na She-shaiza walipanga njama ya kumfitini Afida kwa mumewe madhumuni yao yakiwa kuivunja ndoa hiyo yao. Jambo hili linaonyesha namna ambavyo washiriki wa familia wanavyokuwa na nguvu ya kutatiza ndoa na kuivunja kwa maslahi ya kibinafsi.

Madhumuni yalikuwa kuivunja ndoa yangu na Neshboch na hatimaye ipatikane nafasi ya kuibiwa mtoto wangu kwa ukavu kabisa..... (uk. 157).

Aidha, ndoa ya Afida na Neshboch iligeukia kuwa ya karaha kwani alimfanya Afida kama ngoma ya kuchapwa. Alimchapa nusura kumuua siku moja:

Alikusudia kuniua kama Dinda asingeliingilia na kuninusurisha na pigo la babake aliyekuwa akiniekea guu juu ya koo la shingo yangu.... (uk. 167)

Madharau pia yalikuwapo katika ndoa hii. Madharau ni ile hali ya kutomheshimu ama mke wako au mume wako katika ndoa na kumuona kiumbe duni kisicho kuwa na maana tena. Hili linadhihirishwa na Neshboch ambapo tunaona baada ya kuwa katika ndoa na Afida kwa miaka kadha anaanza kumuona kiumbe duni kisichofaa machoni mwake tena.

Lolote ambalo Afida anafanya Neshboch mumewe analiona baya:

Chakula ki tayari mezani, Afida alimwendea Neshboch aliyekuwa kaketi sofani ameghadhabika, “nani anayetaka kula chakula kichafu na kisicho thamani?.....”(uk. 168).

Maneno ya Neshboch kwa mkewe Afida yanaonyesha madharau makubwa kwani kwa miaka kadhaa alikuwa anampikia huku akichangamkia chakula chake. Aidha, kama chakula kina matatizo angemueleza Afida kwa upole na upendo naye Afida arekebishe.

Ukatili pia unajitokeza katika ndoa. Ukatili ni mwendelezo wa vitendo vinavyovuka mpaka wa udhalilishaji na kusababisha madhara ya kimwili na kihisia. Neshboch anaendeleza jambo hili katika ndoa yake na Afida pale tunaona kuwa baada ya kumchapa Afida kichapo cha mbwa nusura kumuua anamfukuza nje pasipo kujali kuwa ilikuwa usiku wa manane. Hakujali atakokwenda Afida ilhali alifahamu bayana kuwa Afida hakuwa na jamaa wengi huko Peponi. Ilimbidi Afida kutafuta msaada toka kwa rafiki wenye asili ya kiafrika kama yeye Profesa Marjan na mkewe Maryan:

Amekufukuza? Alitamka kwa mshangao na hasira Profesa Marjan huku kaketi kitandani, amenifukuza eeee!, amekufukuza usiku huu?.....(uk. 168).

Kuhusu talaka ambayo ni dhana ya kuachana kati ya mume na mke baada ya kutofautiana katika ndoa na kukosa kupata suluhu, ndoa ya Afida na Neshboch inaishia katika talaka baada ya kukosa kuelewana. Wanapelekana hadi kortini na tunaona Neshboch akishinda kesi ya kuwachwa na kitoto chao Dinda baada ya kumhonga hakimu:

Baada ya miaka mitatu kuachana na mumewe Neshboch, Afida alikwisha kupoteza kila kitu..... (uk. 171). Kabla ya hapo, pale alipopewa talaka tu na kufukuzwa na Neshboch, mahakama ilimpa haki ya kukitunza hicho kitoto chake..... (uk. 172).

Ukweli ni kuwa talaka ina gharama yake kwa mfano tunamuona Neshboch anapompa talaka Afida anaamriwa kuwa ampe kiwango fulani cha pesa Afida kila mwezi cha kujimudu yeye na kitoto chao Dinda na vile vile anapewa baadhi ya mali yake:

Mahakama iliamuru Neshboch amtafutie Afida pahali pa kuishi pia alitakiwa ampe Afida pesa za mahitaji ya kitoto,vilevile kuwapa mojawapo ya flats zake (uk. 172).

Ndoa hii yao haikudumu kwani iliishia kwa talaka. Afida na Neshboch walienda kinyume na amri ya Mwenyezi Mungu kwa mujibu wa dini ya Kikristo, ambaye aliamuru kuwa ndoa inapaswa kudumu maisha hadi kifo kiwatenganishe wawili hao. Mtunzi anaamini kuwa ndoa ambayo ina ukavu wa mapenzi ina matatizo chungu nzima. Haina haja kuivumilia kwani ni vyema kutengana na kudumisha uhai wako. Hizi ni fikra za kiulimwengu mzima kwamba kama ndoa imekumbwa na matatizo makubwa watu wapeane talaka. Hili linadhihirisha kuwa, mtazamo wa mtunzi kuhusu ndoa ni kwamba si mpaka kifo kiwatenganishe bali ni mpaka pale mnaacha kushirikiana na kupendana.

Afida akiwa kwao “Motoni” alikuwa na mchumba wake Shabani ambaye walikuwa wameahidiana kufunga pingu za maisha baadaye siku za usoni:

Usilie Afida, Mungu akipenda tutakutana tena kutekeleza ahadi yetu ya ndoa, Shabani hakuweza pia kujizuia kupukutikwa na machozi..... (uk 15).

Mwanzo wa ndoa huwa kwanza kuchumbiana kisha baada ya kuchumbiana huweza kuoana baadaye. Wachumba hawa hawakuweza kuoana kutokana na usaliti wa Afida. Alipofika Peponi huko Ulaya, alianza kuwapenda watu wengine mwishowe akamsahau Shabani naye Shabani aliugua ugonjwa wa moyo na kuiaga dunia. Said A. Mohamed anatuonyesha kuwa ndoa yaweza kuwa baina ya watu wenye asili tofauti ambayo ni mawazo ya kitandawazi.

Itikadi hii inaonekana kutawala fikra zake kuhusu ndoa, anatuonyesha kuwa Mwafrika yoyote anaweza kuolewa katika nchi za Ulaya kwani siku hizi dunia imekuwa kama kijiji watu wanaweza kukutana kwa urahisi kwa sababu ya teknolojia, ndege zipo za kusafirisha watu, simu na kompyuta. Bi Marneti ambaye ni Mwafrika ameolewa na Bw. Bawa ambaye ni Mzungu naye Afida ambaye ni Mwafrika ameolewa na Neshboch mzungu mwenye asili ya Kijerumani. Si lazima Mwafrika amuuoe Mwafrika ndio maana Said A. Mohamed alituangazia kuhusu Shabani mwenye asili ya Kiafrika akikataliwa na Afida na badala yake anaolewa na Mzungu Neshboch.

Aidha, katika swala zima la ndoa mtunzi hajaonyesha kuhusu malipo ya mahari ama kuhusishwa kwa wazazi kabla ya ndoa kufungwa. Haya yote yanadhihirisha kuwa msimamo wa S. A. Mohamed kuhusu ndoa umeongozwa na itikadi yake ya utandawazi kwamba watu wanaingiliana na kuwa na uhusiano wa kimapenzi na kuoana kutoka mataifa tofauti na asili tofauti, wanakumbwa na changamoto zinazowiana na tamaduni na mila kama vile nafasi ya wazazi katika ndoa na mahari yanatupiliwa mbali. Aidha, wanapoachana wanaenda kortini na kupata uamuzi huko badala ya kupata ushauri wa wazazi na kwa ujumla mapenzi ya kweli ni muhali kupatikana bali kigeu cha kiuchumi na tamaa kinazingatiwa zaidi katika swala la ndoa. Haya yote yanaonyesha kuwa S. A. Mohamed anaongozwa na itikadi ya urari mataifa.

6.6.7 DINI

Dini inamaanisha jumla ya imani ya binadamu pamoja na mafundisho wanayotoa kuhusu yale ambayo wanazingatia ama kuyasadiki. Huhusiana na mambo ya roho kama vile kuhusiana na Mungu, maisha na uumbaji. Ibada ni nguzo mojawapo iliyo dhahiri miongoni mwa dini kadha katika kuunganisha dhamira za mwenye kushika dini na mhimili wa imani. Lakini dini inahusu pia mafundisho kuhusu maadili mema na mabaya, imani na jinsi ya kushiriki katika jumuiya za waumini.

Dini huwa na taratibu za sheria za kufanya na za kutofanya, ambazo mtu lazima azitunze ili ahesabiwe kuwa muumini mwaminifu wa dini, na papo hapo hana ubaya na Mungu wa hiyo dini. Hili huendeleza dhana ya utiifu na unyenyekevu na kwa hivyo hutumiwa kuendeleza itikadi tawala kwa kuwafanya watu wawe watiifu wakiadini kuwa hali zao ni

majaliwa na hivyo kuwa na ung'amuzi potoshi kama Marx alivyosema akielezea dhana ya itikadi. Mifano miwili ya dini mbili ambazo ni za sheria ni za Kiislamu na Kiyahudi. Dini ya Kiislamu ina nguzo zake tano ambazo ni lazima zitunzwe. Dini ya Kiyahudi iko na mamia ya amri na tamaduni ambazo zinatunzwa. Dini hizi zote, kwa kiwango fulani zasema kuwa kwa kuzitii sheria za dini mtu atachukuliwa kuwa wa Mungu. Dini zingine zaangazia sana katika kuzitimiza kanuni kwa kutoa kafara hizi, kutenda jukumu hili, kushiriki katika ibada, kula chakula hiki na mengine ili amakaribie Mungu.

Afida na familia yake walikuwa waumini wa dini ya Kiislamu na alilazimika kuvaa buibui. Babake alikuwa mcha Mungu na hakuchelea kumhimiza Afida kumshukuru Mungu na kupenda dini yake, na kila mara katika mazungumzo yake na Afida hakisita kumhimiza jinsi Mungu alivyotenda mema: “Mungu katuonyesha vitendo vingi vya utakatifu na upotofu, si maneno tu.....” (uk. 118). Hadithi alizosumuliwa na babake pia hazikuchelea kujaza dhana ya Mungu hili linadhirika kama ifuatavyo:

Hadithi alizonihadithia baba, aliweza kunidokezea *Sufism* bila ya kujua, *Sufism* ni njia ya ndani yenye utata mwingi wa jinsi ya kumwambudu Mungu, njia ya kutafuta uelewa na mapenzi ndani ya uelewa wa mungu.....(uk 126).

Vilevile mhusika Darwesh (babake Afida) anaendeleza vyema jambo hili la dini kwani tunafahamishwa kuwa alikuwa kiongozi wa harakati zote za kidini: Afida anasema, “Babangu alikuwa kiongozi wa harakati zote za kidini pamoja na kaida za *Sufism*.....” (uk. 127). Mashehe wa siku hizi wamekuwa waongo na hawasemi ya kweli. Haya yanadhihirika “Motoni”. Hili linadhihirisha kuwa S. A. Mohamed anaamini kwamba hapo mbeleni dhana za kidini na viongozi wa kidini walikuwa na mashiko kamili lakini

sasa dini pamoja na viongozi wengi wa kidini hawana mashiko kamili na hivyo hawaaminiki kamwe. Hii ni kutokana na imani katika utandawazi ambapo katika ulimwengu mzima sasa maswala ya dini na viongozi wa kidini hayachukuliwi kuwa ndio ukweli kwani misimamo ya kidini yaonekana kusambaratika na hivyo kuafiki mkabala wa Louis Althusser kuwa dini ni chombo cha kiitikadi kinachotumiwa kuiendeleza itikadi tawala.

Mohamed pia anatuonyesha kuwa dini haiwezi ikamkomboa mtu toka kwa ulimwengu wa kisasa bali mtu binafsi ndiye anayepaswa kujikomboa na nafsi yake mwenyewe. Hii ina maana kuwa mtu binafsi ndiye huweza kuamua afanye lipi aache lipi wala si misingi ya kidini ambayo haina mashiko katika ulimwengu wa kisasa. Hali hii inamfanya Afida kufanya uamuzi wa kupata mtoto nje ya ndoa, kuolewa na Nesboch ambaye ni mkristo, kunywa vileo na kufanya mambo bila kuzingatia misingi yoyote ya kidini. Haya pia yanadhihirisha kuwa mtunzi anaaridhia itikadi ya utandawazi ambapo mtu binafsi hufanya maamuzi kwa kuzingatia ubinafsi tu na uhuru wa fikra zake.

6.6.8 MAADILI

Dhana hii inaendelezwa na wahusika kadha katika riwaya hii. Bi.Marnet; ijapokuwa yeye ni shangaziye Afida hajali wala haoni soni kusema uongo kwa daktari anayemkagua Afida wakati alipompeleka Afida hospitalini baada ya Afida kuugua homa kali ya mapafu kwa sababu alikuwa analala katika chumba ambacho hakina umeme wa kutosha na

kilikuwa baridi mno: “Aaa chumba anacholala kina vuguvugu la kutosha. Kina “heater” zima na ni jipya.....” (uk. 37).

Neshboch wakiwa pamoja na wakili wake wanatoa ushahidi wa uongo mahakamani ndiposa waweze kupewa jukumu la kubaki na kitoto chao Dinda:

Na kama hilo halikutosha basi alipigwa pigo kubwa zaidi la kutoruhusiwa kukilea kitoto chake Dinda. Mambo hayo yalifanyika kwa kisingizio kwamba yeye Afida ni mama mlevi asiyestahiki kupewa dhamana ya kulea kitoto kile alichodhani kilikuwa chake....(uk. 172).

Kwa kusawiri wahusika hawa wakisema uongo ikiwemo Waafrika na Wazungu, mtunzi anaonyesha namna anavyoamini kuwa uongo ni jambo ambalo limekithiri ulimwengu mzima na kwa hivyo, unadhihirisha fikra zake za kiulimwengu.

Katika riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu*, wahusika wanaendeleza dhana ya wivu jambo linalowafanya wawatendee wengine mabaya. Mohamed anadhihirisha fikra za kimataifa kuwa wivu ukitawala basi maovu mengi hushuhudiwa hata baina ya jamaa wa karibu. Bi Marneti shangaziye Afida alikuwa na wivu wa hali ya juu kwa Afida na hakutaka kumwona karibu na mumewe Bw. Bawa. Wivu huu wake twaweza kudhihirisha kuwa ulitokana na tatizo lake la kutoweza kuzaa, alikuwa tasa, hivyo basi kumdhania kuwa Afida angempokonya mumewe. Wivu huu wake ulimpelekea kumpa Afida chumba cha kulala ambacho huwa na uvuguvugu mwingi na baridi sana kwa kuhofia kumpa kilicho karibu na wao kilicho na umeme wa kutosha. Wivu huu wake unamfanya kuwa na ugomvi usioisha na mumewe.

6.6.9 ASASI ZA UTAWALA

Sheria za Peponi zinakubali serikali kumpa pesa mwanamke ambaye amelemewa kumlea mtoto wake ili aweze kujikimu kimaisha yeye na mwanawe. Hili linadhihirika pale tunapoona serikali ya Peponi ikimfadhili Afida na pesa za kukitunza kitoto Mkombozi kwa kuwa hakuwa na kazi rasmi ya kufanya ili kupata pato na zaidi ya hayo alikuwa hana mume kwani Bw. Neshboch alikuwa ashampa talaka: “gharama za kumchukua mtoto kwa hali na mali angezibeba yeye mwenyewe Afida. Ndio alipewa pesa na serikali kumhudumia mtoto ijapokuwa hazikutosha”(uk85)

Sheria ya Peponi kama Afida alivyotambua baadaye, ilikuwa na mapendeleo. Hili alitambua baada ya kupeleka kesi yake mahakamani hukumu ilitolewa na hakim ambayo ilimpendelea Neshboch kwani alikuwa m-Peponi hivyo basi Afida alinyanga'ywa kitoto chake Dinda. Hili linaonyesha kuwa katika mataifa yote asasi za utawala kama vile sheria na mahakama hutumiwa na wenye uwezo kuendeleza na kulinda maslahi yao. Nesboch kwa sababu ya pesa na uraia wake anapewa haki za kukaa na mtoto wake ilhali Afida ndiye mamake. Nesboch aliweza kusema uongo kortini na kuthibitisha kuwa Afida alikuwa mlevi kupindukia na kwa hivyo hawajibiki ndio Neshboch alipewa haki ya kukaa na mtoto wao. Afida hakupata haki katika mahakama. Sheria inatumiwa kumdhulumu kwani hata Neshboch hakishtakiwa wala kuhukumiwa kwa kumpiga na kumuumiza Afida nusura afe, kuonyesha kuwa sheria na mahakama

kama Louis Althusser alivyodai ni vyombo tu vya kuendeleza itikadi tawala kwa kuwanyamazisha wanaodai haki zao.

6.6.10 MFUMO WA KUUMENI

Mwanamke amechorwa kwa vigezo viwili vikuu: uzuri na ubaya. Tukiegemea katika kitengo cha wanawake kuwa wazuri, hili linadhihirishwa na shangaziye Afida Bi Sinangoa ambaye hakuchelea kumsaidia Afida alipokuwa anasoma ambapo wazaziwe Afida mara nyingi hawakuwa na hela za kutosha za kuikimu familia. Bi Sinangoa alikuwa akiingilia na kumsaidia Afida: Tunaambiwa “Siku zile alipokwenda shule bila ya kupata kisabeha kwa sababu wazazi wake hawakuwa na senti nyekundu, alikuwa akimpitia shangazi yake nyumbani kwake. Afida siku zote hakuambulia patupu....” (uk. 8). Mke wa profesa Marjan (Maryam) alikuwa kama mamake wa kupanga na Afida alipomwendea kumwambia kuwa alikuwa na uja uzito na ingebidi aache masomo ya Chuo Kikuu kwanza ndiposa amlee mtoto wake, Maryam alikuwa tayari kumlelea mtoto ndiposa aendelea na masomo yake: “Usijali mimi nitakulelea mwanao mpaka atapokuwa mkubwa....” (uk. 158). Aidha, Afida alikuwa na msimamo thabiti na hakuiingia katika mtego wa Sapataro, Bw. Bawa au wa Yakrobich ambao walijaribu kwa lolote lile kumnasa katika mtego wao wa mapenzi ya uongo.

Alitaka niwe rafiki wa kucheza naye mchezo wa kurithisha na kufurahisha miili. Kila aliponibembeleza nikubali mchezo huu, nilikataa katakata nikamwambia bora urafiki wetu umalizike...(uk. 123).

Huyo ni Yakrobich akijaribu kumshawishi Afida aingie katika mtego wake. Hili linadhihirisha mawazo ya mtunzi kuwa kuna tofauti kubwa baina ya mapenzi na urafiki. Maneno haya ya Afida yanaonyesha msimamo wake kuwa urafiki haumaanishi kushiriki ngono na mtu mawazo ambayo yanaafikiana na mtazamo wa kiutandawazi ambapo watu wana uhusiano wa kirafiki na jinsia tofauti bila kushiriki ngono. Vilevile tunaona kwamba, Afida alikuwa na msimamo thabiti alipokataa kunywa pombe licha ya Yakrobich kumshawishi anywe (uk. 135). Aidha, mtunzi anadhihirisha Afida na mamaye Bi. Mwamuda ni wenye bidii katika kazi zao. Licha ya mumewe kuaga dunia na kumwacha na watoto pekee yake wakiwa wangali wachanga, alijitosa katika uwanja wa biashara ndiposa kuikimu familia yake:

Bi Mwamuda ni mtu mwenye utashi mkubwa wa biashara, ingawa hajawahi kuwa mfanyi biashara wa maana. Kupika nyungu za uji wa mtama, mikate ya gole na supu ya makongoro kuwauzia asubuhi wafanyakazi wa sulubu walioenda kazini... (uk. 12).

Afida anatia bidii katika masomo yake akiwa Peponi na kuishia kutuzwa tuzo kwa kuwa mwanafunzi bora wa asili ya kiafrika (Motoni) kuweza kufuzu Peponi:

Leo sherehe ya kuhitimu masomo ya miezi tisa ya lugha ya Peponi imewadia. Hivi sasa napokea zawadi ya kuwa mwanafunzi wa kwanza wa Motoni kufaulu vizuri kiPeponi tokea miaka kumi na tano iliyopita ... (uk. 96)

Mwanamke amesawiriwa kama adui wa mwanamke mwenzake. Hili linadhihirishwa na Bi. Marneti shangaziye Afida anapomfitini Afida katika ndoa yake kwa lengo la kuwatenganisha ndiposa aweze kupata fursa ya kuchukua kitoto chake kwa urahisi: “kwa sababu yeye alikuwa tasa, alimshawishi Neshboch akubali tumpe mtoto wetu amlee....” (uk. 156). She-shaiza (dadake Neshboch) alishinda kila mara akimchochea Afida kwa

Neshboch kwa kusudi waachane kwa sababu alimchukia Afida kutokana na rangi yake na hakumuona akiwa binadamu kamili.

Mtunzi pia amezungumzia kudunishwa kwa mwanamke katika riwaya hii. Katika nchi ya “Peponi” wanawake wa asili ya Kiafrika wanadunishwa sana ambapo wengi wanachorwa kama vyombo vya kumaliza ashiki ya wanaume. Wanawake wenyewe wanashikilia hili jambo na kulitenda bila kujali. Mfano ni Shuhuda rafikiye Afida anayeamini haya:

Baada ya kimya cha kitambo, Shuhuda aligeuza shingo yake ndefu kuniambia,...hapa upo Peponi bibi, kila mtu ana uhuru wa kufanya apendavyo hapa..usisahau kwamba wewe ni mwanamke na mwanamke lazima aonyeshe mwili wake kama anataka kufanikiwa... (uk. 73).

Saparata alikuwa na matamano ya kimwili na Afida ndiposa alishinda akimfuatafuata:

Ukiwa huna kitu utamfaa nani? Na wewe utafaliwa na nani? Huku kunyweshwa na kulishwa nako kwa mtindo wa Saparata kunahitaji kulipwa, si kwa pesa bali kwa mambo mengine salaale!... (uk. 85).

Hili linaashiria kuwa wanawake ni chombo cha kumaliza ashiki za wanaume na mtazamo huo unaathiri namna wanavyoiona jinsia ya kike, yaani kama kitu cha “kuliwa” tu na kuachwa wala si binadamu kamili. Hali hii inasababishwa na mfumo wa kuumeni ambapo wanaume huonyesha kuwa, hao ndio viumbe bora zaidi duniani ilhali jinsia ya kike haina thamani yoyote. Dhana hii inajitokeza wazi kwa kupitia wahusika kadha katika riwaya hii wanaoendeleza hali hii. Bw.Neshboch akiwa mmoja wao anamfunza mwanawe wa kiume Dinda kuwa wanawake hawana thamani yoyote na kuwa wao (wanaumme) ndio walio na mamlaka na maana zaidi duniani (uk. 163).

Maelezo kuhusu wanawake yanadhihirisha jinsi wanawake wanavyoonewa na kunyanyaswa na wanaume wa Peponi. Kwa ujumla mtunzi anaonyesha kuwa mfumo wa kuumeni huwepo kote ulimwenguni. Mfumo huu humfanya mwanamke kuonewa na kuteswa na kutumiwa vibaya. Mtunzi anaonyesha kuwa pindi mfumo huu upo basi mwanamke hana haki kwani muundo mzima wa jamii hata sheria na mahakama zinampendelea mwanamume. Hili linadhihirisha kuwa mfumo wa kuumeni ni mojawapo ya vipengele vya utawala vya kuendeleza itikadi tawala ya kuhimiza utiifu kwa sehemu ya jamii yaani wanawake ili itikadi ya kitawala iendeleo kudumu. Haya maelezo yote yanatilia mkazo dhana na imani kwamba, S. A. Mohamed anaongozwa na itikadi ya utandawazi ndio sababu anawasilisha mambo yanayoathiri ulimwengu mzima na hapa anaonyesha mfumo huu wa kuumeni upo duniani kote na ndio msingi wa maonevu ambayo mwanamke anapitia.

Wanawake pia wamesawiriwa kama makahaba. Jambo hili linaendelezwa na Afida ambapo baada ya mambo kumwendea mrama aliingia katika ukahaba. Alifanya haya pindi tu anapokunywa pombe.

Aliingia katika mtego wa kukaribishwa ulevi na wanaume kwa mtindo wa nipe nikupe. Afida akawa hatoki tena kwenye baa kuwafuata wafadhili wake ambao nao walitaka kufadhiliwa... (uk. 177).

Ni bayana pia kuwa rafikiye Afida, Shuhuda alikuwa anafanya ukahaba kutokana na mavazi yake aliyokuwa anayavaa ili kuwavutia wanaume ni kupitia njia hii ambapo aliweza kupata ugonjwa wa ukimwi (uk. 72). Hili linadhihirisha kuwa Mohamed anawasilisha dhana zinazoathiri dunia nzima kama ukimwi ambao anaona kuwa

utandawazi umechangia sana katika maenezi yake. Kwa ujumla Mohamed anaonyesha kuwa mfumo wa kuumeni ni kipengele mojawapo cha vipengele vya kuendeleza itikadi tawala kwa kuhimiza utiifu kwa jinsia ya kike ili kurahisisha utawala dhalimu na kuhlalisha matendo yasiyofaa ya watawala.

6.6.10 UBAGUZI WA RANGI

Ubaguzi wa rangi ni kitendo cha kuthamini au kutenga binadamu kwa misingi ya rangi za ngozi. Hii ni dhana ya kumbagua mtu kwa kulingana na rangi ya ngozi yake. Ina maana katika maisha ya kila siku, kulingana na tofauti za makundi ya kikabila kutengwa ili jamii hiyo kukosa uwezo wa kutumia nafasi ya umma au huduma. Binadamu huwa na rangi ya ngozi ya aina mbili ama uwe mweusi au mweupe. Waafrika huwa weusi ilhali wazungu huwa weupe. Ubaguzi wa rangi ulikuwa maarufu sana katika nchi kama Afrika Kusini na Marekani ambapo Waafrika walikandamizwa kutokana na rangi yao katika kupata huduma mbalimbali za kijamii na kimaendeleo. Wakati wa ukoloni, rangi ilitumika kama msingi wa utoaji huduma muhimu na haki nyingine za kibinadamu. Rangi nyeusi ilipewa hadhi ya chini zaidi. Aidha, visiwani Zanzibar rangi ilitumiwa kumuweka mtu katika tabaka fulani na hata kukataliwa na familia yake kama Rehema katika *Nyota ya Rehema*. Siku hizi katika karibu nchi zote sheria zimewekwa za kupinga ubaguzi wa rangi lakini katika nchi nyingi bado kuna wabaguzi wachache ambao wanavunja sheria kwa kuendelea kubagua. Kwa mfano, kuna wabaguzi wanaobagua watu weusi nchini Marekani na katika nchi za Ulaya.

Said A. Mohamed anawasilisha dhana ya utandawazi kwa kutuonyesha jinsi dhana ya ubaguzi wa rangi ni jambo linalotendeka ulimwengu mzima na si kwa baadhi ya nchi pekee. Anatumia wahusika Afida na mtoto wake Dinda kuonyesha haya. Ubaguzi wa rangi unajitokeza katika afisi za serikali kama vile kortini/mahakamani ambapo kesi huamuliwa kulingana na rangi ya mwili wako. Iwapo wewe ni mweupe basi hukumu inayotolewa huwa inatolewa kwa kipendeleo. Afida alibaguliwa na waPeponi kwa sababu ya rangi yake. Alikuwa mweusi ilhali wao waPeponi ni waeupe. Afida alibaguliwa kila mahala si shuleni bali pia katika basini na hata katika ndoa yake:

Nilianza kumzoea mwalimu wangu na mwalimu wangu
akaanza kunizoea mimi. Labda wanafunzi wenzangu ndio
waliokuwa hawajanizoea. Walinitenga, wengine wakanibagua
na kudhani kama mimi si mtu bali ni dude tu, au labda mtu
aliyetoka mwezeni... (uk. 90).

Dinda ambaye alikuwa mchangayniko wa asili ya kiafrika na kizungu pia hakusazwa bali alibaguliwa sawia na Waafrika wenzake:

Suala la sheria ambalo daima Afida alidhani lingekuwa la
uadilifu, sasa anajua kwamba sheria ya Peponi inaweza kuwa
na upendeleo wa kijinga kwa kutegemea nani kamshtaki nani,
nani ana jinsia na rangi gani.... (uk. 171).

Ni bayana kuwa kesi baina ya Afida na Neshboch kuhusu atakayepewa fursa ya kukilewa kitoto chao Dinda iliamuliwa kulingana na rangi ya ngozi, ambapo hakim alitoa uamuzi kwa kumpendelea Neshboch kwa kuwa alikuwa wa asili ya kizungu.

Basini mlikuwa na watu watatu, mimi nilikuwa wa nne, bibi
mmoja, niliyezoea kupanda naye basi hilihili kila siku
aligeuka kama anavyogeuka kila siku kunitazama kwa
mshangao usiokwisha... (uk. 63).

Ni wazi kuwa bibi huyu hakutaka kukaa naye kiti kimoja kwa kuwa alikuwa mweusi ilhali yeye alikuwa mweupe. Sapataro vilevile anafahamu kuwa wazazi wake hawangekubali mtoto wake na Afida kwa jina Mkombozi kwa kuwa hakufanana na wao wa Peponi. Hivyo basi hakuwa anatamani hata ya kumpeleka Afida na Mkombozi kuwaona wazazi wake:

Wazazi wangu wasingemkubali mtoto huyu kwa sababu hakufana na mimi na kwa hivyo hakufanana na mtu yeyote anayeishi Peponi (uk. 184-185).

Kasumba ni matokeo ya mabadiliko ya fikra za mtu yanayosababishwa na elimu au utamaduni wa kikoloni ambayo yanamfanya mtu afuate mwenendo fulani wa kikoloni. Wazungu huwa na fikra ya kuwa hakuna chema ambacho chaweza toka katika nchi za watu weusi (waafrika). Nao Wafrika huamini kuwa uzunguni ndiko mambo yote mazuri huwa ikiwemo elimu, kazi na hata maisha mema kwa ujumla. Katika riwaya hii, kasumba inajitokeza kwa uwazi sana kupitia wa-Peponi na wa-Motoni akiwemo Afida.

Mwanzoni mwalimu wangu wa darasa hakuamini kabisa kama ningeweza kuwa na akili ya kufahamu kiPeponi, hasa aliponilinganisha na wanafunzi waliotoka mashariki ya Peponi...(uk. 91).

Yakrobich vile vile alikuwa na kasumba ya kuwa hakuna m-motoni ambaye angeweza kujiunga na vyuo vya Peponi kwani aliwadhania wanafunzi wa Motoni kuwa wa kiwango cha chini katika masomo yao, na hivyo basi alishangaa sana Afida alipomwambia kuwa yeye ni m-motoni. Jambo hili ni dhihirisho kuwa ubaguzi wa rangi ni kigeu tu cha kuiendeleza itikadi tawala kwa kuhimiza utiifu na unyenyekevu kwa watu walio na rangi tofauti na pia kuhimiza ukawaida na ukubalifu kama Antonio Gramsci alivyosema hivi

kwamba kwa mfano mtu mweusi kama Afida anapodhulumiwa watu wengine wanaona ni hali ya kawaida tu kwa mtu mweusi kukumbwa na masaibu na kuteswa.

6.6.11 HITIMISHO

Katika sura hii mtafiti alidhamiria kuonyesha itikadi zinazojitokeza katika riwaya ya *Dunia Yao* na *Mhanga Nafsi Yangu* ili kudhihirisha kuwa itikadi zinabadilika kila baada ya kipindi maalum cha utunzi. Imedhihirika kuwa itikadi ya watawala katika riwaya hii ni ya kitandawazi na inajitokeza kupitia vigeu kama vile mfumo wa kiuchumi na biashara, teknolojia, matabaka, elimu, utamaduni, dini, ndoa na asasi za utawala.

Kuhusu mfumo wa kiuchumi Mohamed anaonyesha kuwa itikadi ya utandawazi inajitokeza kwa kuuendeleza mfumo wa kibepari ulimwengu mzima. Hii inatokana na dhana kuwa mataifa ya Ulaya yaliyoendelea kiuchumi katika juhudi za kutaka kuhifadhi na kuendelea nyadhifa zao huendeleza itikadi ya utandawazi na kupendekeza mifumo ya kibepari ya uzalishaji mali na ufanyaji wa biashara na uwekezaji. Mohamed ameonyesha kuwa mifumo hii huzua matabaka katika dunia hivi kwamba kuna matabaka baina ya mataifa ulimwenguni. Matabaka ya nchi matajiri za Ulaya ambazo huwa na usemi mkubwa kiuchumi na kiutawala na ambazo hunufaika zaidi na mikataba ya kibiashara na kisiasa inapowekwa na matabaka ya mataifa masikini ambayo huendelea kujidanganya kuwa yanapiga hatua kubwa kiuchumi, kisiasa na na kijamii bila kufahamu kuwa yanakandamizwa kabisa na mataifa yaliyoendelea.

Akizungumzia teknolojia, mtunzi ameonyesha namna ambavyo inatumika kuwadhuru watu wa mataifa yanayoendelea ingawa wengi hawajatambua hayo kwa kuwatenganisha na kueneza maafa mengi mno. Hili linadhihirisha kuwa teknolojia ni kipengele mojawapo cha kuendeleza itikadi tawala ya utandawazi ili mataifa ya Ulaya yaendeleo kuyadhibiti mataifa masikini huku yakifikiria kuwa ni kwa manufaa yao. Kufungamana na mkabala wa Louis Althusser (1981) ni kweli kuwa vyombo vya habari hutumiwa kueneza itikadi tawala na hivyo ni sehemu tu ya kusaidia watawala kuendeleza itikadi za kitawala.

Kuhusu elimu mtunzi anaonyesha namna elimu hutumiwa kama kigeu cha kuendeleza itikadi tawala pale ambapo anaonyesha kuwa katika dunia ya leo elimu haihakikishii mtu nafasi ya juu au upataji wa ajira. Kwa hakika wengi waliopata elimu bado hawana kazi na kwa hivyo anaonyesha elimu kama asasi tu ya kudhibiti watu na kuwafanya wanyenyekevu kwa matabaka tawala yaliyohodhi mali nyingi.

Kuhusu siasa mtunzi anaonyesha kuwa mifumo ya kisiasa inayopendekezwa kama vile mifumo ya kidemokrasia ni vipengele tu vya kuendeleza utawala wa mataifa ya Ulaya. Anaonyesha kuwa mifumo mibaya ya utawala imepelekea maafa na mivutano mingi kwa sababu mifumo hiyo haiyafai mataifa machanga lakini kwa sababu ni kipengele cha udhibiti, kuendeleza itikadi ya utawala inaendelezwa kijuujuu ikionekana kama ni mifumo mizuri sana ya uongozi na si kweli. Mifumo hii hutumiwa kuhalalisha matendo ya kidhalimu ya mataifa haya yalioendelea na hivyo kufungamana na mkabala wa Louis

Althusser kuwa itikadi huendelezwa na vyombo vya kiitikadi visivyotumia nguvu ama matumizi ya nguvu ili kuudhibiti ulimwengu.

Kuhusu utamaduni Mohamed ameonyesha vile utandawazi umeathiri watu hivi kwamba maadili yameporomoka, vijana wanavalia mavazi mabaya, ukahaba umekithiri, misingi ya familia imesambaratika na hayo yote yanatokana na athari ya utandawazi. Vijana wanaiga mitindo ya Ulaya ya maisha, miziki wanayopenda ni ya Ulaya na kwa hivyo mtunzi ameonyesha kuwa kufungamana na mawazo ya Louis Althusser tamaduni za kigeni zinatumiwa kueneza itikadi ya kitandawazi ili mataifa ya Ulaya yaendeleo kudhibiti watu kimawazo na kihisia kwa manufaa yao wenyewe.

Kuhusu dini anaonyesha kuwa dini haizingatiwi tena bali inatumiwa kama kitega uchumi na kuwadanganya watu wa mataifa ya chini kuwa hali zao zitaimarika lakini dini ni kigeu kimojawapo cha kuuendeleza utiifu na unyenyekevu ili kuendeleza itikadi tawala kufungamana na mkabala wa Marx kuhusu itikadi kuwa ni ung'amuzi potoshi.

Mohamed anaamini itikadi ya mapinduzi ya mifumo hii, kwamba mataifa ya Kiafrika yafanye mapinduzi na yaweze kuirekebisha hali hii ili yaweze kujinasua. La sivyo basi mataifa hayo anaona kuwa yatasambaratika kutokana na athari za utandawazi. Hivyo warejeele Uafrika wao kwani utandawazi ni itikadi ya mataifa matajiri inayotumiwa kuendeleza maslahi ya mataifa hayo.

Kwa kusawiri itikadi ya utandawazi katika riwaya ya *Dunia Yao* mtunzi ameonyesha mabadiliko kwa kutoa kazi zake katika mandhari ya Kiafrika ama Zanzibar na kusawiri mandhari ya kilimwengu. Hivyo amepevuka sana katika kusawiri maswala mazito yanayoathiri dunia nzima kama vile mifumo ya kiuchumi na kibiashara, sayansi na teknolojia ya mawasiliano na usafiri, tamaduni za dunia nzima na athari zake dini tofauti za ulimwengu, mifumo ya kilimwengu ya kiutawala kati ya maswala mengineyo yanayoathiri jamii nzima. Kinyume na ilivyo katika *Kiza Katika Nuru* anapoamini katika mapinduzi ya nguvu na makabiliano, katika *Dunia Yao* anaamini katika marekebisho ya asasi zinazoendeleza utandawazi. Anaonyesha kuwa anaamini mabadiliko ya amani licha ya kuonyesha kuwa nguvu zinahitajika kubadilisha hali. Lakini haonyeshi hali za makabiliano ya kivita kama alivyofanya katika *Kiza Katika Nuru*.

Ni kauli ya mtafiti kuwa kwa kuisawiri jamii ya kimataifa na mandhari ya kiulimwengu riwaya hii, Mohamed amebadilisha itikadi anayoiwasilisha katika riwaya zake za awali kama *Asali Chungu* na *Kiza Katika Nuru* na kuwasilisha utandawazi kama itikadi tawala na mapinduzi ya marekebisho kama itikadi yake binafsi. Amefanya hivyo ili kazi yake iwe faafu kwa jamii pana anayoizungumzia ikichukuliwa kuwa riwaya hii aliiandika akiwa anafanya kazi nchini Ujerumani mwaka wa 2006. Hivyo mazingira yake yameathiri itikadi yake ya mwanzoni anayoonekana kuiamini katika *Kiza Katika Nuru* kwani fasihi ni zao la jamii kwa mujibu wa nadharia ya kimaadili. Kwa hivyo mtafiti amedhihirisha kuwa msimamo wa mtunzi si mmoja na tengemano hubadilika katika vipindi tofauti vya utunzi wake na pia dhana ya itikadi ina mikabala mingi ikiwemo ule

wa Marx kuwa itikadi ni ung'amuzi potoshi, ule wa Althusser kuwa itikadi huendelezwa na vyombo vya utawala na vya kiitikadi na ule wa Antonio Gramsci kuwa itikadi hutokana na ukubalifu na ukawaida na hivyo kuthibitisha kuwa itikadi ni dhana telezi na matini huwa na fasili nyingi kwa mujibu wa nadharia ya udenguzi.

Katika sehemu ya pili ya sura hii, mtafiti amejadili itikadi zinazojitokeza katika riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu*. Imedhihirika kuwa itikadi tawala inayojitokeza ni itikadi ya kitandawazi na kudhihirika kuwa mtunzi naye anaaridhia itikadi ya mapinduzi kutokana na imani kuwa utandawazi ni itikadi inayoathiri ulimwengu mzima lakini chanzo chake ni mataifa ya Ulaya kwa lengo la kuudhibiti ulimwengu na kuutawala. Mtunzi anaona kuwa utandawazi hauwezi kuyasaidia mataifa machanga kama ya Kiafrika kwani lengo la mataifa ya Ulaya la kueneza itikadi hii ni mbinu tu ya kuendeleza mifumo ya kibepari na kuhifadhi nyadhifa zao katika dunia kwa maslahi yao wenyewe na nchi zao hasa tabaka tawala.

Kuhusu mfumo wa kiuchumi imedhihirika kuwa mfumo wa kibepari ndio ambao Mohamed anazungumzia na kuonyesha namna mfumo huu umeathiri dunia nzima, jambo ambalo anaamini linaenezwa zaidi na utandawazi kwani mataifa ya Ulaya yangependelea mfumo huu uendeleo ili waendeleo kuyadhibiti mataifa mengine kiuchumi na kimaendeleo. Imedhihirika mfumo huu huzua matabaka mawili katika jamii ambapo kuna wale walionavyo na wale ambao hawana. Mtazamo wa mwandishi umepevuka sana

kiasi cha kuamini kuwa utandawazi unasababisha utabaka huu kuendelea katika viwango vya kimataifa. Kuna mataifa ya Ulaya yanayoaminiwa kuwa ya tabaka la juu na hivyo kufananishwa na Peponi; mahali penye raha zote na mataifa ya tabaka la chini ambayo yanaitwa motoni penye matatizo chungu nzima.

Kuhusu utamaduni imedhihirika mtunzi anaamini kuwa utandawazi ndio umeleta athari hizi na hivyo wapaswa kuondolewa na kuchukuliwa kama mfumo kandamizi wa kuyadhibiti mataifa ulimwenguni. Anaamini kuwa dhana ya utamaduni wa kilimwengu ni kipengele tu cha watawala kueneza dhana ya utandawazi ili waendeleze itikadi ya watawala na mataifa tajiri katika juhudi za kudhibiti mawazo ya ulimwengu mzima na hivyo kuthibitisha mawazo ya Althusser (1981) kuhusu itikadi kuwa utamaduni ni kipengele kimoja cha kuendeleza itikadi tawala.

Mohamed ameonyesha namna utandawazi umeathiri asasi ya ndoa na ameonyesha kuwa ndoa ni kigeu tu cha kueneza itikadi tawala za utandawazi jambo linalofungamana mawazo ya Althusser (1981) kuwa ndoa na familia ni asasi moja itumiwayo kueneza itikadi ya watawala hasa inapofungamanishwa na utamaduni na dini.

Kuhusu dini Mohamed amedhihirisha kuwa dini ni kipengele cha kueneza itikadi tawala kwa kuhimiza utiifu na ukubalifu wa hali ilivyo na hivyo kudhihirisha imani ya mtunzi kuwa ni ni kipengele tu cha kuendeleza itikadi tawala kwani inahimiza utiifu na unyenyekevu na hata kusababisha ung'amuzi potoshi kama Marx (1973) anavyosema.

Mohamed pia amedhihirisha namna utandawazi umesababisha kuporomoka kwa maadili na anaamini kuwa utandawazi huchangia sana kueneza maovu haya yaliyokithiri na kuathiri sana mataifa machanga ambayo hayana mbinu mwafaka za kukabiliana na athari zake kama magonjwa ya ukimwi na saratani.

Asasi za utawala kama vile mahakama na sheria zinatumiwa kueneza itikadi tawala ya utandawazi kwa kulinda maslahi ya walio navyo na wazungu na hivyo hutumiwa kuhalalisha matendo yao maovu jambo linalodhihirisha mkabala wa Louis Althusser (1981) kuhusu itikadi kuwa sheria na mahakama hutumiwa na watawala kuendeleza itikadi tawala.

Kuhusu mfumo wa kuumeni Mohamed amedhihirisha namna unavyotumiwa kuwakandamiza wanawake dunia nzima. Imedhihirika kuwa mfumo huu ni sehemu ya kueneza itikadi tawala ya utandawazi ya utiifu na unyenyekevu na kudhihirisha mtazamo wa Gramsci (1985) kuhusu itikadi kuwa huendelezwa kwa ukubalifu na ukawaida, kwamba ni kawaida tu mwanamke kukumbwa na masaibu kama haya.

Kwa ujumla wake mtafiti ameonyesha kuwa itikadi inayojitokeza katika riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu* ni ya utandawazi kupitia kwa vipengele kama mfumo wa kiuchumi, elimu, ndoa, dini, asasi za utawala, maadili, na mfumo wa kuumeni. Ameonyesha kuwa mtunzi anapendekeza mapinduzi ambapo mataifa machanga kama ya Kiafrika yatafute namna ya kusuluhisha matatizo yao kwani kutorokea mataifa ya Ulaya hakubadilishi hali.

Kwa hakika Mohamed anaupinga utandawazi na kuonyesha kuwa unaathiri mataifa machanga ya Kiafrika vibaya. Kupitia kwa kuzaliwa kwa mtoto Mkombozi mtunzi ameonyesha kuwa matumaini ya ukombozi yapo lakini si kupitia utandawazi bali Waafrika wajinasue kutokana na itikadi hii ya utandawazi na wafanye mambo yao wenyewe kama Afida alivyomzaa mtoto wake mwenyewe na kumuita Mkombozi na hivyo kudhihirisha kuwa itikadi inayotawala ni utandawazi inayojitokeza katika riwaya nzima huku mtunzi akidhihirisha itikadi ya mapinduzi.

SURA YA SABA

7.0 HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

7.1 UTANGULIZI

Katika sura iliyopita, mtafiti amejadili itikadi zinazojitokeza katika riwaya za *Dunia Yao* na *Mhanga Nafsi Yangu*. Imedhihirika kuwa itikadi kuu inayojitokeza katika riwaya hizi ni ya utandawazi ambapo maswala yanayohusu dunia nzima yamejadiliwa kama vile mifumo ya kiuchumi na biashara, teknolojia, utamaduni, na asasi za utawala kati ya mungineo. Mohamed naye amedhihirisha kuwa anaupinga utandawazi kwani anaamini kuwa licha ya faida chache unaoletea mataifa ambayo hayajaendelea kiuchumi itikadi hii inatumiwa na mataifa ya Ulaya kuendeleza malengo yao ya kibinafsi hasa mifumo ya kiuchumi ya kibepari na tamaduni potovu. Katika sura hii mtafiti anajadili muhtasari wa utafiti, matokeo na mchango wa utafiti, changamoto na mapendekezo ya tafiti za baadaye kuhusu itikadi.

7.2 MUHTASARI WA TASNIFU

Katika tasnifu hii, mtafiti amejadili itikadi katika riwaya za S. A. Mohamed. Katika sura ya kwanza, mtafiti amejadili utangulizi wa utafiti na malengo na maswali ya utafiti. Ameonyesha swali ambalo alishughulikia katika utafiti ambapo alichunguza kama itikadi za utunzi katika riwaya za S. A. Mohamed zimekuwa zikibadilika katika miongo mitatu ya utunzi wake na ameweza kubaini kuwa kwa hakika itikadi hizi zimebadilika katika kila kipindi ili kazi zake ziwe faafu kwa jamii aliyoandikia katika kila kipindi. Aidha, mtafiti amejadili upeo na mipaka ya kazi hii ambapo amebaini kuwa riwaya nne teule

zilizandikwa na S. A. Mohamed ndizo zilizotumiwa katika utafiti huu. Malengo ya utafiti pia yameshughulikiwa ambayo ni kuonyesha uhusiano uliopo baina ya itikadi na mtazamo wa mtunzi, kuonyesha itikadi zinazojitokeza katika riwaya zote nne na kudhihirisha mabadiliko ya kiitikadi yanayojitokeza katika vipindi tofauti vya utunzi.

Katika sura ya pili mtafiti amejadili mambo yaliyosemwa na wahakiki wengine kuhusiana na itikadi na riwaya ambapo imebainika kuwa kabla ya utafiti huu hakuna utafiti uliokuwa umefanywa kuhusu itikadi katika riwaya za S. A. Mohamed hasa kuhusu kubadilika kwake na kujadili dhana ya itikadi katika mikabala mbalimbali. Aidha, mtafiti amejadili nadharia za udenguzi na kimaadili zilizotumika katika utafiti huu.

Katika sura ya tatu mtafiti amebainisha mbinu zilizotumiwa katika utafiti ambazo ni maktabani na nyanjani na pia ameonyesha sampuli lengwa kuwa ni riwaya teule zilizandikwa na Mohamed S.A katika vipindi tofauti. Ameonyesha pia njia za usampulishaji kama kimaksudi na utabakisho ili kuwakilisha vipindi maalum. Mtafiti pia ameonyesha njia zilizotumiwa kukusanya data na vifaa vilivyotumika. Aidha, mtafiti amejadili namna data ilivyochanganuliwa na kuwasilishwa kwa njia ya maelezo.

Katika sura ya nne, mtafiti alidhamiria kuonyesha uhusiano uliopo baina ya itikadi na msimamo wa mtunzi kwa kurejerea riwaya za S. A. Mohamed. Mtafiti alianza kwa

kuelezea mikabala mbalimbali ya dhana ya itikadi ambapo alibaini mikabala mitatu muhimu kwa mujibu wa utafiti huu. Mikabala iliyojadiliwa ni ile ya Karl Marx (1973) iliyobaini kuwa itikadi ni ung'amuzi potoshi na kuungwa mkono na wahakiki wengi kama Njogu (1997), Lorrain (1979), Rossiland (1990), Stoika (1972) kati ya wengineo. Mkabala mwingine uliojadiliwa ni ule wa Louis Althusser (1981) aliyesema kuwa itikadi ni dhana inayoweza kutokana na matumizi ya nguvu ya serikali, jeshi, magereza na vile vile vyombo vya kiitikadi kama kanisa, elimu, vyombo vya habari na kadhalika. Mkabala wa tatu uliojadiliwa ni mkabala ulioendelezwa na Antonio Gramsci (1985) anayesema kwamba, itikadi ni dhana ambayo huendelezwa kwa ukubalifu na ukawaida. Kauli iliyojitokeza ni kwamba itikadi ni dhana telezi na changamano kuelezea kama wanaudenguzi wanavyodai kuwa maana ni telezi na haishikiki.

Katika sura ya tano mtafiti alishughulikia itikadi katika riwaya ya *Asali Chungu* na *Kiza Katika Nuru*. Mtafiti ameonyesha kuwa Said Ahmed Mohamed anawasilisha itikadi ya kimwinyi kama itikadi tawala anayojidhihirisha kwa vipengele kama mfumo wa kuumeni, mfumo wa utawala, mfumo wa kiuchumi, utabaka, sheria na haki, mapinduzi, ndoa, mapenzi, dini na maadili. Naye Mohamed kama mtunzi anadhihirisha itikadi ya kimapinduzi na kurekebisha asasi na mifumo ya utawala wa kimwinyi.

Hii inamaanisha kuwa Mohamed anapendekeza marekebisho ya mfumo wa kitawala wa kimwinyi na asasi zote ambazo zinauunga mkono ili kurekebisha hali ilivyo na kujenga jamii mpya yenye usawa. Mtafiti alionyesha itikadi ambazo mtunzi S. A. Mohamed

anaaridhia katika riwaya ya *Kiza Katika Nuru* na kuona ama kuna dalili zozote za mabadiliko. Imedhihirika kuwa, itikadi ambazo zinajitokeza ni itikadi tawala ya kibepari na itikadi ya kimapinduzi ya mwandishi hasa mapinduzi ya matumizi ya nguvu na makabiliano ya moja kwa moja na hivyo anadhirisha mabadiliko ya kiitikadi. Itikadi tawala imejitokeza kwa matumizi ya vipengele kama mfumo wa kuumeni, utabaka, ndoa, familia, dini, mapenzi, mapinduzi, uchumi, siasa na uongozi kwa ujumla wake.

Imedhihirika kuwa S. A. Mohamed amedhihirisha mabadiliko mbalimbali kuhusu itikadi katika utunzi wake. Ukiangalia itikadi zinazojitokeza katika *Asali Chungu* na ulinganishe na itikadi zinazojitokeza katika *Kiza Katika Nuru* anadhihirisha mabadiliko ambayo yanaathiri mielekeo na mitazamo yake. Kwa hivyo, msimamo wake si mmoja na tengemano kwani anajipinga mwenyewe na kwa mujibu wa nadharia ya udenguzi amejidengua mwenyewe kutokana na azma ya kutaka kutimiza mahitaji ya jamii yake kwa kipindi hiki cha ujamaa kuelekea ubepari.

Katika sura ya sita, mtafiti alidhamiria kuonyesha itikadi zinazojitokeza katika riwaya ya *Dunia Yao* na *Mhanga Nafsi Yangu* ili kudhihirisha kuwa itikadi zinabadilika kila baada ya kipindi maalum cha utunzi. Imedhihirika kuwa itikadi tawala katika riwaya hii ni ya kitandawazi na inajitokeza kupitia vipengele kama vile mfumo wa kiuchumi na biashara, teknolojia, matabaka, elimu, utamaduni, dini, ndoa, na asasi za utawala.

Mohamed anaamini itikadi ya mapinduzi ya mifumo hii; mataifa ya Kiafrika yafanye mapinduzi na yaweze kuirekebisha hali hii ili yaweze kujinasua. La sivyo basi mataifa hayo anaona kuwa yatasambaratika kutokana na athari za utandawazi. Hivyo warejeele Uafrika wao kwani utandawazi ni itikadi ya mataifa matajiri inayotumiwa kuendeleza maslahi ya mataifa hayo. Kwa kusawiri itikadi ya utandawazi katika riwaya ya *Dunia Yao* mtunzi ameonyesha mabadiliko kwa kutoa kazi zake katika mandhari ya Kiafrika ama Zanzibar na kusawiri mandhari ya kilimwengu. Hivyo amepevuka sana katika kusawiri maswala mazito yanayoathiri dunia nzima kama vile mifumo ya kiuchumi na kibiashara, sayansi na teknolojia ya mawasiliano na usafiri, tamaduni za dunia nzima na athari zake, dini tofauti za ulimwengu, mifumo ya kilimwengu ya kiutawala kati ya maswala mengine yanayoathiri dunia nzima. Kinyume na ilivyo katika *Kiza Katika Nuru* anapoamini katika mapinduzi ya nguvu na makabiliano katika *Dunia Yao* anaamini katika marekebisho ya asasi zinazoendeleza utandawazi. Anaonyesha kuwa anaamini katika mabadiliko ya amani licha ya kuonyesha kuwa nguvu zinahitajika kubadilisha hali. Lakini haonyeshi hali za makabiliano ya kivita kama alivyofanya katika *Kiza Katika Nuru* na hivyo anadhamiria kuonyesha mabadiliko ya kiitikadi labda katika kuifaa jamii ya kimataifa anayoiandikia inayoamini katika mabadiliko ya amani wala si vita na makabiliano na mapinduzi ya matumizi ya nguvu

Ni kauli ya mtafiti kuwa kwa kuisawiri jamii ya kimataifa na mandhari ya kiulimwengu riwaya hii, Mohamed amebadilisha itikadi anayoiwasilisha katika riwaya zake za awali *Asali Chungu* na *Kiza Katika Nuru* na kuwasilisha utandawazi kama itikadi tawala na

mapinduzi ya marekebisho katika riwaya za hivi karibuni *Dunia Yao* na *Mhanga Nafsi Yangu* kama itikadi yake binafsi. Amefanya hivi ili kazi yake iwe faafu kwa jamii pana anayoizungumzia ikichukuliwa kuwa riwaya hii aliiandika akiwa anafanya kazi nchini Ujerumani. Hivyo mazingira yake yameathiri itikadi inayomwongoza. Hii ni kwa sababu fasihi ni zao la jamii kwa mujibu wa nadharia ya kimaadili. Kwa hivyo msimamo wa mtunzi si mmoja na tengemeni; hubadilika katika vipindi tofauti vya utunzi wake. Aidha, dhana ya itikadi ina mikabala mingi ikiwemo ule wa Karl Marx kuwa itikadi ni ung'amuzi potoshi, ule wa Louis Althusser kuwa itikadi huendelezwa na vyombo vya utawala na vya kiitikadi na ule wa Antonio Gramsci kuwa itikadi hutokana na ukubalifu na ukawaida na hivyo kuthibitisha kuwa itikadi ni dhana telezi na matini huwa na fasili nyingi kwa mujibu wa nadharia ya udenguzi.

Aidha, mtafiti amejadili itikadi zinazojitokeza katika riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu* katika sura hio. Imedhihirika kuwa itikadi tawala inayojitokeza ni itikadi ya kitandawazi na kudhihirika kuwa mtunzi naye anaaridhia itikadi ya mapinduzi kutokana na imani kuwa utandawazi ni itikadi inayoathiri ulimwengu mzima lakini chanzo chake ni mataifa ya Ulaya kwa lengo la kuudhibiti ulimwengu na kuutawala. Mtunzi anaona kuwa utandawazi hauwezi kuyasaidia mataifa machanga kama ya Kiafrika kwani lengo la mataifa ya Ulaya kueneza itikadi hii ni mbinu tu ya kuendeleza mifumo ya kibepari na kuhifadhi nyadhifa zao katika dunia kwa maslahi yao wenyewe na nchi zao hasa tabaka tawala.

Kwa ujumla wake mtafiti ameonyesha kuwa itikadi inayojitokeza katika riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu* ni ya utandawazi kupitia kwa vipengele kama mfumo wa kiuchumi, ubaguzi wa rangi, ndoa, dini, asasi za utawala, maadili, na mfumo wa kuumeni. Ameonyesha kuwa mtunzi anapendekeza mapinduzi ambapo mataifa machanga kama ya Kiafrika yatafute namna ya kusuluhisha matatizo yao kwani kutorokea mataifa ya Ulaya hakubadilishi hali. Kwa hakika Mohamed anaupinga utandawazi na kuonyesha kuwa unaathiri mataifa machanga ya Kiafrika vibaya. Kupitia kwa kuzaliwa kwa mtoto Mkombozi mtunzi ameonyesha kuwa matumaini ya ukombozi yapo lakini si kupitia utandawazi bali Waafrika wajinasue kutokana na itikadi hii ya utandawazi na wafanye mambo yao wenyewe.

7.3 MATOKEO NA MCHANGO WA UTAFITI

Katika utafiti huu, mtafiti alilenga kujibu maswali kwamba kuna uhusiano gani baina ya itikadi na mtazamo wa mwandishi kwa kurejelea riwaya za S. A. Mohamed na ni itikadi ipi inayojitokeza katika riwaya ya *Asali Chungu* na *Kiza Katika Nuru* kutokana na usawiri wa maudhui na wahusika. Aidha, mtafiti alidhamiria kuonyesha itikadi inayojitokeza katika *Dunia Yao* na *Mhanga Nafsi Yangu* kwa mujibu wa maudhui na wahusika ni ipi na ama kuna mabadiliko yoyote. Swala lingine lilikuwa ni kuonyesha ikiwa mabadiliko yanayotokea yanadhihirisha marekebisho na kujisahihisha katika mielekeo na mitazamo ya mtunzi na yanaashiria mabadiliko yepi kuhusu dhana ya itikadi.⁹

Mtafiti ameonyesha uhusiano uliopo baina ya itikadi na msimamo wa mtunzi kwa kurejelea riwaya za S. A. Mohamed kwa kudhihirisha kuwa kadri historia ilivyobadilika katika vipindi tofauti vya utunzi wa S.A Mohamed, ndivyo itikadi zake za utunzi zilivyobadilika. Nao msimamo wa mtunzi ukazidi kubadilika kwani msimamo huelekezwa na itikadi. Kwa hivyo itikadi ina ufungamano mkubwa na msimamo wa mtunzi hivi kwamba ikibadilika nao msimamo wake huathirika na kubadilika. Hii ina maana kuwa kazi yake ya fasihi pia hubadilika kwani ndiye anayeiumba na hivyo msimamo wa mtunzi hauwezi kuwa mmoja na tengemano kila wakati hubadilika kufungamana na mabadiliko ya itikadi.

Katika kushughulikia swala la pili, mtafiti aliangalia itikadi katika riwaya ya *Asali Chungu* na *Kiza Katika Nuru*. Katika *Asali Chungu* ameonyesha kuwa Said Ahmed Mohamed amewasilisha itikadi tawala ya kimwinyi iliyojitambulisha kwa vigeu kama vile mfumo wa kiuchumi, matabaka, elimu, utamaduni, mfumo wa kuumeni, dini, ndoa, asasi za utawala na maadili. Aidha, mtafiti ameonyesha kuwa Mohamed anadhihirisha itikadi ya kimapinduzi ya marekebisho katika riwaya ya *Asali Chungu* kama mwandishi. Anaunga mkono mapinduzi ya marekebisho ya asasi zote zinazoendeleza itikadi tawala ya kimwinyi na kuamini kuwa asasi hizi zikifanyiwa marekebisho basi jamii itabadilika na maisha yatakuwa bora. Katika *Kiza Katika Nuru* mtafiti ameonyesha kuwa itikadi tawala ni ya kibepari kupitia vigeu kama mfumo wa kiuchumi, matabaka, elimu, familia na ndoa, mfumo wa kuumeni, utamaduni na asasi

za utawala. Naye mwandishi itikadi anadhihirisha itikadi ya mapinduzi ya matumizi ya nguvu na hivyo kuonyesha mabadiliko ya kiitikadi.

Mtafiti pia amedhihirisha kuwa itikadi zinazojitokeza katika riwaya ya *Dunia Yao* na *Mhanga Nafsi Yangu* ni itikadi ya watawala utandawazi na inajitokeza kupitia vigeu ma kama vile mfumo wa kiuchumi na biashara, sayansi na teknolojia, matabaka, elimu, utamaduni, dini, ndoa na asasi za utawala. Mtunzi naye amedhihirisha itikadi ya marekebisho. Aidha itikadi zinazojitokeza katika riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu* ni itikadi ya watawala ya utandawazi na kudhihirika kuwa mtunzi naye anaaridhia itikadi ya mapinduzi kutokana na imani kuwa utandawazi ni itikadi inayoathiri ulimwengu mzima lakini chanzo chake ni mataifa ya Ulaya kwa lengo la kuudhibiti ulimwengu na kuutawala. Mtunzi anaona kuwa utandawazi hauwezi kuyasaidia mataifa machanga kama ya Kiafrika kwani lengo la mataifa ya Ulaya la kueneza itikadi hii ni mbinu tu ya kuendeleza mifumo ya kibepari na kuhifadhi nyadhifa zao katika dunia kwa maslahi yao wenyewe na nchi zao hasa tabaka tawala.

Mtafiti amedhihirisha itikadi katika riwaya za S.A Mohamed na kuthibitisha kuwa zimekuwa zikibadilika katika vipindi tofauti vya utunzi wake na kwa sababu itikadi ndio hufumbata mitazamo na mielekeo ya mtunzi basi msimamo wake si mmoja na tengemano. Aidha, mtafiti amedhihirisha kuwa Mohamed alifanya hivyo ili kazi zake ziwe faafu katika jamii aliyoilenga na katika kujisahihisha na kujirekebisha ameipinga mitazamo yake ya awali katika kazi zake. Hili lilidhihirisha kuwa dhana ya itikadi ni

changamano na badilifu kwani ina mikabala tofauti na hivyo ni dhana telezi na maana yake ni changamano zaidi na hivyo kuweza kuzua fasili tofauti katika matini moja. Katika kupata matokeo hayo, mtafiti ameweza kutekeleza malengo ya utafiti huu na kujibu maswali yote manne yaliyoshughulikiwa ipasavyo kwa kuzingatia nadharia ya udenguzi na kimaadili kama alivyolenga kufanya.

Kwa kufanya haya, mtafiti amechangia katika fasihi na usomi wa riwaya kwa kutambua kuwa itikadi ni kiungo muhimu sana katika riwaya na hivyo yapaswa kuzingatiwa kama kipengele kikuu cha uhakiki kinyume na ilivyokuwa kabla ya utafiti huu ambapo itikadi ilishughulikiwa pembezoni tu wala sio kipengele cha kimsingi. Jambo lingine ambalo tumechangia ni kuwa kauli ya kimapokeo kuwa mtunzi huwa na itikadi moja haina mashiko kwani mtafiti amedhihirisha itikadi inaweza kubadilika inapoangaliwa katika kipindi kirefu cha wakati na hivyo hata tatizo likiwa lilelile la kijamii na kiuchumi, mtunzi anayewajibika atajaribu kulisuluhisha kwa njia nyingine. Aidha, mtafiti ameonyesha kuwa mtunzi hubadilika na kujisahihisha katika juhudi za kuifaa jamii anayoiandikia na hivyo itikadi hubadilika kila baada ya kipindi fulani cha kiutunzi.

Kwa ujumla wake mtafiti amedhihirisha itikadi katika riwaya za S.A Mohamed na kuthibitisha kuwa zimekuwa zikibadilika katika vipindi tofauti vya utunzi wake na kwa sababu itikadi ndio hufumbata mitazamo na mielekeo ya mtunzi basi msimamo wake si mmoja na tengemano. Aidha, mtafiti amedhihirisha kuwa Mohamed alifanya hivyo ili kazi zake ziwe faafu katika jamii aliyoilenga na katika kufanya hivyo ameipinga

mitazamo yake ya awali katika kazi zake. Dhana ya itikadi pia imejadiliwa na kudhihirika kuwa ni changamano kwani ina mikabala tofauti na hivyo ni dhana telezi na maana yake ni changamano zaidi na hivyo kuweza kuzua fasili tofauti katika matini moja. Katika kutekeleza haya mtafiti ameweza kutekeleza malengo ya utafiti huu kwa mujibu wa nadharia za utafiti alizopendekeza.

7.4 CHANGAMOTO ZA UTAFITI

Mtafiti alikumbwa na changamoto mbalimbali katika kutekeleza utafiti wake. Changamoto kuu ilikuwa katika kumhoji mwandishi wa kazi zilizochunguzwa, S. A. Mohamed. Changamoto ilizuka kwa sababu ya umbali baina yake na mtafiti. Kadhalika, mwandishi ni mtu mwenye shughuli nyingi. Changamoto hii ilikabiliwa kwa kutumia mtandao ambapo tulimtumia hojaji kwa baruapepe. Aliijaza na kisha kututumia.

Kadhalika, kuwapata wataalam waliohojiwa kulizua changamoto pia. Licha ya kuwa hawakuwa mbali sana kama ilivyokuwa na mtunzi mwenyewe, wao pia huwa na shughuli nyingi. Haikuwa rahisi kupata upenyu wa kuwahoji lakini hatimaye tulifanikiwa kupata maoni yakatupatia data iliyotusaidia kushadidia data kutoka kwa riwaya teule pamoja na data tuliyopewa na mtunzi mwenyewe tulipomhoji.

7.5 MAPENDEKEZO

Katika utafiti huu mtafiti alidhamiria kuonyesha kuwa itikadi katika riwaya za S. A. Mohamed zinabadilika katika kila kipindi cha utunzi wake ili kuthibitisha kuwa itikadi ni

dhana nyumbufu na changamano na hivyo msimamo wa mtunzi si mmoja na tengemano kama wahakiki wengi wanavyochukulia wanapohakiki kazi za fasihi. Mtafiti amefanikiwa kufanya hayo kwa kutumiwa riwaya nne teule kuwakilisha vipindi maalum vya kiutunzi na kutumia nadharia za udenguzi na kimaadili akathibitisha kuwa ni kweli S. A. Mohamed anabadilisha itikadi anazowasilisha katika riwaya zake na itikadi zake kama mwandishi katika vipindi tofauti ili kuafikiana na jamii yake. Imebainika kuwa katika kufanya hivyo, Mohamed ameipinga mitazamo yake ya awali na kuthibitisha kuwa mwandishi huibadilisha mitazamo yake kila mara na hivyo msimamo wa mtunzi si mmoja na imara Hivyo katika tahakiki za baadaye katika fasihi dhana ya msimamo wa mwandishi inapaswa kuchukuliwa kuwa ni changamano zaidi kuliko inavyofikiriwa na wahakiki wengi kuwa msimamo wa mtunzi ni mmoja na tengemano kila wakati bali na changamano zaidi.

Utafiti zaidi unafaa kufanywa kuhusu kazi nyinginezo zilizoandikwa na S. A. Mohamed hasa zile zilizoandikwa katika kipindi kimoja kama tamthilia na mashairi ili kubaini itikadi zinazojitokeza na itikadi ya mtunzi mwenyewe katika vipindi tofauti. Aidha, mikabala mingine kuhusu itikadi inaweza kutafitiwa ili kuona ama inajitokeza katika kazi hizi na nyinginezo. Utafiti pia unapaswa kufanywa kuhusu vipengele vinginevyo kama mtindo na ploti na kuona namna vipengele hivyo vinadhihirisha itikadi ya mtunzi .Pia swala la tikadi katika kazi za watunzi wengine linaweza kuangaziwa.

Kwa ujumla wake dhana ya itikadi ni dhana pana na changamano inayohitaji utafiti zaidi hasa inapoangaliwa katika makabala tofauti na hivyo imani yetu ni kuwa utafiti huu umechangia katika kuonyesha namna inavyobadilika na kujitokeza katika riwaya lakini utafiti zaidi kuhusu dhana ya itikadi, mikabala mbalimbali na kutumia nadharia za kisasa kama udenguzi na ujumi mweusi utafaa kuipanua dhana hii na kuifanya ieleweke zaidi.

MAREJELEO

- Achebe, C. (1975). *Morning Yet on Creation Day: Selected Essays*. London: Heinemann.
- Achebe, C. (1988). *Hopes and Impendments: Selected Essays*. London: Heinemann.
- Althusser, L. (1981). Ideology and Ideological State Apparatuses. Katika *Lenin and Other Essays*. (B. Brewster, Mtaf.). London: New Left Books.
- Aristotle, (1952). *Nichomachian Ethics* (W. D. Ross, Trans.) Chicago: Chicago University press
- Babu, O. (2005). *Kala Tufaha*. Nairobi: Phoenix Publishers.
- Barthes, R. (1977). *The Death of The Author. Image-Music-Text*. (S. Heath, Mtaf.). London: Fontana
- Bennet, A. na Royle, N. (2011). *An Introduction to Literature, Criticism and Theory*. New York: Pearson.
- Borg, W. R. na Gall, M. D. (1989). *Educational Research: An Introduction*. New York: Longman.
- Chuachua, R. (2011). *Itikadi Katika Riwaya za Shaaban Robert*. Dar es Salaam: Taasisi ya Taluma za Kiswahili.
- Derrida, J. (1976). *Of Grammatology and Writing and Difference*. (G. C. Spivak, Mtaf.). Baltimore: John Hopkins.
- Derrida, J. (1987). Structure, Sign and Play in The Discourse of The Human Sciences. in *Writing and differences*. (A. Bass, Mtaf.) Chicago: University of Chicago Press.
- Eagleton, T. (1976). *Marxism and Literary Criticism*. London: Methuen.

- Eagleton, T. (1976). *Criticism and Ideology: A study in Marxist Literary Theory*. London: NLB.
- Eagleton, T. (1983). *Literary Theory: An Introduction*. Minnesota: University of Minnesota Press.
- Friedman, T. L. (2005) *The World is Flat: A Brief History of The Twenty-first Century*. New York: Farrar Straus and Giroux.
- Gramsci, A. (1985). *Selections From Cultural Writings*. London: Lawrence and Wishart.
- Habwe, J. (2005). *Paradiso*. Nairobi: JKF.
- Hegel, G. (1977). *Phenomenology of Spirit*. (A.V. Miller, Mtaf.).Oxford: Oxford University Press.
- Hobbes, T. (1970). *Leviathan*. London Collier: Macmillan Ltd.
- Hough, G. (1966). *An Essay on Criticism*: London: Redwood Press.
- Hussein, E.(1971) *Mashetani*.Nairobi:Oxford University Press.
- Kamunde, M. (1983). Kilio Cha Wanyonge Katika Riwaya za Said Ahmed Mohamed. Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa. Nairobi: Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Kant, W. (1968). *Religion Within The Bounds of Pure Reason*. (T. M. Green & Hoyt, H. Wataf.). London: Torch book.
- Kezilahabi, E. (1971). *Rosa Mistika*. Dar es Saalam: East African Literature Bureau.
- Kezilahabi, E. (1974). *Kichwamaji*. Nairobi: EAPH.
- Kezilahabi, E. (1971). *Gamba la Nyoka*. Nairobi: EAPH.
- King'ei, G. K. (1997). *Mwongozo wa Amezidi*. Nairobi: EAPH.

- Lofchie, M. (1965). *Zanzibar: Background to The Revolution*. New Jersey: Princeton University Press.
- Lorrain, J. (1979). *The Concept of Ideology*. London : Hutchinson&co publishers ltd
- Lukacs, G. (1971). *History and Class Consciousness: Studies in Marxist Dialects*. London: Merlin Press.
- Lugano, C. (1989). Mwanamke Katika Riwaya za Kezilahabi. Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa: Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Marx, K. (1973). *On Literature and Art*. New York: International General.
- Marx, K. na Engels, F. (1977). *The German Ideology*. London: Lawrence and Wishart.
- Marx,K(1979). *Pre-Capitalist Social Economic Formations*.Moscow:Progress Publishers
- Mbatiah, M. (1990). Dhana ya Kukua Kwa Mwandishi Kama Inavyodhihirika Katika Kazi za S. Robert na S.A Mohamed. Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa. Nairobi: Chuo Kikuu Cha Nairobi.
- Mbatia, M. (1997). Commitment in the Swahili Novel: An Appraisal of The Works of Said Ahmed Mohamed. Katika D. P .B Massamba na M. M. Mulokozi (wah.) *Kiswahili Juzuu 60*. Dar-es-Salaam: TUKI.
- Mbatiah, M. (1999). The Origin and Development of The Swahili Theses Novel in Tanzania. Tasnifu ya Uzamifu ambayo haijachapishwa: Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Mkangi, G. K. (1984). *Mafuta*. Nairobi: Heinemann.
- Mkangi, G. K. (1995). *Walenisi*. Nairobi: Sasa Sema.

- Mofolou, J. (1974). Ideology and National Building; The Tanzanian case. Tasnifu ya Uzamifu ambayo haijachapishwa: Chuo Kikuu cha Boston.
- Mohamed, S. A. (1974). *Vito Vya Hekima, Simo, Milio na Tashbihi*. Nairobi: Longman.
- Mohamed, S. A. (1977). *Asali Chungu*. Nairobi: EAEP.
- Mohamed, S. A. (1980). *Utengano*. Nairobi: Longhorn Publishers.
- Mohamed, S. A. (1980). *Dunia Mti Mkavu*. Nairobi: Longman Kenya.
- Mohamed, S. A. (1980). *Sikate Ttamaa*. Nairobi: Longman Kenya.
- Mohamed, S. A. (1984). *Kina Cha Maisha*. Nairobi: Longman Kenya.
- Mohamed, S. A. (1988). *Pungwa*. Nairobi: Longman Kenya.
- Mohamed, S. A. (1988). *Kiza Katika Nuru*. Nairobi: Oxford University Press.
- Mohamed, S. A. (1990). *Tata za Asumini*. Nairobi: Longman Kenya.
- Mohamed, S. A. (1990). *Kivuli Kinaishi*. Nairobi: Oxford University Press.
- Mohamed, S. A. (1990). *Mbinu na Mazoezi ya Ushairi*. Nairobi: Evans Brothers (Kenya) Ltd.
- Mohamed, S. A. (1995). *Kunga za Nathari ya Kiswahili: Tamthilia, Riwaya na Hadithi fupi*. Nairobi: E.A.E.P
- Mohamed, S. A. (1995). *Amezidi*. Nairobi: E.A.E.P.
- Mohamed, S. A. (1997). Learning From Mwenda Mbatia: The literary Critic. Katika D. P. B. Massamba na M. M. Mulokozi (wah.). *Kiswahili. Vol. 60*. Dar es Salaam: TUKI.
- Mohamed, S. A. (2000). *Kitumbua Kimeingia Mchanga*. Nairobi: Oxford University Press.

- Mohamed, S. A. (2001). *Babu Alipofufuka*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Mohamed, S. A. (2002). *Sadiki Ukipenda na Hadithi Nyingine*. Nairobi: JKF.
- Mohamed, S. A. (2002). *Jicho la Ndani*. Nairobi: Longhorn Publishers.
- Mohamed, S. A. (2005). *Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine*. Nairobi: Longhorn Publishers.
- Mohamed, S. A. (2006) *Dunia Yao*. Nairobi: Oxford University Press
- Mohamed, S. A. na King'ei, K. (2008). *Posa za Bi Kisiwa*. Nairobi: Longhorn Publishers.
- Mohamed, S. A. (2010). *Nyuso za Mwanamke*. Nairobi: Longhorn Publishers.
- Mohamed, S. A. (2011). *Janga La Werevu*. Nairobi: Longhorn Publishers.
- Mohamed, S. A. (2012). *Mhanga Nafsi Yangu*. Nairobi: Longhorn Publishers.
- Mohamed, S. A. (2013). *Mkamandume*. Nairobi: Longhorn Publishers.
- Mohamed, S. M. (1976). *Nyota ya Rehema*. Nairobi: Oxford University Press.
- Mohamed, S. M. (1972). *Kiu*. Nairobi: E.A.E.P.
- Momanyi, C. (1999). *Usawiri wa Mwanamke Mwislamu Katika Jamii ya Waswahili Kama Ilivyobainishwa Katika Ushairi wa Kiswahili. Tasnifu ya Uzamifu ambayo haijachapishwa*. Nairobi: Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Momanyi, C. (2006). *Tumaini*. Nairobi: Videmuwa Publishers.
- Msokile, M. (1992). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: E. A. P.
- Mugenda, A. (2008). *Social Science Research: Theory and Principles*. Nairobi; Arts Press.
- Mugenda, O. & Mugenda, A. (1999). *Research Methods: Quantative and Qualitative Approaches*. Nairobi: Arts Press

- Muindi, C. (1990). *Usawiri wa Wanawake Katika Vitabu Vya S.A. Mohamed. Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa. Nairobi: Chuo Kikuu cha Kenyatta.*
- Mukobwa, J. N. (1985). *Maendeleo ya Kimaudhui Katika Tamthilia Tano za Ebrahim N. Hussein. Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa. Nairobi: Chuo Kikuu cha Nairobi.*
- Musembi, N. (2008). *Matumizi ya Taswira na Ukinzano Kama K.ichocheo cha Zinduko Katika Riwaya za G. K. Mkangi: Mafuta (1984) na Walenisi (1995). Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa. Nairobi: Chuo Kikuu cha Kenyatta.*
- Ngara, E. (1985). *Art and Ideology in African Novel: A Study of The Influence of Marxism On African Writing. London: Heinemann.*
- Ngugi, T. (1972). *Homecoming: Essays on African and Caribbean Literature, culture and politics. London: Heinemann.*
- Ngugi, T. (1975) *The Novelist as a Teacher. Katika Morning yet on creation day. London: Anchor Books.*
- Njogu, K. (1987). *Maudhui ya Mapinduzi Katika Riwaya za Visiwani Zanzibar. Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa. Nairobi: Chuo Kikuu cha Nairobi.*
- Njogu, K. na Chimera, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu. Nairobi: JKF.*
- Njogu, K.(1997). *Uhakiki wa Riwaya za Visiwani Zanzibar, Nairobi: U.O.N Press.*
- Njogu, K.(2001). *Mwongozo wa Kilio Cha Haki .Nairobi. E.A.P*

- Nocera, P. (2005). An Interpretation of Said Ahmed Mohamed's Novel *Kiza Katika Nuru* and Some Aspects of Translation. Katika Beck R. M. (mha.) *Swahili Forum uk.* 63- 80. Universitat Zu Koln: Institut Fur Afrikanistik.
- Osore, K. (2008). Defamiliarization in the Novels of Euphrase Kezilahabi and S. A. Mohamed. Tasnifu ya Uzamifu ambayo haijachapishwa. Nairobi: Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Plato. (1969). *The Republic*. I. A. Richards (mtaf. na mhar.) Cambridge: Cambridge University Press.
- Rossiland, F. (1990). *Marxism and Ideology*. Oxford: Clarendon press.
- Rousseau, J. (1973). *The Social Contract and Discourses*. G. D .H. Cole, (mtaf.). London: Dent.
- Sanja, W. (2012). Maudhui ya Ndoa na Dini Katika Riwaya za *Kala Tufaha* na *Paradiso*. Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa. Nairobi: Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Shafi, A. (1978). *Kasri ya Mwinyi Fuad*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.
- Shafi, A. (1979). *Kuli*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.
- Sirucha, R (1986). Hadhi na Hali ya Mwanamke katika Riwaya za S. A. Mohamed. Tasnifu ya Uzamifu ambayo haijachapishwa. Nairobi: Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Stoika, J. L. (1972). Ideology and Nation Building in Tanzania: A micro-study of shinyanga district 1961-1970. Tasnifu ya Uzamifu ambayo haijachapishwa. New York: Chuo Kikuu cha Washington.
- Swaleh, A. (2011). A Critique of the Mapping and Construction of Gender Identity and

Authority in Selected Kiswahili Novels. Tasnifu ya Uzamifu ambayo
haijachapishwa. Nairobi: Chuo Kikuu cha Nairobi.

TUKI. (2013). *Kamusi ya Kiswahili sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.

Vonyoli, A. (2004). Hadithi kama chombo cha maudhui katika fasihi: Uchanganuzi
katika riwaya za Mkangi, G.K. *Mafuta* (1984) na *Walenisi* (1995).
Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa. Nairobi: Chuo Kikuu cha
Kenyatta.

Wafula, R. na Njogu K. (2007). *Nadharia za uhakiki wa fasihi*. Nairobi: JKF.

Walibora, K. na Mohamed, S. A. (2007). *Damu nyeusi na hadithi nyingine*. Nairobi:
Moran Publishers.

Wanyonyi, C.M. (2011). Uhakiki wa Riwaya ya Nyuso za Mwanamke na
S.A. Mohamed: Mtazamo wa Saikolojia Changanuzi. Tasnifu ya
uzamili ambayo haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Nairobi.

KIAMBATISHO I

MASWALI KWA MTUNZI

1. Naomba unieleze ulizaliwa wapi?
2. Wazazi wako ni nani?
3. Ukoo wako ni upi?
4. Ulizaliwa lini?
5. Ulizaliwa katika mazingira ya aina gani?
6. Ulisomea wapi?
7. Ulifunzwa na walimu wepi na nani kati yao amekuathiri sana?
8. Hupenda kusoma vitabu vya aina gani?
9. Imani gani imekuwa ikitawala katika maisha yako?
10. Imani yako ya kidini ni ipi?
11. Kiuchumi unaendelea vipi?
12. Msimamo wako wa kisiasa ni upi?
13. Utamaduni unaofaa ni upi?
14. Umeandika vitabu vingapi kufikia sasa?
15. Kati ya vitabu hivyo vyote, kipi kinachokupendeza zaidi?

KIAMBATISHO II

MASWALI KWA WATAALAMU WENGINE

1. Je, wamfahamu mtunzi S.A. Mohamed?
2. Wamfahamu vipi tafadhali?
3. Umesoma kazi zake zozote?
4. Kati ya kazi zake umesoma riwaya zake zipi?
4. Ni mambo yepi yameshughulikiwa katika vitabu vyake vya riwaya ulivyovisoma?
5. Kwa maoni yako fikra zipi na mitazamo ipi inayojitokeza katika vitabu vyake vya riwaya ulivyosoma?
6. Je, wahisi kwamba S. A. Mohamed ameathiriwa na watunzi wengine? Ikiwa ni hivyo wataje tafadhali?
7. Ukilinganisha kazi zake za awali na sasa kuna mabadiliko yoyote kwa upande wa vitushi, maudhui, wahusika na mbinu za lugha?
8. Kama kuna mabadiliko wafikiria ni kwa nini yanajitokeza katika kazi zake?
9. Je, maoni yako ya kijumla kuhusu kazi za S A Mohamed ni yepi?
10. Je, maoni yako kuhusu imani fikra na falsafa yake kwa ujumla ni yepi?